Kueneza upandaji kanisa ni kiini cha lengo la “Z” kufikiri kwa sababu tu kupitia kanisa kazi zingine za uombaji, munganiko wa kupendana, maono, kuinjilisha, na utoaji inaweza kutendeka ulimwenguni. Kwa sababu kanisa lazima limfikie kila mmoja, kueneza upandaji kanisa lazima kuendeshe “Z” kufikiri. Mungu anataka “Z” na kanisa linapofanya kazi kulingana na mapenzi ya Mungu, kazi ya kueneza upandaji kanisa itazidi haraka. Kueneza au kulijaza taifa makanisa inafanya kazi kuelekea kwenye lengo la watu wote kuisikia injili.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni nini tofauti kati ya mpanda kanisa kwa “Z” kufikiri na wapanda kanisa wengine?
- Je, unaomba kwa ajili ya taifa zima? Mkoa? Mji? Vijiji na ujirani?
- Je, unaomba kwa ajili ya watenda kazi kwa mavuno ya Mungu? Kama Yesu ametuamru kuomba kwa ajili ya hili, atakuwa mwaminifu kujibu kama tunaomba kwa uaminifu? Kwa nini kuna watenda kazi wachache?
- Uko tayari kufanya kazi na kuwapenda ndugu wa madhehebu mengine na kutoa ushauri kwa yale yasiyo asili yake kuelekezwa Kwenye “Z?” Hivi maombi ya Yesu ya umoja yatajibiwa au aliomba tu kwa ajili ya bure? Utaweza kuwa sehemu ya majibu ya maombi yake?
- Je, watu kwa nje wanalitazama kanisa lako kama tu dhehebu au dini , au kama watu wanaopendana?
- Maono yako ni kupanda kanisa moja au kuwa miongoni mwa harakati zitakazoujaza ulimwengu na makanisa yanayohubiri injili?



- Je, unazidisha utoaji wa fedha? Je, kanisa lako linazidisha utoaji wa fedha? Unafundisha juu ya utoaji? Kama ni la, kwa kuwa utoaji umefundishwa katika maandiko, kwa nini wewe usiufundishe?
- Lengo la uinjilisti wako ni kusudi ufanye kanisa lako kuwa kubwa, au pia upande makanisa mengine mapya?

#### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Anza kifikiri juu ya mbinu za kueneza upandaji kanisa ambao ni pamoja na maombi, umoja, upendo, maono, uinjilisti, na upandaji wa makanisa. Andika baadhi ya mawazo ya kuanzia na mshirikishe mshauri au mkufunzi wako wa baraza.
- Fikiria juu ya ujirani wako, kijiji, mji, eneo, au nchi. Tafakari jibu lako kwenye swali, Ni nini Mungu anataka kwa \_\_\_\_\_? Orodhesha vitu vitatu utakavyofanya kuona “Z” inatimia katika eneo lako.

MAONO YA KUM

SOMO LA

2

# Utume Mkuu na Upandaji Kanisa

## KUENEZA UFUASISHAJI

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuwasilisha maono kwa uhamasishaji wa kueneza harakati za upandaji kanisa, kwa kuutii Utume Mkuu.

### ☞ Wazo Kuu

- Kuuelewa Utume Mkuu ni kwa lazima kwa kueneza upandaji kanisa.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujua kwa nini Mathayo 28:18-20 inajulikana kama Utume Mkuu.
- Kuelewa jinsi kanisa litakavyokwenda na kufanya wanafunzi wa mataifa yote linapongezeka
- Kuelewa jinsi gani kanisa linakamilisha Utume Mkuu.
- Kuanzisha maono juu ya harakati za kueneza upandaji kanisa katika taifa unalotoka.

## UTANGULIZI

Katika Mathayo 28:18-20, Tunajifunza kuwa kuna kazi kubwa inayotukabili. Utume Mkuu ni amri ambayo lazima kila kizazi cha wakristo kiitii. Pamoja na amri, Yesu ameahidi kuwa atakuwa pamoja nasi mpaka kazi itakapomalizika. Amri hii inaitwa Utume Mkuu kwa sababu ya ukubwa wa kazi ambayo Yesu aliwaitia wanafunzi wake kuitimiza.

### I. KUELEWA UTUME MKUU


Katika Utume Mkuu, Yesu anaweka wazi kusudi lake kwa ajili ya kanisa lake mpaka hapo atakaporudi. Maneno haya ni muhimu sana na yanastahili kutazamwa kwa uangalifu. Chini kuna tafsiri halisi ya Mathayo 28:18-20 kutoka katika chimbuko la lugha ya Kiyunani.

“Mamlaka **yote** nimepewa mbinguni na duniani. Basi, enendeni mkawafanye mataifa **yote** kuwa wanafunzi wangu, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika **yote** niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku **zote**, hata ukamilifu wa dahari.” (Tafsiri halisi ya Mathayo 28:18-20).

Katika Utume Mkuu, Yesu anaweka wazi kusudi lake kwa ajili ya kanisa lake mpaka hapo atakaporudi.

Neno la kati na muhimu kupita katika Utume Mkuu ni “fanya wanafunzi.” Kama tendo pekee la kuamuru katika Utume Mkuu wa Mungu, inabeba kwa kiwango cha juu sana haja aliyonayo Yesu kwa wafuasi wake. Kufanya wanafunzi kwa hiyo ni moyo wa Utume Mkuu. Matendo mengine mawili, yote viwakilishi, “kubatiza” na “kufundisha” pamoja na maungo yake kamili, yanapanua na kuelezea tendo kuu “fanya wanafunzi.” Tendo la kufanya wanafunzi kwa njia ya ubatizo na mafundisho ina nia iliyoenezwa katika kifungu cha “mataifa yote.” Amri inatwaa kuwa yule anayefanya wanafunzi “anakwenda.” Zaidi ya hayo, ahadi kwamba Yesu yuko pamoja na hao wanaofanya mambo haya “nami nipo pamoja nanyi siku zote, hata mwisho wa dunia” inazunguka amri nzima.

## Kielelezo 2. 1 Utume Mkuu



### A. Agizo la: Kufanya Wanafunzi

Msisitizo mkuu wa Utume Mkuu uko kwenye kiini cha amri ya “fanya mataifa kuwa wanafunzi wangu.” Kwa hiyo kazi kubwa ya kanisa, ni kuwafanya mataifa kuwa wanafunzi, siyo tu waliokata shauri. Vitendo vidogo viwili vilivyotumika vinadhihirisha umuhimu wa kipengele cha kufanya wafuasi.

#### 1. Kubatiza – ‘Kumgeukia Kristo’

Ubatizo ni ushuhuda wa wazi kuhusu kugeuzwa, ni ishara kwamba mtu amefanyiwa uinjilisti. Ili kwamba mtu awe mfuasi wa Yesu Kristo, ni lazima atubu na kuamini (Mk 1:15, Mdo 20:21). Ubatizo ni ishara na kifungo cha vizazi, ni ishara ya msamaha wa dhambi na ya maisha mapya katika Yesu Kristo (Tit 3:5, Mk 1:4, Rum 6:3-4).

Utume Mkuu unaonyesha kwamba ubatizo ni “katika” utatu. Kutokana na hili tunajifunza kitu fulani cha asili ya upya wa wanafunzi. Mojawapo ya sifa ya ajabu ya Utatu ni ushirika wa jamii ya Baba, Mwana na Roho. Katika namna sawa, muumini anabatizwa katika jamii ya kanisa; jamii ambayo Yesu anahitaji awe na ushirika wa aina hiyo (Yoh 17) kama utatu.

#### 2. Kufundisha – ‘Kuwa Kama Kristo’

Wakati wa kukata shauri, wanafunzi wapya lazima wafundishwe kuhusu ni nani waliyeamua kumfuata. Mabadiliko yanahusisha uhusiano wa Mungu mtu. Tumeamriwa kuwafundisha waumini kuwa “wafuasi” au “wanaojifunza” kwa Yesu, tukiwafundisha kuzitii amri.

Ni kazi ya kanisa kufundisha utii kwa Kristo. Nukuru kwa uangalifu kwamba mstari hausemi kwamba lengo ni kufundisha amri, badala yake, lengo ni kufundisha utii kwa yote ambayo Yesu aliyowaamuru. Hii inamaanisha kwamba, kanisa lazima lifundishe mapenzi yote ya Kristo, bila kuacha hata moja. Utii usiokamili, ambao ni rahisi hupelekea kuwa kama kawaida, hautoshi. Isipokuwa, ni lazima tuyachunguze maandiko, huku tukijiuliza wenyewe, tumetii kila kilichoandikwa mahali hapa?” Na “namna gani tunaweza kutii kila amri kwa uaminifu zaidi?” Mafundisho juu ya utii kamili ni hali inayoendelea. Tambua kuwa siyo tendo la muda linalotangulia mbele ya ubatizo, lakini katika fungu, inafuatia ubatizo na kuendelea katika maisha yote ya muumini.

## B. Upeo: WOTE

Utume Mkuu haukuwa mpango wa muda hasa kwa wale tu waliousikia mara ya kwanza. Kujirudiarudia kwa neno **“Wote”** Inaonyesha matumizi yake ya hali ya juu.

### 1. *Chanzo cha amri ni mamlaka ya Yesu*

Yesu alitangaza cheo chake ulimwenguni mwote kabla ya kuwaagiza wanafunzi wake. Wakati mtu mwenye amri anatangaza cheo chake kabla ya kutoa agizo, ni kusisitiza umuhimu wa amri. Kwa hiyo, wale wote wanaokiri mamlaka ya Yesu lazima watii Utume Mkuu.

Yesu Kristo ni kichwa cha kanisa (Efe 1:22-23). Hao wanaokiri ukuu wake ni miongoni mwa mwili wake, yaani kanisa. Jukumu la kufuasisha taifa siyo tu jukumu la mwinjilisti; ni jukumu la wale wote wanaojitua kwenye ukuu wa mamlaka ya Yesu. Utume Mkuu unawapa waumini hisia ya kutambua kusudi.

### 2. *Jinsi ya tabia ya amri ni “kwenda.”*

Kiyunani cha kwanza kwenye “nenda” inaweza kutafasiriwa ‘kama unakwenda’ au ‘umekwenda.’ Inadhaniwa kuwa wote wanaotii Utume Mkuu “wanakwenda.” Kinyume cha “kuja” kwenye hekalu la Yerusalemu kuona utukufu wa Mungu, tunakwenda na utukufu wa Mungu ukiwa pamoja nasi (2Kor 3:18). Yesu hakufanya wanafunzi katika darasa pweke lililojitenga lisiloweza kuzaa, lakini katika mazingira ya kuendelea na maisha. Huduma ya kanisa inapaswa pia kuwa na hali ya kuendea ulimwengu na siyo ulimwengu kulifuata.

Yesu aliweka wazi kuwa makusudio yake ni habari njema kuwafikia mataifa yote. (Mt 24:14). Upande mwingine fungu la Utume Mkuu la (Luk 24:47 na Mdo 1:8) tunasoma kwamba kuenea kwa kanisa kungeanzia Yerusalemu. Kwa jinsi hiyo, Tangu mitume aliowaagiza Yesu walibakia Yerusalemu, Inaonekana kanisa la kwanza lilikuwa na mwamko mdogo wa umishenari mpaka Mdo 8. Kanisa la kwanza, linaonekana, lilielewa neno tu, “kuanzia Yerusalemu” na siyo maneno “na kwa mataifa yote.

- Mamlaka Yote
- Mataifa Yote
- Vitu Vyote
- Siku Zote

#### *Kwenda kwa sababu ya mateso*

Yesu anaweza kutumia ukuu wa mamlaka yake kulifanya kanisa kwenda kwa mataifa kama ni lazima. Baada ya kipindi cha adha na mateso ya kufia dini ya Stefano, kanisa lilianza kuiteleka injili nje zaidi. Mdo 8:1 inaorodhesha, “Siku hiyo kukatokea adha kuu ya kanisa lililokuwa katika Yerusalemu, wote wakatawanyika katika nchi ya Uyahudi na Samaria.” Mdo 11:19-20 inasema, Basi wale waliotawanyika kwa sababu ya ile dhiki iliyotukia kwa habari ya Stefano, wakasafiri hata Foinike na Kipro na Antiokia, wakihubiri...” Yesu aliruhusu dhiki kuwafanya wakiristo kutenda, katika kuitikia kwenye misukosuko, amabcho wangukuwa wamefanya juu ya amri yake.

#### *Kwenda kwa sababu ya utii*

Katika Mdo 13: 1-3, katika kanisa la Antiokia walikuwa waminifu kwa Utume Mkuu. Kama walivyoongozwa na Roho Mtakatifu, walimtumia Paulo na Barnabas huko Kipro, ambako “walilhubiri neno la Mungu katika masinagogi ya Wayahudi” (Mdo 13:4-5). Kutoka Kipro, Paulo na watumishi wao wakasafiri sana kabla ya kurudi Antiokia (Mdo 113:6ff).

Mungu amelipa kanisa jukumu la kuhubiri habari njema. Kama vile Paulo anavyoliandikia kanisa la Korintho, “Lakini vyote vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo na kutupatia huduma ya upatanisho: yaani, Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao. Naye ametia ndani yetu neno la upatanisho” (2Kor 5:18-19). Kama kanisa la antiokia, kanisa lazima liyafikie mataifa kwa utii, lakini kama kanisa halitii, Yesu ametumia misukosuko kukamilisha kazi yake,

3. *Shabaha ya amri ni “kwa ajili ya mataifa yote.”*

Kifungu, “Kwa ajili ya mataifa yote” kinasimama moja kwa moja kinyume na habari ya mwisho ya Yesu akiwatuma wanafunzi wake, ambapo shabaha ya wakati huo ilikuwa kwa ajili ya kondoo waliopotea wa Israeli (10:5,6). Hapa tumeitiwa kuipeleka injili kwa mataifa yote kwa kuwa Yesu ametununia kwa damu yake “watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa” (Uf 5:9). Mtume Yohana alipata bahati ya kuiona amri hii ikitimia katika maono yake ya mbinguni ambayo ilikuwa ni pamoja na watu kutoka mataifa yote wakimwabudu Bwana (Uf 7:9).

Ni nini maana ya taifa? Neno la Kiyunani katika kifungu hiki ni neno ethnos. Hili ni neno kutoka “makabila yanakotoka” kikundi cha makabila ni kikundi cha watu walioungana kutokana na lugha zao, mila na desturi. Nchi inaweza kuwa na vikundi tofauti vya kabila ndani ya mipaka yake. Ili harakati za kueneza upandaji kanisa kufanikiwa, mara nyingi mataifa mbali mbali (ethnos) lazima yafikiwe miongoni mwa kila nchi. Kila kundi la kabila lazima lifikiwe katika lugha yao na kulingana na mila na desturi zao kama tunataka kutii Utume Mkuu kwa kuipeleka injili kwa ‘mataifa yote.’

4. *Muda wa kudumu wa amri ni “Mpaka miisho ya dunia”*

Kwa maneno haya “mpaka miisho ya dunia” Yesu anaonyesha taratibu hizi ni kwa ajili ya kanisa mpaka atakaporudi, siyo tu kwa ajili ya wanafunzi kumi na wawili. Tunatakiwa kuvumilia katika mambo haya matatu “mpaka mwisho wa dunia,” hii ni mpaka Yesu atakaporudi kulichukua kanisa lake. Ni wakati gani, Yesu atakuwa “amehubiriwa katika dunia yote kama ushuhuda kwa mataifa yote” (Mt 24:14).

C. Ahadi

Kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi inaweza kuonekana kama kazi ya kulemeza. Kwa jinsi hiyo, kadiri tunavyokwenda kufuasa, tunaweza kwenda kwa ujasiri. Tumehakikishiwa ushindi mwishoni kwa sababu Yesu sasa ana **mamlaka yote** na ameahidi kuwa pamoja nasi **siku zote** mpaka mwisho wa dunia. Yesu mwenyewe ni hakikisho la ushindi, tukikaa ndani yake, kutegemeana na uwepo na mamlaka yake (Yoh 15:4-17). Yesu analipa kanisa lake lote agizo lake kuu mpaka atakaporudi na ahadi ambayo ushindi wake umehahakikishwa!

Yesu analipa kanisa lake lote agizo lake kuu mpaka atakaporudi na ahadi ambayo ushindi wake umehahakikishwa!

Katika ukumbusho wa Agano la Kale, tunaona jinsi kanisa la kwanza lilivyoishi kwa utii wa agizo hili. Mtume Paulo, akiwa gerezeni, aliliandikia kanisa la Wafilipi kwa ujasiri (Flp 1:6) “Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Yesu Kristo.” Kwa sababu alitambua kuwa Mungu alikuwa akitenda kazi na kwamba Roho wa Mungu alikuwa akikaa ndani ya waumini na katikati ya ushirika wa waumini, alijua kazi yake haikuwa bure. Na hii ni habari njema kwetu tunapokuwa tukifikiri namna na tukitimiza Utume Mkuu.

II. UTUME MKUU NA KUENEZA UPANDAJI KANISA

Kueneza upandaji kanisa inatimiza maelekezo na malengo ya Utume Mkuu. Kulingana na Mathayo 24:14, Marko 13:10, Luka 24:45-47, na Matendo 1:8, Utume Mkuu utatimizwa endapo kutakuwa na wanafunzi katika kila taifa. Kadiri makanisa yanavyopandwa katika kila taifa, wanafunzi wanapatikana katika taifa hilo.

A. Utume Mkuu na Kusudi la Kanisa

Kutimiza kazi ya Utume Mkuu ni wajibu wa kanisa. Kanisa halipo ili kujitumikia, au kuendeleza taratibu zao isipokuwa kuipeleka injili kwa “mataifa yote.” Huduma ya kanisa ya kuwafikia watu siyo tu mojawapo ya huduma nyingi; kuna sababu ya kuwepo kwa huduma hiyo. Kanisa lazima likue kwa kupitia uinjilisti na kuongezeka lenyewe kwa njia ya upandaji kanisa ili kwamba wengi waendeleo kuwa wanafunzi wa Yesu. Taratibu na huduma za kanisa lazima zitathiminiwe na kuendelezwa kulingana na namna gani kusudi hili linafanyika. Je inatokea katika namna ya kufuasa kulikokusudiwa na Yesu alipotoa Utume Mkuu?

Viongozi wa kanisa lazima wawawezeshe waumini kutimiza kusudi la Utume Mkuu kwa kuwafundisha kushirikisha imani yao kwa waliopotea, kwa kuweka wazi hali halisi ya

umishenari, na kwa kuwapa maono ya kuomba na kutoa fedha kwenye mavuno. Viongozi wa kanisa mara nyingi wanazingwa na kuendesha huduma peke yao na kukataa kuwaelimisha wengine kufanya huduma hizo. Kwa jinsi hiyo, kupitia kuelimisha, huduma inaweza kuendesha na wengi kuliko mtu mmoja. Kumbuka kuwa Yesu alikabidhi habari njema na huduma kwa wanafunzi wake, na kwa kufanya hivyo, ikasababisha kazi yake kuongezeka mara dufu.

## B. Utume Mkuu na Upandaji Kanisa

Kama nia ya Mungu Mkuu ni kufanya wanafunzi wa kimataifa, hivyo lazima tuendelee kutafuta njia bora ya kufanikisha hili. Baada ya yote, Wengi wameyatoa maisha yao kwenye kutimiza kusudi la Utume Mkuu. Ni jambo la busara kulinganisha njia mbalimbali za huduma kufanikisha kusudi la Utume Mkuu. Je, kila moja ni mfano wa chimbuko linalohitajiwa na Utume Mkuu? Njia ipi ni bora kufanya wanafunzi kulingana na Utume Mkuu? Kusaidia kujibu swali hili, tutaangalia katika njia tatu za huduma kuona ni namna gani zimelinganishwa katika ufanisi wa Utume Mkuu.

Njia ya kwanza katika kulinganisha itakuwa ni kanisa lililoanzishwa. Kwa dhumuni la somo hili, kanisa "lililoanzishwa" litaelezwa kama kanisa ambalo lina zaidi ya miaka 10. Njia ya tatu inaitwa "huduma ya kuwafikia watu isiyo ya kanisa." Huduma hii inaweza kuelezewa kama huduma yeyote isiyo ya kanisa bali ya juhudi za kiinjilisti kama vile mikutano ya nje ya mapokeo, uinjilisti kwa njia ya Redio, n.k. Wazo kuu ni kwamba, ni aina ya huduma ya uinjilisti isiyotokana na kanisa na siyo lazima iwe ni sehemu ya kanisa la mtaa. Njia ya tatu tutakayoichunguza itakuwa ni kupanda kanisa jipya. Kwa upandaji kanisa, tuna maana kufanya mawasiliano, kuwaongoza watu kwenye toba, kuwafundisha waumini, kuwabatiza na kuanzisha huduma ya kuabudu itakayotelea kuwa kusanyiko ambalo linatimiza kazi ya agano jipya kwa wafuasi wa Yesu.

### Kelelezo 2.2 Utume Mkuu na Upandaji kanisa


UTUME MKUU  <i>KANUNI:</i>	UINJILISTI  <i>"ubatizo" Kumgeukia Kristo</i>	KUFUNDISHA  <i>"Kufundisha Utii" Kuwa Kama Yesu</i>	Matokeo:  <i>"KUFUASA"</i>
Kanisa Lililoanzishwa	SIYO MARA KWA MARA	NDIYO	LABDA...
Uinjilisti Usio wa Kanisa	NDIYO	SIYO MARA KWA MARA	LABDA...
Upandaji Kanisa	NDIYO	NDIYO	NDIYO!!

Kama inavyoonekana katika kielelezo 2.2, kwa kulinganisha njia hizi tatu kunadhihirisha upandaji kanisa unatimiza zaidi Utume Mkuu. Makanisa yaliyokwisha anzishwa yanasisitiza juu ya kufuasa bila kuhusika kikamilifu katika kuwaleta watu kwa Yesu, wakati huduma za kiinjilisti zisizo za kanisa zinawaleta watu kwa Yesu lakini bila msisitizo zaidi wa mafunzo ya kutosha (yamkini kuna chache katika hizi). Upandaji kanisa, kwa hiyo, unaunganisha asili zote hizi, kufanya wakata shauri wapya na kisha kutoa mazingira asili ya ufuasishaji wao.

Ni wazi, njia nyingi zinatimiza kutimiza kusudi la Utume Mkuu, yeyote inaweza kulinganishwa na upandaji kanisa. Mifano iliyoorodheshwa hapo juu ilitimika kwa kifupi kukazia ukweli kwamba upandaji kanisa kikamilifu unakamilisha kanuni na kusudio la Utume Mkuu kadiri wanafunzi wapya wanapofanywa kupitia uinjilisti na ufuasishaji. Njia zingine zipo, lakini upandaji kanisa unastahili wakati wote kipao mbele kinachoongezeka kutokana na ukweli kwamba unaelekeana zaidi na Utume Mkuu uliotolewa na Bwana wetu.

Upandaji kanisa unasahili kipao mbele kinachoongezeka daima kutokana na ukweli kwamba unaunganisha Utume Mkuu uliotolewa na Bwana wetu

### Kelelezo 2.3 Utume Mkuu na Kanisa



#### SULUHU

Utume Mkuu ni amri ya kufanya wanafunzi tunapobatiza waliokata shauri wapya na kuwafundisha kumtii Yesu. Kazi yetu inahusu kwenda ulimwenguni kufanya wanafunzi katika makundi yote ya watu, na siyo kusubiri wao kutufuata. Mamlaka yetu na hakikisho letu ni katika yeye mwenyewe, aliyeahidi kuwa pamoja nasi mpaka kazi itakapotimia.

Kanisa lipo kufanya wanafunzi wa mataifa yote na hivyo kutimiza kazi aliyotoa Kristo. Kila vipindi na juhudi za huduma kwa namna fulani zinachangia kufikia kwenye lengo hili. Utume Mkuu utakamilika tu endapo kanisa litakapotambua mamlaka ya Yesu Kristo na kutii kazi aliyotoa.

Kazi yetu inahusu kwenda ulimwenguni kufanya wanafunzi katika makundi yote ya watu, na siyo kusubiri wao kutufuata.

Kanisa jipya lililopandwa linatimiza amri ya “kufanya wanafunzi” kupitia uinjilisti kwa waliokata shauri wapya. Makanisa yanayoelewa kusudi lao na sababu ya kuwepo kwake yataanzisha makanisa mapya na yakiwa na sababu hii moja ya kuwepo, na kwa kufanya hivyo kutatoa njia ya kufikia “mataifa yote” kwa injili. Wapanda kanisa na wote wanaojihusisha katika kuanzisha makanisa mapya wako katika huduma ya pekee na ya kimikakati, kwa kuwa inalenga kanuni iliyofundishwa katika Utume Mkuu. Kuiweka kwa kifupi, upandaji kanisa ni njia bora zaidi ya kutimiza Utume Mkuu.

#### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Umekubali mamlaka ya Yesu kwa kufanya kazi ya Utume Mkuu? Je, kanisa lako linafahamu mamlaka ya amri kuu ya Yesu ya “ nenda na fanya mataifa yote kuwa wanafunzi wangu?” Je wamevutwa na kusudi hilo?
- Ni namna gani unavyoweza kuhamasisha kanisa lako kutimiza Utume Mkuu?
- Je, kanisa lako linajitoa kwa ajili ya mamlaka ya Bwana kwa kufuasa taifa lako na mataifa mengine?
- Hivi Yesu ataweza kutumia mateso tena, matatizo ya kiuchumi, na/au utii wa kutimiza Utume Mkuu?
- Umekwisha kuchagua “kwenda” nje ya utii au unasubiri misuko suko?
- Unaelekeza upandaji kanisa wako kwenye kufanya wafuasi wa Yesu, au kukuza kanisa lako?
- Wewe na hao unaowafundisha mna maono ya kuyafikia mataifa?
- Unawafundisha watu kwa mafundisho ya utii wa vitendo, au mafundisho yako ni maelezo tu?

#### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Endeleza na fuasa kundi la watu watakaoliombea taifa lako na mataifa mengine, anza kutoa fedha kwenye taifa na umishenari wa kigeni, na anza hatua ya kwanza ya upandaji kanisa na maono ya kufikia mataifa yote.



# Mzunguko a Upandaji Kanisa

## KUPATA PICHA KUBWA

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kutambulisha “Mzunguko wa upandaji kanisa”, likisisitizia kwa makini hatua inayohusika katika upandaji kanisa la mtaa na harakati za upandaji kanisa

### ☞ Wazo Kuu

- Mzunguko wa upandaji kanisa hautakiwi kuwa tu kama mtiririko wa matukio ya kubahatisha.
- Utaratibu wa upandaji kanisa ni pamoja na kuweka msingi, kuwavuta waliopotea,
- Kuwaandaa waumini kwenye ushirika, kuwafundisha kwa ajili ya huduma, na kuzidisha kusanyiko la waumini, unaotokea katika harakati za makanisa mapya.
- Lengo la upandaji kanisa siyo tu kanisa moja lakini ni harakati za makanisa kwenye maeneo yanayolengwa.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa mafunzo ya kufundisha kwa wapanda kanisa na utaratibu wa upandaji kanisa
- Kuweza kuchanganua hatua muhimu sita katika kuzalisha makanisa.
- Kuelewa kuwa lengo la kueneza upandaji kanisa siyo tu kusanyiko la kanisa moja jipya, lakini makanisa zaidi na harakati za upandaji kanisa katika kila nchi.

### ☞ Ziada

3A Vielezo vya upandaji kanisa

### ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Tengeneza mwonekamo au kibao cha matangazo kutokana na kielelezo 3.1 na rejeza kwake mwanzo kila kipindi kuwakumbusha wapanda kanisa ni mahali gani ulipo kwa wakati huo katika maelekezo yako na ni wapi unaelekea juu ya utaratibu wa upandaji kanisa.

Jadili na wafunzwa juu ya miundo mbalimbali ya upandaji kanisa kama ilivyoelezewa katika ziada 3A. Ni upi kati ya miundo hiyo imedhihirisha ufanisi katika mazingira yao na ni ipi haikudhihirisha? Ni ipi miongoni imepelekea utayari wa harakati za upandaji makanisa?

## UTANGULIZI

Mafundi wanatumia mara nyingi vielezo kuwakilisha wazo lao. Chapa ya bluu ni mfano mmojawapo wa kielezo anachoweza kuutumia fundi. Kwa kuangalia chapa ya bluu, fundi anaweza kuona sura mbalimbali za kazi ya majengo pamoja na kulinganisha na nyingine kabla jengo halijajengwa hasa. Inatumika pia kama mwongozo wa namna ya kujenga jengo. Inamwezesha zaidi fundi kuona ni katika utaratibu gani vifaa tofauti vya ujenzi vinaweza kukusanywa.

Katika namna sawa, kueneza upandaji kanisa siyo mtiririko wa matukio ya kubahatisha. Ni msukumo wa lengo. Lengo la kueneza upandaji kanisa linaweza kuelezewa katika ngazi tofauti, kutegemeana na hatua inayofaa kwenye utaratibu. Watu lazima wawe wamevutwa kwenye imani katika Kristo na kulishwa neno na kuwekwa katika jamii ya kanisa la mtaa la wanaoamini. Viongozi lazima wawe wamefundishwa kukubali mwelekeo na maendeleo ya kanisa. Makanisa yanayokomaa lazima yazidi mara dufu yenyewe kupitia juhudi za upandaji kanisa jipya. Matokeo ya yote haya ni kwamba eneo




lako na taifa vijazwe na mtikisiko, makanisa yanayozaliana. Hakika, lengo la mwisho ni kwamba bibi arusi awe ameandaliwa tayari kwa uzima wa milele pamoja na Bwana.

“Mzunguko wa upandaji kanisa” (kielelezo 3.1) ni mchoro unaoonyesha utataratibu wa upandaji kanisa., kutokana na mtazamo maalumu, mahusiano ya kanuni muhimu na mazoezi kazini katikati ya utaratibu huo.

Ziada 3A ina vielezo tofauti vya njia ambazo utaratibu huu umetumika katika kupanda makanisa.

### Kielelezo 3.1 Mzunguko wa Upandaji Kanisa



#### I. AWAMU YA 1—MISINGI

Mwanzo unaweza kuwa mgumu katika kila utaratibu mgumu. Wapanda kanisa wanaanza utaratibu wa upandaji kanisa kwa kuendeleza kutembea na Yesu binafsi kunakohitajiwa kwa mtu kuwa mtumishi wa injili. Mtume Paul anaonya dhidi ya kujenga msingi kwenye msingi mwingine isipokuwa wa Yesu (1Kor 3:11). Kuchukulia hili kama jambo la kawaida tu inapelekea kushindwa katika huduma.

Kutokuwa na picha halisi akilini ya kanisa linalohitaji kupandwa kunaweza kukatiza upandaji kanisa. Kwa hiyo, kuchanganua maono na kupanga mikakati ya upandaji kanisa ni muhimu sana katika hatua hii. Utafiti ni sehemu muhimu katika hili. Taarifa ya kimikakati juu ya nguvu ya mavuno na shamba la mavuno zitasaidia kuweka sura ya mkakati. Lengo la utafiti ni kupata kuelewa watu hao ambao wapanda kanisa wanatamani kuwafikia...na vileville kujifunza ni rasilimali zipi zilizopo kuwafikia.

#### A. Mstari wa Ufunguo wa Maandiko

*“Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi na mtu mwingine akajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake. Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni uliokwisha kuwekwa, yaani Yesu Kristo” (1Kor 3:10-11).*

#### B. Shughuli na Lengo

##### Shughuli:

- Anzisha maono kwa maombi
- Tafiti wakazi wanaolengwa.
- Endeleza uzoefu binafsi katika imani yako.
- Endeleza uzoefu binafsi katika kujifunza Biblia.
- Anza kuonyesha mkakati wa upandaji kanisa na njia.

**Lengol:** Jiandae mwenyewe, maono yako na mwelekeo kwenye misheni ya upandaji kanisa.

#### C. Mambo ya Ufunguo ya kufikiri katika Awamu Hii

- Ni nini misheni ya Mungu duniani? Ni kwa jinsi gani kanisa linaingia katika misheni hiyo?
- Ni nini shamba langu la mavuno? Ni nini Mungu anataka kwangu katika eneo langu?
- Ni nini namna ya kipengele cha kipekee cha wito na maono anayonipa Mungu?
- Ni aina gani ya kanisa linaloweza kukidhi mahitaji haya? Linatakiwa liwe la kuzaliana?
- Ni vizuizi gani vikubwa vya kuendeleza upandaji kanisa?
- Ni nani atasaidia? Nani ni nguvu ya mavuno? Ni jinsi gani tunafanya utafiti?

## II. AWAMU YA 11—KULETA WATU

Uinjilisti kamwe hauishii kanisani tu, hata hivyo hatua hii ya kipekee ni kipindi wakati mpanda kanisa anapokazania zaidi kwenye uinjilisti. Mfano wa mpanda kanisa katika hatua hii utakuwa ufunguo katika kuweza kuongoza na kuandaa wengine kufanya uinjilisti katika hatua ya baadaye.

Haiwezekani kupanda kanisa bila kufanya uinjilisti. Mara nyingi sana, wapanda kanisa wanakazania katika kutafuta wakristo wengine kuwa katika kanisa lao mapya, badala ya kukazania katika uinjilisti wa mtu binafsi. Bila kutumia muda unaotakiwa kuwa na wasio-wakristo na kutumaini kuwa Mungu atawapeleka katika kanisa jipya, mara chache sana hili linatoa matunda ya kiunjilisti.

Wapanda kanisa wanatakiwa kuanzisha vikundi vya kiinjilisti vinavyokazia katika kuanzisha mahusiano, na kuhusisha majadiliano ya jinsi Biblia inavyohusika katika hali za maisha, maombi kwa mahitaji binafsi, na kutiana moyo. Kama watu hawajazoea kushirikisha kibinafsi, katika awamu ya uwazi, hili lazima liendelezwe katikati ya kipindi maalumu. Kutumia muda binafsi na pamoja na wanakikundi wa vikundi kiini itapanua uhusiano na kukuza ushirika. Viongozi wa vikundi kiini wanapaswa kuendeleza viongozi wa vikundi mapema iwezekanavyo. Mikutano inapaswa kuwa rahisi ili kwamba iweze kuzaa. Kama wanategemea viongozi, mtindo wake, au ufahamu wake kisha itakuwa vigumu kutafuta viongozi baadaye.

#### A. Mstari wa Ufunguo

*“Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nikijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi. Nalikuwa kama Myahudi kwa Wyahudi, ili nipate Wayahudi... Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia*

*zote nipate kuwaokoa watu. Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya injili ili kushiriki pamoja na wengine” (1Kor 9:19-23).*

## B. Shughuli na Lengo

### **Shughuli:**

- Wasiliana na Viongozi muhimu na fanya uhusiano nao.
- Injilisha waliopotea
- Anzisha kikundi cha kiinjilisti cha kujifunza Biblia.
- Uwe kielelezo cha huduma kwa waliokata shauri.
- Fuasa waliokata shauri wapya kumtii Kristo.

**Lengo:** Wasiliana na Injilisha wajumbe muhimu wa wakazi wanaolengwa

## C. Mambo Muhimu ya Kufikiria Katika Awamu Hii

- Ni njia zipi za kiinjilisti ambazo ni za ufanisi zaidi kwetu kuweza kufikia malengo yetu?
- Ni namna gani tunafanya mawasiliano na viongozi nyeti? Ni nani hao? Ni namna gani tunawapata?
- Ni namna gani tunawafundisha waumini wapya kushuhudia marafiki na familia zao?
- Ni namna gani tunaanza kuwafuasa na kuwaanda kwa ajili ya huduma? Nini na namna gani tunawafundisha?
- Ni namna gani unagundua mtandao wa marafiki zao na kuanza kuwainjilisha?
- Ni makundi mangapi ya kiini tunahitaji kuanzisha kabla ya kuwakusanya katika makundi makubwa?

## III. AWAMU YA 111—KUANZISHA

Inaweza kuchukua mwaka au zaidi kufikia hatua hii, viongozi wengi wa kanisa wanaichukulia nafasi hii kama mahali ambapo kanisa “limezaliwa” kiofisi na kiuhalisi. Kuanzisha makundi kama kanisa la mtaa ina namna ya kipekee ya kuanzishwa. Katika hatua hii, vikundi kiini vinatakiwa kuwa vinakua na kuongezeka na vinaweza kuanza kukutanika pamoja kusherehekea huduma, hata kuanzisha kuabudu wazi mara chache chache. Kama inafaa, ukumbi unaweza kukodishwa kwa ajili ya hilo, lakini uwe macho kuwa hili linafanyika mapema sana mara kwa mara. Wapanda kanisa inabidi wawe na vikundi kiini mbalimbali vyenye nguvu vinavyofanya mkutano wa kati ya watu 30-40 wanaohudhuria kabla ya kukodisha ukumbi. Makundi madogo yanaendelea hata baada ya mkutano wa kuabudu mkubwa kuanza na wanaendelea kuwa msingi wa kulisha neno na ukuaji wa kanisa.

Mkazo wa kuinjilisha unaendelea wakati wote wa maisha ya kanisa. Lakini wakati wa hatua hii, mpanda kanisa anasisitiza hasa kufuasa katika maisha ya waliokata shauri wapya, na hapo kuunda namna ya huduma ya ufuasishaji itakayoendelea baadaye. Tatizo sugu wakati wa hatua hii siyo kutoelewa vya kutosha kwa wakristo wapya. Baadhi ya wapanda kanisa wanatarajia waumini wapya kuhitaji sawa na yale ambayo kila mmoja anataka, au hawajaandaliwa kuwapa wakristo wapya hatua kwa hatua njia kwenye ukuaji kiroho. Wengine wanaweza kuwa wagumu kwa wakristo wapya, kulazimisha sheria na kufanya uhalalishaji bila kuwa na neema, au kutafuta ukomavu kwa haraka sana kutoka kwa watoto wachanga wa kiroho. Kukubalika na uvumilivu ni tabia ya pekee katika kuwasaidia wakristo wapya.

## A. Mstari wa Ufunguo

*“Tukaangaliane sisi kwa sisi, kuhimizana katika upendo na kazi nzuri. Wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine, bali tuonyane na kuzidi kufanya hivyo, kwa kadiri muonavyo kuwa siku ile inakaribia.” (Ebr 10:24-25)*

## B. Shughuli na Lengo

### **Shughuli:**

- Fuasa waliokata shauri.
- Shauri viongozi wanaoibuka.
- Panua juhudi za uinjilisti kupitia mtandao wa marafiki.
- Zidisha vikundi kiini.
- Anza kuabudu kunakoendelea kwa mara kwa mara.

**Lengo:** Kusanya waumini na washiriki wote kusherehekea huduma za ibada

## C. Mambo ya Ufunguo ya Kufikiria katika Awamu Hii

- Ni jinsi gani viongozi wapya wa vikundi kiini watafundishwa na kutolewa?
- Ni lini tunahitaji kubatiza waumini? Lini na nani awapatie Ushirika wa meza ya Bwana?
- Ni jinsi gani unaanzisha waumini wapya katika hakikisho la ubatizo wao?
- Ni jinsi gani utanzisha 'maisha ya mwili?' ' Ni jinsi gani waumini wapya watajisikia kuwa sawa?
- Tunapokusanyika, tunakutana wapi? Ni jinsi gani tunawaalika watu?
- Ni mifumo gani tutatumia kufikia lengo lililokusudiwa? Ni mtindo gani wa kuabudu tutakaotumia?

## IV. AWAMU YA 1V—KUFUNZA

Wakati wa hatua tatu za kwanza za kanisa jipya, mfanyakazi wa kimishenari mara nyingi anachukua majukumu makubwa ya kanisa, zaidi kama mzazi anavyoweza kuchukua majukumu makubwa ya kazi katika familia ya watoto wadogo. Katika namna sawa watoto hao watatakiwa kuchukua majukumu makubwa au zaidi watakapokua, hivyo waumini wapya wanatakiwa kuchukua majukumu makubwa watakapokomaa. Wakati wa ngazi hii, wapanda makanisa wanarithisha majukumu ya uinjilisti, kufuasa, na majukumu ya uongozi mpya.

Kama wapanda kanisa hawatachukua muda kugawa majukumu, kutoa mafunzo na kuwatoa wengine katika huduma, kisha kanisa halitaweza kukua kupita uwezo wa mchungaji mmoja na mhudumu kwa wengine

Kwa kutumaini kwanza katika Bwana, wapanda kanisa wanatakiwa kuwa na ujasiri wa kutosha kwa wengine kuwaandaa kuongoza huduma za kanisa. Mungu amempa kipawa kila muumini, na wote wana wajibu wa kuhudumu. Kama wapanda kanisa hawatachukua muda kugawa majukumu, kutoa mafunzo na kuwatoa wengine katika huduma, kisha kanisa halitaweza kukua kupita uwezo wa mchungaji mmoja na mhudumu kwa wengine. Anajikaza kupita uwezo wake, na kwa kifupi wakristo wapya hawawezi kujisikia nyumbani katika kanisa jipya. Watu katika kanisa wanaweza kukua kwa kudanganywa pia, bila kuwa na majukumu ya maana kwa huduma ya kuwavutia kuendelea kuhusika. Wanageuka kuwa wapekuzi. Vielelezo vibaya katika utamaduni viliruhusu hili Mashariki ya Ulaya.

### A. Mstari wa Ufunguo

*"Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine" (2Tim 2:2).*

## B. Shughuli na Lengo

### **Shughuli:**

- Jenga sura ya viongozi wanaohitajika katika kila eneo la huduma
- Gundua vipawa walivyonyavyo wajumbe wote
- Fundisha viongozi wa kikundi kiini
- Panga na kutoa viongozi kwenye huduma
- Andaa muundo na nafasi ya huduma uliyonayo akilini kwa ajili ya huduma.

**Lengo:** Funza Viongozi na wafanyakazi wa kanisa.

## C. Mambo ya Ufunguo ya Kufikia katika Awamu Hii

- Ni jinsi gani tunawaweka waumini wapya kutambua vipawa vyao vya kiroho? Nani atawafundisha?
- Ni eneo gani la mafundisho linalohitajika? Wapi na jinsi gani mafundisho haya yatatolewa?
- Nani ni viongozi muhimu? Ni nini uwezo wao na vipawa vyao? Ni waaminifu, katika kuwahudumia watu?
- Ni wapi hao waliofundishwa watakuwa na huduma? Ni mahitaji gani muhimu na ni mambo gani ya kuangalia katika eneo hilo? Ni lini huduma yao itaanza katika eneo hilo? Ni kwa nani watatoa taarifa? Ni nini mgawanyo wao wa kazi?

## V. AWAMU YA V—KUZIDISHA

Ili Utume Mkuu utimizwe, ongezeko lazima liwe sehemu ya kawaida ya huduma ya kanisa katika kila ngazi. Mwalimu mzuri wa Biblia hatafuti tu kutoa wanafunzi, lakini walimu zaidi wa Biblia. Alama ya kiongozi mzuri siyo tu wafuasi, lakini pia viongozi wapya. Huduma ya uinjilisti haitoi tu walioamini wapya, lakini wainjilisti wapya. Katika namna sawa, mara kanisa linapokuwa limeanzishwa, kuongezeka na kuzaa makanisa binti kunatakiwa kuwe kitu cha kawaida.

Badala ya kuongezeka, viongozi wengi wapya, wanajaribu kukalia kudumisha au kuongeza kwenye kile amabacho wameshakuwanacho. Wanaweza kuridhika na ukubwa wa kanisa, na bila kukazia hasa kufanya kazi ya kuongeza. Haja ya kujenga jengo kama sehemu kuwepo kwa “kanisa” mara nyingi kunalemeza katika awamu hii.

Viongozi hawa wanatakiwa kutambua kuwa kuna kipimo cha kukua. Kiasili, kila kiumbe hai mwanzoni au baadaye inapofikia katika kiwango fulani cha kukua, na kisha kufa, wakati matunda au vizazi vyake vitaendelea kuishi. Kanuni zinafanana na za huduma ya kanisa. Kiakili, “tunda” la kweli la kanisa siyo waumini wapya, isipokuwa kanisa jipya. Njia hasa ya uhakika kwa kanisa kuwa na matokeo mapana ni katika kujiongeza lenyewe. Kupanda watoto wa kanisa. Viongozi bora kwa kanisa binti wanaotoka miongoni mwa kanisa lenyewe, kuliko kutoka sehemu ya umbali kama vile kwenye vyuo vya Biblia au shule ya seminari. Viongozi wanahitaji kutia moyo maono ya kuongezeka ili kwamba makanisa mengi yaweze kuanzishwa katika mji na maeneo.

### A. Mstari wa Ufunguo

*“Lakini mtapokea nguvu, akisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika uyahudi wote, na Samaria na hata mwisho wa nchi” (Mdo 1:8).*

## B. Shughuli na Lengo

### **Shughuli:**

- Waongoze viongozi kuunda timu za upandaji kanisa
- Wafundishe wafanya kazi katika ngazi mbali mbali za huduma.
- Tafiti maeneo mapya unapojisikia tayari kuanzisha huduma.
- Panga na endesha juhudi za kiinjilisti za kimkakati.
- Anzisha na teua viongozi kwa ajili ya chama cha shirika la huduma.

**Goal:** Anzisha msingi wa viongozi kuunda timu za upandaji kanisa

## C. Mambo ya Ufunguo ya Kufikiria Katika Awamu Hii

- Ni aina gani ya utafiti unahitaji kufanyika? Nani atafanya? Je kuna Kikundi cha watu karibu na eneo hilo ambao hawajafikiwa kwa injili? Kuna viongozi nyeti miongoni mwao wanaoweza kufunzwa?
- Ni malengo gani yanahitaji kuandaliwa na kuchapwa? Ni nani anaendesha juhudi za maombi kuwezesha huduma hii?
- Ni nani anagawa na kusimamia shughuli zote za huduma? Ni nani atakayewafundisha katika elimu inayoendelea?
- Kuna huduma zingine ambazo zinaweza kuunganishwa katika juhudi hii? Ni nani awaalike kujiunga na nguvu hii? Ni mchango gani wa kipekee watakoachangia kwa ujumla katika juhudi za kimishenari?
- Tunahitaji ngazi ya juu ya huduma ya elimu kufunza ngazi mbalimbali za uongozi katika harakati hizi? Nani atafundisha? Ni namna gani itachangiwa?

## VI. AWAMU YA V1—HARAKATI

Lengo la upandaji kanisa siyo tu kwa ajili ya kusanyiko moja, bali kuongezeka zaidi kwa makanisa katika kila eneo. Harakati za upandaji kanisa zinaweza kuelezewa kama upandaji na ukuzaji wa makanisa katika eneo fulani kwa mtindo usio wa kawaida chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Harakati za upandaji kanisa zina sifa ya umoja, kufundisha na kuhamasisha mwili wote wa Kristo, lengo maalumu na maono.

Paulo, Mtume na mpanda kanisa alitumiwa na Roho Mtakatifu. Baada ya kupanda kanisa huko Efeso, alitumia muda wa miaka miwili akiwa anawafundisha wanafunzi katika shimo la Tirano. Alifanya kazi kwa namna kwamba “Uyahudi yote na Asia wakalisikia neno la Mungu” (Mdo 19:10). Makanisa yaliyopandwa huko Asia (Efeso, Kolosai, Laodikia, -, yanatoa ushahidi wa harakati hizi za upandaji kanisa na kilikuwa chanzo cha Paulo kueleza kuwa Asia yote wamesikia neno la Bwana.

Wapanda kanisa na viongozi inabidi waanzishe huduma zao ikiwa ni pamoja na maono ya harakati za upandaji kanisa. Mfano wa kisasa wa huduma hii unapatikana wakati injili inapokuwa imeenea katika njia za harakati za upandaji kanisa katika nchi mbalimbali ulimwenguni mwote leo. Kwa kujifunza harakati hizi kwa mwanga wa kanuni za huduma za kibiblia, wapanda kanisa wanaweza kuanza huku wakiwa na mwisho akilini, inakuza zaidi ufanisi.

### A. Mstari wa Ufunguo

“...maana dunia itajawa na kumjua Bwana, kama vile maji yanavyoifunika bahari” (Isa 11:9).

## B. Shughuli na Lengo

### **Shughuli:**

- Funika koo za wakazi wote.
- Anzisha mipaka ya kuenea kwa harakati.
- Onyesha miradi ya tamaduni tofauti itakayodhaminiwa na vikundi
- Endesha maombi na shukurani za kutia moyo.
- Tenga eneo na/malengo ya taifa.
- Anzisha ngazi za juu za mafunzo kwa viongozi nyeti wa harakati.

**Lengo:** Mkanisa yaliyoongezwa kuenea eneo, taifa na kupita.

## C. Mambo ya Ufunguo ya Kufikiria

- Harakati zinajieneza zenyewe, kujisaidia, na kujitawala? Kama siyo, nini kinahitajika kifanyike kuhakikisha kwamba ndivyo?
- Ni eneo gani au watu bado hawajafikiwa? Ni miradi gani ya kimishenari Bwana anatuongoza kuianzisha?
- Ni aina gani ya mafunzo yanahitajika kwa ajili ya harakati? Jinsi gani itasaidiwa?
- Ni akina nani ni “aina ya mitume” viongozi wa harakati? Jinsi gani tunafanya kazi pamoja nao? Jinsi gani tunaweza kuwatia moyo na kuwasaidia? Ni nini mahitaji yao?

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni hatua gani inaonekana kuwa ngumu zaidi kwako na kwa hali yako ya upandaji kanisa?
- Ni kwa jinsi gani majukumu ya wapanda kanisa yanabadilika katika kipindi kizima cha utaratibu?
- Ni kwa nini ni muhimu kuwa kanisa liongezeke lenyewe?
- Unadhani ni kwa muda gani itachukua kwako wewe kuweza kufikia hatua ya harakati katika maeneo yako?
- Kuna juhudi zozote za kihuduma katika mkoa wako (uinjilisti, kufuasa, kufundisha) ambazo siyo sehemu ya mzunguko wa upandaji kanisa? Ni kwa jinsi gani huduma hizi zinaweza kuwa sehemu ya mzunguko wa upandaji kanisa?
- Fikiria vielezo tofauti tofauti vya upandaji kanisa vilivyoelezewa katika ziada 3A, “Vielezo vya Upandaji Kanisa.” Ni kipi miongoni mwa hivyo kimefanyiwa majaribio katika mandhali yako? Ni kipi kimekuwa na mafanikio na kipi ambacho hakikufanikiwa?

## UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Pamoja na hao unaofanya nao kazi katika juhudi za upandaji kanisa, jibu kila swali lililoorodheshwa kwa kila hatua ya mzunguko. Katika hatua hii ya utaratibu wa upandaji kanisa, Inaeleweka kuwa kihalisi huwezi kujibu maswali yote. Kwa jinsi hiyo, kuyajibu vizuri uwezavyo itakuwa mwanzo mzuri wa huduma yako ya baadaye.



# Vielezo vya Upandaji Kanisa

*Kuna njia nyingi za kupanda makanisa; Mandhali mara nyingi ndiyo yanayoonyesha nini kinafanya vizuri zaidi. Chini kuna miundo kadhaa. Bila shaka, hali yako ya upandaji kanisa inaweza ikawa ni pamoja na asili kutoka miundo iliyoelezewa hapa.*

## I. KIELEZO CHA KANISA BINTI

Muundo huu wa binti huenda ndio unaotumika zaidi kwa wingi na mara nyingi ndio unaokuja akilini wakati linapoanzishwa swala la upandaji kanisa. Muundo huu yamkini ndio unaotoa hali inayoonekana kuwa hai, kanisa lililopandwa linalokua kuwa kanisa mama linatoa rasilimali, msaada na kuwajibika tokea mwanzoni. Kuna hali tatu za kawaida zinazochochea upandaji wa kanisa binti.



### A. Washiriki Hutoka Sehemu Nyingine Tofauti

Kama idadi ya watu wanaoshiriki katika kanisa maalumu wanasafiri nje ya eneo hilo ambalo ndipo kanisa linahudumu kimsingi, kanisa linaweza kuona hilo kuwa kama nafasi ya kupanda kanisa jipya kwa kutuma kikundi cha watu kutoka kanisa mama.

### B. Kuna Hitaji la Mitindo Tofauti ya Kuabudu

Inawezekana kuwa aina ya kuabudu katika kanisa mama ikiwa sawa kwa walio wengi, lakini kuna wengine katika kanisa na jamii ambao wangependa zaidi aina tofauti ya kuabudu. Kama aina mpya inaweza kuanzishwa kanisani bila kusababisha kufarakana, kisha kanisa binti kwenye jengo hilo hilo au karibu ni uchaguzi mzuri. Kanisa binti linaweza kuwavutia watu wasio wa kanisa wanaoifurahia namna mpya ya kuabudu.

### C. Kuna Haja ya Kufikia Makundi Yote Kiuchumi na Kijamii

Hata wakati kanisa limekua na linawafikia watu wapya katika eneo fulani, inawezekana ikawa bado linashindwa kuwafikia makundi fulani ya watu katika sehemu. Tofauti ya madaraja, taifa, umri inaweza kuwa kwamba wengine hawatajisikia sawa kuabudu katika kanisa fulani. Mahitaji ya makundi haya yanaweza kuwa chanzo cha kuhitaji kanisa jipya ambalo litakidhi kawaida ya tamaduni zao kwa ufanisi zaidi

## II. UPANDAJI KANISA KWA KANUNI YA KUTAWANYA MATAWI.



Kiasili, mmea wa tunda linaloitwa strawberi unatoa nje shina, au kusukuma kwa nguvu, nje ya ardhi umbali kidogo kutoka pale ulipo. Shina hili linaitwa 'mtambaaji.' Mmea mpya binti uliopandwa mara nyingi unaanzia mwishoni mwa mtambaaji. Katika wakati, mmea binti utakapotuma watambaaji wenyewe kuanzisha mimea mingine ili kwamba kuwe na mimea pekee kadhaa. Lakini yote imeunganika kwa watambaaji.

Baadhi ya makanisa mama hupanda kusanyiko jipya ambalo halikusudiwi kuwa kanisa linalojitegemea, lakini lililo na kipimo cha kujitegemea na kiwango cha uhusiano unaoendelea. Kusanyiko kama hilo kijiografia liko karibu sana na kanisa mama ili kwamba yakutane pamoja kwa ibada ya pamoja kila wiki au kila mwezi. Kwa hivyo, kwa mfano, makusanyiko kadhaa yanaweza kukutana kitofauti kwa ajili ya ibada ya asubuhi na kuungana jioni kusherehekea.



## UPANDAJI KANISA KWA NJIA YA KURITHISHA

Wakati mwingine kundi lililopo (maombi, vikundi kiini, Kikundi cha kujifunza Biblia) hukaribisha kusanyiko au dhehebu kuchukua kazi yao. Kikundi kilichorithiwa kinategemea makanisa mama kutoa maono, mwongozo, uongozi, na mara nyingine nyongeza ya rasilimali za fedha na au/ watu ili kwamba waweze kuanza kufanya kazi kama kanisa.

## VIELEZO KWA UPANDAJI MAKANISA KWA UMBALI

### A. Upandaji Kanisa Kwa Njia ya Kutawala

Kielezo cha kutawala ni wakati familia moja au mbili zinapotumwa maeneo ya nje umbali fulani kutoka kanisa linalotuma lilipo kuanza kazi mpya. Katika hali hii umbali uliopo mara nyingi ni mkubwa kiasi kwamba kanisa mama halitumi watu wengi kwa sababu kielezo hki kinahitaji wavumbuzi kwenda kuwa na nyumba na ikiwezekana kupata kazi katika eneo hilo la kuandaa kanisa jipya.

### B. Upandaji Kutumia Timu ya Misheni ya Kiinjilisti

Baadhi ya madhehebu na mawakala wanatumia timu za wamishenari kuongoza na kusaidia katika utaratibu wa upandaji kanisa. Timu ndogo ya watu wawili mpaka watano wanaweza kukaa katika eneo fulani kuinjilisha, kuongoza vikundi kiini, na kuanzisha kanisa. Wanaweza kupata usaidizi kutoka kwenye timu za muda mfupi kwa mwaka.

### C. Upandaji Kanisa Kwa Njia ya Tukio Maalumu

Baadhi ya vikundi hutumia mikutano ya nje au picha ya mkanda wa Yesu kama njia ya kupanda makanisa. Hii inaweza kuanzishwa na kikundi kidogo cha wanaoamini hasa katika eneo ambalo halina kanisa. Kwa hakika, mchungaji wa muda au mwinjilisti anaweza kuongoza kikundi kuendeleza mawasiliano mapya. Kila inapowezekana, waumini wanya wanapatikana ili kwamba kundi la watu angalau ishirini linaundwa kabla ya mkutano wa nje wa kiinjilisti kufanyika. Wanaojitolea kutoka sehemu yoyote wanaweza kutangaza na kusaidia kuongoza tukio, ambalo linaweza kudumu kuanzia wiki moja mpaka mwezi. Lengo linaweza kuwa, kwa mfano, kuona angalau watu hamsini wanaamini na kufanya jumla ya watu sabini pamoja na mchungaji aliyekwisha kuwepo katika eneo, ili kuweza kuunda 'kanisa la mara moja.

## UPANDAJI WA MTU PEKEE

### A. Upandaji na Mvumbuzi

Baadhi ya watu, kiasili, ni wavumbuzi. Kwa kifupi wanataka kuanzisha makanisa! Inaonekana kwamba hata kama wangukuwa wameachwa katika jangwa bila kuwa na mtu karibu yao, kwa namna moja wangukua maji yalipo na kuchimba kisima ili kuweza kuwavuta watu kwao. Watu kama hao wanaweza kuona uwezekano wa kuwepo kanisa hata katika sehemu zingine ambapo hakuna mtu amewahi kufikiria. Wavumbuzi wako tofauti, baadhi wanaweza kufanya kazi na madhehebu makubwa au wakala wa upandaji kanisa. Wengine ni wepesi wa kutenda kiasi kwamba wanaona vigumu kujiunga na taratibu za mashirika na hivyo kufanya vizuri zaidi peke yao. Wagunduzi wanaweza kuanzisha makanisa mengi katika kipindi cha uhai wao. Mara kusanyiko linapokuwa limeanzishwa, ni wakati wa wavumbuzi kusonga mbele. Kukaa inaweza kuwa hasara kwa kile walichoanzisha kwa sababu hawana kipawa cha kutunza vitu.

### B. Upandaji na Mchungaji Mwanzilishi

Mara nyingi, wenye vipawa vya uchungaji, wanapokuwa wamesukumwa na huruma na maono, pia hupanda makanisa. Wanaweza kuwa hawana vipawa vyote vinavyohitajika kupanda kanisa. Lakini vipawa ambavyo hawana vitadhihirika katika maisha ya wajumbe wa timu pana. Wapanda makanisa hawa wanaongoza timu katika kipindi kirefu cha muda ili kwamba, mara kanisa linapokuwa limeanzishwa, wanakaa kama wachungaji wa kudumu.



## VYANZO

Robinson, Martin and David Spriggs. *Church Planting, The Training Manual*. Oxford, England. Lynx Communications, 1995



# Kanuni za Utafiti

## TAARIFA ZA MAKUSUDI YA KIMKAKATI

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuelewa maana ya nafasi ya kukusanyika na kuchanganua taarifa kwa ajili ya kuendeleza mikakati ya upandaji kanisa kwa ufanisi.

### ☞ Wazo Kuu

- Utafiti ni kukusanya taarifa kwa malengo ya mikakati
- Utafiti ni wazo la Kibiblia.
- Wapanda kanisa wanaweza kutumia utafiti kuendeleza mikakati na kuhamasisha rasilimali.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Aweze kuchanganua, kufundisha, na kuwawezesha watafiti kukusanya na kutumia taarifa kuendesha maono na shauku kwa kazi ya upandaji kanisa.
- Kuweza kuanzisha mradi wa utafiti katika eneo linalolengwa upandaji kanisa.
- Kujua hitaji na umuhimu wa utafiti kuvutia na kuandaa watu kwa ajili ya upandaji kanisa.

### ☞ Ziada

4A Kutambua eneo lako linalolengwa

4B Mfano wa Maswali ya utafiti

### ☞ Ushauri Kwa Wakufunzi

Kama inawezekana, uwe na mfano wa utafiti, ramani na kitu kilichofanyiwa mafunzo katika sehemu moja. Kitu cha kuonekana kitasaidia kutia moyo utafiti. Vilevile, wanafunzi watahitajika kufanya kazi ya utafiti iliyomo kwenye ziada 4A. Ruhusu muda wa kujadili kazi hii pamoja na washiriki.

## I. NINI MAANA YA UTAFITI?

### A. Utafiti ni kukusanya taarifa kwa malengo ya mikakati

Utafiti ni kifaa kinachosaidia kuhamasisha makanisa kuelekea kutimiza Utume mkuu. Unasaidia mawakala na makanisa kujua ni wapi makanisa yanahitajika kupandwa, na ni njia ipi ya uinjilisti yenye ufanisi /na isiyo na ufanisi miongoni mwa makundi mbalimbali ya watu. Utafiti pia unawasaidia wafanyakazi wa Kikiristo kuelewa picha kubwa ya nini Mungu anataka kufanya katika taifa au kikundi cha watu, inawasaidia kuendelea kuwa makini katika kazi ya kutimiza Utume Mkuu, kuhakikisha kuwa mikakati yao inaendelea kuwa ya kudumu na ya ufanisi, na kuwasaidia kujua ni lini kazi itamalizika.

Kadiri watu wa Mungu wanavyojiandaa kufanya kazi katika sehemu wasizozijua, taarifa ni daraja kutoka panapojulikana mpaka pasipojulikana. Taarifa zinawasaidia kufanya hatua ngumu ya kwanza.

Kabla ya kuingia kwenye eneo geni lisilojulikana la upandaji kanisa kimishenari, Paulo na Barnabas walikwenda Kipro, nyumbani kwa Barnabas alipojua na kuelewa hali halisi (Mdo 13:4-5). Kadiri watu wanavyozoea katika eneo, ndivyo wanavyokuwa na ujasiri zaidi kufanya kazi pale. Utafiti unatoa elimu, ambayo inaweza kuwa daraja kati ya sehemu inayojulikana na

isiyojulikana. Unapokuwa unafanya utafiti, inashauriwa kufanyia mazoezi mbinu za utafiti wetu katika sehemu zinazojulikana kabla ya kuhamia kujifunza sehemu isiyojulikana.

Lengo la utafiti siyo kuonyesha iwapo tupande makanisa, lakini kwa kifupi ni jinsi ya upandaji makanisa zaidi kwa ufanisi. Yesu anapanda kanisa lake kwa kupitia wale wanaojitoa kufanya upandaji kanisa. Kwa kuwa ameamuru kanisa lake kukua na kuongezeka, kanisa lake lazima litii kwa namna ya kihalisi na kuwajibika, kufanya takwimu halisi na wazi.

Utafiti wa **shamba la mavuno**, eneo ambalo upandaji kanisa utafanyika, na **nguvu ya mavuno**—hao watakaoshiriki kikamilifu katika upandaji kanisa—kunapelekea kwenye suluhu. Suluhu hii inaweza kuitwa, “wito kwa ajili ya kutenda.” Ni jumla ya kile ambacho utafiti umegundua, na kutafasiriwa katika mtazamo wa Mungu. Kwa mfano, “neni la kinabii” kwa Yohana ilikuwa, “kuchukua nchi aliyopewa” (Yos 1”1-11).

## B. Utafiti una Chanzo cha Kibiblia

Mara nyingi Mungu alipowaita watu katika huduma mpya, Kwanza Aliwaongoza kuchukua ghala la hali inayowazunguka. Katika kila hali zilizoenezwa chini, utafiti ilikuwa sehemu ya mpango wake kufanya kazi yake katika kipindi na sehemu maalumu na watu maalumu.

- Katika kitabu cha Hesabu, Mungu aliwaamuru Waisraeli kupigana. Hesabu 1:1-46 ni kadiri ya watu waliokuwepo kupigana katika jeshi. Mungu aliwaahidi waisraeli ushindi, lakini bado aliwataka wahesabu namba ya maaskari waliokuwapo kuendesha mapigano. Hii iliwaruhusu waisraeli kupanga watu wao kwa ajili ya kuimiliki nchi. Kupanda kanisa, taarifa zilizopatikana kutokana na utafiti kuhusu waliopo kufanya kazi ni nyenzo muhimu kwenye shirika.
- Mungu aliwaamuru wapelelezi kwenda kukusanya habari mpya za nchi ambayo waisraeli walikuwa waimiliki na kuongezeka kama ilivyoandikwa katika hesabu 13:1-14:38. Kwa kupitia uchunguzi wa wapelelezi’ Waisraeli waliweza kuona nchi ambayo walihitaji kuimiliki na kuona aina ya mbinu ambayo watatumia na ni vipingamizi gani wataweza kukabiliana navyo watakapoivamia nchi. Kwa upandaji kanisa, utafiti mzuri wa eneo ambao kupanda kanisa kutafanyika unaweza kuonyesha kanisa litakuwa na aina gani ya watu, namna ya kuwakabili, na ni vipingamizi gani vitahitajika kukabiliwa.
- Nehemia alifanya utafiti wa Yerusalemu kabla hajajaribu kuanza kazi ya kujenga ukuta wa mji (Neh 1:4, 2:1-6). Alifanya kwa akili tathimini ya mioyo ya watu ambao wangeweza kufanya kazi na hali halisi ya ukuta. Akiwa na taarifa hizi angeweza kuona, ni aina gani ya hatua ya kiutendaji atachukua kuweza kuimaliza kazi, na aliweza kujitayarisha mwenyewe kwa kazi ngumu iliyoko mbele yake. Kwa upandaji kanisa, kanuni hizi sawa zinahitajika.
- Yesu alikwenda miongoni mwa watu na kuona mahitaji yao kabla hajatuma wanafunzi wake kwenda kufanya kazi miongoni mwao (Mt 9:35-10:1). Kadiri alivyokuwa akitembea miongoni mwa watu na kuona mahitaji yaliyowalemea kwa wakati huo, alipatwa na huruma kuu kwa ajili yao kulingana na aliyoyaona. Uchunguzi huu pia ulimvuta kuhamasisha watu kwa ajili ya maombi na huduma. Kwa upandaji kanisa, utafiti wa habari mpya unaleta huruma, maombi ya kuhamasisha na huduma.
- Katika Yohana 4:35, Bwana aliwaamuru wanafunzi wake “kutazama” au “kuchunguza” (ambayo ni maana ya kiyunani) mavuno ya roho za watu. Wakati mwingine tunasahau jinsi Mungu anavyowaangalia watu. Ni namna gani tunawaangalia watu? Je tunawaangalia tu, tunawaona tu kama vipingamizi? Tunatingwa na kazi zetu wenyewe, kutatua matatizo yetu wenyewe. Ni rahisi kusahau kuwa Mungu anatutaka twende nje kwa watu na kuwaleta kwake. Anatumia ulinganifu wa mavuno, wakati ambapo wavunaji huenda shambani, na kuvuna mavuno yaliyoiva, na kuyaleta kwa mmiliki wa ardhi (Yoh 4:35-38).
- Bwana alipoongeza kwenye idadi yao, kanisa la kwanza lilitunza kumbukumbu za kuongezeka kwa kanisa na kutoa habari zake ( Mdo 2:41, 47, 4:4, 5:14, 9:31). Taarifa za namna hii zinatoa picha ya wapi na namna gani Mungu anatenda kazi katika maisha ya watu katika sehemu yoyote.

## II. NI WAPI UTAFITI UNAPASWA KUFANYIKA?

Kutafiti sehemu ambayo upandaji kanisa utafanyika inaweza kupelekea kukazia yale Mungu anayoyafanya na kusaidia kubainisha jinsi ya kuhudumu. Hatua ya kwanza na muhimu zaidi ya kufanyia utafiti eneo kwanza ni kutoa tafsiri ya eneo linalolengwa linalojulikana pia kama “mzunguko.”

Tafuta au chora eneo lengwa, na tafuta kila kitu iwezekanavyo kuhusu nani na nini kilichomo kwenye ukingo uliozungushiwa. Anza na eneo linalowezezana kuwa chanzo. Kuanza na eneo dogo kunajenga ujasiri wa kuirudia kazi katika kiwango na namba kubwa. Mara unapokuwa umechora mzunguko wako, hatua zinazofuata zitakusaidia kufanya utafiti.

- Jifunze iwezekanavyo juu ya nguvu ya mavuno na shamba la mavuno katika mzunguko
- Pima ramani ya eneo
- Punguza ramani kuonyesha takwimu muhimu kama vile wapi kanisa lilipo na ni aina gani ya makanisa vile vile na sehemu zingine zote muhimu kwa kazi hiyo (kwa mfano: Maeneo ya kidini, maeneo ya kisiasa, masoko, sehemu za kihistoria, n.k).

## III. NANI ANAPASWA KUFANYE UTAFITI?

Yeyote anaweza kufanya utafiti wa kawaida kwa ajili ya huduma ambayo Mungu amewaitia kufanya. Ingawa neno ‘utafiti’ linaweza kuwa kama la kiufundi na gumu, halitakiwi kuwa namna hiyo. Kwa kifupi sema, hao wanaofanya utafiti wanakusanya habari na kuwashirikisha wengine.

### A. Hao Wanaofanya Utafiti Wanakusanya Habari

Watu wanaopenda kukusanya mambo ya uhakika katika tabia ya ukamilifu wanafanya utafiti mzuri. Watafiti wanahitaji kuandaa na kugawanya takwimu zao katika namna ambayo inaashiria lengo la kueneza upandaji kanisa.

### B. Watafiti Lazima Watoe Habari ya Taarifa Walizokusanya

Watafiti wazuri wanajua namna ya kuweka vifupi vya maneno ya utafiti wao na kuwaelezea wengine ili kwamba waweze kupata picha halisi ya shamba la mavuno na nguvu ya mavuno. Wanaeleza katika namna inayovuta huruma na kujenga ujasiri wa kile Mungu anachotaka kufanya. Mueleza lazima awe wazi na hakika na aepuke kujivuna juu ya yote. Wanahitaji kutafuta kitu kikubwa kwenye mambo waliyotafiti kitakachovuta uangalifu wa wapanda kanisa na kutia moyo juhudi zao za upandaji kanisa.

Hao wanaofanya utafiti wanakusanya taarifa na kisha kuwashirikisha wengine.
---

Kumbuka Hesabu 13. Isipokuwa Yoshua na Kalebu walistahili kutoa utafiti hata kama wapelelezi wote 12 walifanya uchunguzi. Wote walisema kutoka kwenye uhakika, lakini kumi kati ya wapelelezi waliuona mtazamo kinyume na kukazia kwenye vizuizi, walisahau ahadi za Mungu. Kalebu na Yoshua walitambua ushindani na matatizo lakini hawakuwa na mashaka kwamba Mungu hatatimiza kusudi lake na wakaonyesha picha halisi ya kile Mungu anachoweza kufanya kutokana na hali halisi.

- Hao wanaoeleza utafiti wanatakiwa kuangalia hali halisi zenye maana zaidi ambazo zitaendana na kile wapanda kanisa wanachofikiria.
- Utafiti inabidi uguse hali halisi ya mambo yasiyo mazuri kuchochea huruma na kuunda juhudi za kushinda vizuizi.

## IV. LINI UTAFITI UNATAKIWA UFANYIKE?

Kuna angalau sehemu tatu katika mzunguko wa upandaji kanisa ambapo utafiti unahijika ufanyike (angalia maono ya KUM somo la 3, “Mzunguko wa upandaji Kanisa”).

### A. Awamu ya Kimsingi: Katika Matayarisho ya Kupanda Kanisa Maalumu

Unapopanda kanisa, ni muhimu kukusanya habari za kuonekana kuhusu watu, historia yao, hali ya kijiografia na hali iliyopo wakati huo, na kwa nini wanafikiri, kuamini, na kutenda kama wanavyofanya. Kujifunza juu ya mtazamo wa ulimwengu na mahitaji ya watu wanaoishi katika ‘mzunguko’ yaliyoachwa kunaweza kusaidia kuonyesha uinjilisti na mikakati ya upandaji

kanisa. Utafiti katika ngazi hii unaweza pia kusaidia kuonyesha rasilimali zilizopo za upandaji kanisa ambazo zinaweza kuhamasishwa kusaidia juhudi za upandaji kanisa. Utafiti lazima utafute mlango wazi ambao Mungu ameuruhusu katika eneo hilo kwa watu kuongea habari za Yesu.

#### **B. Awamu ya Kuanzisha: Kutathimini Ufanisi wa Kanisa**

Mara kanisa linapokuwa limepandwa, ni muhimu kutathimini ukuaji na ufanisi wa huduma. Ukuaji unaweza kupimwa kwa kuweka chati ya namba ya makundi madogo mapya, na kutunza kumbukumbu za mahudhurio. Huduma ya shughuli ya kutengeneza chati itasaidia kugundua namna watu wanavyoafiki njia iliyotumika kuwafikia.

#### **C. Awamu za Kuzidisha na Harakati: (Kupata Picha Kubwa)**

Kimkoa (au hata kitaifa) mradi wa utafiti unaweza kusaidia makanisa katikati ya eneo maalumu kuinjilisha waliopotea na kujaza eneo hilo kwa makanisa. Aina hii ya utafiti inaweza kuwa muhimu kugundua ngazi ya uchumi wa kijamii, makundi ya tamaduni, makundi ya umri fulani, habari za nyuma za kidini kwa hao waliopokea injili na ni kwa namna gani wanalinganisha na jamii ya watu kwa upana. Picha halisi ya hali ya ukristo katikati ya taifa inaweza kuwakilishwa katika mikutano ya ngazi ya mkoa. Aina hii ya utafiti inatia changamoto viongozi wa mkoa na wa mtaa kwa hitaji la upandaji kanisa na kuwafikia waliopotea.

### **V. KWA NINI WAPANDA KANISA WANAPASWA KUFANYA UTAFITI?**

#### **A. Taarifa Zinachochea Huruma kwa Watu Kwenye Mzunguko**

Yesu aliuafanya mji wa Galilaya kuwa eneo lililozungushiwa. Yesu alipokwenda miongoni mwa makutano, aliona mahitaji yao ya kimwili na kiroho, na aliwahurumia kwa sababu “walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji” (Mt 9:35-37). habari zote za wakati huo na taarifa kutoka kwenye uzoefu wa mtu zinasaidia kuhamasisha waumini wa makanisa yaliyopo kupanda makanisa mapya.

Taarifa zilizo na **masimulizi halisi ya maisha** ya watu za mahitaji ya injili zinasaidia kuleta umoja zikizingatia upendo kwa waliopotea. Mungu ametupa hisia ambazo, zinapoguswa, mara nyingi tunavutwa kuomba, kutoa au kujihusisha kwenye huduma kwa namna nyingine. Habari za takwimu mara nyingi hazitoi matokeo sawa kama masimulizi halisi ya maisha yalivyo. Masimulizi karibu mara nyingi yanatoka katika uzoefu wa kujionea kwa kwenda miongoni mwa watu.

*Ni aina gani ya vitu ambavyo vinaweza kuvuta huruma kwa watu wengine kuweza kuwafikia waliopotea?*

#### **B. Taarifa Huzaa Maombi**

Yesu alipoyaona mahitaji, aliagiza maombi kabla ya kitu kingine chochote. Taarifa zinasababisha watu kumlilia Mungu na kumtegemea kuweza kufanya kazi yake iliyopo kwenye mzunguko. Yesu aliwaamuru wanafunzi wake “kumuomba Bwana wa mavuno, ili kupeleka wafanya kazi shambani mwake” (Mt 9:38).

- Amri ya, kuomba kwa ajili ya wafanyakazi zaidi, kwa ajili ya mashujaa wa kiroho tu, au kwa ajili ya wafuasi wote wa Yesu?
- Kanisa lako linapoomba, ni mambo gani wanayoyaombea mara nyingi? Kanisa lako linamwomba Mungu kuongeza wafanyakazi kwa ajili ya mavuno? Kama siyo, ni kwa nini?

#### **C. Taarifa Zinasukuma Maono ya Kupanda Makanisa**

Habari nzuri zinahamasisha watu walioitwa na Mungu kwa ajili ya nguvu ya mavuno kutokana na maombi. Baada ya Yesu kuwaamuru wanafunzi wake kuomba, Aliwatuma nje kwenda kuvuna mavuno yaliyokuwa yakisubiri wafanyakazi (Mt 9:36-10:1). Katika kazi nyingine, aliwatuma sabini na mbili miongoni mwa wafuasi wake na amri hiyo hiyo ya kuomba Luk 10:1-2).

- Je watu katika makanisa yako wanafahamu juu ya mahitaji yaliyopo katika eneo lako?
- Wanavutwa kufuata maono hayo?

#### D. Taarifa Zinaimarisha Nguvu ya Mavuno Kuwa ya Ufanisi Zaidi

Hesabu halisi ya hesabu za rasilimali, watu, na hali tulizonazo vinatoa msingi wa kuanza kufanya kazi kwa busara. Utafiti unasaidia nguvu ya mavuno kugundua ni vitu gani vilivyopo na ni vitu gani havipo kwa ajili ya shamba Luk 14:28-33). Inatusaidia kujua ghala na kufanya mipango halisi, tukiamini kuwa Mungu atatoa kile kinachopungua.

- Ni nini ilikuwa kazi katika Yohana 6:5-14?
- Ni rasilimali gani zilizopo zilizodhihirishwa na matokeo ya utafiti?
- Ni nini utafiti ulionyesha kuwa idadi ya watu kwa wakazi waliolengwa?
- Ni nini Yesu alifanya kwa kutumia rasilimali kwa wakazi waliolengwa?
- Kama Yesu alijua ni nini alihitaji kufanya, kwa nini utafiti ulikuwa wa muhimu?

#### VI. NI KWA JINSI GANI UTAFITI UNAPASWA KUFANYIKA?

Utafiti lazima utumie njia zote zinazoweza kupata habari. Aina tofauti za habari zinaweza kutoa mtazamo tofauti. Chini kuna mifano mbalimbali ya aina za utafiti.

Ni bora kutojaribu kufanya utafiti peke yako. Funza wasaidizi watakaofanya kazi nawe. Utafiti unaofanyika pamoja na wengine unakuwa kamili zaidi na mchanganuo unakuwa bora kwa sababu unajenga juu ya mitazamo tofauti. Vilevile, kila mmoja wetu ana upungufu. Mara nyingi, mtu mmoja ataweza kugundua habari fulani nyeti, ambayo imeachwa au "kutoonwa" na mtu mwingine.

##### A. Uchunguzi

Habari mpya zilizoshuhudiwa na kuchunguzwa zina matokeo makubwa zaidi na zitakuwa sahihi zaidi. Baada ya mtu mwenyewe kwenda kwenye eneo lililozungushiwa, watafiti wanaweza kuzungumza na watu, kupata habari ya mahudhurio, kuona hali halisi kama zilivyo, kuchunguza kawaida za ibada, mila na utamaduni, na hasa kuuliza maswali.

Ufunguo wa kufanya utafiti wa kushuhudia ni kujua ni maswali gani ya kuanza nayo na ni maswali gani yatafuatia kuulizwa. Swali linaloanza na nani, nini, lini, wapi, kwa nini na jinsi gani (hasa mangapi na vingapi) linaleta majibu wazi. Kuuliza maelezo kwa yale unayoyaona inaweza kutoa picha wazi zaidi. Aina hii ya utafiti ni nyenzo bora kwa kuendeleza uhusiano.

##### B. Kuhoji

Kuhoji wengine wanaofahamu eneo linalolengwa kwa kuona inasaidia. Baada ya kulinganisha matokeo mbalimbali ya mahojiano, inawezekana kupata picha pana ya namna watu wanavyotambua hali pale. Inasaidia kupata baadhi ya habari ambazo mtu anayeangalia kutoka nje hawezi kuzipata. Hii pia inahitaji ujuzi katika mahusiano.

Unapowahoji watu, jua ni habari gani unazotafuta na jiandae kwa maswali yanayohusu shamba la mavuno na nguvu ya mavuno. Uliza maswali haya kiasili katika mazungumzo. Hii inawafanya watu kujua kuwa unathamini maoni yao. Kusoma maswali yaliyoandikwa inaweza kuwafanya watu wengine kuona kama wanapewa mtihani au kuwa wanafanyiwa utafiti. Wanaweza pia kujisikia kuogopeshwa kwa kusomewa kutoka kwenye orodha ya maswali.

##### C. Ukaguzi na Maswali ya Utafiti

Ukaguzi ulioandikwa na maswali ya utafiti yanaweza kutoa picha yote ya kitu gani watu wanafikiri na hasa ni namna gani wanaamini mambo yalivyo (au wanavyotaka mambo yawe). Kwa mfano, uliza wachungaji kumi ni nini wastani wao wa mahudhurio kila jumapili. Kisha nenda kanisani kwao na hesabu watu. Ni kwa ukubwa gani unafikiri tofauti inaweza kuwa miongoni mwa unaowajua? Wanajaribu kutoa taarifa kamili au pungufu? Mfano wa maswali ya utafiti yapo katika Ziada 4B.

##### D. Takwimu za Idadi ya Watu Kiofisi

Takwimu za kiofisi za idadi ya watu zinategemeana na usahihi wa njia iliyotumika kukusanya habari. Inategemea pia kusudi lilikuwa nini la kukusanya habari na wakala aliyezikusanya. Ni ya thamani sana, kwa jinsi hiyo, na inatoa wazo kwa ujumla la namna ya kulinganisha hali

katika mzunguko wako pamoja na namna ya takwimu zinavyoonyesha ukubwa wa idadi ya wakazi itakavyokuwa.

#### **E. Mtazamo wa Maandishi**

Kama wengine wamefanya utafiti unaofanana, au kutoka katika wakati uliopita na hasa kazi ya sasa, ni msaada wa ajabu. Unapopata mambo muhimu yenye uhakika unaohusu upandaji kanisa, inawezekana kuyaangalia, na kukazia utafiti kuwa wa ufanisi zaidi kwa sababu ya yale ambayo wengine wamegundua. Maktaba inaweza kuwa na vitabu vinavyohusu sehemu hiyo; vitabu vyenye mambo yote, mradi wa utafiti wa chuo kikuu unaweza kutoa kumbukumbu muhimu.

#### **SULUHU**

Utafiti ni sehemu muhimu katika upandaji kanisaji. Inadhihirisha aina tofauti za watu wanaoishi katika eneo linalolengwa, mahitaji yao ni nini, matumaini, hofu, imani zao ni nini. Hii inatoa ufahamu kuwa katika namna ya vitendo na njia ya kushirikisha injili. Utafiti pia utadhihirisha ni watu gani wengine Mungu anaofanya nao kazi katika eneo ulilokusudia, makanisa, makundi ya kimishenari, makundi yanayohudumu na namna gani wanaweza kushiriki katika kuona eneo lililokusudiwa likijaa makanisa. Katika hatua ya baadaye ya mzunguko wa upandaji kanisa, utafiti unaweza kusaidia kuonyesha ufanisi wa huduma ya wakati huo na kutoa ufahamu wa wapi makanisa mapya yanahitaji kupandwa.

#### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Nini unafikiri utafiti wako utagundua juu ya sehemu unayolenga?
- Ni faida gani za kuchukua muda kufanya utafiti katika sehemu yako unayolenga? Namna gani utafiti utafanya juhudi zako za upandaji kanisa kuwa za ufanisi?
- Vipande vipi vitano au sita vya habari unafikiri unahitaji kuvijua kuhusu sehemu yako unayolenga ambavyo vitaongeze ufanisi katika upandaji wako wa kanisa?
- Unafahamu watu ambao watafanya vizuri kutafiti baada ya kuwaelimisha?
- Hao waliopo katika shamba lako la mavuno wako tayari kusikia injili? Ni baadhi ya uchunguzi gani umefanya unaoonyesha kwako kuwa watu wako tayari au wanapinga injili?

#### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Ziada 4A ina agizo la ujuzi wa vitendo kwenye utafiti wa sehemu inayolengwa. Tazama kwa upya kazi katika ziada hii na ikamilishe itakapofika wakati wa kipindi kijacho. Muombe Mungu kutumia kazi hii kukupa ufahamu na huruma kwa watu waliopo kwenye sehemu unayolenga. Muombe kutumia utafiti huo kukupa mawazo mazuri ya wapi na namna ya huduma yako ya upandaji kanisa katika sehemu hiyo iliyolengwa. Unaweza ukapenda kutumia mfano wa maswali ya utafiti yaliyopo katika Ziada 4A kuyatumia kama sehemu yako ya utafiti.

#### **VYANZO**

- Wingerd, Ray A. Jr. DAWN Research Handbook: Principles of Research for a DAWN Project. Pasadena, CA: DAWN Ministries, 1992. A copy may be obtained through DAWN Ministries, 7899 Lexington Dr., Suite 200-B, Colorado Springs, CO 80920 USA. Tel. 1-719-548-7465, Fax. 1-719-548-7475
- Kui Kristlik on Eestimaa? (How Christian is Estonia?). Research project of the status of Christianity in Estonia. For information, contact Merike Uudam, Kungla 16, Tartu, EE2400, Estonia Tel/Fax: +372-7-428898. Email: merike.u@online.ee
- Introductory Research On The Slovak Evangelical Churches And Their Progress Towards Evangelizing Slovakia. Banská Bystrica, Slovakia: New Eastern Europe For Christ, 1997. A copy may be obtained from The Alliance for Saturation Church Planting, Budapest, Hungary. E-mail: [scpalliance@compuserve.com](mailto:scpalliance@compuserve.com).



## Kuelewa Eneo Unalolenga AGIZO LA UTAFITI

*Kusudi la agizo hili ni kukupa uzoefu katika kutafiti kwa vitendo kama zana ya ufanisii kwa upandaji kanisa. Unatakiwa kufanya kila kipengele ulichopangiwa. Unaweza kukuta baadhi ya kazi zikiwa rahisi kuliko zingine. Hata kama ni ngumu au rahisi, Mungu atakuwa na vitu vya kukufundisha kuhusu watu na sehemu unayojaribu kuifikia, kupitia kila aina ya kazi ya agizo hili.*

*Huhitaji kufanya kazi hii uliyogizwa peke yako. Unaweza kuifanya pamoja na wengine. Hata hivyo inashauriwa kuwa ufanye pamoja na wengine iwezekanavyo. Uwe tayari kumshirikisha uliyoyapata kiongozi wako wa utafiti, mshauri na wengineo. Kazi hii inahitajika mara tu unapopata mwongozo wa pili wa mafunzo.*

*Ukumbusho kwa anayetafsiri: Kumbuka kutengeneza Ziada 4A na 4B katika vijitabu tofauti vidogo ili kwamba washiriki waweze kuweka taarifa zao za utafiti katika sehemu moja.*

### HATUA YA 1: TAMBUA ENEO LAKO UNALOLENGA

Pata au tengeneza ramani ya mji wako, eneo, au mkoa. Pata ambayo ina mambo mengi zaidi unapoweza kupata vituo vyote vya wakazi, majina ya mitaa, na njia za usafiri. Chora duara kwenye sehemu unayolenga. Hili ni eneo la huduma yako, mkoa ambao unaamini Mungu anakutaka kulifanya jina lake lilulikane, na anapotaka kupanda makanisa.

### HATUA YA 2: KUSANYA TAARIFA ZA NGUVU YA MAVUNO

Kama ilivyoelezwa katika somo la 4—"Kanuni za Utafiti"—nguvu ya mavuno ni rasilimali zote za Mungu zilizokwisha kuwa kazini katika eneo lako unalolenga. Onyesha ni rasilimali gani zilizopo katika mzunguko wako kwa kujifunza yafuatayo:

#### 1. Makanisa ya Mtaa Yaliyopo

- Weka alama kwenye kila kanisa la mtaa katika ramani yako kwenye mkoa wako. Onyesha ni dhehebu gani kwa kila moja.
- Kama inawezekana, orodhesha watu wao wazima wanaohudhuria.
- Onyesha mwaka ambao kanisa lilipandwa au kutumika.
- Yakinisha ni kundi gani la watu linafikiwa na kila kanisa (M.f. --, vijana, watoto, wasio na makazi maalumu, wazee, wa kutoka mataifa mbalimbali n.k.) Ni namna gani wamefanikiwa katika juhudi zao?
- Ni aina gani ya muhusiano yaliyopo miongoni mwa makanisa yaliyopo katika mzunguko? Wameungana au wamegawanyika?
- Watu wanakutana kuomba kwa ajili ya waliopotea katika jamii yao au kwa ajili ya kutuma wamishenari?

#### 2. Misheni na Makundi ya Makanisa ya Kando Kando

- Orodhesha misheni na makundi ya makanisa ya kando kando katika eneo linalolengwa.
- Kwa kifupi eleza kila huduma ambayo ina (maandishi, wafungwa, huduma ya waislamu, vijana n.k.)
- Wangependa kushirikiana na wewe au wengine katika uinjilisti na juhudi za upandaji kanisa?



### 3. Historia ya Ukristo

- a. Lini ukristo uliletwa kwa mara ya kwanza katika eneo na ni namna gani uliletwa? Watu walilazimishwa au walipenda wenyewe kupokea injili?
- b. Eleza historia ya namna ambayo kila dhehebu liliingizwa katika eneo.
- c. Ni dini zipi zingine kuu zimeweza kuwa na mguso kwa wingi katika eneo lako unalolenga? Ni dini zipi zingine/ibada zilizopo katika sehemu yako sasa na ni kwa namna gani zinafanikiwa kuvuta wafuasi?
- d. Ni namna gani historia hii inaathiri harakati zako za upandaji kanisa?

### HATUA YA 3: KUSANYA TAARIFA JUU YA SHAMBA LA MAVUNO

Shamba la mavuno ni kundi la watu miongoni ambamo utafanya kazi na sehemu ambayo utapanda kanisa. Shughuli zifuatazo zitakusaidia juu ya shamba la mavuno katika eneo unalolenga.

#### 1. Habari za Kitakwimu

- a. Idadi ya wakazi
- b. Namba na asilimia ya wakazi ambao ni wanaume, wanawake, vijana, watoto
- c. Namba ya watu wazima wanaofanya kazi...ikiwa ni pamoja na taarifa za shughuli na kiwango cha mapato.
- d. Namba ya waliostaafu na wazee, na wasiojiweza na vilema
- e. Asilimia na eneo la jamii ya walio wachache. Ni lugha gani wanaongea?

#### 2. Habari za Kijiografia

Alama za kijiografia zinaweza kuwa na mguso makubwa katika harakati za upandaji kanisa. Zinashika nafasi ya jinsi gani na wapi watu wanaishi na kuhusiana na wengine. Kwa mfano, njia ya reli ya magusi inayopita kati kati ya ujirani wa mji. Upande mmoja wa magusi, watu ni matajiri zaidi kuliko upande mwingine. Watu hawako tayari kuvuka njia ya reli ya magusi. Kwa hiyo, magusi ni kizuizi kisichoonekana, na watu wa upande mwingine wa njia ya reli ya magusi wanaonekana kutokuhudhuria kanisa la upande mwingine wa magusi haya. Mfano mwingine unaweza kuwa kwamba kwa sababu mji umezungukwa na milima mizuri, watu mara nyingi wanakwenda nje ya mji siku za jumapili na hivyo kuwa na uwezekano kidogo wa watu kuhudhuria ibada za jumapili.

- Ni vitu gani vinagawanya mkoa (mito, njia ya reli, barabara, n.k.)? Ni jinsi gani vitu hivi vinavyogawanya vinagusa mtindo wa usafiri, utajiri, n.k?
- Mji unazungukwa na milima? Kuna maziwa, kingo, mbuga za wanyama au sehemu zingine ambazo watu watapenda kwenda kufurahia?
- Kama sehemu yako unayolenga ni mkoa au mji, weka alama kwenye ramani yako mahali vilipo viwanda, na mahali wanapoishi watu. Kuna sehemu maalumu za kununulia vitu? Je watu wanaishi karibu na sehemu zao za kazi au kusafiri umbali mrefu?
- Pia nukuu njia kuu za usafirishaji. Je, watu wengi wanasafiri kwa gari, basi, reli?
- Ni wapi watu wanakwenda kwenye faragha, starehe? Wanakaa kwenye mji na kwenda kwenye mbuga za wanyama? Wanatumia muda wao mwingi wa mapumziko kwenye bustani au kwenye nyumba?

#### 3. Taarifa za Kijamii na Kiutamaduni

Kwa kujifunza juu ya mtazamo wa watu wa kidunia na mahitaji yanayowagusa, tunaweza kupata ufahamu katika njia ambazo zinaweza kuwa za maana kuonyesha upendo wa Yesu Kristo. Njia nzuri ya kujifunza kuhusu watu ni kuwauliza maswali na kuchunguza tabia zao. Nenda katika sehemu yako unayolenga na ongea na watu kama 15-20. Jaribu na jifunze yafuatayo:

- Mtazamo kuhusu Mungu

- Watu wanamwamini Mungu? Wanaamini nini juu ya Mungu? Wamewahi kusikia juu ya Yesu? Wanajua nini juu ya Yesu? Wanaamini kama kuna mbingu na jehanamu? Wanaamini juu ya malaika, mapepo, au Shetani? Wanapokuwa wanaumwa wanakwenda wapi kupata msaada? Wanaamini katika bahati? Wanaamini kama wanaweza kumudu maisha yao ya mbeleni au kufanya maisha yao kuwa mazuri kwa ajili ya watoto wao? Wanaamini kuwa dhambi ni nini? Wanahudhuria kanisa mara kwa mara? Kama ndiyo ni mara ngapi? Kama siyo ni kwa nini hawahudhurii kanisa?
- Zipi ni sikukuu muhimu au siku za mapumuziko katika eneo hilo? Watu wanazisherehekeaje?
- Ni nini wanapenda zaidi juu ya maisha yao? Ni kitu gani kimoja wangebadilisha?
- Ni kitu gani wanaona kimoja au viwili katika jamii yao kuwa matatizo ya kijamii? (ulevi, mayatima, ukosefu wa huduma za hospitali, wazee wasio na uangalizi, n.k.)
- Ni viongozi gani wanakubalika katika jamii? Kwa nini wanaonekana kama viongozi?
- Nani wanadhaniwa kuwa mashujaa?
- Orodhesha vitu sita ambavyo watu wanathamini kwa wengine? (uaminifu, uhodari, ukarimu, n.k?)

#### HATUA YA 4: MCHANGANUO WA HABARI ZA SHAMBA LA MAVUNO NA NGUVU YA MAVUNO

Mara unapokuwa umekusanya taarifa zako zote, umeandika ufupisho wake, na kutia maelezo kwenye ramani yako, chukua mda kurudia na kutafakari juu ya habari hizi. Muulize Mungu kukupa huruma juu ya watu walio kwenye eneo lako lengwa. Muombe Mungu kukupa ubunifu wa mawazo juu ya namna ya kushirikisha watu upendo wake. Kama sehemu ya utaratibu huu, changanua habari zako kwa kujibu maswali haya:

Ni makanisa mangapi yanahitajika ili kwamba kila mwanaume, mwanamke, mtoto katika eneo lengwa ataweza kuona, kusikia, na kuelewa habari ya injili kwa njia inayofanana na utamaduni wao?

- Ni makanisa mangapi yanahitajika kukumilisha Utume Mkuu katika eneo unalolenga? Ni makanisa mangapi yanahitajika ili kwamba kila mwanaume, mwanamke, mtoto katika eneo lengwa ataweza kuona, kusikia, na kuelewa habari ya injili kwa njia inayofanana na utamaduni wao? Anza kuomba na kumuuliza Mungu kukuongoza kufanya kile anachotaka ufanye.
- Onyesha mugao wako: Ni makanisa mangapi Mungu anataka umwamini kwa ajili ya huduma yako.
- Chagua mahali unapoanzia: Ni wapi utanzia? Ni wapi zaidi watu wanaitikia? Paulo mara nyingi alipata kwanza waliokubali kutoka kwenye sinagogi. Kisha alifanya kazi kuanzia pale kwa mtandao wa mahusiano.
- Chagua njia zako: Ni nini ilikuwa moja au mbili ya mahitaji makuu ya watu katika jamii? Ni njia zipi utatumia kukidhi mahitaji ya watu? Ni njia ipi inatumika na kuleta matokeo mazuri zaidi katika makanisa mengine katika sehemu hiyo? Ni rasilimali gani zilizopo kwako kwa njia hizi? Nini kipawa chako na unayoweza kufanya?
- Onyesha rasilimali zako: Ni rasilimali zipi zilizopo na shirikisha maono hayo hayo? Kuna wengine ambao unaweza kushirikisha maono haya na kushirikiana katika lengo lililofikiwa? Nani vibarua, fedha, na watu binafsi walio na vipawa wanaopatikana kwa ajili yako? Makanisa katika eneo yana shauku kwa ajili ya uinjilisti na upandaji kanisa? Wako tayari kufanya kazi pamoja au pamoja na wewe katika juhudi zako? Wako tayari kuomba kwa ajili ya uinjilisti na juhudi za upandaji kanisa na kwa Mungu kujidhihirisha katika maisha ya watu katika jamii zao?
- Watu wana ueleo au kuamini katika Mungu au Yesu Kristo? Ni katika hatua gani utianza kushirikisha habari ya injili? (Mf. unaweza kuanza na Yesu Kristo au kuanza na kuwepo kwa nguvu ya juu, Mungu muumbaji?)

## **HATUA YA 5: MASOMO YALIYOJIFUNZWA KUTOKA KWENYE UTARATIBU WA UTAFITI**

Tathimini uzoefu wako katika kufanya utafiti uliopangiwa. Ni nini Mungu amekufundisha wewe mwenyewe kutokana na utafiti uliopangiwa, haja yako ya kushiriki katika upandaji kanisa? Ni mahangaiko gani umepata wakati unafanya utafiti? Ni kwa namna gani umeyashinda? Ni nini kilikuwa rahisi kuhusu utafiti? Kama ingekuwa kwamba urudie utafiti huu, ni nini ungefanya tofauti?

## **HATUA YA 6: KUSHIRIKISHA MATOKEO YA UTAFITI**

Katika kipindi kingine cha mafunzo, jiandae kutoa matokeo ya utafiti wako. Taarifa yako inatakiwa kuwa ya wastani wa dakika 10-15 na iwe na mambo yafuatayo:

### **1. Sehemu ya Kwanza—Taarifa za Msingi Zilizokusanywa (dakika 5-7)**

- Elezea eneo lako unalolenga.
- Namna gani umekusanya habari zako (kukagua, kuhoji mtu, uchunguzi/kuweka ramani, utafiti kwenye maktaba, n.k.).
- Jadili matatizo au ugumu uliokuta na namna gani umeweza kuushinda. Nini utahitaji kufanya tofauti wakati mwingine?

### **2. Sehemu ya Pili—Uchanganuzi wa Habari za utafiti (dakika 5-8)**

Ukumbusho wa utoaji unatakiwa kukazia juu ya matokeo ya utafiti wako. Utoaji unatakiwa kujibu maswali yafuatayo ya ufunguo:

- Ni taarifa ipi uliyojifunza iliyokuvutia juu ya eneo lako unalolenga na watu wanaoishi mahali pale?
- Kulikuwa na taarifa yoyote iliyokushangaza?
- Ni kitu gani maalumu ulichojifunza ambacho kitakusaidia kuonyesha mkakati wako wa upandaji kanisa katika eneo unalolenga?
- Ni nini kimoja cha kweli muhimu kwenye upandaji kanisa ulichodhihirisha kwamba umeshakifahamu juu ya shamba la mavuno?
- Ni ugunduzi gani mpya ambao ni muhimu kwa upandaji kanisa uliofanya juu ya shamba la mavuno ambao hukuujua mwanzoni?
- Ni nafasi zipi ulizopata kama mlango wazi kwa ajili ya injili?
- Ni vipingamizi gani ulivyopata na namna gani vinaweza kudhibitiwa?
- Ni utafiti gani ufuatao unaohitaji kufanya ili kuendeleza uinjilisti na mikakati ya upandaji kanisa katika eneo unalolenga?



# Mfano wa Karatasi ya Mazoezi

*Katika Ziada hii kuna maswali mawili ya mfano wa maswali ya utafiti: ukaguzi wa kanisa la mtaa, na maswali ya utafiti kwa ajili ya kutafiti eneo linalolengwa. Hii ni mifano tu na inaweza kuundwa upya kukidhi malengo yako.*

*Ukumbusho kwa anayetafasiri: Maswali haya ya utafiti yanaweza zaidi kwa uhakika kuchapishwa katika wingi (hasa katika vijitabu vodogo) ili kutengeneza kopi nyingi zaidi zitakazokuwepo kwa ajili ya wapanda kanisa AU kwa viongozi wengine wa kanisa kwa wote wanaotumia lugha hiyo.*

## UKAGUZI WA KANISA LA MTAA

### A. SURA

1. Jina la kanisa \_\_\_\_\_
2. Dhehebu (Wanachoamini) \_\_\_\_\_
3. Anwani ya kanisa /mahali lilipo \_\_\_\_\_
4. Mahali kanisa linapokutana: Panamilikiwa na kanisa \_\_\_\_\_ Ni mahali pa kupanga \_\_\_\_\_
5. Tarehe lilipoanzishwa \_\_\_\_\_ Tarehe lilipoandikishwa \_\_\_\_\_
6. Jina la mchungaji/kiongozi \_\_\_\_\_ umri \_\_\_\_\_
7. Mchungaji/kiongozi anafanya kazi katika nafasi nyingine? Ndiyo \_\_\_\_\_ Hapana \_\_\_\_\_
8. Lugha kuu inayozungumzwa kanisani \_\_\_\_\_ Nyinginezo \_\_\_\_\_
9. Idadi ya waumini kwa wakati huo \_\_\_\_\_
10. Wastani wa wanaohudhuria \_\_\_\_\_

### B. WATU

*Jaribu kujaza idadi ya watu kulingana na makundi haya:*

	Wanaohudhuria		Wanaoamini		Wajumbe	
	Mm	Mk	Mm	Mk	Mm	Mk
Umri 0-10						
11-17						
18-24						
25-30						
31-55						
55+						

*Dhana:*

- Waliohudhuria siyo waumini na /au wajumbe.
- Idadi ya wanaohudhuria inatakiwa kuwa kubwa kuliko ya waumini na wajumbe.
- Mtu anaweza kuhudhuria na kuwa muumini, na si lazima awe mjumbe.

- Mjumbe lazima awe muumini.
- Idadi ya wanaoamini lazima iwe ndogo kuliko idadi ya wanaohudhuria na kubwa kuliko idadi ya wajumbe.
- Idadi ya ubatizo: 92—93—94—95—96—97—98—99—2000
- Idadi ya familia (mme/mke wanaohudhuria:\_\_\_\_\_)

**C. VIPINDI**

*Angalia kila shughuli iliyotolewa na kanisa na tambua kushiriki katika shughuli hizo*

Shughuli	Kanisa kutoa	Idadi ya walioshiriki
Shule ya jumapili ya watoto (kwa umri )		
Kuabudu		
Vikundi vya vijana		
Vikundi vya watoto		
Kikundi cha wanawake		
Kikundi cha wanaume		
Umishenari		
Uinjilisti		
Mafunzo ya kufuasa		
Kikundi cha kujifunza Biblia nyumbani		
Mafundisho kwa waumini wapya		
Mafundisho ya uongozi		
Mafundisho ya ualimu		
Mkutano wa maombi		
Kwaya		
Huduma ya jeshi		
Huduma ya kanisa jipya		
Huduma ya maandishi		
Huduma kwa njia ya Redio/TV		
Huduma ya wafungwa		
Huduma ya walevi/wavuta madawa ya kulevya		
Huduma ya hospitalini		
Huduma ya watoto yatima		
Huduma ya kutunza wazee		
Huduma ya maombi		

**D. MPANGO**

1. Kuna mpango wowote maalumu wa huduma kwa mwaka huu?  
Ndiyo\_\_\_\_\_Hapana\_\_\_\_\_

2. Ni mipango ipi hiyo?

---

---

---

3. Mipango ya mwaka ujao imeanza? Ndiyo\_\_\_\_\_Hapana\_\_\_\_\_

4. Ni nini mipango hii?

---

---

---

5. Kuna uongozi unaopanga kwa ajili ya kanisa? Ndiyo\_\_\_\_\_Hapana\_\_\_\_\_

6. Kanisa lina hati ya dhumuni? Ndiyo\_\_\_\_\_Hapa\_\_\_\_\_

7. Kanisa lina mipango ya kifedha? Ndiyo\_\_\_\_\_Hapana\_\_\_\_\_

8. Kanisa lina mpango wa kukua kiroho kwa waumini? Ndiyo\_\_\_\_\_Hapana\_\_\_\_\_

9. Kanisa linashirikiana na makanisa mengine? Ndiyo\_\_\_\_\_Hapana\_\_\_\_\_

10. Kanisa linashirikiana na madhehebu mengine? Ndiyo\_\_\_\_\_Hapana\_\_\_\_\_

## ENEO LINALOLENGWA AU UKAGUZI WA “MUZUNGUKO”

### A. NANI

1. Kuna kundi lolote maalumu la watu katika kanisa wanaoshawishi mzunguko?

---

---

---

2. Kuna daraja moja la jamii linalotawala zaidi katika mzunguko? Ndiyo\_\_\_ Hapana
3. Kama ni “ndiyo” ni lipi

---

---

---

### B. NINI?

- Ni tabia zipi dhahiri za “mzunguko” wa kanisa?

---

---

- Ni hitaji lipi la watu linalohitaji ufumbuzi wa haraka katika “mzunguko”?

Kiuchumi\_\_\_ Kiroho\_\_\_ maadili\_\_\_ kijamii\_\_\_ kielimu\_\_\_ kiutamadini\_\_\_ kifamilia\_\_\_  
kidini\_\_\_

- Ni kundi gani la kidini lililopo katika “mzunguko” wa kanisa?

Othodox\_\_\_ #\_\_\_ Babtisti\_\_\_ #\_\_\_ Pentekosti\_\_\_ #\_\_\_ Romani Katoliki\_\_\_ #\_\_\_  
Lutherani\_\_\_ #\_\_\_ Wapinzani\_\_\_ #\_\_\_ Wasio wa dhehebu\_\_\_ #\_\_\_  
Waislamu\_\_\_ #\_\_\_ makundi ya kimishenari ya nje\_\_\_ (tafadhali nukuru makundi haya  
yanaweza kuwa yapi:\_\_\_\_\_)

- Kanisa linajaribu kugusia mahitaji ya watu? Ndiyo\_\_\_ Hapana\_\_\_

Kama ndiyo, ni nini hasa kanisa linafanya kuhudumia mahitaji yaliyopo katika “mzunguko”  
wao?

---

---

---

- Maelezo ya kusudi la kanisa yanaonyesha haja ya kugusia mahitaji ya “mzunguko” wao?  
Ndiyo\_\_\_ Hapana\_\_\_

- Mpango wa huduma ya kanisa unaonyesha kujali kuhudumu kihistoria kwenye mzunguko  
wao? Ndiyo\_\_\_ Hapana\_\_\_

**C. JINSI GANI?**

1. Kanisa linajifananisha na mzunguko wake? Ndiyo\_\_\_\_Hapana\_\_\_\_
2. Kama ni “ndiyo” Jinsi gani?

---

---

---

3. Kama ni “hapana” ni nini kanisa lifanye kuanza kujifananisha na “mzunguko” wao?
4. Shughuli za kanisa zimepangwa katika namna ambayo zinaufikia “mzunguko” wake?  
Ndiyo\_\_\_\_Hapana\_\_\_\_
5. Ni jinsi gani kanisa linalingana na makanisa mengine ya kiinjili ya kiprotestanti katika “mzunguko” wake?

Linaendana vizuri na yote\_\_\_\_

Linaendana vizuri na baadhi, lakini si vizuri sana na mengine\_\_\_\_

Haliendani vizuri na lolote\_\_\_\_

**D. RASILIMALI**

- Ni aina gani ya rasilimali zilizopo kwenye kanisa kwa ajili ya “mzunguko” wake?
- TV/Radio\_\_\_\_ Maandishi\_\_\_\_ Nyumba ya uchapaji\_\_\_\_ Kibali cha kiofisi cha “kusaidia” huduma\_\_\_\_ Kushirikiana na makundi mengine ya wakristo wa makanisa ya kiinjili ya kiprotestanti (makanisa mengine ya mtaa\_\_\_\_mawakala/mashirika ya kigeni ya kimishenari\_\_\_\_ Vyama\_\_\_\_ palipo katikati\_\_\_\_ miungano\_\_\_\_ mashirika ya kielimu-\_\_\_\_)
- Ni makundi gani ambayo kanisa linashirikiana nayo kwa sasa katika mradi maalumu wa huduma?

---

---

---

- Juhudi zimefanywa na kanisa kuzungumza na makanisa mengine yaliyo kwenye“mzunguko” juu ya kufikia wasiookoka kwenye “mzunguko” kwa ajili ya Kristo? Ndiyo\_\_\_\_ Hapana\_\_\_\_
- Uongozi wa kanisa utakuwa tayari kufanya kazi na makanisa mengine na mashirika kumfikia kila mmoja katika “mzunguko” kwa ajili ya Kristo?
- Kama “ndiyo” ni lini watajaribu kukusanya “mzunguko wa rasilimali” kuzungumzia juu ya kutimiza Utume Mkuu katika mzunguko wao?

---

---

---

- “kama hapana,” Ni kwa nin Siyo?

---

---



---

# **KANISA**

---



# Misingi ya Kibiblia Kwa Kanisa

## KANISA KATIKA MPANGO WA MUNGU KWA VIZAZI

### **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuonyesha jinsi misingi ya kibiblia kwa kanisa inavyofanana na ufalme wa Mungu na makusudi ya ukombozi.

### **Wazo Kuu**

- Kanisa ilikuwa ni mpango wa Mungu kutoka milele iliyopita.
- Siyo kama Israeli, Kazi ya kanisa ni KWENDA na kuwa chunvi na nuru kati ya mataifa.
- Kanisa ni chombo cha Mungu cha kueneza injili kwa kila mmoja.

### **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kufahamu nafasi ya kanisa katika mwanga wa ufalme wa Mungu na mpango wa ukombozi, na kutafakari wazo la msingi kuhusu kanisa.
- Uwe na shukurani kwa Mungu kwa ajili ya mpango wake wa milele kwa ajili ya vizazi, na katika kushiriki kwake yeye mwenyewe katika mpango huu.
- Fikiria jukumu lililopo kwenye kazi ya upandaji kanisa kwenye picha kubwa ya kusudi la Mungu

## I. MPANGO WA MUNGU KWA VIZAZI

### A. Ufalme wa Mungu wa Milele (Zab 10:16; 103:19)

Biblia inamweleza Mungu kama Mfalme wa milele, Mkuu kuliko uumbaji wote. Ufalme wa Mungu unaweza kuelezewa kama upeo ambao Anatawala, Anakoendeshea madaraka yake ya ukuu na ufalme. Mwonekano wa utukufu wake katika utawala wake ulikuwa ni ukuu mzuri—(Zab 29:10; Dan 2:21; 3:34-35; 5:21)

### B. Kuasi Kwa Ulimwengu

Kila alichokiumba Mungu kilikuwa kizuri, lakini katika hatua fulani, dhambi ikaingia katikati ya uumbaji. Lini na namna gani hii ilitokea hajielezwa sawasawa katika Biblia, lakini baadhi ya vifungu vinataja juu juu tu juu ya ukweli huu) Isa 14:3-21, Eze 28:11-17).

Nabii isaya, akimwelezea mfalme wa Babeli, anajaribu kulinganisha kati ya kiburi cha mfalme wa Babeli na kuanguka kwa nyota ya alfajiri (Isa 14:3-21). Nyota hii ya asubuhi ilijaribu kujilinganisha na Mungu aliye juu. Wataalamu wengi wa Biblia wanauona huu kama mfano wa anguko la Shetani, malaika aliyeumbwa na aliyetaka kuwa kama Mungu.

Kifungu kinachofanana na hiki kipo kwenye Ezekieli 28:11-17 wakati mfalme wa Tiro akiambiwa. Maelezo yanaonekana kumwelezea kama kerubi mwenye kutiwa mafuta ambaye aliwekwa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu na alikuwa mkamilifu katika njia zake zote. Kwa sababu ya kiburi chake alitupwa chini.

### C. Kuasi Kidunia

Mungu alipoumba dunia, Mamlaka ya kuitawala yalikabidhiwa kwa mwanadamu (mwanaume na mwanamke) (Mwa 1:26). Mtu, aliyumbwa kwa mfano wa Mungu ili kuwa na ushirika naye, na uhuru wa uchaguzi (Mwa 1:28; 2:7). Kwa sababu ushirika wa kweli ni pamoja na uchaguzi

kimaadili, mwanaume na mwanamke walijaribiwa kwa kukataliwa kula baadhi ya matunda katika bustani. Walijaribiwa na shetani juu ya kuwa kama Mungu, walichagua kukubaliana kutokutii juu ya makubaliano. Kwa tendo la uchaguzi huu, mwanadamu alitangaziwa kuwa peke yake na mpinzani kwa mapenzi ya Mungu. Matokeo ya dhambi za mwanadamu ilikuwa:

- Uhusiano wao na Mungu ulivunjika.
- Mfano wa Mungu kwa mwanaume na mwanamke ukatiwa giza
- Mwanadamu akaanza kupatwa na kifo cha mwili na kiroho.
- Mwanamke atapata uchungu wakati wa kuzaa.
- Mwanaume atapata mazao kwa jasho lake.
- Ardhi (asili) ililaaniwa (Rum 8:21-22).
- Mahusiano kati ya mwanaume na mwanamke yalivunjika.
- Utawala wa dunia ulitwaliwa na Shetani aliyekuwa “dhahabu ya dunia hii.”

#### D. Mpango wa Mungu wa Ukombozi

Tangu anguko la mwanadamu, Mungu amekuwa akifanya kazi katika historia nzima ya kurudisha uhusiano wake na mwanadamu. Alimchagua mwanadamu, (Ibrahimu), Aliyezaa taifa (Israeli) miongoni ambamo alizaliwa masihi (Yesu) kudhibiti kazi ya shetani na kurudisha uhusiano wa kweli wa mwanadamu na Mungu. Hatima ya mpango wa Mungu wa ukombozi ni pamoja na:

- Kukombolewa kwa mwanadamu, kumrudisha katika sura ya Yesu (2Kor 3:18).
- Kurudishwa kwa ushirika kati ya Mungu na mwanadamu na kati ya mtu na mtu (1Yoh 1:3-7).
- Kurudishwa kwa ufalme wa Mungu duniani (Ufu 11:15) na wanadamu kutawala na Mungu.
- Kuumbwa kwa mbingu mpya (Ufu 21:1).

## II. KUENZISHWA KWA KANISA

### A. Chimbuko Kwa Kanisa: Israeli

Kanisa halikutajwa katika Agano la Kale. Paulo analieleza kuwa ‘maajabu’ (kitu ambacho hakikudhihirishwa mwanzoni—angalia Efe 3:9-10; Rum 16:-26; Kol 1:25-26). Maelezo mengi yameelekezwa juu ya uhusiano wa kanisa na Israeli. Baadhi wanasisitiza juu ya kufanana kwake, kwa kuvitazama kama watu wamoja katika nyakati tofauti. Katika hisia hizi, Israeli ni ‘watu wa kiroho’, na kanisa ni Israeli mpya. Na wengine wanatazama Israeli na kanisa kama hatua tofauti katika ufalme wa Mungu na mpango wa ukombozi, wote pamoja wakiwa watu wa Mungu. Bila kujali, ni muhimu kuelewa tofauti kati ya Israeli na kanisa, linapohusiana kwenye upandaji kanisa na harakati za uinjilisti.

#### 1. Taifa La Israeli

Mwanzo 12:1-3 Mungu alimwahidi Ibrahimu kwamba kwa kupitia yeye Angejenga taifa kubwa na kwamba kwa kupitia yeye mataifa yote ya dunia yangebarikiwa. Taifa aliloahidi lilikuwa ni Israeli. Mmoja wa wafalme wa Israeli, Daudi, alikuwa ameahidiwa kuwa ufalme wake ungekuwa wa milele (2Sam 7:8-16). Agano Jipya lilitangaza kuwa Yesu alikuwa ‘mwana wa Daudi’ ambaye kwa kupitia kwake ahadi hizi zingetimizwa.

Moja ya kusudi la Israeli ilikuwa kumzaa masihi (mfalme). Paulo anafupisha kama hivi: “...watu wa Israeli. Wenye kule kufanywa wana, na ule utukufu, na maagano, na kupewa torati, na ibada ya Mungu, na ahadi zake. Ambao mababu ni wao, na katika hao alitoka Kristo kwa jinsi ya mwili. Ndiye aliye juu ya mambo yote, Mungu mwenye kuhimidiwa milele Amina” (Rum 9:4-5).



2. *Kanisa*

Kipindi cha muda kati ya kipindi cha kwanza na cha pili cha kuja kwa Kristo kimeitwa 'Umri wa kanisa' au muda ambao Mungu anafanya kazi kukamilisha ufalme wake na kusudi la ukombozi kupitia kanisa lake. Kanisa siyo mpango 'B' baada ya Israeli kishindwa kukamilisha mpango 'A,' au mpango wa baadaye katika akili ya Mungu. *Alilipangia* katika milele, na kulitolea kwa kifo na ufufuko wa mwanae, Yesu (Efe 1:19-23). Yesu *aliandaa* kutokea kwake na kuendelea kwa kuwaelekeza wanafunzi wake kama misheni yao (Yoh 16:5-15; Mt 28:18-20). *Aliliunda* siku ya pentekosti (Mdo 2:1-13) na *kulitia nguvu* (Mdo 1:8) kwa Roho wake Mtakatifu atakayekaa milele.

Kanisa ni chombo cha Mungu alichokichagua kuchukua habari njema ya injili mpaka miisho ya dunia. *'Ili sasa kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho; kwa kadri ya kusudi la milele alilokusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu'* (Efe 3:10-11). Ni mpango wa Mungu kwa kanisa kuufikia ulimwengu sasa, kudhihirisha ushindi wake unaoendelea dhidi ya shetani, na kuwaweka huru wale ambao wangukuwa sehemu ya watu wa Mungu.

3. *Ulinganifu Kati ya taifa la Israeli na Kanisa (kielelezo 1.1)*

**Kielelezo 1.1 Israeli na Kanisa**

Taifa la Israeli	Kanisa
<p>Mstari au mwelekezo wa 'taifa' ulikuwa wa <i>kuelekea kati</i>. Mpango wa Mungu uliweka Israeli kama mwanga kwa mataifa, ambao kwao mataifa <b>yangukuja</b> kuona na kusikia utukufu wake. Kushiriki katika utukufu wake kulimaanisha kuja kwenye taifa</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kukua kwa kuongeza (kuzaliana, kuchukua kwa nguvu, wanaomwogopa Mungu)</li> <li>• Kuweka chini ya mpango mmoja 'wanapokuja katika nyumba hii'</li> <li>• Utukufu wa Mungu kukaa kwa muda katika Yerusalemu (1Kor 28:; 2Kor 6-7)</li> </ul>	<p>Mstari aumwelekezo wa kanisa ni <i>kutokea kati</i>. Mpango wa Mungu unaliweka kanisa kama mwanga wa mataifa. Watu wa kanisa wanatakiwa kwenda na kuwa chumvi na mwanga miongoni mwa mataifa (Mt 5:13-14; 28:18-20).</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kukua kwa kuzidisha (kukata shauri, kupanda kanisa)</li> <li>• Kuweka chini ya mipango mingi '...katika ulimwengu wote'</li> <li>• Kutolewa na kuimarishwa kwa kukaa milele kwa Roho Mtakatifu (Mdo 1-2); Utukufu wa Mungu unakaa katika mioyo ya watu (2Kor 3)</li> </ul>
 <p><i>Kukua kupitia mvuto (Kuelekea Kati)</i></p>	 <p><i>Kukua kupitia kupanuka (Kutokea Kati)</i></p>

**B. Kutabiriwa Kwa Kanisa: Mathayo 16:18-19**

Yesu anatabiri kuanzishwa kwa kanisa katika Mathayo 16:18-19. Yafuatayo ni marudio ya Mathayo 16:18-19 kwa matumizi ya upandaji kanisa.

1. *Kanisa Limejengwa kwenye Mwamba: "Na Juu ya Mwamba Huu"*

Maana ya "mwamba" katika Mathayo 16:18-19 inasisimua majadiliano zaidi. Mabishano yanasisimua katika tafasiri ya petra2, Neno la kiyunani la 'mwamba' ambalo jina la Petro linatokana.

Petra= 'mwamba mkubwa, mwamba mgumu ulio chini ya ardhi' (Mt 7:2444-25; 27:60; Mk 15:46).

Petros3 (Petro)= 'jiwe lililoungwa' ambalo linaweka kuwa rahisi kuhamishwa

*Tafsiri kuu za 'mwamba'*

- Yesu Masihi: Petra ilitumika kama Yesu
- Kukiri kwa imani kwa Petro juu ya Yesu
- Petro mwenyewe

Wanathiolojia wengi wa kiinjili kihistoria wametafsiri mwamba kuwa kukiri imani kwa Petro juu ya Yesu. Katika namna yoyote, methali ya mwamba inajulisha umuhimu wa msingi mgumu, somo muhimu sana kwa wapanda makanisa.

2. *Kanisa ni Mali ya Yesu: "Nitalijenga Kanisa Langu"*

Yesu anamiliki kanisa. Alilianzisha na ni mali yake. Alijitoa mwenyewe kwa ajili ya kifo msalabani, ili kanisa liweze kuzaliwa (Efe 5:25; Yoh 12:24). Alilinunua kanisa kwa damu yake mwenyewe (Mdo 20:28). Analiita kanisa lake nje ya ulimwengu, anawaweka wajumbe wake wote pamoja, na kulitakasa kwa ajili ya maandalizi ya mwisho ya kulikabidhi na kusudi lake (Efe 5:26-27). Mbeleni, Yesu atalitukuza kanisa lake mbele ya Mungu na malaika watakatifu (1The 4:13-18; Uf 4-6).

Paulo anasema kuwa alipewa mamlaka na Yesu ya Kujenga kanisa lake, na siyo kulivunja (2Kor 10:8). Ingawa viongozi wa kanisa wanapaswa kujisikia hisia ya ndani kabisa ya wajibu na kushiriki katika huduma, hakuna mchungaji wala mpanda kanisa ambaye amewahi kumiliki kanisa lake. Yesu, siyo mpanda kanisa au mchungaji, ni kichwa cha kanisa.

3. *Yesu Analijenga Kanisa Kupitia sisi: "Nitalijenga Kanisa langu"*

Kujenga kanisa ni misheni kubwa ya Yesu hata leo duniani. Yesu anatumia watu waliozaliwa upya kama vifaa vyake vya kujengea (1Pet 2:5). Yesu atafaa na kujenga mawe hayo yaliyo hai kama jengo la Mungu (1Kor 3:9). Makao ya Mungu kiroho (Efe 2:21-22). Yesu anatumia viongozi wenye vipawa kuwaandaa watu kujenga kanisa lake (Efe 4:11-12; 1Kor 3:12).

4. *Kanisa litakuwa mshindi: "Milango ya Kuzimu haitainuka juu yake"*

Kipengele hiki muhimu kilichosemwa na Yesu kimejaa maana na msingi wa imani inayoshinda na matumaini ambayo wafanya kazi wa kanisa wanahitaji kuwa nayo. Inatuambia kuwa Kristo analijenga kanisa lake kama nguvu ya jeshi kuungurumisha milango ya kuzimu na kuwa mshindi juu ya nguvu ya uovu. Hata kama tunasumbuka kwa sasa, kuna siku kanisa litakuwa mshindi kikamilifu (Rum 16:20). Mpaka sasa, tunatakiwa kuzivaa silaha alizotupa Kristo na kutegemea nguvu zake kuongoza na kushinda (Efe 6:10-18; 2Kor 2:14). Mfano wa kazi ya mwanajeshi unafaa hasa kwa mpanda kanisa (2Tim 2:3-4, Flp 2:25). Paulo alisema kuwa amevipiga vita vizuri (2Tim 4:7) Nasi tunapaswa kufanya hivyo.

**C. Kuzaliwa kwa Kanisa: Matendo 2**

Kutabiriwa kwa Yesu kulitimia katika Matendo 2 wakati mwezeshaji Roho Mtakatifu aliposhushwa juu ya watu kutoka mataifa mbalimbali ikapelekea kuzaliwa kwa kanisa. Muujiza wa kunena kwa lugha siku ya Pentekosti ilionyesha alama kwamba tukio hili jipya katika mpango wa ukombozi wa Mungu ingeweza kuufikia ulimwengu wote, kwa kuunganisha wanaume na wanawake wa kila lugha katika kanisa. Kwa hiyo Kanisa ni la kimataifa kutokana na lilivyojaliwa.

### III. NAFASI NA ASILI YA KANISA LEO

#### A. Kanisa—Watu Walioitwa Nje kwa Yote Kujidhihirisha Kimtaa na Mahali Pote

Tangu anguko la mtu, hatima ya kusudi la Mungu imekuwa ni kuwaita watu kuja kwake ambalo kwa sasa tunaita kanisa (Efe 1:10). Neno la kiyunani 'ekklesia' mara nyingi linatumika kueleza kanisa katika Agano Jipya. 'Ekklesia' maana yake ni jamii au mkusanyiko wa wakazi walio huru walioitwa nje ya nyumba zao au shughuli zao kujikusanya pamoja na kutoa shauri lililopo kwa ajili ya manufaa ya jamii (Mdo 19:39). Wazo la 'watu walioitwa nje' lina mzizi wake katika Agano la Kale (Rum 4:11; Yer 33:7), pamoja na w


Waisraeli kama watu wa Mungu walioitwa. Katika Agano Jipya *ekklesia* haikuwahi kutumika kutaja jengo au dhehebu (kati ya njia kuu mbili tunatumia neno "kanisa" la sasa) lakini mara nyingi ikimaanisha kundi la watu.

Kati ya mara 109 inamaanisha kanisa katika Agano Jipya, Mara nyingi linataja kundi la watu wanaoamini katika sehemu maalumu au 'katika kanisa la mtaa' (angalau mara 63). Waumini wanawajibika kukusanyika kwa ajili ya ushirika (Ebr 10:25). Kwa hakika, ilikuwa ni sehemu ya mitume kuwaleta watu kwa Yesu na kuwakusanya katika makanisa mapya.

Tambua kwamba kanisa la mtaa linaweza kuelezewa katika namna tofauti:

- Nyumba ya kanisa: 1Wakorintho 16:19 (kanisa linalokutana katika nyumba ya Akila na Priska) Wakolosai 4:15 (kanisa linalokutana katika nyumba ya Nimfa)
- Kanisa la mji: 1Wathethalonike1:1 (kanisa la wathethalonike) 1wakorintho1:2 (kanisa la mungu lililoko Korintho) Matendo 13:1 Kanisa lililoko Antiokia)
- Kanisa la Eneo: Wagalatia 1:2 (kanisa lililoko Galatia) Matendo 9:31 (kanisa katika Uyahudi yote na Galilaya na Samaria) !Wakorintho 16:19 (makanisa yote ya Asia)

#### Kielelezo 1.2 Kanisa Moja na Makanisa Mengi



Hatimaye, kunaweza kuwa na *ekklesia* moja tu (1Kor 12:13; Efe 4:4-5). Hivyo, (angalau mara 27) tunaona *ekklesia* likiashiria kanisa la wengi ambalo ni huo mwili wa waumini katika Yesu Kristo, wanoishi na kufa kutoka kila kabila, kila lugha, watu na taifa. Wakiwa sehemu ya kanisa ya wengi na wasihusike katika kanisa la mtaa ni namna ambayo haipatikani katika agano Jipya. Kinyume chake, kanisa la wengi linaonekana kupitia makanisa ya mtaa yaliyoko kila mahali.

Kama 'watu walioitwa nje' kanisa siyo tu kundi la watu walioungana kwa imani ya kidini. Ni Kazi ya Mungu kupitia Roho Mtakatifu

## B. Kanisa ni Mwili wa Kristo

Kanisa limeelezewa mara nyingi katika maandiko kama mwili wake (Rum 12:12-31; Efe 1:22-23; 4:4-16). Yesu Kristo anapofanya kazi duniani leo, anafanya hivyo kwa kutumia mwili wake, kanisa, sisi!) Efe 1:22-23; 3:10-11). Kumbuka maana halisi ya methali zifuatazo:

### 1. Mwili Unategemeana

Kama mwili wa kristo, kanisa lina viungo mbalimbali vinazofanya kazi pamoja katika namna ya ajabu na namna ya kutegemeana. Viungo vinafanya mambo tofauti lakini vina dhumuni moja, sawa na viungo mbalimbali vya mwili (Rum 12:3-8; 1kor 12:12-31). Kanisa linahitaji viungo vyote kufanya kila kimoja kwa namna yake ili kufanya kwa ukamilifu kile Mungu anachohitaji.

### 2. Mwili Una Kichwa Kimoja

Kristo ni kichwa cha kanisa (1Kor 1:18). Kama mwili, kanisa haliwezi kuwa na vichwa zaidi ya kimoja. Hakuna mchungaji wala mpanda kanisa ambaye kihakika ni kichwa cha kanisa analohudumia. Kila kiungo cha mwili, ikiwemo viongozi, wanawajibika kwenye ukuu wa Kristo. Vinginevyo mwili hauwezi kufanya kazi.

## C. Kanisa ni Chombo cha Kwanza cha Mungu cha Kuenezea Injili

Kanisa ni chombo cha Mungu alichochagua kubeba habari njema ya injili mpaka miisho ya dunia. Kabla ya msalaba *mataifa* yalikuwa yametengwa kutoka kwenye tumaini la wokovu (Efe 2:11-13). Lakini baada ya kifo na ufufuo wa Kristo, kanisa lina wajibu wa kuipeleka injili kwa *mataifa* (Mt 28:19-20). Iko wazi katika agano Jipya kwamba kanisa la kwanza lilichukua wajibu huu kwa makini, kwa kuwa haiwezekani kutenganisha kuenea kwa injili na kupanuka kwa kanisa katika kitabu cha Matendo. Ilikuwa misheni ya kanisa kupeleka injili kuanzia Yerusalemu mpaka Yudea na Samaria na mpaka miisho ya dunia. Kwa bahati mbaya leo tunazungumzia juu ya kanisa na misheni kama vitu tofauti. Katika Agano Jipya, misheni ilikuwa ni kanisa na kanisa ilikuwa ni misheni.

Harakati za uinjilisti ambazo hazikuongana na kanisa hazikuongozwa vizuri kutoka mwanzoni. Ufuatiliaji na kukua kwa polepole, kwa mfano, kuna matatizo sugu watu wanapoinjilishwa kupitia juhudi zisizohusiana na kanisa. Mungu ameanzisha kanisa ambalo kwa kupitia kwake mataifa yatafuaswa. Maandiko yananena kuwa: 'Ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho; kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Bwana wetu' (Efe 3:10-11). Ni mpango wa Mungu kanisa kuufikia ulimwengu leo, kuthibitisha maendeleo ya ushindi dhidi ya Shetani, na kuwafungua hao ambao wangekuwa sehemu ya 'watu wa Mungu.'

## SULUHU

Katika Yesu Kristo, Mungu anapatanisha watu na yeye mwenyewe, anarudisha uhusiano wao na yeye (Efe 1:9-10). Mungu amelipa kanisa lake huduma hii ya upatanisho (2Kor 5:18-20). Kwa hiyo, ni mpango wa Mungu kanisa kuufikia ulimwengu leo, kuthibitisha maendeleo ya ushindi dhidi ya Shetani, na kuwafungua hao ambao wangekuwa sehemu ya watu wa Mungu.

Kuanzishwa kwa kanisa kwa dhumuni hili ni hatua ya kwanza ya sasa ya mpango wa ukombozi wa Mungu. Kushiriki katika kuanzisha na kuimarisha kanisa siyo kazi ndogo. Ni shughuli muhimu kwa kila muumini na inaleta matokeo ya milele. Hata siku moja usidhanie kuhusika kwako katika upandaji na kuongoza kanisa ni kudogo!

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni nini muonekano wa kanisa kama kanisa linalotoka nje?
- Ni kwa jinsi gani kueleweka kwa Agano la Kale (kuja ndani) kunaathiri uzima wake? Ni wakati gani kueleweka huko ni mwafaka kwa kanisa la mtaa? Na kwa nini?
- Ni nini msingi wa huduma yako ya kanisa? Ni nini kinatokea wakati Kristo anapokuwa siyo msingi wa kanisa jipya?
- Kanisa lipo kwa ajili ya ulimwengu (Efe 3:1-10). Ni nini muonekano wake?

- Kristo ni kichwa cha kanisa. Ni nini muonekano wa vitendo kwa hili? (Efe 1:23; Col 1:18). Jinsi gani tunamruhusu kuwa yote Bwana na mkuu katika ngazi ya vitendo?
- Muumini anaweza kuwa sehemu ya kanisa la wengi na siyo sehemu ya kanisa la mtaa?
- Ina maana gani kwa kanisa kuwa mwenyeji?
- Jifunze baadhi ya mifano halisi iliyotumika kuelezea kanisa (Efe 2:15,19,21; 1Pet 2:9-10). Ni ipi kati ya hii inaleta maana zaidi kwako binafsi?

#### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Ni kwa jinsi gani Mungu anafanya kazi katika kata yako kutimiza ahadi zake? Ni nini Mungu amefanya kwa mwaka uliopita, miaka 5, au miaka 50, kinachodhihirisha uaminifu wake wa kujenga kanisa lake? Andika angalau mambo 10 ya uchunguzi kuonyesha uaminifu wa Mungu katika mandhali ya nchi yako.

#### VYANZO

- Billheimer, Paul. *Destined for the Throne*. Fort Washington, PA: Christian Literature Crusade, 1975.
- Ellisen, Stanley. *The Biography of a Great Planet*. Wheaton, IL: Tyndale House Publishers, 1978.
- Pate, Larry, *Starting New Churches*, Irving, TX: International Correspondence Institute, 1984.
- Saucy, Robert. *The Church in God's Program*. Chicago, IL: Moody Bible Institute, 1972.
- Smith, Dwight. Notes on The Local Church Paradigm from *The Alliance for Saturation Church Planting* and United World Mission, 1994.
- Thompson, Paul. *Planting Reproducing Churches*. Warrington, PA: World Team, 1992.





# Kusudi la Kanisa

## KWA NINI KANISA LIPO?

---

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kueleza namna kanisa linavyokusudia kuwa nguvu ya kueneza injili duniani.

### ☞ Wazo Kuu

- Kanisa lina makusudi matatu—matokeo, mwonekano wa nje, mwonekano wa ndani
- Kanisa ni wakala wa kuhamasisha kuliko tu kitu cha huduma

### ☞ Matokea Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa...

- Afhamu makusudi ya Biblia kwa kanisa
- Atambue kuwa makusudi ya kanisa kama wakala wa kuufikia ulimwengu inahitaji upandaji kanisa na kufanya huduma.

### ☞ Ziada

2A Ukurasa wa maswali kuhusu Utume Mkuu

### ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Hakikisha kuwa washiriki wanaweza kutamka muonekano wa nje na ndani wa kanisa. Inaweza kuwa vizuri kama utatumia muonekano mkubwa kwa wafunzwa kuwatia moyo juu ya mifano mbalimbali ya kusudi la kanisa. Unaweza kuchora mchoro kwenye ubao. Au, kulingana na mazingira yako, ubao wa kuandika kwa chaki au senema inaweza kufaa zaidi.

## UTANGULIZI

'Kusudi' linaweza kuelezewa kama '*mwisho ambako juhudi zetu zinatufikisha.*' Shirika lolote lina kusudi. Biashara ipo kwa ajili ya kutengeneza pesa kwa kuuza bidhaa au huduma inayotoa. Serikali ya nchi ipo kwa ajili ya kulinda watu wake na kutawala watu wake.

Bwana Yesu anasimama kama kielelezo kikubwa katika nafasi ya kanisa. Alijua kwa nini alikuja duniani na wapi anakwenda. Alikuwa na kusudi kubwa. 'Roho wa Bwana yuko juu yangu, kwa sababu amenitia mafuta kuwahuburi masikini habari njema. Amenituma kutangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu wapate kuona tena, kuwaweka huru walioteswa, kuutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa' (Luk 4:18-19).

Ili kanisa kuleta makusudi ya kweli katika ulimwengu leo, lazima wawe na mwanga wazi juu ya kusudi. Bila hivyo, viongozi wa kanisa na wafanyakazi wanaweza kuwa wanapoteza nguvu na rasilimali zao kufanya mambo ambayo hawakuitiwa. Kila mpanda kanisa anatakiwa kuelewa dhumuni la kibiblia kwa kanisa na kufikiri juu ya dhumuni hili katika mwanga wake wa kazi ya upandaji kanisa na misheni.

Kuelewa sawasawa kwa kusudi la kibiblia kunaweza kulifanya kanisa:

- Kuwa la madhumuni na matarajio.
- Uaminifu na uwazi, kusimamia ukweli wa maandiko.
- Lenye neema na mahusiano, na kusisitiza upendo wa Mungu na msamaha.

- Furaha na kuadhimisha (watu wanatarajia hili).
- Lenye uhai na mabadiliko, kuwaandaa watu kwa ajili ya huduma hai.
- Linakua na kuongezeka, kupanda makanisa mapya.

## I. KUSUDI LA KANISA

Yesu ameanzisha kanisa akiwa na kusudi akilini. Ni kusudi la ajabu sana, lililothibitishwa katika milele iliyopita, na kuandaliwa utukufu ujao. Tunaweza kufupisha kusudi la kanisa kwa kusema *kanisa lipo kumtukua Mungu kwa kulea waumini na kuinjilisha waliopotea*. Kielelzo 2.1 kinaonyesha mifano mikuu mitatu ya dhumuni la kanisa.

**Jedwali 2.1 Mifano Mikuu Mitatu ya Dhumuni la Kanisa**

HATIMA YA KUSUDI	KUSUDI KWA NJE	KUSUDI KWA NDANI
Kumwinua Bwana	Kuinjilisha waliopotea	Kuadirisha watenda kazi
Kanisa lipo kwa ajili ya Bwana	Kanisa lipo kwa ajili ya ulimwengu	Kanisa lipo kwa ajili ya lenyewe

### A. Kumtukua Bwana

Biblia inafundisha kuwa kuna kusudi kwa kila kiumbe kujongea.; ni kwa utukufu wa Mungu mwenyewe. Utukufu wa Mungu unaonyesha kila kilicho kweli juu yake: Asili yake, namna ya kupambanua, tabia, na matendo. Utukufu wa Mungu mwenyewe ndilo dhumuni lake kuu la milele na dhumuni kuu la kuwepo kwa mwanadamu. Analifanyia kazi kusudi lake la milele kufikia mwisho huu. Utukufu wa Mungu mwenyewe ndilo kusudi la mwisho la kanisa (Rum 15:6,9 Efe 1:5ff; 2The 1:12; 1 Pet 4:11).

Mungu anatukuzwa (kudhihirishwa, kutambulishwa) tunapomwabudu yeye (Yoh 4:23), kumuomba na kumtukua yeye (Zab 50:23) na kuishi maisha ya kimungu (Yoh 15:8). 'Lolote ufanyalo, fanya kwa utukufu wa Mungu (1Kor 10: 31). Hii ni kweli kwa mkristo mmoja mmoja na kwa kanisa lake.

- Ina maana gani kwako kumtukua Mungu?
- Ni jinsi gani kanisa linamtukua Mungu?
- Ni jinsi gani Mungu ametukuzwa katikati yetu?

### B. Kuinjilisha Waliopotea

Biblia inafundisha waziwazi kuwa kuna dhumuni la nje kwa kanisa, kuweza kukamilishwa katika kizazi hiki. Ni dhumuni linaloweka kanisa kukazia na kuweka juhudi nje ya lenyewe. Ndiyo kusudi Yesu alikuja kwa ajili ya waliopotea na ulimwengu unaokufa (Luk 19:10). Yesu alisema, 'kama Baba alivyonituma mimi nami nawatuma ninyi' (Yoh 20:21). Dhumuni hili la nje ya kanisa ni kuwafikia kwa uinjilisti na umishenari waliopotea.

Huenda hakuna kipengele cha maandishi kinachoelezea dhumuni la nje la kanisa 'Utume Mkuu' kuliko kifungu cha Mathayo 28:18-20. (Tazama ziada 2A, "Ukurasa wa maswali kuhusu Utume Mkuu").

### C. Kuadilisha Watenda Kazi


Biblia inafundisha kuwa kanisa pia lina dhumuni la ndani. Ni kuwaadilisha au kuwajenga waumini wake. Sehemu kubwa ya Nyaraka katika Agano jipya waliandikiwa waumini kuwaimarisha katika maisha yao ya ukristo na katika huduma ili kwamba waweze kutimiza kusudi la nje la kufikia waliopotea na ulimwengu unaokufa.

Waefeso 4:11-16 inaelezea vizuri dhumuni la ndani la kanisa. Kanisa lipo kuwaadilisha waumini. Kufundisha na kuwaandaa watu wa Mungu kama jamii iliyokusanyika ( katika kuabudu, mafundisho, ushirika na kazi ya kulisha neno) inapelekea ukamilishaji wa kusudi la nje, la kufanya wanafunzi.

- Uongozi umetolewa (v..11) kuwaandaa watakatifu kwa ajili ya huduma (v. 12), siyo tu kufanya kazi za huduma peke yao. Ni nini muonekano wa uhai wa kweli katika kazi yako ya upandaji kanisa? Ni namna gani hii itaathiri kufanya unachofanya?
- Ni uchunguzi gani unafanya kutoka katika kifungu hiki juu ya upandaji kanisa? Uandike hapo sasa.

Kusudi la kanisa linaweza kuelezewa kwa ufupi kama kutukuza, kuadilisha, na kuinjilisha. Watu wa Mungu wanakusanyika kwa ajili ya kuabudu na kuadilishana, ili kutawanyika kufanya kazi ya uinjilisti. Haya ni makusudi yanayoendana. Hakuna moja ambalo lingekuwapo bila jingine kuwepo. Kusudi la ndani (kuadilisha) linatumikia kusudi la nje (uinjilisti) na makusudi yote yanafanya kumtukuza Mungu (kumwabudu). Wafuasi wa Yesu wanapokusanyika pamoja kwa ajili ya dhumuni la ndani la kuadilishana Efe 4:11-16), kupendana wao kwa wao (Yoh 13:34-35), na kufanya kazi ya kanisa la Agano Jipya (Mdo 2:42-43), waliandaliwa vizuri kwa kazi ya nje ya kuwafikia na huduma kwa ulimwengu uliopotea.

### Kielelzo 2.2 Madhumuni Makuu Matatu ya Kanisa



## II. MAPANA KATIKA KUELEWA KUSUDI LA KANISA


Mapana kwa kifupi maana yake ni namna ya kuangalia kitu fulani. Mapana yanatoa sababu ya msingi na maelezo ya jinsi mfumo fulani, hatua, au kitu kilivyo na kitakavyokuwa. Kundi la vifungu vifuatavyo vya kutofautisha mapana ni njia za kuangalia kanisa katika mwanga wa asili yake na kusudi.

### A. Kanisa Linalozingatia Vipindi Likilinganishwa na Kanisa la Utume Mkuu

#### 1. Kanisa Linalozingatia Vipindi

Makanisa mara nyingi yanahangaika katika kufanyia mazoezi pande kadhaa za kusudi. Kushindwa kuendeleza kile ambacho Mungu ametuitia kufanya inaweza kupelekea kuelekeza kipindi chenye vipengele kadhaa, kila kipengele kikishindania rasilimali na washiriki, (angalia kielelezo 2.3). Katika kipindi hiki mtazamo uliowekwa kati, kanisa linaweza kufanana na mfumo wa kufundishia wa kidunia au biashara ndogo ndogo katika muundo wake na matengenezo. Baada ya muda, kanisa linajifikiria lenyewe na siyo kufikiria waliopotea, na kutofungamana na jamii ambamo inatokana.


### Kelelezo 2.3 Kanisa Linalozingatia Vipindi



#### 2. Kanisa la Utume Mkuu

Mtazamo wa kibiblia wa kanisa, ulioonyeshwa katika kielelezo 2.4, inaweka Utume Mkuu kwenye moyo wa kusudi la kanisa, na kutokea hapo vinaendelea vipindi na huduma za kuandaa. Katika mtindo huu asili na vipindi vya kanisa la jamii lililokusanyika linatumika kuandaa muumini kwa kazi ya nje ya mbeleni au kusudi—kazi ya uinjilisti na Utume Mkuu. Mahitaji ya waumini yanaendelea kutunzwa lakini katika mtazamo wao halisi kwa mwanga wa kusudi la Mungu la kuleta waliopotea kwake.

### Kielelezo 2.4 Kanisa la Utume Mkuu




- Ni mtawanyiko upi kwa njia hizi mbili kwenye miundo ya kanisa? Uhamasishaji wa wajumbe wa kanisa kwa ajili ya kazi za kanisa? Maendeleo ya uongozi?
- Ni kitu gani kinatokea kwa kanisa linapotambua kwamba 'kusudi la kuwepo ni kueneza injili?

**B. Kanisa kama ‘Chombo cha Huduma’ Ikilinganishwa na Kanisa Kama ‘Wakala wa Uhamasishaji’**

1. *Kanisa kama chombo cha Huduma*

Baadhi ya waumini wanafikiri kanisa ni sehemu ya kukusanyikia kuwa na waumini wengine na kuhudumiwa na mchungaji (angalia umbo 2.5). Hiki yamkini ni kielezo kinachotumika mara nyingi hasa kulitazama kanisa. Kielelezo hiki kwa upande ni cha kweli. Kanisa linahitaji kusanyiko mahali tunapofurahia kukutana na vilevile kupata virutubisho vya kiroho kutoka kwa viongozi wa kiroho. Kwa jinsi hiyo, kielelezo hiki kinashindwa kuweka kusudi la nje la kanisa katika mtazamo maalumu na kuwapa madaraka isivyo kibiblia/wasio na maarifa ya madaraka.

**Kielelezo 2.5 Kanisa Kama Kielelezo cha Huduma**




Imerithiwa kutoka Brock Uk. 66,67

**2. Kanisa kama Wakala wa Uhamasishaji**

Kanisa siyo chombo cha huduma, isipokuwa wakala wa kuhamasisha injili duniani. Kama ilivyoonyeshwa katika kielelezo 2.6, nafasi ya uongozi kanisani ni kuwaandaa (kufundisha na kuwatia

nguvu) wajumbe wa kanisa kwa ajili ya huduma ulimwenguni. Hili ni dhumuni la kuadilisha kanisa. Waumini wanakusanyika pamoja kumwabudu Bwana, kukua katika imani zao, kujifunza neno la Mungu, kutiana moyo, kuombea, na kwa vitendo kusaidiana. Wajumbe hawa wa kanisa wanaanza kupata tabia ya kiroho na ujuzi wa kihuduma unaohitajika kuinjilisha waliopotea (kusudi la kutoka nje la kanisa). Kutimiza Utume Mkuu siyo tu kazi ya mchungaji, au kazi ya wachache kanisani, isipokuwa ni kazi ya mwili wote wa Kristo (kanisa)

**Kielelezo 2.6. Kanisa Kama Wakala wa Kuhamasishaha**



Imerithiwa kutoka Brock Uk66,67

**SULUHU**

Wazo lililo wazi la kusudi linasaidia kanisa kuwajibika. Bila kuelewa kusudi lake, viongozi wa kanisa na wafanya kazi wanaweza kupoteza nguvu na rasilimali kufanya mambo ambayo hawakuitiwa kuyafanya. Kila mpanda kanisa anatakiwa kuelewa dhumuni la kibiblia la kusudi la upandaji kanisa na kutafakari juu ya kusudi hilo katika mwanga wa upandaji kanisa lake mwenyewe na kazi ya miseni.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Kwa nini ni muhimu kwamba kanisa linaelewa kusudi lake? Ni nini kinachotokea kanisa linapokuwa halielewi kusudi lake?
- Ni kwa jinsi gani unaweza kuweka kwa ufupi kusudi la kanisa?
- Kwa nini kanisa liwafikie nje waliopotea? Nani anawajibika kuinjilisha?
- Ni kwa namna gani Utume Mkuu unaelekeana na kusudi la kanisa? Ni vifungu vipi vingine vya biblia vinatusaidia kuelewa kusudi la kanisa?
- Kwa nini kanisa liwe nguvu na siyo shamba tu?
- Je makanisa katika eneo lako yanafahamu wazi kwa nini yapo kama makanisa?
- Ni nini nafasi ya uongozi katika kusudi linaloliendesha kanisa?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Tafakari juu ya kusudi la kanisa kwa kufanya ukurasa wa maswali yaliyomo katika Ziada 2A, "Ukurasa wa Maswali ya Utume Mkuu."

### **VYANZO**

- Brock, Charles. *Indigenous Church Planting. Practical Guide.* Neosho, MO: Church Growth Institute, 1994.
- Getz, Gene. *Sharpening the Focus of the Church.* Wheaton, IL: Victor Books, 1984.
- Morris, Linus. *The High Impact Church.* Houston, TX: Touch Publications, 1993.
- Warren, Rick. *The Purpose Driven Church.* Grand Rapids, MI: Zondervan, 1995.
- Excerpts from lectures on the Church from Project 250 and Russian Ministries. Moscow, Russia: 1994.
- Cook, Jerry. *Love, Acceptance and Forgiveness.* Glendale, CA: Gospel Light Publications, 1979.



## Karatasi ya Maswali ya Utume Mkuu

---

Soma na tafakari juu ya vifungu vitano vya Utume Mkuu. Kisha, Jibu maswali yaliyotolewa katika kila kifungu.

### **Mathayo 28: 18-20**

1. Ni faraja gani iliyopo katika ukweli kwamba “mamlaka yote” amepewa Yesu?
2. Kwa kuwa yeye ni Bwana mwenye enzi, Ni kitu gani ametutaka tufanye?

### **Marko 16:15-20**

1. Ni onyo gani unapata hapa kwa wasioamini?
2. Nini itakuwa ishara itakayofuatana na wanaoamini?
3. Ni jinsi gani Bwana alijidhihirisha mwenyewe baada ya kupaa mbinguni?

### **Luka 24:45-53**

1. Ni vitu gani wanafunzi wanatakiwa kushuhudia?
2. Ni ahadi gani Kristo aliwapa?

### **Yohana 20:19-23**

1. Yesu alikuwa na maana gani aliposema, “amani iwe nanyi”?
2. Ni kwa jinsi gani hii inaelekeana na maelezo yake katika vv..22-23?
3. Ina maana gani kupelekwa?

### **Matendo 1:1-11**

1. Ni matokeo gani ya asili Roho Mtakatifu anapokuwa anafanya kazi katikati yetu?
2. Ni kwa umbali gani matokeo ya injili yatafika?

### **MASWALI YA KUTUMIA**

- Ni hofu gani niliyonayo ninayotakiwa kuishinda kwa kutambua ukuu wa mamlaka ya Kristo? Ni kwa jinsi gani naweza kuinjilisha vizuri zaidi?
- Ni kwa jinsi gani injili ihubiriwe “kwa mataifa yote” katika nchi yangu?
- Je ninahudumu nikiwa na nguvu za Mungu ndani yangu? Ni kwa jinsi gani niruhusu uweza wake kukua zaidi kwa ajili ya utukufu wake?
- Ni kwa kiasi gani ninajali hali ya waliopotea? Ni kwa jinsi gani hii itagusa namna ninayoongoza kanisa ninalopanda? Ni tofauti gani inayofanya?



## MISTARI SAMBAMBA YA UTUME MKUU

	UTANGULIZI	AMRI	AHADI
<b>MATHAYO</b> <b>28:18-20</b>	Mamlaka yote ya mbinguni na duniani nimepewa (18)	Kwa hiyo enendeni mkawafanye mataifa kuwa wanafunzi wangu, mkiwabatiza kwa jina la baba na Mwana na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru (19) (20).	Na tazama, Amini nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari (20).
<b>MARKO</b> <b>16:15-20</b>	Ushuhuda wa ufufuko (9).	Nenda ulimwenguni mwote na kuhubiri habari njema kwa kila kiumbe (15).	Kila aminiye na kubatizwa ataokoka; na kila asiyeamini atahukumiwa (16).
<b>LUKA</b> <b>24:45-53</b>	Imeandikwa hivi: Kristo atateswa na kufufuka kutoka kwa wafu siku ya tatu (46)	Na kwamba mataifa yote yatahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanzia Yerusalemu. Nanyi ndiyo mashahidi wa mambo haya (47-48).	Nitakwenda kuwapa kile Baba yangu alichoahidi; lakini kaeni katika mji mpaka mtakavikwa nguvu kutoka juu 949)
<b>YOHANA</b> <b>20:19-23</b>	"Amani iwe nanyi!" Baaada ya kusema hayo, aliwaonyesha mikono yake na ubavu. Basi wale wanafunzi wakafurahi sana walipomwona Bwana (19) (20)	Kama baba alivyonituma, Nami nawatuma ninyi (21).	Pokea Roho Mtakatifu (22).
<b>MATENDO</b> <b>1:1-11</b>	Baada ya mateso yake, alijitokeza kwa watu hawa kwa kuwadhihirishia kwa dalili nyingi kwamba alikuwa hai (3). "Akawaambia, si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba alivyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe (7).	Na mtakuwa mashahidi wangu, Yerusalemu, na Yudea yote na Samaria, na miisho ya duni	Mtabatizwa kwa roho Mtakatifu (5)...Lakini mtapokea nguvu akisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu (8)



# Mfumo na Kazi

## MTAZAMO WA KIBIBLIA NA KIUTAMADUNI

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuelezea wazo muhimu la kazi na mfumo katika kanisa, kutoka katika mtazamo wa kibiblia na kiutamaduni.

### ☞ Wazo Kuu

- Utendaji wa kibiblia ndio lazima ufanyike—Ulitolewa na Mungu na hauwezi kuongezwa.
- Mfumo wa kibiblia ndiyo jinsi tunavyofanya utendaji—ni wa kiutamaduni na unatakiwa kurekebisha kadiri iwezekanavyo.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa wazo na maswala ya 'mfumo na kazi.'
- Kutambua jinsi nguvu ya utamaduni na uzoefu wa mtu binafsi vinavyobadili sura na mfumo wa kanisa la mtaa.
- Kushawishika kuanzisha mfumo wa kanisa ukizingatia kazi ya kibiblia na inavyostahili kiutamaduni.

### ☞ Ziada

3A Mfumo na Kazi iliyotumika: Kutumia masomo yaliyo katika Matendo 2

## UTANGULIZI

Kuelewa mfumo na kazi ni msingi kwa upandaji kanisa. Uzoefu wetu mkubwa unarekebisha ufahamu wetu, na kujitoa kwenye mifumo inayokubaliwa na makanisa yetu. Ni lazima tushawishike kuuliza kwa nini tunafanya tunachokifanya kutimiza misheni Mungu aliyopa kanisa. Somo hili litatoa nafasi ya kufikiri upya 'mfumo' wa huduma na kutoa maelekezo ya kuanzisha mifumo mingi inayokubalika na yenye ufanisi.

## I. MFUMO NA KAZI ILIYOELEZEWA

Katika jamii, kazi ni *shughuli inayohitaji kufanyika*. Shughuli hii inaweza kuachana na nyingine kama ilivyo vigumu kupata chakula au kulea watoto, kwa nyingine ambayo inaweza kuwa rahisi kama kupata usingizi. Hivi ni vitu vinavyohitajika kufanyika. Mfumo ni njia iliyochaguliwa kuendeshea kazi hiyo.

Mfano unaweza kuwa jinsi unavyoweza kupata chakula. Katika nyakatu za zama za zamani, ungeweza kuwinda au kuotesha mazao. Hizi ni njia mbili tofauti, lakini zote zinatoshesha kazi ya kupata chakula.

Swali ni kwamba: jinsi gani unaamua ni mfumo upi bora kwako? Baadhi ya vigezo vya kuamua vinatokana na vyanzo vya ndani, kama vile uwezo na upendeleo. Una jicho zuri na hujali kuwa peke yako kwa kipindi cha muda mrefu? Kama ni hivyo utakuwa mwindaji bora. Na kama sivyo, basi ng'ang'ania kilimo. Baadhi ya vigezo ni vya nje, kutegemeana na mazingira yako. Unaishi kwenye au karibu na ardhi yenye rutuba? Kama ni hivyo basi unaweza kufanya vizuri kuwa mkulima. Baadhi ya vigezo ni vya kiutamaduni,

- ◆ **Kazi** = Shughuli inayohitaji kufanyika
- ◆ **Mfumo** = Njia inayochaguliwa ya kuendeshea kazi

kutegemeana na mawazo ya jamii uliyopo. Wakulima wanazawadiwa kwa sababu ya kuchangia kiasi cha mazao katika kijiji, au wawindaji wanazawadiwa kutokana na ujuzi wao hasa wakati wa vita? Baadhi ya vigezo vinaweza kuwa vya maadili. Mauaji ya wanyama yanaonekana kama upotofu wa maadili? Kigezo kingine ni cha mapokeo. Ni nini wazazi wako na wazazi wao walifanya?

Mfumo unategemeana na vigezo vingi na unaweza kubadilika kulingana na muda. Shamba lako linaweza kuwa halizalishi tena, au mawindo yanaweza kuwa haba. Kulingana na muda, uvumbuzi mpya unaweza kubadili uwezo wako wa kufanya kulingana na ujuzi wako, au kukufanya kuchagua ujuzi mpya ambao haukuwepo mwanzoni, kama vile uuzaji wa duka.

Usafirishaji ni mfano mwingine wa kanuni za mfumo na kazi katika jamii. Usafirishaji ni kazi inayoweza kutekelezwa katika mifumo mbalimbali inayoweza kama vile: Baiskeli, Treni, Gari kama trekita, pundamilia, na mkokoteni. Swali ni kwamba:

- Ni nini kitayakinisha njia ya usafiri unayotumia? Kwa nini?
- Ni kitu gani kinafanya njia moja kuwa bora kuliko nyingine?
- Unaweza kufikiri mfano wa mfumo na kazi katika namna yako?

## II. MFUMO NA KAZI KATIKA KANISA

Mfumo na kazi vinaweza kuelezewa kwa upana kama mfano ulio hapo juu, au inaweza kuzingatia eneo maalumu. Kwa mfano, kuna mifumo ya kibiblia na kazi zilizoelezewa kote katika Agano la Kale na Agano Jipya. Kwa jinsi hiyo, ili kuelewa umuhimu wa wazo hili katika upandaji kanisa, tutazingatia tafsiri zaidi kwa mkazo, na kuangalia juu ya mifumo ya kanisa na kazi za kanisa.

### A. Kazi za Kanisa

Agano Jipya ni pamoja na amri, sheria, maelekezo, usia, makatazo na kanuni ambazo kanisa lazima lifanye. Kazi hizi ni za muda na za kiutamaduni. Hazibadiliki na zinahitajika kwa waumini wote, bila kujali taifa, utamaduni, umri, au lugha.

**Kazi za kanisa** ni shughuli ambayo Bwana ameamru kanisa lake kuzifanya.

*Mifano:* Kuabudu, ushirika, agizo, maombi, uinjilisti, ufuasishaji, utoaji, ufundishaji, ushirika wa meza ya Bwana (Pasaka ya Bwana).

### B. Mifumo

Mifumo ya kanisa ni pamoja na miundo yote, mapokeo, njia, na taratibu ambazo kanisa linachagua ili kuendeleza kazi katika umri maalumu, utamaduni, hali halisi iliyopo. Mifumo hii inaweza na hutofautiana sana miongoni mwa makanisa ya mitaa—hupelekea mifumo mingi inayokubalika kwa kila kazi ya kanisa.

**Mfumo wa Kanisa** ni njia kanisa linazotumia kufanyia kazi ya kanisa.


*Mifano:* Matoleo kwa watakatifu walioko Yerusalemu, Mkanda wa sinema ya Yesu, Wanaosimama mlangoni kusalimia, wahubiri wanaolipwa, siku za jumatano (mf. “mara moja kwa juma”) kufanya mafunzo ya Biblia.

### C. Mfumo na Kazi Pamoja

Uhai wa kanisa lolote la mtaa hauwezi kuondolewa nje ya utamaduni/mazingira ya kihistoria. ‘uzoefu’ wetu wa kanisa hautokani tu na mafundisho ya kibiblia. Njia ‘tunazofanyia’ kanisa zinatokana na mchanganyiko wa mapokeo ya kihistoria, matukio ya tamaduni, (na zinakaribiana na utamaduni), na thibitisho la kibiblia.

Kazi ya mpanda kanisa ni kuendeleza kwanza mifumo ya kanisa kutoka katika misingi ya kibiblia, na baadaye katika mwanga wa desturi zinazohusiana na kiutamaduni. Katika kielelezo 3.1, tunaona kwamba kuna idadi ya kazi za kanisa ambazo zimeagizwa katika maandiko. Hizi hazibadiliki kulingana na muda wala utamaduni. Kwa jinsi hiyo, mstari wa mwisho wa kielelezo unaonyesha kwamba kila kanisa la mtaa linahitaji kurithi mfumo tofauti kabisa kuweza kukidhi kazi hizi katika mazingira yao. Mifumo inayohitajika haihitaji kufanana na ya makanisa mengine—lazima itosheleze mahitaji ya kazi ya kanis

Kielelezo 3.1 Mfumo na Kazi



### III. KUTATHIMINI MFUMO NA KAZI KATIKA KANISA

Inaweza kuwa vigumu kutofautisha kati ya mfumo na kazi katika kanisa isipokuwa mpaka kuchukua muda kunyambulisha. Katika jedwali lifuatalo, idadi ya kazi zimeorodheshwa kushoto, na baadhi ya mifumo mingi inayowezekana ya kila mfumo iko kulia

Mchoro 3.2 Mifumo na Kazi

Kazi ya Kibiblia	Mifumo inayowezekana
Kuomba	Kupiga Magoti au Kusimama
	Kimya Kimya au kwa Sauti
	Katika Makundi au Mmoja Mmoja
	Kabla ya Chakula au Mwishoni Mwa Ibada
	Toba au Kusihi
Kufundisha Neno	Darasa la Jumapili
	Mahubiri
	Mafunzo ya Biblia Katika Vikundi Vidogo
	Sala katika Familia
Kuinjilisha	Uinjilisti wa Kirafiki
	Mikutano ya Nje
	Mwaliko Wakati wa Ibada

Tafadhali tambua kuwa orodha ya mifumo iliyoko upande wa kulia mwa jedwali haitoshelezi kabisa—kuna mingi, mingine mingi inayowezekana. Je mfumo mmoja ni bora zaidi kuliko mingine ilivyo? Hapana. Yote inaweza kustahili au isistahili katika tukio maalumu na namna utamaduni ulivyo. Hakuna mmojawapo wa mifano hii imeamriwa katika Biblia kama njia pekee. Isipokuwa kazi tu ndiyo imeamriwa. Ni lazima tuchague mifumo kadiri inavyohitajika.

Katika jedwali hapo chini, mifano miwili ya kazi kibiblia imeorodheshwa. Chukua dakika chache kujaza mifumo inayowezekana upande wa Kulia. Kisha linganisha mawazo yako na mawazo ya wanafunzi wengine.

**Jedwali 3.3 Kazi Dhidi ya Mfumo**

Kazi za Kibiblia	Mifumo Inayowezekana
Kutoa sadaka	
Kuabudu	

Katika jedwali chini, idadi ya mifumo imeorodheshwa upande wa kulia. Kwa kila mfumo, amua ni kazi gani ya kibiblia inatimiza na kisha iandike hiyo upande wa kushoto. Kisha linganisha na jadili majibu yako.

**Jedwali 3.4 Mifumo Dhidi ya Kazi**

Kazi	Mfumo
	Kambi ya Vijana
	Mkutano wa Maombi ya Kanisa
	Kwaya ya Kanisa
	Kupitisha Chombo cha Sadaka
	Jengo la Kanisa
	Mziki Maalumu Katika Ibada
	Kanisa la watoto
	Utaratibu wa Ibada
	Kusema Mashairi Kanisani

#### IV. KANUNI KUHUSIANA NA MFUMO NA KAZI

##### A. Kazi ni Muhimu Zaidi Kuliko Mfumo

Katika Biblia, kazi inakaziwa. Yesu alikuwa na haja zaidi na kazi na siyo mfumo. Hao waliompa upinzani zaidi Kristo walikuwa wale ambao walizoea mifumo, ibada za sanamu na mapokeo.

- Tazama Mathayo 9:14-17. Jinsi mafundisho ya Yesu juu ya mavazi na 'viriba vipya' yanahusiana na mfumo na kazi? Ina maana gani kuanza 'viriba vipya' aina ya kanisa?
- Ni kitu gani 1Samweli15:22-23, Hosea 6:6, na Mathayo 12:1-6 zinachangia katika swala hili?

Mifumo mara nyingi haikuelezwa katika Biblia. Kuna huduma ya kipekee ya hekaluni, ambapo mtindo wa hema na mapambo yake yamewekwa wazi kwa undani, lakini hili lilifanywa kwa kusudi tofauti. Ilitumika kufundisha juu ya Mungu, kazi yake na heshima yake. Siyo mfumo

ambao umeendelezwa mpaka kwenye kanisa la Agano Jipya kwa sababu ufahamu huo ulikuwa umeshakuwepo.


### B. Kazi ni Dhahili na Zinavuka Mipaka ya Tamaduni; Mfumo Siyo Dhahili na Hubadilika

Mfumo unapoelezewa katika Biblia tunaona mabadiliko yakifanywa juu yake. Pasaka ilikuwa ukumbusho wa Mungu kuwaokoa watu wake kutoka Misri. Yesu alibadilisha hili wakati wa chakula chake cha mwisho na akadokeza ukombozi ambao Mungu alikuwa karibu kuukamilisha katika kifo cha Yesu. Katika kanisa la karne ya kwanza hii ilibadilika tena na kuwa karamu ya upendo. Lakini hii ilianza kutumika kinyume (1Kor 11:17-34), kwa hiyo matumizi yalipunguzwa na kuwa kushiriki kikombe na mkate. Lakini hata hivyo hili linafanyika katika mifumo tofauti tofauti. Baadhi hutumia vikombe vya kawaida na wengine hutumia vikombe vya kipekee. Baadhi hutumia divai na wengine hutumia maji ya matunda ya mزابibu. Mfumo unaweza kuwa tofauti ili mradi kazi inatunzwa.

Mifumo ambayo imeelezwa katika vifungu fulani imebadilika au kuachwa bila kutumiwa na wengine. Inatofautiana kutoka hali moja na nyingine.

- Uwakili mwema (1Kor 16:1-2; 2Kor 8-9)
- Vipawa vya kiroho (1Kor 12-14; Rum 12; Efe 4)
- Malezi ya wajumbe wa kanisa (Mt 18; 1Kor 5; 2Kor 2)
- Ubatizo (Mt 28; Rum 6; Mdo 1)
- Siku ya kuabudu (Kut 20:8; Mdo 20:7)
- Utawala wa kanisa (1Tim 3; Tit 1; 1Pet 5)

#### Kielelezo 3.5 Kubadilisha Mifumo



Ni jinsi gani kanuni hii itaathiri njia unayotumia kuunda mifumo katika kanisa lako jipya, ukizingatia maandiko?

### C. Watu Mara Nyingi Hujilinganisha na Mifumo Zaidi Kuliko Kazi

Ni bahati mbaya, lakini watu hujiegesha kwenye mfumo na kukosa kazi. Wanaweza kuendeleza mifumo iliyopoteza uhai katika utamaduni wao unaoheshimiwa (Mf. Namna ibada ya kuabudu inavyoendeshwa). Kuna masimulizi ya zamani ya mtu aliyekuwa ndiyo ametoka kuolewa, aliyepika chakula cha kuku cha kwanza kwa ajili ya mme wake. Alipomtengea chakula hicho, vipande vya kila mwisho havikuwepo. Alimwuliza kwa nini havikuwepo. Alimjibu kuwa mama yake mara nyingi alipika hivyo. Basi mwanaume huyu akamuuliza mama mkwe kwa nini alipika hivyo alimjibu 'sijui. Mama mara nyingi alipika hivyo.' Tena Bwana

arusi alipomuuliza bibi kwa nini alikata vipande vya mwisho, jibu lake ilikuwa “Sufuria ya kupikia ilikuwa ndogo kwa huyo kuku.” Umepata wazo.

Watu wanapoamini kuwa kuna mfumo halisi unaotawala, matokeo yake wanahalalisha namna ya kuuendea. Mara nyingi, kukatalia mfumo unaohitaji kubadilika kunasababishwa zaidi na kutokujiamini na hofu ya mabadiliko kuliko kutoka katika ukweli wa kitheolojia. Hii inaweza kuwa ibada ya sanamu. Kuelewa mfumo na kazi kunaweza kusaidia watu kuona kuwa mabadiliko siyo kitu cha kutisha wakati wote.

#### **D. Mifumo Inatakiwa Isibadilishwe Bila Uangalifu**

Siyo kitu cha kawaida kwa kijana, ambaye ndiyo anamaliza seminari au chuo cha Biblia, bila kuwa na uzoefu wowote wa kichungaji, kuwa mchungaji wa kanisa na kujidhania kuwa anafahamu kikamilifu mambo yanavyotakiwa kufanyika. Ana ufahamu wa mfumo kamili ukoje na ni shupavu kubadili kila kitu kiendane na matakwa yake. Hana ufahamu juu ya namna watu walivyo, wala kujua ni nini wanataka kufanya. Anaweza hata asijue kama mawazo hayo yamewahi kujaribiwa na matokeo yake yakoje. Hii inaweza kupelekea hali ambayo wataanza kuhisi kama mchungaji hawajali isipokuwa anawaona kama sehemu ya majaribio na amekuja kuwatuma wao. Wanajisikia pia kama kanisa haliwafai tena na kama ni hivyo mchungaji lazima aondoke au wao wataondoka.

Mifumo inatakiwa kubadilika tu kukazia kazi. Wakati mmoja, ili kukazia kuabudu (kazi), mchungaji alianza ibada kwa nyimbo za sifa (kama kawaida) na kisha kutoa mahubiri. Kawaida mahubiri huwa mwishoni mwa ibada baada ya mziki maalumu, kuimbwa kwa kipindi kirefu, salamu na matangazo, lakini mchungaji huyu akaamua kuongea juu ya Mungu na kazi zake nzuri, kisha kualika kusanyiko kuabudu na kumshukuru Mungu kwa maombi, nyimbo za kumsifu (kutoka nyimbo za sifa) na kisha kushiriki meza ya Bwana. Badiliko lilikuwa la nguvu. Hii haina maana kwamba alifanya hivyo kila jumapili. Ilifanyika mara moja tu ili kuwafanya watu wafikirie katika namna mpya juu ya kuabudu kama sehemu ya ibada. Kisha walirudia mfumo wao wa kawaida.

#### **E. Mifumo Inapokufa Ganzi, Mkanisa Hufa**

Madhumuni ya kanisa ni kumtukuza Mungu kwa kuadilisha wajumbe na kuinjilisha waliopotea. Hii ni ya milele, kusudi ambalo halibadiliki. Kazi ni namna tunavyokamilisha kusudi hili. Zimetolewa na Mungu ambaye ametuambia namna anavyotaka tumtukuze yeye. Ni za milele pia na zisizobadilika. Mfumo ni mojawapo ya njia zinazobadilika kutimiza kazi maalumu. Mifumo inaweza kubadilika kwa sababu ni namna jamii inavyojionyesha.

Kuna nyakati ambazo umuhimu wa mifumo unaweza kukua na watu wasiruhusu ibadilike. Mifumo inapokuwa muhimu kiasi kwamba haiwezi kubadilishwa, kanisa litakufa mara moja kwa sababu jamii itabadilika na kanisa litaonekana halifai. Kama kanisa haliwezi kubadilisha jinsi ya kazi ya ndani, kanisa litakuwa halifai kwa jamii hiyo.

Kulikuwa na kanisa ambalo liliamua kuwafikia aina ya kundi la watu katika ujirani. Kusanyiko liliridhika na mfumo uliokua kwa ajili ya watu hawa. Lakini mifumo ikawa ya maana zaidi. Ujirani ukabadilika na kukawa na wachache zaidi wa kundi hili katika ujirani. Kipindi ambacho kanisa liling'amua kuwa walihitaji mabadiliko, ilikuwa wamechelewa. Walijulikana kama kanisa ambalo halikuwa na cha kutoa kwa watu wa ujirani na jengo la kanisa likafungwa na wajumbe waliobaki wakatawanyika.

### **V. VIDOKEZO VYA MFUMO NA KAZI KWA WAPANDA KANISA**

Wapanda kanisa lazima wafikiri kwa uangalifu juu ya mfumo na kazi. Mingi kati ya mifumo iliyoanzishwa wakati kanisa linazaliwa inaweza kutatanisha katika maisha na matengenezo ya kanisa. Inaweza ikawa vigumu kuibadili baadaye; na kama siyo ya kiufanisi, inahitaji tu kuondolewa. Zaidi ya hayo, Kama wapanda kanisa hawafanyii mazoezi mnyumbuliko unaohusu mfumo kisha utaratibu wa upandaji kanisa unaweza kuwa wa pole pole, wa gharama na mgumu.

Kama wapanda kanisa hawafanyii mazoezi mnyumbuliko unaohusu mfumo kisha utaratibu wa upandaji kanisa unaweza kuwa wa pole pole, wa gharama na mugumu.

Wapanda kanisa wanaokwenda katika mojawapo ya hatari inayozidi katika huduma zao. Wanaweza:

- Kutumia mfumo wa mapokeo wa kanisa ili kwamba njia ya kuhubiri, aina ya mziki, na njia ya kuinjilisha ni sawa na za makanisa mengine yaliyopo katika eneo. Matokeo inaweza kuwa kwamba kanisa litafikia watu wa namna moja badala ya watu wanaotarajiwa.
- Kurithi mifumo iliyotoka nje ambayo ni migumu kuzaliana katika utamaduni huo. Wapanda kanisa wanapodhani kuwa baadhi ya taratibu, vifaa au mtindo wa mziki ni muhimu kwa sababu unafaa katika hali zingine, kisha kanisa linaweza kuwa na muonekano wa nje kuanzia mwanzoni. Katika eneo lako, 'Umagharibi' au kundi kubwa la wamishenari wa nje wanaweza kuchangia tatizo hili.

Mifumo unayochagua itachangia kwa kiwango kikubwa ni sehemu ipi ya watu katika jamii yako watakutwa. Mifumo inatakiwa kutokea kikawaida kutoka katika utamaduni ili kwamba watu wanaolengwa waweze kuelewa kwa maelezo kidogo au bila maelezo ina maana gani. Sehemu ya utafiti inaangalia nani anaishi katika eneo lako linalolengwa, nani ambaye hajafikiwa na makanisa yaliyopo, na kutafuta namna ya kuwavutia kwenye kanisa lako kwa kuchagua mifumo itakayoleta maana kwao na uaminifu kwa kazi kibiblia.

### **MASWALI YA MARUDIO, KUTAFAKARI NA UTENDAJI**

- Kwa nini 'mfumo na kazi' ni muhimu kwa upandaji kanisa?
- Jinsi gani mifumo imeendelezwa katika kanisa lako? Namna gani imetunzwa?
- Mifumo katika uzoefu wako wa kanisa inakidhi kusudi/ kazi kibiblia?
- Ni kwa namna gani uimarisha zaidi mifumo katika kanisa lako kukidhi haja ya kiutamaduni?
- Mifumo ipi ni kizuizi cha kupeleka injili kwa waliopotea? Kuleta waumini wapya katika maisha ya kanisa?
- Ni aina gani ya upinzani unaoweza kukutana nao kama ungeamua kuanzisha kanisa jipya lenye mifumo tofauti na makanisa mengine katika utamaduni wako?
- Ni kwa njia zipi mifumo yako ni migeni na ya nje kwa waumini wako wapya?
- Ni kwa jinsi gani unaweza kuanzisha mifumo ambayo waumini wapya wataridhika nayo bila kubisha juu ya misingi ya kibiblia? Elezea mifumo hii inavyoelekeana na utamaduni wa kundi lako unalolenga katika kuabudu, ushirika, kushirikiana, meza ya Bwana, Kutoa fungu la kumi, na maelekezo ya kibiblia.
- Kwa mafunzo ya nyongeza, soma Matendo 6:1-15, na angalia jinsi viongozi wa kanisa la kwanza walivyoshughulikia tatizo la kimuundo, na namna walivyoweza kurekebisha mfumo kutengeneza muundo ili kukidhi zaidi mahitaji.
- Ni wakati gani mifumo ni dhambi? Toa mifano na oanisha na kanuni za kibiblia.

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Fanya mafundisidho ya Biblia kwa kufuata neno lilivyo kwenye Ziada 3A, "Mfumo na Kazi Iliyotumika: Mafunzo kwa Kulifuata Neno kutoka Matendo 2."
- Onyesha kazi dhidi ya mifumo katika kanisa lako.

### **VYANZO**

- Thompson, Paul. *Planting Reproducing Churches; A Basic Course*. Toronto, Canada: World Team Institute of Church Planting, 1992.
- Webster, Robert D. *Growing Churches for God's Glory*. Workbook written for BEE International, 1995.





# Mfumo na Kazi Iliyotumika

## MAFUNZO YA KUFUATA NENO YA MATENDO 2

---

### I. UCHUNGUZI

Soma Matendo 2:42-47 na tambua kazi za kwanza na matendo ya waumini. Orodhesha kila aina ya shughuli hizi katika nafasi ya kushoto kwenye jedwali chini.

### II. UFAFANUZI

Amua ni ipi kati ya shughuli hizi ni “mfumo” na ni ipi ni “kazi” na andika jibu lako katika nafasi ya kulia kwenye jedwali. Kama utaamua kuwa shughuli ni mfumo, amua ni kazi ipi inawiana na iandike kwenye sehemu sambamba na mfumo. Ni hali zipi zimekupelekea kuchagua mfumo huo hasa?

Shughuli	Kazi au mfumo

### III. MATUMIZI

- Tazama tena kwenye kazi dhidi ya kila mfumo iliyoonyeshwa katika jedwali hapo juu.
- Orodhesha angalau mfumo mwingine ambao ungekuwa umetumika.
- Ni mfumo upi kanisa lako linatumia kwa kazi hiyo?
- Kuna mifumo mingine inayofaa ambayo ingetumika kutimiza kazi hizo za aina moja leo?
- Ni jinsi gani utakavyofanya mabadiliko ya mfumo katika kusanyiko au katika kikundi kidogo? Ni mambo gani
- muhumu ya kufikiri unapokuwa unafanya mabadiliko?



# Kutafsiri Kanisa la Mtaa

## “NI NINI TUNACHOPANDA?”

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuvumbua tafsiri ya kanisa la mtaa katika mwanga wa kazi ya upandaji kanisa.

### ☞ Wazo Kuu

- Kutotosheleza kwa tafsiri ya kanisa la mtaa kutarudisha nyuma upandaji wa kanisa
- Kazi za kibiblia ni ufunguo kwa tafsiri ya kanisa la mtaa.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa umuhimu wa kuanzisha tafsiri ya kibiblia ya kanisa la mtaa
- Kuelewa jinsi mtu anavyoelewa kanisa la mtaa ni nini kunaweza kuongeza au kurudisha nyuma jinsi ya upandaji kanisa.

## UTANGULIZI

Haijalishi ni kazi gani tunafanya ya kanisa, kama ni wapanda kanisa au tunaongoza kanisa lililopo, ni lazima tuwe na mvuto kabisa juu ya kanisa ni nini. Swali hili la msingi, “Kanisa la mtaa ni nini?” Haliwezi kuchukuliwa tu kwa mzaha. Kuwa na uhakika tuko katika njia halisi, ni lazima tujiulize juu yake mara kwa mara. Ni jinsi gani tutalitafsiri?

Pengine maelezo yafuatayo yataonyesha kwa nini somo hili ni muhimu. Kabla ya vita vya 11 vya dunia, Uswisi ilitengeneza na kuuza karibu asilimia 90 ya saa duniani. Kwenye mwaka 1970, Uswisi bado ilikuwa na asilimia 60 ya soko la saa duniani, lakini mwanzoni mwa mwaka 1980, sehemu yao ilianguka mpaka kwenye asilimia 10. Ni nini kilitokea? Saa aina ya quartz ilikuwa imegunduliwa mwishoni mwa miaka ya 1960 na Waswisi hawakuendeleza ujuzi huo wakati watengenezaji wengine wa saa kama (Seiko, na Texas Instruments) waliendeleza. Watengenezaji wa quartz wa Uswisi waliacha kwa sababu ya walivyojua juu ya saa. Hawakuweza kudhani saa bila vifaa (mfano wa vifaa vya gari) kama gia, springi na whili. Kwa kuwa matengenezo ya quartz hayakutumia vifaa hivyo, waliacha. Kwa ufupisho, tunaweza kusema walipoteza dira ya kazi ya saa (kueleza muda) na badala yake wakatafsiri saa kwa mfumo waliokuwa wanaufahamu. Na kwa hiyo wakapoteza nafasi kubwa ya soko.

Kama vile tu Uswisi, tafsiri ya saa iliyokuwa ikifanya kazi ilipelekea kupoteza nafasi kubwa, kwa hiyo tafsiri ya kanisa inaweza kuathiri mafanikio ya mfululizo wa utaratibu wa upandaji kanisa. Tafsiri ya kanisa inadhihirisha ni nini wapanda kanisa wanatarajia kuzalisha na kuonyesha mbinu na mifumo wanayotumia. Tafsiri itakuwa hatua ya kielelezo, fimbo ya kupimia ufahamu wa mafanikio au kushindwa. Kama mpanda kanisa anaanza na tafsiri isiyo nzuri ya kanisa inaweza kupelekea kushindwa.

## I. UGUMU WA KUTAFSIRI KANISA

Makanisa yanaweza kutofautiana. Tambua uchunguzi ufuatao:

- Baadhi ya makanisa yanakutana katika majengo makubwa. Mengine yanakutana katika majengo madogo. Mengine hayakutani kwenye jengo. Mengine yanakutana majumbani.

- Mekanisa mengine yanakutana mara moja kwa juma. Mengine yanakutana mara mbili kwa juma. Mengine yanakutana mara tatu kwa juma. Baadhi ya makanisa yanakutana angalau kila siku ya juma.
- Baadhi ya makanisa yana mtu anayehubiri. Mengine yana mtu ambaye anaongea tu. Mengine yana mtu anayefundisha kama shuleni.
- Baadhi ya makanisa yanaonekana kuwemo kwa mzaha. Katika makanisa mengine hakuna anayetabasamu.
- Baadhi ya makanisa yana ibada changamfu, huku watu wakizunguka zunguka na kujibu kwa maneno juu ya kinachotokea. Baadhi yana ibada tulivu ambapo watu wengi hukaa kimya na kusikiliza.

Pamoja na tofauti zote hizi, Ni namna gani inawezekana kuelezea kiini muhimu ambacho lazima kiwepo kabla kundi halijaitwa kanisa? Je kuna kanuni ya msingi ambayo inaweza kuwa kweli juu ya kanisa la mtaa wakati wowote na katika jamii yoyote? Na kama ni kweli, Ni ipi tunafikiri kuwa kiini muhimu?

Tumia dakika kadhaa na zungumza katika makundi ya watu watatu au wanne na jibu maswali haya-

1. Ni wakati gani kundi la watu linakuwa kanisa?
2. Ni nini vipingamizi wakati wa kuamua kuwa ni kanisa ama siyo?
3. Itika kwenye hali zifuatazo. Ni kila moja ni kanisa? Kwa nini na kwa nini siyo?
  - Waumini wanane huko Amesivile wanakutana kila jumanne kujifunza Biblia na kushirikiana. Hawana mchungaji aliyeajiliwa ingawa mtu mmoja anaendesha mkutano. Wamekuwa wakifanya hivyo kwa miaka mingi. Baadhi ya washiriki wanahudhuria kanisa jumapili pia.
  - Katika mji wa kiasi cha kati, kuna jengo la kanisa la kihistoria lenye historia nono ya wachungaji wa maana na jamii iliyojihusisha. Utalii wa kanisa unaotolewa mara mbili kwa siku, mtu anaweza kujifunza juu ya ufundi wa kipekee na historia.
  - Mwinjilisti amewaongoza watu 10 kwa Yesu mwaka uliopita. Angependa kuona waumini hawa wapya wakishirikishwa katika kanisa lililopo lakini kanisa lililoko karibu ni umbali wa kilometa 50 kutoka hapo. Badala yake, Wanakutana katika nyumba yake kila jumapili jioni kuabudu na kujifunza Biblia.
  - Mtu mmoja na familia yake ndio waumini katika mji wao. Familia inachukua muda kila Jumapili kumwabudu Bwana.

## II. MIFANO YA TAFSIRI ZA KANISA

Katika kundi la watu 4 au 5, jadili tafsiri zifuatazo na jibu maswali yanayohusiana.

### A. Mfano # 1

Tafsiri zifuatazo ni jaribio la kuelezea kanisa kwa kutumia vielelezo maalumu kutoka kwenye maandishi vinavyoeleza jinsi watu wa Mungu wanavyopaswa kuhusiana wao kwa wao. Tafsiri inasisitiza mahusiano ambayo yanahitajika kuwepo katikati ya waumini.

*“Kanisa ni kundi la watu ambao wamejitoa na kutoa upendeleo wa mmoja kwa mwingine (Rum 12:10), kukubalika wao kwa wao (Rum 15:7), kujaliana (1Kor 12:15), kubebeana mizigo (Gal6:2), kusameheana (Efe 4:32), kutiana moyo na kujengana (1The5:11), kuungama dhambi zao wao kwa wao (Yak 5:16), kuombeana wao kwa wao (Yak 5:16), kuhudumiana (1Pet 4:10), na kupendana wao kwa wao (1Yoh 4:11).”*

- Ni jinsi gani tafsiri hii itawezesha au kurudisha nyuma hatua ya upandaji kanisa?
- Litakuwa ni kanisa la namna gani litakalozalishwa na kundi la watu waliojitoa kwenye tafsiri hiyo?
- Tafsiri hii inatosheleza? Kwa nini na kwa nini siyo?

## B. Mfano # 2

*“Kanisa la mtaa katika Agano Jipya ni kusanyiko lililojitengeneza la waumini waliobatizwa, ambamo uwepo wa kipekee wa Yesu Kristo unakaa; wanaokusanyika mara kwa mara kuabudu, kuelekezana, kushirikiana, kushiriki meza ya Bwana, na kubatiza waumini wapya, chini ya utii wa neno la Mungu, ikisimamiwa na wazee wa kanisa wakisaidiwa na wasaidizi kuweka katika vitendo kutayarisha vipawa ambavyo Mungu amewapa wajumbe wake kujenga kusanyiko la mtaa, litakalopelekea ushuhuda wa injili mitaani na hata dunia nzima.”*

- Ni jinsi gani tafsiri hii inaweza kuendeleza au kurudisha nyuma hatua ya upandaji kanisa?
- Litakuwa ni kanisa la namna gani litakalozalishwa na kundi la watu waliojitoa katika tafsiri hiyo?
- Tafsiri hii inatosheleza? Kwa nini na kwa nini siyo?

## C. Mfano # 3

Mfano wa tafsiri ufuatao ni wa kimapokeo zaidi na unaweza kuwa tafsiri utakayoisikia kutoka kwa wastani wa wasioamini mitaani.

*“Kanisa la mtaa ni jengo ambamo watu hukusanyika kupokea huduma ya kidini kutoka kwa mtumishi mtaalamu ambaye amefundishwa maalumu kuendesha mikutano kila Jumapili asubuhi ikiwa ni pamoja na shughuli nyingine kwa watu kama vile ndoa na misiba.”*

- Ni jinsi gani tafsiri hii itaendeleza au kurudisha nyuma hatua ya upandaji kanisa?
- Litakuwa ni kanisa la namna gani litakaloweza kuzalishwa na kundi la watu waliojitoa kwenye tafsiri hiyo?
- Tafsiri hii inatosheleza? Kwa nini na kwa nini siyo?

## D. Mfano # 4

*“Kanisa la mtaa ni mwili wa waumini waliobatizwa na kujiunda, wakiongozwa na mlishaji anayestahili kiroho, anayethibitisha uhusiano wao kwa Mungu na kwa wao kwa wao kwa kukumbuka mara kwa mara meza ya Bwana, ambaye anawajibika kwa mamlaka ya neno la Mungu, kukusanyika mara kwa mara kuabudu na kujifunza neno, na kuugeukia ulimwengu kushuhudia.”*

- Ni jinsi gani tafsiri hii itaendeleza au kurudisha nyuma hatua za upandaji kanisa?
- Litakuwa ni kanisa la namna gani litakaloweza kuzalishwa na kundi la watu waliojitoa kwenye tafsiri hiyo?
- Tafsiri hii inatosheleza? Kwa nini na kwa nini siyo?

## III. MIPAKA KATIKA KUTAFSIRI KANISA

### A. Epuka Kuamuru Mifumo, Miundo na Vipindi Kwenye Tafsiri ya Kanisa

Kuna kawaida ya kukazia kwenye mifumo na miundo kuliko kwenye kazi kibiblia wakati wa kutafsiri kanisa. Wapanda kanisa wanapofanya hivi, wanaweza kugeuka kuwa kama mafarisayo, kukalia muonekano wa nje wa kiroho na siyo hali halisi ya ndani kiroho ambao ni sura ya moyo sahihi kwa Mungu na uhusiano wa haki kwa wengine, nje na ndani ya kanisa. Mifumo kwa hiyo, inakuwa marejeo ya uongo kwenye hatua ya mafanikio, wakishauri kuwa kanisa la mtaa ni sawa na kama kwaya, katiba, n.k. Wakati hakuna kitu kibaya na vitu hivi, havitafsiri kanisa kama watu wa kiroho.

Wakati mifumo, miundo na vipindi inapokuwa sehemu ya tafsiri ya kanisa, ni kizuizi kizito kwenye uwezo wa kanisa kuwa msukumo wa nguvu ya mabadiliko, kushuhudia kwa jamii inayoendelea kubadilika, upendo wa Mungu unaokoa na usiobadilika. Wakati kazi za kibiblia zinapokuwa viungo muhimu kwenye tafsiri ya kanisa, tunakuwa kwenye ardhi ya mwamba kwa kuunda njia ya mapito ya huduma za kanisa ambazo hakika ni za mafanikio.

## B. Kazia Kazi za Kibiblia Ambazo Kanisa Lazima Lizifanye

Tafsiri inayosaidia zaidi ya kanisa la mtaa inakazia kwenye kazi ya watu wa Mungu kama inavyodhirishwa katika maandiko badala ya mfumo fulani wa utaratibu wa kanisa. Kanisa ni mkusanyiko wa watoto wa Mungu. Uhusiano wa watu wa Mungu kwa Mungu na kwa wao kwa wao ndiyo inatakiwa kuwa kielelezo ambacho vipindi vya mkusanyiko vinatiririka. Kuanza upandaji kanisa ukikazia vipindi inaweza kupelekea muundo ambao haukidhi hitaji la mahusiano. Ni busara kuegemea kwenye mahusiano kibiblia na kuruhusu muundo na utaratibu wa muungano kujiendeleza.

Kwa mfano, mpanda kanisa anayeyakinisha kuwa maombi ya Jumatano muda wa usiku yalikuwa muhimu kwa kila kanisa. Mwanzoni mwa maisha ya kanisa alilopanda, aliweka muda wa usiku Jumatano kuwa wa maombi, lakini kukawa na mvuto mdogo kwa kuwa majukumu ya jamii yaliwafanya wajumbe wengi kuwa na kazi nyingi wakati huo. Hii ilikuwa inakatisha tamaa kwa mpanda kanisa kwa sababu alifafanua kutohudhuria kama kukosekana kwa ari ya maombi. Kwa jinsi hiyo, kama angeruhusu kazi ya maombi kutumia mfumo tofauti, pengine kungekuwa na mwikio mkubwa.

Mpanda kanisa mwingine alikuwa ameshawishika kwamba jengo zuri la kanisa lililopambwa lingekuwa muhimu kwa kuabudu. Baada ya mwaka mmoja wa huduma ya upandaji kanisa, akiwa na watu 15 waliojitoa kwenye kanisa lake, aliamua kuanzisha jengo. Kibali hiki kilichohitajiwa kutoka ngazi ya serikali, kuchangisha fedha, kununua ardhi, kukodi kampuni ya ujenzi, kujenga, n.k. kazi hii ilichukua muda wote wa mpanda kanisa na hivyo akawa tena hana muda kuhudumia wale waumini wake 15 katika zizi lake. Zaidi ya hayo, upatikanaji wa fedha ulionekana kuwa mgumu na serikali ilionekana kufanya juu chini kuchelewesha hatua za ujenzi. Alishangaa kama siku moja ataona kanisa limeanzishwa.

## IV. KUANDIKA TAFSIRI YAKO YA KANISA

Kujiandaa kuanza tafsiri yako ya kanisa, soma vifungu vifuatavyo ukiangalia kanuni zinazoelezea kanisa ni nini. Ziandike kanuni katika nafsi iliyotolewa. Tumia mifano mingine ya Biblia kama unaamini inasaidia.

Mdo 2:42-47

---

Mdo 11:26

---

Mdo 14:23

---

Mdo 20:7

---

Mdo 20:28

---

1Kor 1:2

---

1Kor 12:28

---

1Kor 14:33

---

Efe 1:22

---

Efe 4:11-16

---

Efe 5:27

---

1Tim 3:15

---

Ebr 10:24-27

---

Mingine:

---

Katika nafasi chini andika tafsiri yako ya kanisa

Fikiria maswali yafuatayo kuhusu tafsiri yako

- Tafsiri yako inaeleweka?
- Inaelekeana na maandishi?
- Tafsiri yako inatosha kimsingi kuelezea makanisa yote mahali pote na wakati wote?
- Je tafsiri yako inaruhusu kanisa ambalo ni la kuongezeka?

Shirikisha wengine kuhusu tafsiri yako na kwa uangalifu angalia namna wanavyoichukulia.

### **SULUHU**

Wapanda kanisa wanahitaji kutambua kuwa hawapandi makanisa yaliyokwisha kuendelea, isipokuwa wanapanda mbegu inayokua katika makanisa yaliyokomaa (1Kor 3:6). Waumini wa kwanza kuwa viongozi wanatakiwa kuwa na baadhi ya misemo katika mifumo, miundo, na taratibu. Kwa nini? Ili kwamba kanisa jipya lifae kwenye utamaduni na mahitaji ya hao litakaohudumia.

Kama tunatarajia kushiriki na Mungu katika kuanzisha harakati za upandaji kanisa katika eneo hili, hivyo tafsiri ya kanisa lazima ifanane na 'mbegu' na siyo sawa na 'mti' uliokwisha kua. Inahitaji kukua na kuingia ili iweze kufikia vizuri waliopotea kuizunguka.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni vitu gani halisi visivyohitajika vimeongezwa kwenye tafsiri ya watu inayofanya kazi ya kanisa?
- Ni wakati gani jengo ni muhimu kwa upandaji kanisa? Jinsi gani jengo linaweza kusaidia au kurudisha nyuma ukuaji wa kanisa?
- Kwa nini ni makosa kuegemea mfumo wakati tunapotafsiri kanisa?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Pamoja na timu yako ya upandaji kanisa, anzisha na kubaliana juu ya tafsiri ya kanisa ambayo itakumbusha kanisa lako utaratibu wa upandaji kanisa. Shirikisha tafsiri yako wapanda kanisa wengine, mkufunzi wako au mshauri wako.

### **VYANZO**

- Petersen, Jim. *Church Without Walls*. Colorado Springs, CO: Navpress, 1992.
- Julien, Tom. *The Essence of the Church*. Evangelical Missions Quarterly. Vol. 34, No. 2, 1998.

---

## **TABIA YA KIROHO**

---



# Kuhesabiwa Haki kwa Imani

## MSINGI WA UHUSIANO WETU NA MUNGU

### Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuwafundisha wapanda kanisa jinsi ya kuwekwa huru kutokana na hatia, kujiachilia, na maisha yanayoendana na kutunza hadhi yao, kwa kuwa utakatifu wa Kristo ndiyo msingi wa maisha ya kikristo.

### Wazo Kuu

- Kuhesabiwa haki ni kubadilishana asili yetu na asili ya Mungu.
- Kuhesabiwa haki kwa imani ndiyo msingi wa uhusiano wetu na Mungu.

### Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujua kuhesabiwa haki kuna maana gani
- Kuwa na shukurani ya ndani kabisa na uhakika kuwa neema ya Mungu imesimikwa katika utakatifu wa Yesu Kristo.

## UTANGULIZI

Kama waumini, uhusiano wetu na Mungu ndiyo mwelekeo wa kiini cha maisha yetu. Hakuna chenye maana zaidi kuliko tunavyojihusisha na Mungu na jinsi anavyojihusisha nasi. Lakini katika uhusiano huu tuna maswali mengi:

- Tunawezaje kumjua Mungu kiundani?
- Ni kweli Mungu anatukubali
- Ni wapi kukubaliwa kwetu na Mungu kunatoka?
- Ni jinsi gani tunaweza kuishi maisha yanayompendeza?
- Ni nini kinatokea tunapotenda dhambi?

Kujibu maswali kama haya, tunarudi nyuma mwanzoni—kwenye injili, msingi wa uhusiano wetu na Mungu. Agano Jipya linaelezea wokovu kama swala la “kuhesabiwa haki kwa imani.” Katika somo hili, tutachunguza ina maana gani kuhesabiwa haki kwa imani na namna gani msingi huu, umejengwa juu ya utakatifu wa Yesu Kristo, ndiyo msingi pekee wa uhakika kwa ajili ya uhusiano wetu na Mungu.

## I. KUHESABIWA HAKI SI...

Kwa kifupi imeelezwa, kuhesabiwa haki maana yake kutangaziwa haki. Kuna angalau makosa mawili ambayo watu wanafanya juu ya elimu hii.

### A. Kuhesabiwa Haki si kwa Matendo

Mwana falsafa mkuu Aristotle aliamini kuwa watu **wanaweza kuwa wazuri (na kuhesabiwa haki) kwa matendo**. Wengi wamekubaliana naye. Katika nyakati za Yesu, inaonekana Mafarisayo wangekubaliana na Aristotle. Kwao, namna ya uzuri, kukubalika mbele za Mungu ilikuwa kwa matendo hasa kuishi kufuatana na sheria ya Mungu. Mwana theolojia anayejulikana vizuri Thomas Aquinas alikubaliana na Aristotle; na kwa hiyo mfumo wa wokovu kwa njia ya matendo unabakia kuwa msingi wa jiwe kwa wafuasi wengi wa Aquinas.



Hao wanaoafuata mtazamo wa Aristotle wanaweza kuwekwa katika makundi yafuatayo ya dini. Hapa, tunatafsiri dini kama jaribio la kutaka kumfikia Mungu. Kwa hiyo injili, inafundisha tofauti kabisa juu ya namna tunavyokuwa wazuri. Kufuatana na Biblia, njia pekee ya kuhesabiwa haki ni kupokea wokovu kwa imani uliotolewa kwa kifo na ufufuko wa Yesu. Injili, ikiwemo kuhesabiwa haki kwa imani, inasimama moja kwa moja kupingana na mifumo mingine yote ya kidini jinsi ya kukubalika na Mungu.

#### Jedwali 1.1 Injili na Dini

Injili	Dini
<b>(Jaribio la Mungu la namna ya ajabu kumfikia mwanadamu)</b>	<b>(Jaribio la kawaida la mwanadamu kumfikia Mungu)</b>
Neema	Matendo
Imani	Utii
Upendo usioangalia sababu	Kuhukumiana
Roho Mtakatifu anayebadilisha	Juhudi za mtu
Neema inaongoza kwenye utii	Utii unapelekea neema

Wakristo wanaoamini Biblia wataelewa haraka kwamba injili ni kweli na dini ni uongo. Hatutaki kuweka kuwa badala ya injili, lakini tunashawishika kuzichanganya zote mbili. Lakini tunapochanganya injili na kitu chochote, tunaiharibu (Gal 1:6-7).

Mtu mwingine anaweza kusema kwa haraka, “tunafanya matendo mazuri.” Kweli, lakini hatupokei upendeleo wa Mungu kwa hilo. Badala yake tumepokea upendeleo wa Mungu na kwa hiyo tunafanya matendo mema.

#### B. Kuhesabiwa haki siyo kusikilizwa

Waumini wengi kwa usahihi wanaelewa kuwa kuhesabiwa haki mbele ya Mungu ni kwa imani na si kwa matendo, lakini kwa makosa wanatoa suluhu kwamba kuhesabiwa haki ni msamaha hakika mdogo na katika huo, Mungu anaamua kutoziangalia dhambi zetu. Haya ni makosa makubwa. Mungu hachagui tu kutozijali dhambi zetu. Utakatifu wake unazuia uwezekano huo. Dhambi lazima ilipiwe. Kuhesabiwa haki ni tendo ambalo mtu fulani anatangaziwa utakatifu. Tumetangaziwa utakatifu katika misingi kwamba Yesu alilipa kwa ajili ya dhambi zetu.

## II. KUHESABIWA HAKI NI...

### A. Utakatifu wa Mungu: Warumi 3:21-24

Warumi 3:21-24 ni mojawapo ya vifungu wazi juu ya kuhesabiwa haki kwa imani. Kwa kujifunza fungu dogo baada ya jingine inadhihirisha baadhi ya vipengele vingi kadhaa vya kuhesabiwa haki kwa imani na namna haki ya Kristo ilivyounda misingi wa uhusiano wetu na Mungu.

#### 1. “mbali na sheria”

Haki ya Mungu haipatikani kwa misingi ya utii wetu wa sheria za Mungu. Kwa nini siyo? Kwa sababu hakuna mmoja wetu anayetunza sheria za Mungu kikamilifu—ambacho ndicho Mungu anahitaji kama tungehesabiwa haki kwa utii wetu wa sheria za Mungu (Gal 3:10).

#### 2. “Haki ya Mungu... imedhihirishwa”

Haki ya Mungu inadhihirisha “usafi wake kamili.” Haki kwetu ni kidhihirisho halisi cha usafi huu wa Mungu. Kama tukichukua mazingira katika kadiri na ukweli kwamba kuhesabiwa haki kwa imani kunavyoelezewa hapa, “haki ya mungu” maana yake ni usafi kamili unaotoka kwa Mungu au unaotolewa na Mungu.

3. *"kama ambavyo sheria na manabii wanashuhudia"*

Katika akili ya Waebrania, migawanyo miwili ya kwanza ya Agano Jipya ilikuwa sheria na manabii. Katika yote tunakuta ufunuo wa Mungu ukizungumzia utakatifu huu unaopatikana mbali na utii. Kwa maneno mengine, Biblia nzima inashuhudia kwenye ukweli huu wa kimsingi.

4. *"haki hii inayotoka kwa Mungu inapatikana kwa imani ndani ya Yesu Kristo kwa wote wanaoamini"*

Imani ni njia ambayo tunapatia utakatifu huu. Chanzo cha imani yetu lazima awe Yesu Kristo, kwa sababu ndiye aliyekufa badala yetu, kulipia adhabu ya dhambi zetu. Yeye pekee aliweza kulipia dhambi zetu zote, kwa sababu ni mwana halisi wa Mungu. Hii ndiyo sababu tunatakiwa kuweka imani yetu kwake.

5. *"kwa kuwa hakuna tofauti; wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu"*

Wote kati yetu tunahitaji haki hii kupitia imani ndani ya Yesu Kristo. Hakuna tofauti kwa sababu wote tumetenda dhambi na dhambi zetu zimesababisha kuanguka mbali na ukamilifu wa Mungu unaoonyesha utukufu wake wa kweli.

6. *"Kuhesabiwa haki bure kwa neema yake"*

Haki halisi inayohitajika ili tuwe na haki na Mungu inatolewa na Mungu kwetu tanapoamini. Ni zawadi inayotolewa kwa sababu ya tabia ya Mungu ya neema, siyo kwa sababu tunaistahili. Ni zawadi katika maana ya kweli kwamba, haikutestahilika, haikutegemewa, lakini inakubaliwa.

7. *"Kwa kupitia ukombozi ulioletwa na Yesu Kristo"*

Kwa upendo, Mungu alitaka kugawa zawadi hii ya msamaha na haki kwetu, lakini kwa usafi wake ilihitajiwa kuwe malipo ya dhambi, ambayo ni kifo, yalipwe. Kwa hiyo Yesu alikuja na kufa badala yetu, na kulipia adhabu yetu. Matokeo yake, alikamilisha utakatifu uliohitajika na Mungu kutusamehe na kututangazia kuwa na haki machoni pake. Ukombozi kutoka dhambini ilikuwa ni gharama iliyolipwa kununua kuhesabiwa haki kwetu.


## B. Mabadilishano Makuu

Kwa ufupisho, kuhesabiwa haki ni **tendo la neema la Mungu lililosababisha mabadilishano makubwa kutokea**. Mwenye dhambi anapomkaribia Mungu katika toba na imani, Mungu anaondoa hatia yake ya dhambi na kumwekea Yesu. Pia anachukua utakatifu kamili wa Yesu na kumpatia muumini mpya. Matokeo yake ni kwamba dhambi za muumini mpya zimesamehewa kabisa na anapokea kutoka kwa Yesu haki halisi inayohitajika kusimama mtakatifu mbele za Mungu (2Kor 5:21; Isa 61:10; Rum 4:3-5; 8:1; Efe 4:22-24).

Ufunuo 20:12 inazungumzia siku Mungu atakayofungua kitabu ambacho kina kumbukumbu za maisha yetu na atatuhukumu kulingana na matendo yetu. Unadhani ni kitu gani tutakuta katika vitabu vyetu? Nabii Isaya anaelezea kuwa chini ya hukumu ya Mungu mtakatifu, "kila mmoja wetu amekuwa kama ambaye si safi, na matendo yetu ya haki ni kama kitambaa najisi (Isa 64:6). Watu wengi watashangaa kugundua kuwa vitabu vyao vina mlolongo mkubwa wa dhambi. Kwa hiyo, tunapoangalia maisha ya Yesu, tunaona kuwa alikuwa mtiifu kikamilifu kwa Mungu kwa kuwa aliishi maisha ya utakatifu bila kufanya dhambi (Ebr 4:15).

Tunapoungama dhambi zetu na kukubali, kwa imani, Yesu Kristo kama Bwana na mwokozi, Mungu anachukua dhambi zetu na kuziweka juu ya Yesu. Na kisha anachukua haki ya Kristo na kutupatia. Matokeo yake ni kwamba kumbukumbu ya dhambi zetu iliwekwa juu ya Kristo, na kumbukumbu ya utakatifu wa Yesu ilitolewa kwetu. **Kuhesabiwa haki kunaweza kupimwa kama mabadilishano ya "kumbukumbu zetu za dhambi" na "kumbukumbu za utakatifu wa Yesu Kristo."**

Kielelezo cha Mabadilishano Makubwa (Kielelezo 1.2) kinatusaidia kuelewa kuhesabiwa haki kwa imani.



### III. MASWALA NYETI YA KUHEMBAWA HAKI KWA IMANI

#### A. Hatuwezi Kujihesabia Haki Wenyewe

Kuchunguza sura hizi za ufunguo za kuhesabiwa haki kwa ujumla, kuna ukweli muhimu uliozushwa katika mawazo haya. Tunapoambiwa kwamba kuhesabiwa haki ni haki ni inayotolewa mbali na utii wetu wa sheria, kwamba kunakotolewa kwa imani ndani ya Yesu Kristo, kwamba kunakotolewa kwa wenye dhambi kwa neema ya Mungu, na kwamba kunalipiwa kwa ukombozi wa Kristo... mawazo haya yote yanaeleza ukweli kwamba mwanadamu hahusiki na haki hii.

Kuelezea asili ya kweli ya kuhesabiwa haki, Martin Luther kwa ufasaha ameleza kama **“haki ya kutofanyia kazi”**, kwa sababu hatushiriki kuitoa. Yesu aliifanyia kazi haki hii kwa ajili yetu na tunaweza kuipokea tu kwa imani. Ukweli huu ni msingi wa mwanadamu **kuhesabiwa haki mbele ya Mungu na hapa ndipo ukristo unatofautiana na dini zingine, pamoja na mifumo ya kikristo ya uongo**. Na hapa ndipo tunaona ugumu sisi wenyewe, kwa sababu kuhesabiwa haki kwa imani kunatueleza kiwango cha kweli cha dhambi zetu na kuhitaji kwetu kwa neema isiyo na mwisho. Kunatuambia kwamba, kuwa wenye haki mbele za Mungu, ni lazima tuangalie nje wenyewe kwa sababu hatuna haki, na ni lazima kwa unyenyekevu tukubali njia pekee ambayo tunaweza kukubaliwa na Mungu njia ya imani katika Yesu Kristo.

Hili ni swala la ufunguo juu ya kuhesabiwa haki kwa imani, kama tunafikiri tunaweza kusimama wenye haki mbele za Mungu kwa njia nyingine tofauti na kutolewa kwa Yesu, kisha tunahesabu kimakosa na vibaya sana utakatifu wa kweli wa Mungu na undani wa ukweli wa kuwa wenye dhambi. Tunawezaje kudhani kuwa tunafaa wenyewe kuwa na amani na Mungu mtakatifu na mkamilifu? Hiki ni kiburi kibaya zaidi cha majivuno kwa sababu kinamshusha Mungu mpaka kwenye ngazi ya mtu mwenye dhambi na kumwinua mwanadamu aliyeharibika mpaka kwenye ngazi ya Mungu mkamilifu.

#### B. Hatuwezi Kuchukua Sifa Kwa Kile Mungu alichofanya

Kwa kutoa maisha yake, Yesu alilipa adhabu ya wavunja sheria wote. Kwa sababu ya Yesu ni nani, tunaweza kumwamini Mungu kututakasa. Kutokuamini kikamilifu katika kifo cha Yesu Kristo msalabani kama msingi wa msamaha na uhusiano wetu na Mungu ni kumtukana Mungu kusema hana maana.

**Mfano:**

Fikiria mtu aliyefanya uharibifu mbaya, na anasubiri adhabu ya kifo. Anapokuwa anasubiri, mmojawapo wa rafiki zake akaenda kwa jaji kumuomba msamaha. Jaji akajibu, “nitamwachilia, kama utanipa mtoto wako kufa badala yake.” Rafiki akasema, huu ni upuuzi. Nitawezaje kufanya hivi? Lakini jaji akasema, “Hii ni njia pekee nitakayoweza kumwachilia.” Baada ya maumivu makuu, baba akaamua atamtoa sadaka mwanawe kwa ajili ya rafiki... akijua hiyo ndiyo njia pekee. Kwa utii, mtoto akaenda kwa jaji na kukubali kufa badala ya rafiki yake na baba yake. Siku inayofuata jaji akamhukumu mtoto na kumwacha huru yule mtu muhalifu.

Mara tu baada ya hili, baba akasikia vibaya mazungumzo kati ya mfungwa aliyeachiliwa na rafiki. Alipouliza, “Ni namna gani uliwekwa huru dhidi ya adhabu yako ya kifo?” mtu aliyeachiliwa akajibu, “Kweli, nilipokuwa gerezani nilijitunza nakuwa msafi, nikaonyesha tabia njema, na kufanya kile mlinzi alichotaka. Kisha wakaniruhusu kutoka kwa sababu ya tabia yangu nzuri.”

Unafikiri ni namna gani mtu huyu alijibu kwa kile alichosema rafiki yake? Inakuwaje mtu huyu aweze kufikiri kuwa tabia yake nzuri ndiyo iliyochangia kutolewa kwake gerezani baada ya kutoa mtoto kwa ajili yake?

Siyo kwa sababu ya tabia yetu, au ukubwa wa toba yetu, kwamba ndiyo Mungu anatusameha dhambi zetu. Hata kama neno la Mungu linafundisha kuwa imani ya kweli itaonyeshwa na upendo na utii tulionao kwa Mungu, tunatakiwa tusichanganye hili na ukweli kwamba Mungu amesamehe dhambi zetu kipekee kwa sababu ni mwenye upendo na neema, kutoa mtoto wake wa pekee msalabani badala yetu. Yesu amelipa adhabu kwa ajili ya dhambi zetu, na ni kujitua sadaka kulikonunua uhuru wetu kutoka kwenye gadhabu ya Mungu.

**C. Ni Lazima Tumtumaini Mungu Kikamilifu**

Wanaoamini katika dini, na kwa hiyo kuhesabiwa haki kwa matendo, wanajenga uhusiano wao na Mungu kutokana na utii wao kwake. Tatizo hapa kisha ni, dhamiri zao zinaendelea kuwambia kuwa hawafanyi vizuri katika kumtii yeye, na kwa hiyo kuwathibitishia hatia kuwa hawana haki ya kuamini kuwa Mungu huachilia dhambi zao au kuzisamehe kwa haki. Hii inaleta msukosuko, ambao pengine wanafikia uamzi kuwa siyo wabaya sana (kufunga dhamiri zao), au kwamba kama wakifanya kitu kinachomfurahisha Mungu, Mungu ataachilia dhambi zao (--haki ya kweli ya Mungu).

Hata wakristo wanakutana na tatizo hili. Dhamiri zetu zinatambia hatufanyi vizuri kumpendeza Mungu. **Katika hatua hii, tunashawishika kugeukia tiba ya uongo kuliwaza dhamiri zetu na kutatua tatizo la dhambi.** Wakati mwingine tunajaribu kuliwaza dhamiri zetu kwa kufikiri kuwa hatuko wabaya kama mwingine alivyo; na kwa hiyo hatuwezi tukawa wabaya sana. Au tunatafuta kufanya vizuri zaidi, kujaribu kurekebisha kushindwa kwetu. Hili ni kosa la kijanja kwa sababu kunuia kumtii Mungu vizuri zaidi siyo vibaya. Lakini tunachoelekea kufanya ni chanzo cha uhusiano wetu na Mungu kwa matendo yetu, kutokana na dini na siyo na injili. Tunafanya kosa la kiujuzi tunapobadilisha msingi wa tumaini letu katika wokovu kutoka kwenye kazi ya Yesu Kristo msalabani, na kuweka katika matendo yetu na utii. Mawazo haya mabaya yanaweza kutusababisha kutoona hali yetu ya dhambi au kukatishwa tamaa na hata kutudhoofisha.

**SULUHU**

Tunapokuwa tunaishi maisha ya kikristo, hatuwezi kuhamisha imani yetu kutoka kwenye msamaha na haki tuliyopatiwa na Yesu Kristo. Kifo cha Yesu msalabani kililipia adhabu na kuturuhusu kusimama mbele ya Mungu tukiwa wenye haki. Kuhesabiwa haki kwa imani lazima kubaki kuwa msingi wetu wa uhusiano wetu na Mungu. Msalaba ndiyo tumaini letu pekee la amani yetu na Mungu. Hakuna sehemu nyingine ambayo wenye dhambi, hata wenye dhambi waliohesabiwa haki, wanaweza kumuona Mungu isipokuwa kwa njia ya msalaba.

Kujenga maisha yetu juu ya kuhesabiwa haki kwa imani katika Yesu Kristo kunakiwa kutuweka huru kumtumikia Mungu katika namna ya kiujasiri, siyo kwa sababu tunamtii Mungu kikamilifu mara nyingi, lakini kwa sababu tuna ujasiri kwamba uhusiano wetu na Mungu umejengwa juu ya kazi Yesu aliyofanya kwa ajili yetu. Kuhesabiwa haki siyo tu swala la juhudi zetu—lakini badala yake ni kwa neema kwa njia ya imani. Kuhesabiwa haki kwa imani kunaweka neema mbele ya utii wetu, ambayo ni njia Mungu anayohusiana nasi katika Yesu. Tunapojifunza kuwa uhusiano wetu na Mungu wakati wote umekuwa na utazidi kuwa –kujengwa juu ya neema yake, na tunapotumaini katika kazi iliyokamilika ya mtoto wake, tunatambua jinsi hakika upendo wake ulivyo. Tumeokolewa kwa neema, na tunaweza kuishi kwa neema.

#### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Unaweza kwa kifupi, lakini kiuwazi, kutafsiri kuhesabiwa haki kwa imani?
- Ina maana gani tunapoeleza kuhesabiwa haki kwa imani kama “haki ya kutofanyia kazi”?
- Katika kutembea kwetu kila siku na Bwana, kwa nini inakuwa vigumu sana kwetu tulioanza kwa neema kuendelea kwa neema, kutumaini kazi ya Yesu Kristo iliyomalizika msalabani?
- Ni jinsi gani kuhesabiwa haki kwa imani kunagusa jinsi unavyohusiana na Mungu na namna Mungu anavyohusiana nawe?

#### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Mfundishe mtu mwingine maana ya kuhesabiwa haki kwa imani, na kisha mwambie kuandika tafsiri yake mwenyewe. Leta walichoandika wakati wa kipindi kingine.



## Kuishi kwa Injili

### KUKATAA KUJITUMAINIA

---

#### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kusaidia mpanda kanisa kuona umuhimu wa imani iliyojengwa katika Yesu kama njia ya kukua kiroho.

#### ☞ Wazo Kuu

- Injili ni kiini katika kukua kiroho kwa mtu
- Lazima tukatae kujitegemea wenyewe katika ukuaji katika Kristo na mafanikio yetu katika huduma.

#### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mpanda kanisa anatakiwa:

- Kujua jinsi kuielewa injili kunavyochangia ukuaji unaoendelea wa kikristo.
- Kutambua zaidi uhitaji wake wa Kristo na kukua kwa unyenyekevu wa kumtegemea yeye.
- Kuelewa tofauti ya kuishi kwa nguvu zake na kuishi kwa imani ndani ya Kristo na kazi yake aliyoimaliza msalabani.

### UTANGULIZI

Wakristo wengi wanaelewa wazi kuwa kuhesabiwa kwetu haki mbele za Mungu ni kwa imani peke yake. Lakin usemi huo una maana gani katika maisha yetu kutoka katika hatua hiyo na kuendelea? Injili inatakiwa kuwa na maana gani kwa hao walioipokea muda mrefu? Wakristo wengi wanachanganyikiwa katika vipengele hivi. Wengi wanafikiria mawazo yanayohusiana na wokovu kama vile kuhesabiwa haki kwa imani kuwa na thamani ndogo mara mtu anapokuwa mkristo wa siku nyingi. Wanaweza hata kushawishiwa kubadilisha mafundisho haya muhimu katika namna inayotukua utunzaji wa kanuni na kujitumainia. Katika somo hili, tutavumbua jinsi injili inavyowachoma hata wakristo waliokomaa huku wakitazama katika maonyo ya Biblia dhidi ya kuibadili injili kwa chochote.

#### I. VIPINGAMIZI KUTOKA KWENYE INJILI

Mojawapo ya nyaraka za mwanzoni alizoandika Paulo ilikuwa kwa kanisa alilopanda katika safari yake ya kwanza ya kimishenari katika eneo la Galatia. Wakristo hawa walikuwa wamechanganyikiwa juu ya jinsi walivyokuwa wenye haki mbele za Mungu, na vilevile jinsi watavyokua kama wakristo, na pia kujulikana kama waliohesabiwa haki. Kwa kuongeza, walikuwa wamepoteza maana ya furaha katika Kristo (Gal 4:15), na walikuwa wakishambuliana wao kwa wao (Gal 5:15).

Yamkini Paulo alikuwa amechukia juu ya hali ya makanisa mapya yaliyopandwa. Paulo aliwasomea barua ikiwa na maonyo makali juu ya kilichotokea. Anasema, "Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi... kugeukia injili ya namna nyingine: (Gal 1:6-7). Baadaye, Paulo anashangaa kama amepoteza muda kwa ajili yao (Gal 4:11). Katika kuchanganyikiwa kwa Paulo, hata anawaita wagalatia "wajinga" (Gal 3:1,3).

Paulo alielewa kuwa Wagalatia wameacha kuishi kwa kumtegemea Kristo. Anasema kuwa wamegeuka kuwa "waliorogwa" (Gal3:1). Neno hili linaeleza wazo la "kufanyiwa uchawi" na kitu fulani. Walikuwa wameshaongozwa kuamini kuwa walikuwa wameshahesabiwa haki kwa kuzitii sheria. Wameugeza ukristo katika hatua ya utendaji badala ya kuishi kwa kumtegemea Kristo (Gal 4:10-11). Wameshaanza kutafuta kibali cha Mungu kwa kutii sheria na siyo kwa injili (Gal

3:1-5). Kwa kufanya hivyo, walikuwa wakijiondoa wenyewe kutoka kwenye chanzo chao cha kweli cha nguvu. Wamekwishavutwa mbali kutoka kwa Kristo.

Hii ilikuwa ndiyo sababu Paulo aliwaonya wakristo wa Galatia. Walikuwa wamechanganyikiwa jinsi kukua kulivyotokea katika maisha yao. Waligeuka kuwa “waliorogwa” na kanuni na kawaida za maisha ya dini na mtazamo wao ukatoka nje ya Yesu na kujiangalia wenyewe. Wamekwisha kugeukia kwenye kupata haki kwa matendo mema, ambayo hasa ni kujitumainia, na hivyo hawakuelewa kuhitaji Yesu kunakoendelea.

## II. HATARI YA KUJITUMAINIA

Kama wagalatia, tunaweza kuvutwa mbali kutoka kwa Kristo na msalaba. Maisha yetu mara nyingi yanaashiria kukosa kumtegemea Kristo yakiungwa na makadirio ya chini ya nguvu ya dhambi. Kwa mfano, tunaweza kugeuzia maisha ya ukristo kwenye matendo. Tunahudhuria kila ibada zote zilizoelzwa za wiki na kutoka, kila kitu kinaonekana kuwa kizuri, angalau mbele ya wengine. Lakini hata kama tunashiriki katika shughuli hizi, tunaweza kuchoshwa na mahubiri ya neno la Mungu na ibada yetu inaweza kuwa tu ya mdomoni. Na ndani kuna imani kidogo na upendo juu ya Mungu, lakini kinachoashiria hasa ni kwamba hatutambui kabisa kama mabadiliko haya yanatokea.

Hii ilikuwa ni hila na hatari mbaya ambayo Paulo alikabili moja kwa moja kwa Wagalatia 3. Ni ya kufisha, kwa sababu maisha yetu yanakuwa upande wa nje ya ukristo ambapo tunajali tu kuhusu kuonekana nje wakati ndani tunakufa. Ni kama mtu mwenye kansa na hajui kama anayo, na kiini cha kansa kinasambaa na kua kila kitu kinachokutana nacho. Na siku moja atianza kujisikia vibaya na kwenda kwa daktari na kuambiwa kuwa ameshachelewa.

Mfano mwingine ni wa mawazo mabaya kuwa tunaweza kushinda dhambi kwa nguvu zetu wenyewe. Kwa mfano, mtu anadhani anaweza kujifurahisha kwa haja za kitamaa moyoni mwake. Hata hivyo, anajiambia mwenyewe, haja hazionyeshi tabia.” Anajishawishi mwenyewe kuwa tamaa ni kosa dogo analoweza ... siyo kama umalaya, dhambi ambayo hataweza kufanya. Anaamini kuwa ameshinda dhambi maishani mwake, lakini hali halisi ni kwamba anaendelea dhambi, dhambi yoyote, inamtenganisha kutoka kwenye ukaribu wake na Mungu. Katika Mathayo 5:8, Yesu waziwazi anaeleza, “lakini mimi nawaambia, kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.”

Kama kanisa, dhambi ni ugonjwa wa kufisha. Tunatakiwa tusiwe wajinga na kudhani tunaweza kutojali ugonjwa huu au kuushinda kwa juhudi zetu wenyewe au kwa kuukabili kwa nje kwa amri tunazopata katika Biblia. Kama tukiendelea kutegemea njia hizi dhaifu kushinda dhambi, itatua.

## III. UKATI WA INJILI KWA MTU BINAFSI KUKUA KIROHO

Kwa kushindwa kwetu kuishi maisha ya kikristo kwa nguvu zetu ndipo tunapogundua udhaifu wetu na umuhimu wa kuisha kwa imani. Mara kadhaa katika Wagalatia 3:2-5, Yesu anatumia kiwakilisha “je” kuelezea njia ambayo kitu fulani kinapatikana. Kwanza, anahusisha na mwanzo wa maisha ya ukristo na ahadi za Roho Mtakatifu, na anauliza, “je mlipokea roho kwa matendo ya sheria, au kwa kusikia kunakotokana na imani?” (Gal 3:2). Kwa maneno mengine, ni kwa namna gani tumepokea roho? Namna gani maisha yetu ya kikristo yalianza? Kufuatana na Paulo, “ilikuwa kwa imani” katika injili (Gal 3:8). Anaendelea kusema juu ya namna gani wakristo wanakua, pia amehesabu kama mafundisho ya “kuhesabiwa haki.” Anauliza, baada ya kuanza katika roho, mnataka kukamilishwa sasa kwa juhudi za kibinadamu?” (Gal 3:3). Kwa maneno mengine, kama hatukuweza kuanza kazi wenyewe lakini tukamwamini Mungu na kutumainia katika kazi ya Roho Mtakatifu, kwa nini sasa tunafikiri kuwa tunaweza kazi kwa ukamilifu kwa juhudi zetu wenyewe? Kisha akauliza swali kali la mwisho, Basi, yeye awapaye roho na kufanya miujiza kati yenu, je afanya hayo kwa matendo ya sheria, au kwa kusikia kunakotokana na imani? (Gal3:5). Lazima tufikirie juu ya swali hili la mwisho kwa makini, kwa sababu waziwazi Biblia inafundisha kwamba kwa utii wetu tunashuhudia baraka za Mungu.

Gundua tofauti Paulo anayofanya. Anatofutisha utii na imani kama njia Mungu anazotumia kutenda kazi. Hatukuokolewa kwa utii, lakini kwa neema kwa njia ya imani. Zaidi ya hayo, siyo tu kwamba imani ni njia tuliyohesabiwa haki; ni njia tunayotakaswa. Tunakua katika imani kwa injili na tunapokubali Kristo alichokamilisha kwa ajili yetu na ndani yetu kwa imani. Katika yote, kuhesabiwa haki na kutakaswa tumeitiwa kuishi kwa imani.

Kutumainia katika njia zetu pengine ni njia bora ya matendo ya kueleza kutokuamini kwetu, lakini tumeitwa tuache kuendelea kutumainia njia zetu na kuishi kwa imani. Mungu ametuita tuachane na kutafuta haki wenyewe. Hatuna utakatifu isipokuwa uliotolewa kwetu kwa kuungana kwetu na Kristo. Imani ya unyenyekevu inakubali mahitaji yetu na kuangalia nje yetu kwa Kristo na kupokea msamaha na haki kamili anayoweza kutoa.

**Mfano:**

Kipindi wakati Uprotestanti unaanza, Luther na Erasmus walikuwa wakijadili juu ya nini ufafanuzi mzuri wa wokovu wetu na kuhitaji kwetu kwa neema. Erasmus alikubali kuwa dhambi imemfanya mtu kuwa mgonjwa, lakini aliendelea kusema kwamba kuhitaji kwetu kwa imani ni zaidi kama mtoto mchanga anayejifunza kutembea. Mtu anaweza kuchukua hatua fulani kuelekea kwa Mungu, lakini wakati mwingine pia anahitaji baba yake wa mbinguni kumsaidia pamoja naye. Luther alikuwa amesukumwa nyuma na hitaji dogo kama hilo la neema na kumwambia Erasmus kwamba alikuwa na uhakika ni makosa. Alisema kuwa wokovu wetu zaidi ni kama kipepeo anayetambaa ambaye amezungukwa na kengele ya moto kote. Isipokuwa mtu aende chini na kumwoko kipepeo, vinginevyo atakufa.

Hitaji letu la neema katika wokovu ni halisi. Utakatifu kamili wa Mungu unataka usawa kwa mwanadamu aliyejaa dhambi. Ni lazima tuachane na tumaini lolote katika utakatifu wetu wenyewe na kumwegemea Yesu Kristo au hakika tutakufa. Mungu lazima atuokoe kama kipepeo. Lakini Mungu pia anatuitia hili la kuachana na kujihesabia haki. Tunatakiwa kuendelea kuuendea ukweli wa injili na kutafuta haki yetu katika Kristo kama tutamkaribia Mungu. Utakatifu wake utaendelea kuzionyesha dhambi zetu mpaka kwenye kiini, na kama hatuamini kuwa tunasimama mbele ya Mungu tukiwa sawa kwa sababu ya imani yetu peke yake katika haki ya Kristo inayotolewa kwetu, tutatekwa na utakatifu wa Mungu. Na kama tunafikiri kuwa tunaweza kutibu ugonjwa huu wa dhambi ndani yetu kwa nguvu zetu, tumedanganyika katika kupima nguvu ya dhambi. Imani ni kuachana na njia zetu wenyewe, kwa sababu tunaona huzuni ya unyonge wetu. Tunaposikia hitaji letu kubwa, imani inamshika Kristo na fadhili anazoweza kutoa kwetu peke yake. Kadiri tunavyokua katika imani, ndivyo tunavyohitaji kujiunga kwa Yesu na kutafuta nguvu na uweza ambao peke yake anaweza kutoa.

#### IV. UKATI WA INJILI KATIKA HUDUMA

Hii inahusikaje kwenye njia Mungu anazojihusisha kwako kwa namna ya huduma kwa wengine? Waumini wengi wanaishi na wazo la kwamba matokeo ya huduma yao yanategemeana na kufanya kwao vizuri au kiasi gani cha upendeleo wa Mungu kiko juu yao kwa kipindi maalumu. Sababu za huduma kufaulu au kushindwa ni nyingi. Lakini kwa namna Mungu anavyotupenda na kwa sababu ya asili ya injili, mafanikio katika huduma yanategemea nguvu ya Mungu kuliko utendaji wetu.

Kama mfano, ngoja tulinganishe siku mbili katika maisha yako. Jumapili moja unaamka na kwenda kwenye mkutano wa maombi kama ilivyo kawaida yako. Njiani ukienda, umekuwa na mazungumzo mafupi na jirani yako lakini yakuridhisha. Unaendelea kwenda kuwa na siku njema ambayo uwepo wa Mungu ni wazi kwa namna nyingi. Njiani ukirudi nyumbani, umepata nafasi ya kumshirikisha injili mtu, na hivyo unamshirikisha habari za Yesu na wokovu wake. Jumamosi inayofuata inakuwa tofauti kidogo. Unaamka umechelewa, unakosa mkutano wa maombi, na kuongea kwa ukaidi na jirani yako njiani wakati unatoka. Kwa ujumla, siku inakuwa imejawa na kuchanganyikiwa na Mungu anaonekana kutokuwa karibu. Unaanza kujisikia vibaya juu ya uliyofanya, lakini kwa ajabu yako, unapata nafasi nyingine ya kumshirikisha mtu injili. Swali ni kwamba, utaicha nafasi hiyo kwa sababu unajikia kama hustahili kumshirikisha injili mtu huyo? Unafikiri inawezekana Mungu kukubariki unapokuwa na siku mbaya? Kama siyo, kwa nini siyo?

Siku zetu mbaya zaidi hazitaweza kuwa mbaya kiasi kwamba tunakuwa nje ya neema ya Mungu, na siku zetu njema hazitaweza kamwe kuwa nzuri kwamba hatuhitaji neema ya Mungu.



Mara nyingi tunafikiri kwamba wakati tukiwa tumeokolewa kwa neema, labda tunapokea au kupoteza baraka za Mungu kuzingatia utendaji wetu. Lakini ni lazima tuelewe kwamba kama kuhesabiwa haki kwa imani katika Yesu Kristo ndio msingi wetu wa uhusiano na Mungu, siku zetu mbaya zadi hazitaweza kuwa mbaya kiasi hicho kwamba tunakuwa nje ya neema ya Mungu, na siku zetu njema hazitaweza kamwe kuwa nzuri kwamba hatuhitaji neema ya Mungu. Wakati wote tunahitaji neema.

## V. KUJIFUNZA KUSIMIKA MIZIZI YETU YA IMANI KATIKA KRISTO

Suluhu ya mungu juu ya kutoweza kwetu kumpendeza kwa nguvu zetu siyo kwamba tunajitahidi kwa nguvu. Suluhu yake ni kwamba tunaamini kwa nguvu ukweli huo wa injili. Kwa kuuamini ukweli huo, tunaanza kuweka mizizi ya maisha yetu ndani ya Kristo.

Mara nyingi, tunapokutana na vipingamizi katika maisha au ugumu fulani wa majukumu, tunaanza kufanya maarifa na kufikiri njia ambazo tunaweza kukamilisha kazi. Usumbufu wote hapa ni kwa uwezo wetu.

Nini kinachotokea kwetu tunapokuwa tumeshangazwa siku moja na ukweli wa hali yetu ya mioyo ya dhambi? Hata kama tunaweza kupenda kuwa dhambi zetu ziendele kufichika, Mungu anafanya kazi kuzifunua dhambi zetu. Sasa na baadaye, hata tunashitushwa na wingi wa dhambi zetu. Tunafanya nini hii inapotokea? Tunaweza tukataka kuungama ungamo kadhaa. Au tunaweza kuanza kujichukia wenyewe kwa sababu ya hali yetu ya dhambi. Siyo mpaka tunapokuwa tumeteseka kwa muda tunakwenda kwa Mungu na kuungama dhambi zetu kwake.

Unaona kinachotokea? Tuko tunalipia dhambi zetu kwa mateso. Hii ni kanuni dhidi ya ungamo. Tunajaribu kijifanya kana kwamba tunastahili msamaha wa Mungu. Tunapofanya hivi, tunakimbilia njia zetu.

### **Mfano:**

Tarehe 21, mwezi wa nane 1544, Martin Luther alimwandikia rafiki mmojawapo mwaminifu na wa kutumainiwa, George Spalatin. Spalatin alikuwa ameshampa ushauri ambao baadaye alikuja kuuona kama dhambi. Alipofikia suluhu hili, alikuwa amezama katika uchungu na hatia. Alikuwa ameshawishika kwamba angelijua vizuri zaidi na kwamba yeye wa watu wote asingelifanya kosa hilo. Hakuweza kushauriwa, Wakati Luther alipojua juu ya hali yake, alimwandikia kumfariji, kwa kusema, "...ombi langu la uaminifu na onyo la upole ni kwamba uungane na kampuni yetu na ushirikiane nasi, tulio halisi, wenye nguvu na waliojaa dhambi. Ni lazima kwa njia yoyote usimfanye Yesu kuonekana kuwa mnyonge na hafifu kwetu, kana kwamba anahitaji kuwa msaidizi wetu wakati tu tunataka kuepukana na kivuli cha kuwazika, majina, na dhambi za kitoto. Hapana! Hapana! Hiyo haitakuwa nzuri kwetu. Ni lazima afadhali awe mwokozi na mkombozi wa uhakika, mkuu, mzito, anayehukumu uovu na uasi, mwenyezi, na kutoka katika dhambi kuu zaidi na za kutisha kupindukia, kuwa na machache, kutoka kwenye dhambi zilizowekwa pamoja katika jumala..." Kutoka: Martin Luther Mwandamizi kwa Wakristo wa Wakati ule.

Tumekuwa wenye dhambi wadogo tunaohitaji tu mwokozi mdogo au ni wenye dhambi halisi tunaohitaji mwokozi halisi? Imani inatuunganisha na Yesu, na kuungana na Yesu ina maana kwamba tumejiengua kwenye vitu vingine vyote. Hatuwezi tukaongeza kwa kile Kristo alichofanya kwa ajili yetu. Kama mtu mmoja alivyosema, "Chochote tunachoongeza kwa alichofanya Yesu kinatia unajisi. Inakuwa kama harufu ya mnyama mdogo atoaye harufu ya uvundo wakati mzuri wa jua kuchwa. Ungependa uwe pale lakini hutataka kuwa pale."

Hii hasa ni kweli kwa wale tunaishi nao na wanaouona usisi. Kama tunajaribu kuongeza haki yetu kwa ya Kristo, tunakuwa wa kujihesabia haki na tusio wavumilivu kwa wengine. Kama tunaishi kwa nguvu zetu wenyewe, uhusiano wetu ni wa kujihudumia. Kamwe hatutabadilika.

## **SULUHU**

Injili lazima ibakie kuwa kiini katika kutembea kwetu na Kristo. Kuibadilisha injili na taratibu zingine za kuhesabiwa haki kunaharibu thamani ya wokovu wetu. Yesu Kristo alichomaliza msalabani kinawafaidisha wale tu wanaoachana na taratibu zingine za kuhesabiwa haki na kuwa wanaume na wanawake wenye imani iliyosimikwa katika Kristo. Kuhamisha ujasiri wetu kutoka kwa alichokamilisha Kristo kwenda tulichokamilisha sisi na kutawala ulinzi au kitu chochote, kunazalisha haki ya uongo.

Tatizo letu ni kwamba mara nyingi hatuwezi tukagundua hitaji letu. Panapokuwa hakuna utambuzi wa hitaji, hakuna imani. Na panapokuwa hapana imani, hapana uhusiano wa nguvu na Yesu, na maisha yake ndani yetu yanaanza kuyeyuka. Kukua kwetu kunakuja tunapojifunza kuachana na nguvu zetu wenyewe na kuanza kutembea kwa imani iliyojengwa katika Kristo. Ndipo tunapogundua Mungu anachotaka tuone: kwamba tunamhitaji Kristo zaidi kuliko tunavyodhania. Ni kupitia hitaji letu la Kristo kwamba Mungu anachochea imani zetu.

## **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni jinsi gani waumini wa Galatia wameanguka kutoka kwenye injili?
- Je, unapoteza furaha yako katika Kristo? Na kama ndiyo, kwa nini?
- Ni jinsi gani injili inatuhusu kama waumini?
- Nini tofauti kati ya juhudi za pekee na imani?
- Ni jinsi gani kuishi kwa imani kunagusa mawazo yetu ya kila siku na matendo katika maisha?



# Kukua Kwa Mkristo

## KUMFANYA KRISTO KUWA KIELELEZO CHA MAISHA YA MKRISTO

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuona msalaba unakuwa dira ya maisha yetu kama tunahitaji kukua kweli.

### ☞ Wazo Kuu

- Kuna kutokuelewa kwingi juu ya kukua kiroho
- Msalaba unasimamia nafasi kubwa katika kukua kiroho.
- Kutokuelewa kwetu kunarudisha nyuma ukuaji.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Awe mkristo anayetukuka katika Kristo.
- Kujua kuwa ili kukua, lazima aelekee msalaba—kuhusisha maisha yote kwenye kazi ya Kristo.
- Kuweka matumaini yake chini ya miguu ya Kristo na , kwa imani, kudai uweza ambao mwokozi aliyefufuka anaweza kutoa.

## UTANGULIZI

Katika tabia ya mkondo huu wa kiroho, tunatafuta kujenga msingi wa nguvu wa maisha ya kikiristo. Eneo hili nyeti linahitaji kwa ujumla uangalifu kama tunavyoona viongozi wa kanisa wanageuka kuwa kama meli iliyovunjika kwa sababu ya dhambi moja au nyingine. Ni kwa jinsi gani tunaweza kujilinda tusiwe kama meli iliyovunjika? Jinsi gani upendo wetu kwa Mungu utakua na kuwa wenye nguvu na usiwe baridi? Ni jinsi gani tutakua katika imani zetu, ili kwamba tuwe hai, uhusiano hai na Yesu Kristo?

Tungependa kuonyesha picha ya jinsi mkristo anavyokua na kuwa na upendo mkuu kwa Mungu na kuishi kwa imani kunakomwezesha yeye kuendesha kanisa la Yesu Kristo kiroho. Hasahasa, tutajifunza jinsi ya kufanya msalaba wa Yesu Kristo kuwa dira ya maisha ya kiroho.

## I. NI NINI MAANA YA UKUAJI KIROHO

**Kukua kiroho ni kazi ya Mungu inayoendelea katika maisha ya muumini, ya kumfanya yeye kuwa mtakatifu hasa.** Neno utakatifu hapa lina maana “kuchukua mfano halisi wa Mungu.” Tunapokua, kama wakristo, hali yetu ya uadilifu inaletwa katika kuhakikishwa kwa nafasi yetu halali mbele za Mungu (kama waumini, tumetangaziwa haki). Kukua kiroho ni mwendelezo wa kilichofanyika katika wokovu, wakati maisha mapya yanapotolewa kwa muumini na kuwekwa ndani ya muumini.


Gundua pande mbalimbali za ukuaji wetu. Roho Mtakatifu anatumia ili kwamba tuweze kubadilishwa katika sura ya Mungu. Lakini mabadiliko haya ni hatua inayoendelea, na hatua hii inasonga mbele kwa ushirikiano wa Mungu na wakristo. Tumeambiwa katika Wafilipi 2:12-13, “utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka, kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yangu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema.” Hapa tunaona ushirika ambao ni lazima tufanye na Mungu. Hatuwezi kukaa tu bila kufanya kitu na kufikiri kwamba Mungu peke ataweka ndani yetu kumfanana kwetu. Lazima na sisi tujihusishe vilevile. Ni lazima “tufanye kazi.” Lakini kazi hii siyo ya kutufanya tukubalike na Mungu; isipokuwa

ni kuonyesha kuelewa kwetu na kuonyesha shukurani ya msamaha wa dhambi zetu kupitia damu ya Yesu Kristo na kurithiwa kama watoto wa Mungu.

Mifano mingi na michoro imetumika kuelezea hatua za kukua kiroho.

#### A. Daraja au Ngazi za Nyumba

Wakristo wengi wanatazama kukua kiroho kama daraja au kama seti ya ngazi za nyumba tunazopanda. Tunapokuwa wa kiroho kabisa, tunajihesabu kana kwamba tuko kwenye ngazi juu. Na kwa hiyo tunapokuwa si wakiroho, tuko chini kwenye ngazi .



#### B. Kufa kwa Utu wa Kale

Wengine wanatazama kukua kiroho kama hatua ya kubadilisha utu wa kale wa dhambi kwa utu upya unaotokana na Kristo. Kadiri mtu wa kale anapokufa, mtu mpya anatokea. Wakati hii inapotokea, mtu anakua kiroho.

Mchoro kama huu siyo lazima uwe wa uongo, lakini kama tutakavyoona, kuna njia bora ya kuelewa kukua kiroho.

## II. NAFASI YA MSALABA KATIKA UKUAJI KIROHO

#### A. Kukua katika Ufahamu wa Utakatifu wa Mungu

Nafasi ya kwanza ya utaratibu wa ukuaji inahusisha kukua katika mwanga wa Mungu. Bwana ananena katika kitabu cha Yeremia, "Bwana asema hivi, mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake, bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifamu mimi na kunijua ya kwamba mimi ni Bwana, nitendaye wema na hukumu, na haki, katika nchi; maana mimi napendezwa na mambo hayo , asema Bwana" (Yer 9:23-24). Katika Yohana 17:3 Yesu anasema, "Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo aliyetumwa."

Kumjua Mungu ndiyo kusudi na maana ya uzima wa milele. Kisa hasa cha kutaka maisha ya kikristo inatakiwa iwe kumjua Mungu katika kweli. Kwa hiyo, tunapoendelea kukua kumjua yeye katika ukuu wake wote, tunakua kuwa kama yeye. Ufunguo wa kumjua Mungu ni kuelewa tabia yake ya utakatifu. Tunajifunza kuhisi kama mtume Paulo alivyosema, "Naam, zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu" (Flp 3:8a). Hii ni sehemu ya hatua ya utakaso.

#### B. Kujifunza Kutambua Dhambi Zetu

Tunapokuwa tunakua katika mwanga wa Mungu katika ukamilifu wake wote, tunakua na kujitambua wenyewe pia. Kipekee, tunafikia kujua hali yetu ya dhambi tofauti na tabia kamilifu ya Mungu. Kadiri tunavyomsogelea karibu Mungu, ndivyo tunavyojiona kuwa mbali naye. Kadiri tunavyomjua alivyo mtukufu kweli, ndivyo kadiri dhambi zetu zinavyodhihirika mbaya zaidi kwetu.


Kukua katika kujifahamu jinsi ulivyo mwenye dhambi kunaweza kutolewa mfano katika maisha ya Paulo, mtume. Katika 55 BK Paulo alijieleza kama "mdogo kuliko mitume wote" (1Kor 15:9). Baadaye katika 60 BK Paulo anajieleza mwenyewe kama "mdogo kuliko watakatifu wote" (Efe 3:8). Hata baadaye, mwishoni mwa maisha yake katika 64 BK, alijieleza mwenyewe kama "mkuu wa wenye dhambi" (1Tim 1:15). Je Paulo aligeuka kuwa mwenye dhambi alipokua kiroho? Bila shaka haionyeshi kuwa hivyo. Lakini, inaonyesha aliendelea zaidi na zaidi katika unyenyekevu na kujifahamu kuhusu dhambi zake katika maisha yake yote. Alipokua, alikuja kutambua kuwa baadhi ya tabia zake ambazo hazikumsumbua mwanzoni zilikuwa ni dhambi halisi. Hii ni hatua ya kukua kiroho.

#### C. Pengo Linalotokea

Utambuzi wa pengo lililopo kati ya mwenye dhambi na Mungu mtakatifu ndicho, hasa, kilichotuleta katika imani ndani ya Yesu mwanzoni. Msalaba unaliziba pengo wakati wote mtu anapookoka (kilelezo 3.1).

Lakini hata baada ya kumjua Kristo kama mwokozi, tunatakiwa tuendelee kukua katika mwanga wetu wa utakatifu wa Mungu na katika utambuzi wa hali zetu za dhambi. Hii inaweza kuwa uzoefu wa kuhofisha. Kumjua Mungu na Utakatifu wake ni kukaribisha kujiweka wazi wenyewe, na huu ni uzoefu wa kutisha kwa hao wanaopenda kuficha makosa yao na mapungufu. Kwa jinsi hiyo, kwa mkristo anayekua, pengo linaonyesha hitaji la kuendelea kumhitaji Kristo na ukuu wa yale aliyofanya msalabani

Kwa hiyo msalaba unaendelea kuongezeka umuhimu kwetu tunapokua kumjua Mungu na ukuu wake. Kadiri tunavyomjua Mungu ndivyo kadiri tunavyojiona kutofaa mbele zake. Mwanga huu unapokua, tunaona maana ya msamaha wetu na upatanisho wetu kwa Mungu kupitia Yesu Kristo. Tunapoufahamu ukuu wa Mungu, (kama Isaya alivyofanya alipoona utukufu wa Mungu hekaluni, au kama taifa la Israeli walivyofanya walipokutana na Mungu katika mlima Sinai). Tunagundua utukufu wa kweli wa mwokozi. Damu yake inaosha wenye dhambi na kuzisafisha na kutuvalisha mavazi meupe ili kwamba tuweze kumsogelea Mungu huyu wa utukufu.



### III. VIPINGAMIZI KWENYE UKUAJI WA KIKRISTO


Tukiwa kwa kiwango fulani tumekubali ukweli kwamba Kristo amelipa gharama kuziba pengo, tunajitahidi kuendelea katika ukuaji wetu wa kikristo. Wakristo wengi wana moja ya matatizo ya kawaida ya kukua katika imani zao.

#### A. Ufarisayo—tatizo la kiburi

Waumini wenge wanatekwa katika matendo na hivyo kuangukia katika mtego wa kutafuta kupata kukubaliwa na Mungu kwa njia ya matendo. Mara nyingi, mwelekeo unahama kutoka kwenye kazi ya Kristo msalabani kwenda kwa yale wanayomfanyia Mungu. Kama Mafarisayo katika nyakati za Agano jipya, wanaishi kama kwamba maisha ya kikristo ni kwa yale tu tunayomfanyia Mungu.

Tatizo hapa ni kwamba hawagundui kuwa kuna mengine, tena vipengele muhimu zaidi vya maisha ya kikristo kuliko huduma, kama vile kumjua Mungu na kuwa na uhusiano binafsi naye (Luk 10:38-42). Mafarisayo wa siku hizi kimakosa wanaamini kwamba wanaweza kuziba pengo lililopo kati yao na Mungu kwa matendo yao mazuri. Kiburi, au haja ya kutaka kuonekana vizuri machoni pa watu wengine, inaweza kuchangia hili. Matendo yanakuwa msingi ambao juu yake watu hawa wanajenga sifa zao.

Dhambi pia inawasonga Mafarisayo wa sasa. Wanaweza kudhani kuwa dhambi zao hazina uzito wowote kwa Mungu (tambua habari namba 4 katika kielelezo 3.2). Katika hali kama hii, Umuhimu wa msalaba unapunguzwa. Wanachofanya hapa ni kumpunguza Mungu katika akili zao na kumfanya mdogo kuliko alivyo kikweli. Wengine wanaweza kudhani, "Mimi siyo mwenye dhambi mkubwa hasa kiasi hicho!" watu hao wanaweka ukuta (Na. 5 katika kielelezo 3.2) chini karibu na msalaba. Siyo kwamba ni rahisi kuona dhambi za mtu mwingine kuliko dhambi zetu wenyewe? Ni kwa nini hili? Ni kweli kwamba tuna tatizo kidogo na dhambi kuliko wengine walivyo? Kama tunafikiria hivi, tunajidanganya wenyewe. Kwa sababu tunajifikiria kwa juu sana, na tena umuhimu wa msalaba unapungua.



Ili kuuepuka ufarisayo, lazima tukue katika kuelewa utakatifu wa kweli wa Mungu na ukweli wa miyo yetu ya dhambi. Kwa kuliona hili kutatunyenyekesha na kudhihirisha hitaji letu la neema ya Mungu.

## B. Kukata Tamaa—Kutokuamini

Wengine wana mahangaiko tofauti. Wanatambua utakatifu wa Mungu, na hivyo hali yao ya dhambi, na wanakata tamaa kwa sababu hawajui nini la kufanya juu yake. Wanajaribu kuziba pengo kwa matendo mema, lakini wanajisikia kana kwamba hawawezi kamwe kufanya vizuri hasa kumpendeza Mungu. Wanaweza kung'ang'ana kutumia muda mwingi kusoma neno la Mungu kila siku, lakini katika siku wanazoshindwa, wanajisikia vibaya sana kushindwa juu ya kutembea kwao na Mungu. Wanajaribu kulinda ndimi zao, na wanaposhindwa, wanashangaa kama Mungu atawapenda kweli. Kwa sababu ya kushindwa kwao kote, wanafikia suluhu kwamba hawataweza kumpendeza Mungu kamwe. Hivyo kukata tamaa.


Tatizo hapa ni kukosa imani kwenye kile Mungu alichokwisha fanya. Mungu ametoa kila tunachohitaji ili kukubaliwa mbele zake kwa sadaka ya Yesu Kristo (Ebr 10:14). Hatuwezi kuongeza kwa alichokwisha fanya.

## C. Jibu: Msalaba Lazima Ukue

Matatizo yaliyoelezewa hapo juu yanakaribiana kabisa moja kwa jingine. Mfarisayo aliamini kimakosa kuwa anaweza kupokea upendeleo wa Mungu kwa matendo yake wakati mwingine anayekata tamaa kimakosa anajua kuwa hawezi kupokea upendeleo kwa Matendo yake . Lakini katika hali zote upeo siyo kweli. Hali ya kupokea upendeleo wa Mungu kwa matendo ndiyo msingi wa tatizo kwao.

Kwa kuwa matatizo yanafanana, suluhu karibu itakuwa sawa. Hasahasa, ili kwamba pengo liweze kuzibwa, msalaba lazima ukue. Hakuna tunachoweza kufanya kitakachoziba pengo. Kama Paulo alivyosema, "Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu chochote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo" (Gal 6:14a). Yesu Kristo na kazi yake msalabani inaendelea kuwa muhimu kwetu zaidi na zaidi.

### Kielelezo 3.3-Msalaba unaokua



Ni lazima tukubali hali halisi ya upya wa maisha yetu katika Yesu Kristo. Ingawa bado tunaioa dhambi, Mungu amejaa neema na husamehe dhambi zetu. Tunasimama kikamilifu kwenye haki katika Kristo kwa sababu tu ya kazi yake msalabani. Tumekuwa watoto wa Mungu aliye hai na tunapendwa naye. Anapendezwa nasi na amejitoa kutufanya katika kufanana na Kristo.

## **SULUHU**

Msalaba ndiyo tumaini letu pekee la kuwa na amani naye. Hakuna sehemu nyingine ambayo wenye dhambi, hata wenye dhambi waliohesabiwa haki, wanaweza kumwona Mungu isipokuwa msalaba.

Ili kukua kiroho, mkazo wetu unatakiwa uwe kuelewa kikamilifu zaidi hali halisi ya Kristo ya kazi aliyomaliza msalabani kuliko kukalia kujitahidi zaidi. Siku kwa siku na kitambo baada ya kitambo, tunatakiwa kukumbuka alichofanya Kristo msalabani kwa ajili yetu kwa kuzichukua dhambi zetu na kutupa maisha mapya. Katika mtazamo huu wa utakaso, tunafahamu kuwa hali yetu ya mwili inabakia kuwa ya dhambi mpaka siku tunayokufa. Lakini pia tunatambua maisha ya Kristo ndani yetu.

Kadiri tunavyokua katika kumjua Mungu, ndivyo tunavyobadilishwa zaidi na zaidi kuwa katika mfano wake. Kukosa uwezo kwetu wa kufanya hivi kunadhahirika na hivyo kutufanya kumtegemea Kristo kwa ujumla. Injili inaleta maana kwetu na hitaji letu la Yesu linakuwa kubwa zaidi. Tunaelewa zaidi kwa undani tulichoamini mara ya kwanza. Tunajikumbusha juu ya ukweli wa injili ya kweli. Kwa imani tunakamilisha kifo cha Kristo na ufufuko kuwa halisi zaidi katika maisha yetu.

## **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Nini maana ya kukua kiroho? Ni kwa namna gani inahusiana na wokovu?
- Ni kwa jinsi gani unakua katika utakatifu? Elezea hatua katika msingi wa kukua siku kwa siku na jinsi ambavyo umejifunza kuwa ukamilishaji wa Kristo unahusika katika hili.
- Ni nini ugumu wako mkubwa juu ya kukua kiroho?
- Orodhesha yale ambayo kifo cha Yesu msalabani na ufufuko wake kutoka kwa wafu vimekamilisha. Andika maelezo juu ya jinsi unavyoweza kufanya haya yaliyokamilika kuwa dhahiri katika maisha yako.

## **UTEKALEZAJI WA AZIMIO**

Elezeana mmoja kwa mwingine kile ulichojifunza juu ya kukua katika utakatifu na pambanua kwao jinsi unavyotumia ukamilishaji wa Kristo katika maisha yako ya kila siku. Toa mfano maalumu wa mabadiliko katika maisha yako kama muumini kwa matokeo ya kuelewa kwako juu ya utakaso.



# Uwezo wa Injili Unaobadilisha UHURU KUTOKA UTUMWANI MWA DHAMBI

## ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kupambanua jinsi ambavyo tuliwekwa huru kutoka kwenye utawala wa dhambi tulipoungana na Kristo, kwa kifo chake na ufufuko, ili kwamba tuweze kukutana na nguvu ya injili katika maisha yetu kadiri tunavyotembea kwa imani katika hali hii halisi mpya.

## ☞ Wazo Kuu

- Wokovu wetu una maana kuwa tumebadilishwa ndani.
- Kwa sababu ya asili yetu mpya katika Kristo tuna nguvu ya kushinda dhambi.
- Mungu anatumbea kutembea katika roho ili kwamba tusizitimize tamaa za mwili.

## ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa :

- Kuelewa maana ya muungano wa Kristo na nguvu iliyopo kuufisha mwili, hautawaliwi tena na dhambi
- Kutembea kwa imani kibinafsi, kifo cha kiroho na ufufuko uliodhihirika katika Kristo na katika wokovu kutokana na nguvu ya dhambi.

## ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Somo hili lina vielelezo vingi kutoka katika warumi 6:3-10. Kujifunza vifungu hivi kwa uangalifu kwa maandalizi kutakufanya kulifundisha somo hili kikamilifu.

## UTANGULIZI

Injili ndiyo msingi wa uhusiano wetu na Mungu. Kutokana na mtazamo wa Mungu, uhusiano wetu unajengwa kipekee juu ya msamaha wa Yesu na haki kamili inayotolewa kwetu kwa imani. Ukweli huu unatakiwa kuleta uwezo wa kushinda dhambi katika maisha yetu kunakopelekea mabadiliko binafsi ya maana sana. Hata hivyo wengi wetu bado wanahangaika na dhambi na wakati mwingine wanashangaa ni kwa namna gani tunaweza kubadilishwa sasa. Kwa nini waumini wanatenda dhambi? Na, nini kinaweza kufanyika kuhusu hilo? Ni kwa jinsi gani tunaweza kubadilishwa kufuatana na injili?

## I. NEEMA YA MUNGU NA MAZOEYA YA DHAMBI

### A. Tuendeleo Kutenda Dhambi?

Kama kweli neema ya Mungu inazidi zaidi ya dhambi zetu zote na tumehesabiwa haki kwa imani mbali na utii wetu, tuendeleo kutenda dhambi? Kama neema ya Mungu inatolewa hata kwa hao ambao hawaistahili lakini wanapokea kwa imani zao katika Yesu Kristo, ni hali ya kawaida kuuliza swali hili. Tuendeleo kutenda dhambi na kutarajia neema ya Mungu kuzifunika?

Mtume Paulo alilitarajia swali hili katika barua yake kwa Wagalatia aliposema, “Uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili” (Gal 5:13). Na hili ni swali sawa Paulo analojibu katika Warumi 6 alipouliza, “tuzidi kutenda dhambi ili neema izidi kuongezeka? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?” (Rum 6:1b, 2).



## B. Jawabu la Kibiblia

Jibu kwa swali hili ni wazi kuwa “hapana”, hatuwezi kuendelea katika dhambi. Tunalifahamu hili na kujitahidi tusitende dhambi. Kujiongoza na kanuni vinakuwa vitu vya kawaida kwa mkristo aliyejitoa anayetaka kuepuka kufanya dhambi. Lakini hali ya usahihi ya dhambi inahusu mabadiliko ya ndani kwa muumini.

Tunapolisoma jawabu la Paulo katika Warumi 6, tunaewa siyo tu kwa nini hatutakiwi kuendelea kutenda dhambi, lakini pia tunagundua uhuru mpya tulionao kutoka katika nguvu ya dhambi. Hii ni sehemu nyeti ya mafanikio ya kuishi kikristo. Katika wokovu wetu, Mungu ametoa suluhu kwa mahitaji yetu makuu ya msingi mawili: Ametutoa katika adhabu ya dhambi, ametupatanisha na yeye mwenyewe, Na ametutoa katika nguvu ya dhambi, ili kwamba tuishi kwa uhuru wa kweli kumpenda yeye. Warumi 6:1-2 inatuelekeza kuwa hatuwezi kuendelea kutenda dhambi, kama tulivyofanya kabla hatujawa wakristo, kwa sababu “tumeifia dhambi.”

Katika wokovu wetu, Mungu ametoa suluhu kwa mahitaji yetu makuu ya msingi mawili: Ametutoa katika adhabu ya dhambi, ametupatanisha na yeye mwenyewe, Na ametutoa katika nguvu ya dhambi.

## II. KUBATIZWA KATIKA KIFO CHAKE—KUFUFULIWA KATIKA UFUFUKO WAKE (Rum 6:3-10)

Katika barua hii kwa Warumi anapokuwa anajibu swali linalohusu dhambi, Paulo anatumia ubatizo kuelezea mabadiliko yanayotokea mtu anapokuwa mtoto wa Mungu. Soma Warumi 6:3-10 kwa uangalifu.

### A. Kufa Kwetu na Kristo

#### 1. Ni jinsi gani tulikufa?

Katika Warumi 6:2-5 Paulo anafafanua jinsi tulivyofia dhambi. Tuliungana na Kristo na kubatizwa katika kifo chake. Kabla hatujaufikiria ubatizo wetu katika kifo cha Kristo, tunapaswa kukazia katika swala halisi lililopelekea kufa kwetu katika dhambi. Iitokea kwa Muungano wetu na Kristo. Kuna maelezo kadhaa ya utendaji katika fungu hili, ambayo yanaonyesha muungano kati yetu wenyewe na Kristo. Katika mstari wa 3 tunaona kwamba “sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa *katika* mauti yake”. Katika mstari wa 4 “tulikuwa...tumezikwa *naye*”. Katika mstari wa 5, “tumeunganika *naye*,” na katika mstari wa 8, tukiwa “*tulikufa na Kristo*.”

Maelezo yote haya yanaweka wazi kuwa katika muungano wetu na Kristo katika kifo chake tumekufa wenyewe. Kama tunataka kuwa huru na asli ya dhambi ndani yetu, tunahitaji kushuhudia kufa kwa utu wetu wa ndani. Wakati Mungu kwa nguvu za asili anapotuunganisha na Kristo, anaufisha utu wa ndani ingawa utu wa nje unaendelea kuishi.

Neno “muungano” (sumfutoi katika kiyunani) katika mstari wa 5, “... tumeunganishwa naye...” ni neno ambalo lilitumika kuelezea kupandikiza pamoja miti miwili tofauti. Wakati tawi la kigeni lilipopandikizwa kwenye mti, wakati ulipoanza kuchipua kutoka kwenye mti lilimopandikizwa ndipo unakuwa sumfutoi, “kuungana” nao. Hii ni aina ya kuishi kwa muungano kunakotokea tunapoamini katika Kristo. Hii ni aina ya muungano hai unaotokea tunapoamini katika Kristo. Kiasili tumeunganishwa na Yesu Kristo, na uhai wake unatoa uhai kwenye utu wetu wa ndani. Kabla hatujaishi katika uhuru, lazima kwanza tufe, ili kwamba utu wetu wa ndani utenganishwe na dhambi. Kwa hiyo tumeunganishwa na Kristo kwa kifo chake.

Kwa hiyo, kufa kwetu na Kristo kulisababisha mgawanyiko kati ya utu wetu wa ndani na asili ya dhambi, ambayo ilipelekea uhuru wetu kutoka katika kutawaliwa na dhambi. Ingawa asili ya dhambi inaendelea kuwepo, na ni msukumo mbaya ndani yetu, utawala wake juu yetu umevunjwa na hatufungwi tena na nguvu yake. Hii ndiyo yakini yetu, Upya halisi na lazima tuamini ukweli wake kama tunataka kuishi maisha ya Kikristo kwa mafanikio.

## 2. Ni nini kimetokea kwa sababu ya kufa kwetu na Kristo

Warumi 6:6 inatuambia kilichotokea kama matokeo ya kufa kwetu na Kristo: “utu wetu wa kale” ulifufuliwa. Utu wa kale kwa kifupi ni utu wa ndani uliokuwepo kabla hatujaamini katika Yesu Kristo na kupewa maisha mapya naye. Ni utu wa kale ambao ulikuwa umefungwa na dhambi. Kwa jinsi hiyo, tulipoungana na Kristo katika kifo chake, utu huu wa ndani ulifufuliwa na matokeo kwamba mwili wetu wa dhambi “ukaondolewa.” Neno la kiyunani katarge, kuondolewa.” Halishauri kuvunjwa, kana kwamba dhambi imeondolewa ndani yetu. Kwa hiyo, ina maana “kutoa iliyotanguka au isiyofaa” katika hilo jambo fulani limefanywa kutokuwa la mafanikio kwa kuondoa nguvu yake ya kutawala. Paulo alitumia neno linalofanana katika Warumi 3:3 anaposema kwamba kutokuamini kwa mwanadamu “hakutoi uaminifu wa Mungu uliotanguka”. Katika Warumi 7:2, anasema kwamba mwanamke “amefunguliwa” kutoka kwa mwanaume anapokufa. Hii ndiyo maana katika mazingira yetu. Tumeondolewa katika utawala wa dhambi kwa sababu nguvu yake ya kutawala imeondolewa. Minyororo ya dhambi imevunjwa na si watumwa tena kwake.

### B. Matokeo ya Mwisho: Maisha Mapya na Kristo

Hakuna wazo la mwisho lililowakilishwa katika kifungu hiki linalofanua mabadiliko ya utu wetu wa ndani yalikipitia. Tumeambiwa kwamba hatukuungana tu na Kristo katika kifo chake, lakini pia katika ufufuko. Hatukufa tu, lakini pia tumefufuliwa kuwekwa kwenye maisha mapya. Kwa njia ya kuungana kwetu na Kristo, kwa sababu Kristo anaishi, utu wetu wa ndani nao unaishi. Warumi 6:4 inatuambia kwamba kama nguvu ya Baba ilionekana katika kumfufua Kristo kutoka kwa wafu, kwa hiyo tumefanywa kutembea katika upya wa maisha kama onyesho la nguvu hii sawa. Nguvu ileile iliyomfufua Kristo kutoka kwa wafu imetufufua sasa kutoka kwa wafu.

Matokeo ya haya yote ni kwamba kitu chenye nguvu na nguvu ya asili kimefanyika kwetu, na utu wetu wa ndani siyo tena kama ulivyokuwa. Utu wa kale umekufa na utu upya unaishi. Ni aina gani ya utu huu mpya? Katika mstari wa 6 na 7 wa Warumi 6 tunajifunza kwamba huu utu wa ndani uko huru kutokana na dhambi na siyo mtumwa tena wa dhambi. Hivi ndivyo tulivyo sasa katika Kristo.

### C. Kufanya Hesabu Kwa Imani Maisha Yetu Mapya Katika Kristo

Ni amri kwa wakristo kuleta ukweli huu katika maisha yao ya kila siku. Wote tunajua kuwa dhambi bado imo ndani yetu, na tunavyoendelea na mahangaiko yetu ya dunia ya dhambi, tunaweza kupoteza mwelekeo wa maisha yetu mapya yaliyopo kwa hakika katika Kristo. Kuna nyakati zingine hatujisikii kuwa huru na dhambi kabisa, na tunashangaa kama nguvu yoyote ya asili imetukia kwetu hata kidogo. Tunaweza kukubaliana na mtume Paulo aliposema, “Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi, bali lile baya nisilopenda, ndilo nilitendalo.” (Rum 7:19).

Hii ndiyo sababu maneno ya kufungia ya Paulo katika Warumi 6 ni muhimu sana kwetu. Mara tatu katika kifungu hiki Paulo ametuamuru “tujue” ukweli huu (vv. 3,6,9). Anataka tuelewe ni nini hasa kimetokea kwetu katika Kristo. Kisha, katika mstari 11 Paulo anamalizia, “Vivyo hivyo ninyi nanyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika KristoYesu.” Katika mstari huu, neno la kiyunani logizomai, “hesabu” lilikuwa ni neno la kimahesabu lililotumika wakati mtu alipokuwa anahesabu tatizo au anahesabu namba. Limetumika kwa mfano katika kifungu hiki “kuhakikisha kabisa” ukweli uliofundishwa hapa. Paul anatusihi kuweka ujasiri wetu ndani na kamili kuamini ukweli huu wa msingi juu yetu. Utu wa kale hauishi tena ndani yetu. Alikuwa mtumwa wa dhambi, lakini alifufuliwa kama tulivyounganishwa na Kristo katika kifo chake na ufufuko, na sasa tumebadilishwa katika mwanaume mpya na mwanamke mpya. Lazima sasa tuhakikishe na kuamini kwamba tumefanywa kuwa hai katika Kristo na kwamba tumefanywa viumbe vipya ndani.

Maisha yetu ya kikristo ni maisha ambayo tunaishi kwa imani katika ukweli huu. Hata kama hatuoni hivi kwa ukamilifu mara zote, haibadilishi ukweli wa kilichofanyika. Ni lazima tuendelee kila siku kuungama dhambi zetu na kuamini kuwa ni wamoja na Kristo, na kwamba sasa tunaishi katika muungano na yeye.

### III. NGUVU YA KUTOTENDA DHAMBI

Kufuatana na Warumi 6, kwa sababu tumeunganishwa na Kristo, tumekufa na kufufuka naye. Ushindi wake dhidi ya dhambi ulikuwa ushindi wetu dhidi ya dhambi. Dhambi si mtawala wetu tena. Lakini hali kubwa halisi ya Ukristo haina maana kwamba dhambi haitafuti kutufunga. Dhambi siyo mtawala wetu, ingawa mara nyingi inajaribu kupata mamlaka na nguvu zake juu yetu.

Unaweza kuwa unafikiri, “Lakini mara kwa mara nahangaika na dhambi. Ninawezaje kuishinda? Hakikisha kwamba hakuna kanuni wala kujilinda pekee kunaweza kukuwezesha kuwa na maisha ya kikristo ya ushindi. Tunaweza kujaribu na kujaribu kwa nguvu za mwili na hatimaye tutashindwa kwa sababu miili yetu inazoelea dhambi. Kwa pamoja hali halisi ya dhambi inahusiana na mabadiliko ya ndani ya muumini. Tunaipinga dhambi kwa kuimarisha ufahamu wetu wa sisi ni nani katika Kristo.

#### A. Kuifahamu Asili Mpya

Ulipogeuka kuwa mkristo, hukuongeza asili ya kimungu katika asili yako ya zamani ya dhambi. Ulibadilishana asili—ukawa kiumbe kipya (2Kor 5:17). Ulihamishwa kutoka katika ufalme wa giza na kupelekwa katika ufalme wa nuru, ulipogeuka kuwa mtoto wa Mungu. “Utu wetu wa kale (asili ya kale) ulifufuka pamoja naye” (Rum 6:6). Utu wa kale hauna nguvu!

Kama tukiwa na asili mpya, kwa nini tunatenda dhambi? Kuna neno la kiyunani ambalo limetumika mara nyingi sana katika kitabu cha Agano la Kale lote kama chanzo cha dhambi katika maisha ya waumini. Ni neno mwili. Nini maana ya mwili? Ni sehemu ya akili yetu, hisia, na nia ambayo imeamriwa au kufunzwa kutenda dhambi. Mazoea na mtindo wa kufikiri umerithishwa kwetu na ulimwengu, kwa walimu wasio wa kimungu, na kwa mapigo ya moja kwa moja ya Shetani. Mazoea ya kidunia yameweka akili yetu kuishi kwa kujitenga na Mungu na kufuata namna ya njia za ulimwengu.

#### B. Kuishi Katika Roho

Warumi 8:5-7 inatofautisha hao wanaoishi kulingana na mwili na wanaoishi kulingana na roho. Pale unakuta kwamba ni akili ambayo labda imeandaliwa kwenye mwili au kwenye roho. Mwili wako ambao umefundishwa na ulimwengu, unazalisha fikira na mawazo kiulimwengu ambazo zinakuongoza kutenda dhambi. Kama waumini, hatutakiwi kuendelea kuishi katika mwili, lakini katika roho (Rum 8:9), Gal 5:16). Lakini inawezekana sisi tukatembea kufuatana na mwili (Rum 8:12; 13). Wasioamini hawana uchaguzi—wanatembea katika mwili kwa sababu wanaishi katika mwili. Lakini hatulazimishwi kwenye mwili... tuna uchaguzi. Lazima tujifunze na tuchague kutembea katika roho na si katika mwili. Kama Paulo anavyosema: “ishi kwa roho, Basi, enendeni kwa roho wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili” (Gal 5:16).

#### C. Kujitambua Mwenyewe Kama Mtoto wa Mungu

Kabla hatujamtambua Kristo tulikuwa wenye dhambi, Lakini tulipofanywa watoto wa Mungu tukawa ‘watakatifu.’ Je sisi ni watakatifu au ni wenye dhambi? Jibu linaweza kuwa gumu. Lakini kama unajifikiria mwenyewe kama sehemu ya watakatifu au wenye dhambi, upande mmoja nuru na upande mwingine giza, utaendelea kuhangaika na kuishi maisha ya kushindwa. Unapokuja kufahamu mabadiliko yaliyotokea ,waumini wangetakiwa kukazana kutunza hali ya utambuzi wa kwamba wao ni nani katika Kristo aliyefufuka. Tunapokutana na dhambi, tunatakiwa kijifikiria wenyewe kama watoto wa Mungu. Kama tukijifikiria wenyewe kama wenye dhambi, tutajaribu kuishi kama wenye dhambi. Ni lazima tujione wenyewe kama watakatifu, kama watoto wa Mungu, ili tuweze kuishi kama watoto wa Mungu.

#### D. Geuza Upya Nia Yako

Vipande vingi vya dhambi vinaanza na maisha ya fikira mbaya. Kipande cha dhambi cha kufikiri lazima kigeuzwe na kufanywa upya katika akili” (Rum 12:2). Akili ndiyo uwanja wa mapambano dhidi ya dhambi. 2Wakorintho 11:3 inaonyesha kwamba kama Eva alivyodanganywa na Shetani, akili zetu zinaweza kupelekwa kinyume kutoka katika kuwa wakweli na waliojitoa kwa Kristo. Shetani alivuta akili ya Daudi, Solomoni, Anania, wakristo wa korintho, na anaweza kugeuza akili yako pia. Anaweza kuleta fikira zake katika mawazo yako na kukudanganya kana kwamba ni mawazo yako, au kuwa pengine ni mawazo ya Mungu. “ Lakini tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo” (2Kor 10:5).

### **E. Kuujua Ukweli**

Iko wapi nguvu ya Dhambi? Shetani, kufuatana na Yohana 8:44, “ni mwongo na baba wa huo uongo.” Tunapojaribiwa kutaka kufanya dhambi kuna uongo nyuma yake. Lakini Yesu anasema katika kifungu hicho hicho, ‘na utaujua ukweli, na ukweli utakuweka huru’ (Yoh 8:32). Ulinzi wetu dhidi ya dhambi ni ukweli. Kwa kuujua ukweli wetu, kufanywa washindi kama waumini katika Kristo, tunapata uhuru kutoka kwenye nguvu ya dhambi.

### **SULUHU**

Injili ndiyo msingi wa uhusiano wetu na Mungu. Kutoka katika mtazamo wa Mungu, uhusiano wetu unajengwa kipekee juu ya msamaha wa Kristo na haki ya kweli inayotolewa kwetu kwa imani. Ukweli huu unatakiwa ulete nguvu ya kuwa wakweli kuhusu dhambi zetu mbele za Mungu, na hakikisho la neema yake ya kupita kwetu. unatakiwa utuvute kuishi kama wenye haki na si kwa sababu tumejifanya wenye haki, lakini kwa sababu hiyo ndiyo Mungu, kwa neema yake, ametuahidi kuwa.

Ukweli hasa muhimu kuhusu ushindi wa dhambi ni kukua, imani ya nguvu katika Kristo, imani iliyopatikana kwa kile alichofanya Kristo msalabani, ili kwamba nguvu yake kiuwazi inafanya kazi ndani yetu ikidhihilisha dhambi na udhaifu waziwazi. Imani hii inaelewa na kushukuru neema ya Mungu kwa undani zaidi na kutuongoza kumjua Mungu zaidi kwa karibu.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni jinsi gani unaruhusu mawazo yako badala ya imani yako kwenye neno la Mungu kugusa namna unavyotazama maisha yako ndani ya Kristo?
- Unapokuwa unahangaika na dhambi, ni nini kinaleta nguvu zaidi katika maisha yako: kujaribu kwa nguvu au kuamini zaidi?
- Ni kwa jinsi gani “hesabu” katika Warumi 6:11 inavyohusika na imani?
- Nini kimetokea katika hali yako ya asli ya dhambi kufuatana na barua ya Paulo kwa Warumi?
- Unawezaje kuishi kwa roho?



# Kutunza Kitabu cha Kumbu Kumbu za Kiroho

## ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuanzisha kuandika mambo ya kila siku kama chombo cha mazoezi yatakayowasaidia waumini kuzingatia kukua kiroho na kukua kwa huduma.

## ☞ Wazo Kuu

- Kwa nini kutunza kitabu cha mambo ya kila siku ya kiroho?
- Muda wa kila siku na Mungu
- Kuandika mambo ya kila siku

## ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Aweze kutumia kitabu cha mambo ya kila siku kama kifaa cha ufanisi kuandika mambo binafsi yanayohusu muda wake na Mungu, maombezi, na majibu, anwani za huduma vikundi kiini na mafunzo, kutafakari siku kwa siku.

## ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Unaweza ukataka kutengeneza au kuagiza vitabu vya kuandika mambo ya kila siku vya kuwapa washiriki kutumia wakati wa vipindi vya mafunzo ya semina. Kitabu cha mambo ya kila siku ya mpanda kanisa kutoka Bible league ni rahisi na kinachoweza kutumiwa (angalia vyanzo vya habari za anwani)

## UTANGULIZI

Katika hatua ya kwanza ya maisha, watu wachache wanapata muda na sehemu ya kuweza kutafakari juu ya Mungu na neno lake, na matumizi yake katika maisha yao binafsi. Kwa kuwa mwanafunzi ana haja ya kukua na kubadilika, anaendelea kuyachunguza maisha yake. Kama mfalme Daudi, anamuuliza Bwana kuuchunguza moyo wake na maisha kudhihirisha makosa yake yote na dhambi ili aweze kubadilika na kukua (Zab 139:23-24). Kuna hitaji kubwa kwetu kuchukua muda kuwa hodari mbele za Mungu kila siku na kuvunja vifungo vya shughuli nyingi.

Kutunza kitabu cha mambo ya kila siku kutakuwa msaada mkubwa kwako katika hatua nzima ya upandaji kanisa. Masomo yafuatayo yanaelezea asili ya kitabu cha mambo ya kila siku ya mpanda kanisa unayoweza kutumia katika utunzaji mambo yako mwenyewe.

## I. KWA NINI KUTUNZA KITABU CHA KUMBU KUMBU ZA KIROHO?

Wakati Waisraeli walipovuka mto Yorodani, kuingia katika nchi ya ahadi, Mungu aliwaamuru kuchukua mawe kumi na mawili kutoka kwenye mto na kujenga ukumbusho. Dhumuni la ukumbusho lilikuwa kwa ajili ya vizazi vilivyopo na vijavyo vya Israeli juu ya uaminifu wa Mungu na nguvu yake katikati yao (Yos 4:1-9).

Katika namna sawa, tunapoandika masomo ambayo Mungu ametufundisha, au uzoefu tuliopata, au maombezi na majibu, pia vinakuwa kama ukumbusho kwetu juu ya upendo wa Mungu na uaminifu katika maisha yetu tunapokutana na mahangaiko na kukatishwa tamaa. Kutunza kitabu cha mambo ya kila mara ni njia mojawapo ya mafanikio zaidi ya kuendeleza kuwajibika katika kukua kiroho na huduma. Kitabu cha mambo ya kila siku kinatulazimisha kutazama maisha yetu na kurekebisha vipao mbele vyetu. Inatusaidia pia kukua katika imani kwa kuona jinsi ufahamu

wetu na kumwelewa kwetu Mungu kunaongezekaa baada ya muda, vilevile kuona jinsi Mungu alivyojibu maombi yetu.

Kwa karne nyingi, wakristo wamejifunza kutoka katika vitabu vya mambo ya kila siku kutoka kwa wakristo wanaojulikana kama vile Jonathan Edwards, Hudson Taylor na Amy Carmichael. Kumekuwa na shuhuda zilizoandikwa za jinsi Mungu alivyoishi kwa ushirikiano na kutiwa moyo juu ya uhusiano wa karibu tunaoweza vilevile kuwa nao na yeye.

Kwa nyongeza ya kuwa na maandiko ya kukua kwetu binafsi kiroho, kitabu cha mambo ya kila siku kinaweza kuwa zana katika kuendeleza huduma zetu. Kama Mungu anakuita kupanda kanisa au kuwa mmoja wa timu ya wapanda kanisa, utahusishwa katika kazi ya –uinjilisti, Kufuasa, maendeleo ya vikundi vidogo, n.k. Kitabu kinaweza kuwa cha kusaidia kuandika anwani zilizotengenezwa za watu, mawazo na malengo kwa ajili ya mikutano ya vikundi kiini, maswali na mambo yanayokusumbua unayotaka kujadili na mshauri wako, n.k. Kinasaidia kama ukumbusho unaoonekana wa huduma yako na pia kinakuwezesha kuona jinsi Mungu anavyokutumia katika njia maalumu kuwaleta watu kwake na kuanzisha kanisa. Kitabu cha mambo ya kila siku pia kinatoa maandiko ambayo unaweza kurudia na mwalimu wako au mshauri.

## II. MUDA WA KILA SIKU NA MUNGU (KIELELEZO 5.1)

Kielelezo 5.2 ni mfano wa mfumo wa kuandika uliyotafakari kutokana na muda wako katika neno la Mungu na maombezi na majibu kwa maombi. Tambua yafuatayo katika mfumo:


- **Kifungu cha leo:** Waka alama kwenye kifungu unachosoma wakati wa muda wako wa kusoma neno.
- **Ufahamu binafsi:** Soma kifungu cha Biblia, tafakari na kuomba juu yake. Andika kila roho mtakatifu anachokuonyesha kwenye kifungu hicho. Kifungu kinasemaje? Ni nini umegundua? Ni namna gani unaweza kutumia kifungu hiki katika maisha yako sasa?
- **Ahadi za kudai:** Kuna ahadi yoyote katika kifungu hicho? Zinakiri na kisha mshukuru Mungu kwa ukweli huo.
- **Amri za Kutii:** Kifungu hicho kina nukuru amri yoyote unayohitaji kutii?
- **Maombi:** Andika orodha ya maombezi ambayo una mzigo maalumu na vilevile majibu kwa maombezi ya nyuma. Uwe maalumu iwezekanavyo. Hii itakusaidia kumwona Mungu akitenda katika maombi yako.

## III. KUWEKA KUMBU KUMBU ZA KILA SIKU

Kielezo 5.1 ni mfano wa ukurasa wa yaliyoingia kila siku. Kuandika mambo kila siku kunasaidia kuona maendeleo ya huduma ya upandaji wako wa kanisa. Nukuu vichwa vifuatavyo unavyoweza kuandika katika kitabu cha mambo yako ya kila siku:

- **Utekelezaji wa Azimio:** Nukuru kazi yoyote ambayo umefanya wakati wa utekelezaji wa maazimio. Orodhesha shughuli zilizokamilika wakati wa utekelezaji wa azimio au kazi ambayo haijakamilika.
- **Anwani:** Orodhesha anwani ulizofanya mawasiliano ya kiinjilisti ya siku hiyo. Nukuru matokeo na muda wenu pamoja. Umeshirikisha ushuhuda wako? Wamesemaje juu ya ushuhuda huo? Je, wako wazi au hawako wazi katika injili?
- **Mikutano:** Andika kuhusu kikundi kiini chochote, kikundi kinachokutana nyumbani au kwenye sherehe maalumu. Lini na wapi mkutano ulifanyika? Nani aliuongoza? Mlifanya nini (mafunzo ya Biblia, kikundi cha maombi, kuonyesha filamu ya Yesu kwa marafiki)? Watu wangapi walihudhuria? Wangapi ni wahudhuriji wa kila siku? Wageni? Kuna mtu yeyote aliyekata shauri kumfuata Kristo? Nukuru kama kuna tatizo lolote au jambo maalumu linalohitaji kuangaliwa zaidi.
- **Kutafakari:** Chukua muda kufikiri juu ya siku ilivyokuwa. Kuna kitu chochote ambacho kimejitokeza nje kwako? Umejifunza au kuchunguza chochote juu ya maisha yako au huduma unayotaka kunakiri? Haya yanayotokana na kutafakari ni maandishi unayonukuu yanayohusu maisha yako mwenyewe. Huhitaji kuyashirikisha mtu yeyote. Inakusaidia kuweka siku yako katika mtazamo na kunukuru chochote ambacho Roho Mtakatifu anakufundisha.

### Kielelezo 5.1. Sala ya Kila Siku na Kumbukumbu za Kila Siku

<p><b>SALA YA KILA SIKU</b></p> <p><b>Fungu la leo:</b> Wakorintho 13</p> <ul style="list-style-type: none"><li>• <b>Utambuzi Binafsi:</b> <u>Matendo yangu yote lazima yavutwe kwa upendo. Ninaonyesha upendo wangu kwa matendo yangu. Upendo wakati wote huvumilia. Ninahitaji kuvumilia katika kuwapenda wengine. Nina hitaji kujali wengine na siyo kujijali pekee.</u></li><li>• <b>Ahadi za Kudai:</b> <u>Kwa sasa si wakamilifu, lakini mbinguni tutakuwa wakamilifu na tutamwona Mungu uso kwa uso kama alivyo. Kwa sasa tunafahamu sehemu tu.</u></li><li>• <b>Amri za Kutii:</b> <u>Onyesha upendo kutokana na sifa zilizo rodheshwa katika fungu hili, hakikisha matendo yangu yanavutwa na upendo, vinginevyo hayana maana.</u></li></ul>		<p><b>SALA YA KILA SIKU</b></p> <p><b>Matumizi wa Maazimio:</b></p> <ul style="list-style-type: none"><li>• <u>Maombi yaliyoanzishwa ya Utatu</u></li><li>• <u>Eneo linalokusudiwa kuگردulika</u></li><li>• <u>Anza mafunzo ya kujifunza kwa kulifata neno kutoka Yohana 17</u></li></ul> <p><b>Anwani</b></p> <table><tr><td><b>Jina</b></td><td><b>Mchango</b></td></tr><tr><td><u>Dr. Miller</u></td><td><u>Alitoa ushuhuda</u></td></tr><tr><td><u>Shangazi Sally</u></td><td><u>Alionyesha picha ya Yesu</u></td></tr><tr><td><u>Mrs. Jones</u></td><td><u>alishuhudia na kutubu</u></td></tr></table> <p><b>Mikutano</b></p> <p><b>(Vikundi kiini, mikutano ya nyumbani, mambo maalumu)</b></p> <p><i>Katika nyumba ya Jane saa 7 jioni maombi ya utatu yalikutana. (Jane, Mary, na mimi) Tuliombi kwa masaa 2. Tumekubaliana kukutana kila wiki katika nyumba ya Jane.</i></p> <p><b>Kutafakari juu ya siku</b></p> <p><i>Ninafurahishwa na kikundi cha maombi cha ya utatu. Sikuwa nimewahi kuomba kila mara na wengine na kwa ajili ya wasioamini. Nina shauku juu ya namna Mungu atatumia maombi yetu.</i></p>	<b>Jina</b>	<b>Mchango</b>	<u>Dr. Miller</u>	<u>Alitoa ushuhuda</u>	<u>Shangazi Sally</u>	<u>Alionyesha picha ya Yesu</u>	<u>Mrs. Jones</u>	<u>alishuhudia na kutubu</u>
<b>Jina</b>	<b>Mchango</b>									
<u>Dr. Miller</u>	<u>Alitoa ushuhuda</u>									
<u>Shangazi Sally</u>	<u>Alionyesha picha ya Yesu</u>									
<u>Mrs. Jones</u>	<u>alishuhudia na kutubu</u>									
<p><b>MAOMBI</b></p> <p><b>Mambo ya kuombea na Majibu kwa Maombi</b></p> <p><b>MO:</b> Kwa nafasi ya kumshirikisha imani yangu Dr. M</p> <p><b>MO:</b> Kwa ajili ya timu ya huduma kuendeleza</p> <p><b>MJ:</b> Afya ya mama yangu ni nzuri zaidi</p>										

### SULUHU

Kama mwalimu wako au mshauri wako hana kitabu cha kuandika mambo ya kila siku kwa ajili yako kutumia, pata daftari ambalo litakidhi mahitaji yako. Kitu muhimu ni kwamba kitabu cha kuandika mambo ya kila siku kinakusaidia kutafakari juu ya kile Mungu anachokufundisha kupitia neno lake na maombi na kunakiri maendeleo na somo ulilojifunza katika huduma yako ya upandaji kanisa.

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

Katika mzunguko mzima wa upandaji kanisa, tunza kitabu cha mambo ya kila siku kwa ajili ya sala na maendeleo ya huduma za sala na maendeleo ya huduma ukizingatia kielelezo 5.1 Unaweza ukanakili mfano katika kielelezo 5.1 kwenye kijitabu kidogo kwa ajili ya matumizi yako binafsi. Uwe tayari kuonyesha kitabu hicho kwa mkufunzi wako na mshauri.

### VYANZO

*The Church Planter's Daily Journal.* The Bible League, 16801 Van Dam Rd., South Holland, IL 60473 USA. E-mail: bibleleague@xc.org





---

## **MAOMBI**

---



# Kongamano la Maombi

## KUOMBA KWA AJILI YA UAMSHO

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuelezea wazo la kongamano la maombi, na kuonyesha jinsi ya kuyatumia kuomba kwa ajili ya uamsho.

### ☞ Wazo Kuu

- Upandaji kanisa unaanza na uamsho wa waumini.
- Maombi ndiyo ufunguo katika uamsho

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa mfumo wa kongamano la maombi.
- Ashawishike juu ya nafasi ya uamsho wa mtu katika upandaji kanisa.

### ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Hili ni somo la masaa mawili. Litumie kama kidokezo kwa kongamano la maombi ya kwanza. Sehemu kubwa ya somo lazima itumiwe katika maombi, kwa kutumia kipengele cha 11 cha somo kama mwongozo.

## UTANGULIZI

Maombi ni kiungo muhimu katika upandaji kanisa. Bila ya baraka za Mungu na maelekezo, juhudi zetu zote bora zitashindwa. Kwa sababu hiyo kila moja ya semina inakuwa na kuongamano la maombi. Neno “kongamano” inaleta kwenye akili wazo la maonyesho ya mziki ulioandaliwa—kama ni wa vyombo, sauti au vyote. Kongamano la kuimba mara nyingi lina nyimbo zaidi ya moja lakini mara nyingi zinapangwa kulingana na kisa maalumu—kama ni kulingana na mtunzi, aina ya mziki, vifaa, aina ya tukio, au mchanganyiko wa mahusiano yasiyo na mwisho.

Kongamano la maombi pia linapangiliwa kulenga kisa maalumu. Inaweza ikahusisha maombi mengi na watu wengi, lakini kuna mwelekeo bayana. Wasikilizaji wa kongamano la maombi ni Mungu mwenyewe. Kwa hiyo inatakiwa kutokana na visa vya kibiblia vitakavyomfurahisha yeye.

## I. JINSI YA KUPANGA NA KUONGOZA KONGAMANO LA MAOMBI

Mara nyingi wakristo wanachochewa kwa ajili ya maombi kwa kushiriki katika tukio la maombi yenye nguvu ambayo yanawachukua zaidi kupita uzoefu waliokuwa nao nyuma. Kwa kuomba na kundi jingine kubwa la wakristo na makanisa ya namna mbalimbali, waumini wanatambua kuwa hawako peke yao na wala kutengwa isipokuwa sehemu ya harakati kuu za Mungu. Wanaona kuwa maombi si zoezi la kukera isipokuwa la kuisimua, la kujenga imani. Na kuongeza nguvu. Katika mabara makuu matano yote ya ulimwengu, kongamano la maombi limevuta maombi katika kiwango cha juu, linavuta umoja miongoni mwa wakristo, na kuwasha uinjilisti na juhudi za upandaji kanisa.

Kongamano la maombi linazingatia mawazo mawili ya kibiblia:

- Maombi yanayoelekezwa *ndani*—kumuuliza Mungu kudhihirishia kanisa lake “utimilifu” wa Yesu kama Bwana katikati yake.

- Maombi yanayoelekezwa *nje*—kumuuliza Mungu “kutimiza” kusudi lake kwa kupitia kanisa kati ya mataifa. Huu ni utimilifu wa Utume Mkuu—kuinjilisha ulimwengu, uinjilisi wa kanisa la mtaa, na kueneza upandaji kanisa.

Kongamano la maombi linaweza kuandaliwa kwa ajili ya kanisa la mtaa au katika eneo hasa kuhusisha makanisa mengi ya mtaa kwa msisitizo wa umoja na kufanya kazi pamoja. Ufuatao ni muundo unaoshauriwa kwenye kongamano la maombi ambao unaweza kutumiwa katika hali yako ya mtaa. Jambo muhimu ni kuomba mara kwa mara na kwa ushirikiano.

Vifuatavyo ni vitu vinavyoshauriwa ambavyo vinatakiwa kuwemo katika kongamano la maombi. Andaa kati ya masaa 2-3 kwa ajili ya kongamano la maombi, inaweza kuwa asubuhi au jioni. Urefu wa kila kipengele utategemeana na lengo maalumu la kongamano la maombi. Kwa jinsi hiyo, ni muhimu kuwa na vipengele vyote kama sehemu ya maombi ya pamoja. Hii inahakikisha kuwa tukio litaendela kukazia, linganifu na lenye mtiririko sawasawa.

#### **A. Kisa**

Inasaidia kuanzisha maombi yako ya pamoja juu ya kisa maalumu. Hii itasaidia kongamano la maombi kuendelea kuzingatia na kuruhusu maombi kuwa maalumu. Kwa mfano, katika mji mkuu wa Kazakistan, kongamano la maombi liliendeshwa juu ya upatanisho. Sherehe ilizingatia juu ya Mungu kama mshauri wa watu, na juu ya wakristo kama mawakala wa ushauri. Wakati wa kipindi cha maombi, Warusi na Wakazakistan wote waliomba msamaha kwa makosa ya nyuma waliyotendeanana. Kongamano hili la maombi lilisaidia kuleta roho ya umoja na kusudi la wote kati ya makanisa ya miji ya Warusi na Wakazakistan.

#### **B. Jambo Linalozungumziwa**

Kukaribisha kila mmoja na kutumia maandiko kueleza kichwa cha habari cha kongamano la maombi. Ni nini neno la Mungu linasema juu ya kisa hicho? Kutambulisha mambo ya msingi ya mfumo wa kongamano la maombi. Kuchanganua mtiririko wa kongamano la maombi, kwa nini kila jambo ni muhimu na namna kila jambo linavyofaa. Kutoa ushauri juu ya kuwa wepesi wa kutambuana wao kwa wao—ni kwa muda gani maombi yatadumu, na kwa kiasi gani cha sauti, N.k.

#### **C. Sherehe**

Kumtukuza Mungu kwa uaminifu wake, kwa ajili ya ufalme wake, kwa ajili ya mtoto wake Yesu Kristo, n.k. Hakikisha utukufu unakuwa kwa Mungu alivyo. Tumia muda huu kukazia mambo muhimu yanayohusu uamsho na uinjilisi wa ulimwengu mzima. Toa mchanganyiko mzuri wa nyimbo za sifa na mapambio na ukihakikisha kila wimbo unaendana na kisa kikuu cha kongamano la maombi. Hili linaweza kufanyika kwa kuchangia machache yanayoeleweka kutambulisha kila jambo jipya, ukiwa mwangalifu wa kutokuhubiri isipokuwa kuwaongoza wengine katika kutukuza na kuabudu.

#### **D. Ungamo na Matayarisho**

Washiriki wajihakikishe utayari wao wa kusikia sauti ya Mungu na haja yao ya kutumikia kanisa na ulimwengu kwa huduma hiyo ya maombezi. Waongoze katika maombi ya kuungama kila dhambi inayojulikana, ili wawe safi na tayari kwa kuomba. Hii haina maana kwamba ungamu linatakiwa kuwa kwa sauti. Uliza kujazwa na Roho Mtakatifu na uongozi wake juu ya yale yaliyoombewa. Tumia muda kwa ukimya ukimsubiri Mungu kusikia kile anachosema kupitia maandiko au kwa Roho wake Mtakatifu.

#### **E. Kundi Dogo la Maombi**

Uwe na washiriki kutoka makundi madogo ya watu 2-4 na ombea juu ya kichwa kama kinavyohusika kwenye ngazi ya kwanza, mkoa, taifa, na katika ngazi ya mataifa. Baada ya muda wa maombi uliokubaliwa kwa vikundi vidogo, ongoza katika maombi ya kukua kwa harakati za maombi. Omba kwamba Mungu atawafanya washiriki kuwa thabiti na kudumu katika maombi. Omba kwa ajili ya harakati za maombi zinazotokea katika jiji au mji wako au mtaani. Mwombe Mungu kuanzisha maombi ya mkusanyiko katika kanisa ulimwenguni kote.

#### **F. Maonyesho**

Habari na vifaa vinaweza kutumika wakati wa kipindi chote cha maombi kusaidia kuzingatia na kuwatia moyo hao wanaoomba. Ramani zinazoonyesha sehemu zenye mahitaji zinaweza

kuwa msaada wa kuangalia. Ramani za mitaa zinaweza kutengenezwa kuonyesha makanisa yalipo katika eneo na pale ambapo hakuna kabisa. Vilevile ramani zinazoonyesha mahali pasipokuwa na kazi, familia za mzazi mmoja, n.k. Inaweza kuvuta maombi ya utatuzi.

### G. Kutukuza na Kuabudu

Malizia kwa muda wa kumtukuza na kumwabudu Mungu kwa njia zake za ajabu. Jitoe mwenyewe kuwa majibu kwa maombi yako na kuishi kufuatana nayo.

## II. KONGAMANO LA MAOMBI

Kisa cha kongamano hili la maombi ni uamsho. Uamsho ni kurejzwa upya kwa maisha ya kiroho ya muumini. Uamsho ni pamoja na ufahamu wa kimungu, kutoa heshima na kukiri dhambi. Inaleta kumrudia Mungu kwa upendo wa ndani kwake na utii mkuu wa amri zake utambuzi asili, machukizo, ungamo la dhambi. Inapelekea katika kumrudia Mungu kwa upendo wa ndani kabisa na utii mkubwa kwenye amri zake.

Wakati wa nyakati za uamsho wa kanisa, kunakuwa na nguvu ya uamsho ya kiroho inayoambatana miongoni mwa hao ambao walikuwa hawajazaliwa upya. Watu pekee na makundi pekee wanavutwa kwenye imani katika Kristo, makanisa mapya yanazaliwa na jamii kubadilishwa. Hii ina maana kwamba uamsho wa waumini ni muhimu kwa upandaji kanisa.

Tumia muda uliobaki wa somo kuombea haya yafuatayo juu ya uamsho. Tumia muda wa kutosha kushiriki katika kila alama kabla ya kuendelea.

### A. Hali za Uamsho

Uamsho unatokea wakati nguvu ya Roho wa Mungu inapopita katikati ya watoto wa Mungu, akiwathibitishia dhambi na kuwataka watubu. Soma mistari ifuatayo kumsaidia kila mwanafunzi kukumbuka kwamba: "Uamsho unaanza moyoni: MOYO WANGU."

#### 1. *Kumpenda Mungu kwa moyo wako wote na kuzitii amri zake*

- Soma Kumbukumbu la Torati 30:1-10.
- Imba nyimbo za kuabudu na kutukuza zinazotangaza upendo wako kwa Mungu.
- Kuwa na muda wa ukimya wa kipekee kumuuliza Mungu kuwaonyesha maeneo katika maisha yao ambayo hayatii kwa ukamilifu amri za Mungu.

#### 2. *Kumtafuta Mungu kwa kiunyenyekevu*

*"Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kiziacha njia zao mbaya, basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao." (2Nya 7:14).*

- kwa pamoja kama watu wake, kwa unyenyekevu kuatafuta uso wake

#### 3. *Kukiri dhambi za mtu na Hatia*

*"Rudi...asema Bwana, sitakutazama kwa hasira, maana mimi ni mwenye rehema, sitashika hasira hata milele. UNGAMA UASI WAKO TU ya kwamba umemwasi Bwana...wala hukutii sauti yangu." (Yer 3:12,13).*

*"Ee Mungu, unichunguze, ujue moyo wangu, unijaribu, uyajue mawazo yangu; uone kama iko njia iletayo majuto ndani yangu, ukaniongoze katika njia ya milele" (Zab 139:23,24).*

- Kuwa na muda binafsi wa kuungama kwa Bwana kwa kimya dhambi yoyote binafsi inayojulikana na kumwomba akusafishe (1Yoh 1:7,9).

### B. Nafasi ya Uongozi Katika Harakati za Uamsho

Mungu amewaweka viongozi kanisani kuwaelekeza watu wake katika njia zake za haki. Wachungaji na wapanda makanisa wanatakiwa kuwa mfano kwa watu wanaoawaongoza.

#### 1. *Viongozi Kuweka Mfano kwa Kuungama Binafsi*

*"Jikazeni mkaomboleze, enyi makuhani; pigeni yowe, enyi wahudumu wa madhabahu; Njooi mlale usiku kucha katika magunia, Enyi wahudumu wa Mungu wangu; Kwa kuwa*

*sadaka ya unga na sadaka ya kinywaji zimezuiwa katika nyumba ya Mungu wetu” (Yoe 1:3).*

2. *Viongozi Kuwaita watu wa Mungu Kuungama*

*“Takaseni saumu, iteni kusanyiko la dini, wazee na wakusanye wenyeji wote wa nchi; waende nyumbani kwa Bwana, Mungu wenu, na kumlilia Bwana” (Yoe 1:14).*

- Gawanyika katika makundi madogo ya maombi kuombea watu wote katika kundi hilo. Omba kwamba waepushwe na mwovu ili kwamba wamtumikie Bwana kwa utakatifu. Katika roho ya upendo na bila lawama, kuombea viongozi wa madhehebu yao, wachungaji, wazee wa kanisa na wasaidizi kwa majina. Kumshukuru Mungu kwa ajili ya na kumwomba Mungu kuyabariki maisha yao, maisha ya familia zao na huduma zao.
- Kumuuliza Mungu kuwasaidia viongozi kujua hatua watakazochukua katika kuwaita watu kwa ajili ya toba.

**C. Nini Unachoweza Kufanya Kuona Uamsho/Kuchochea Katika Nchi Yako**

- Endelea katika vikundi vidogo, muulize Mungu nini ungetakiwa na unatakiwa kufanya kuanzisha hatua za uamsho katika kanisa lako, mji na taifa.
- Muulize Mungu kwamba anapoleta uamsho katika kanisa lake, kwamba angeweza kuleta uamsho hata katika mioyo ya wasioamini kuwaleta wengi kutubu na kuamini.

**D. Kumtukuza Mungu Kwa Ajili ya Uaminifu Wake**

- Unganeni tena katika kundi kubwa moja na tumia muda uliobaki kumtukuza Mungu kwa uaminifu wake wa kutimiza Utume Mkuu kwa kupitia kanisa lake na kumshukuru kwa nafasi ya kumtumikia katika kazi hiyo.
- Funga mkutano wa maombi kwa nyimbo za sifa au pambio inayowakumbusha uaminifu wa Mungu.

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Fanya mafunzo ya kujifunza kwa kulifuata neno katika Ezr 9:1-10:17. Pamoja na majibu kwenye maswali yafuatayo:

- Ni dhambi gani ilikuwa maalumu kwa watu? (Ezr 9:1-2)
- Ni majibu yapi Ezra na viongozi wengine walitoa kwenye dhambi hii? (Ezr 9:3, 5; 10:1)
- Matokeo ya Mungu kwa kile ambacho Ezra aliweka tumaini lake yalikuwa yapi? (Ezr 9:15aa)
- Ni matokeo yapi yalionekana kwa watu walioona toba ya Ezra? (Ezr 10:1-4)
- Ni jinsi gani uamsho uliivamia jamii? (Ezr 10:9-17)
- Kumbuka kuweka pamoja na matumizi katika maisha yako mwenyewe, kanisa lako na jamii yako.
- Andaa kongamano la maombi kwa ajili ya kanisa lako au vikundi vidogo kwa kutumia kipande ulichojifunza katika somo hili.



# Jinsi ya Kuwezesha Maombi

## JINSI YA KUHAMASISHA MAOMBI KWA KUPANDA KWAKO KANISA

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuwasaidia wapanda kanisa kuelewa kwa mbinu wajibu wa maombi katika upandaji kanisa na kuwapa mawazo ya kimatendo jinsi ya kuhamasisha maombi kwa huduma yao ya upandaji kanisa.

### ☞ Wazo Kuu

- Maombi yanasimama katika jukumu la kimkakati kwa upandaji kanisa.
- Kuna njia nyingi za kuwezesha maombi kusaidia upandaji kanisa.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa jinsi ya kuhamasisha maombi kwa ajili ya upandaji kanisa
- Kujua kanuni ya jukumu la kimkakati la maombi katika upandaji kanisa.
- Kushiriki katika maombi na kuhamasisha maombi kwa ajili ya juhudi za upandaji kanisa maalumu.

### ☞ Ziada

3A Maombi ya Utatu

### ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Hili ni somo la warsha. Fanya marudio ya mistari ya ufunguo inayopatikana katika sehemu ya 1 na kisha zungumza na wanafunzi juu ya mawazo ya kuhamasisha maombi kwa ajili ya upandaji kanisa. Ni mbinu zipi wamezajaribu katika kuhamasisha maombi kwa ajili ya huduma zao wenyewe? Shirikisha uzoefu wako kutoka katika huduma yako au maisha ya huduma, ukionyesha jinsi maombi yanavyoongoza upandaji kanisa.

## I. MAOMBI—SURA MUHIMU KWA UINJILISTI NA UPANDAJI KANISA

Mtume Paulo aliamini kuwa maombi yalikuwa kipengele muhimu cha uinjilisti na upandaji kanisa. Aliomba na kuwatia moyo wakristo wa kanisa la kwanza kuomba kwa ajili ya kuenea kwa injili. Tunaona mifano katika maandiko yote ya Agano Jipya:

- Akizungumzia haja yake kwa Wayahudi kupokea injili, Paulo anawaambia waumini Urumi, “Ndugu zangu, nitakayo sana moyoni mwangu, na dua yangu nimwombayo Mungu, ni kwa ajili Waisraeli ili kwamba waokolewe” (Rum 10:1).
- Paulo alipowaonya wakristo wa Efeso juu ya vita vya kiroho walivyotakiwa kuhusika, aliwaambia kuva silaha zote za Mungu na kusimama kinyume na hila za mwovu. Kusimama kinyume na hila za mwovu ilikuwa ni pamoja na kuelewa ukweli wa Mungu juu ya wokovu, kutumia neno la Mungu kama upanga na maombi ya wakati wote. Paulo aliwahoji waefeso “... kuomba katika roho wakati wote kwa maombezi na maombi ya aina mbalimbali. Mkiwa na hili akilini, muwe tayari na mara zote kuendelea kuwaombea watakatifu wote” (Efe 6:18).
- Kuhusiana na maendeleo ya injili, Paulo kibinafsi aliwauliza waumini, “Pia omba na kwa ajili yangu mimi, nipewe usemi kila ninapofungua kinywa changu, maneno yatolewe kwangu ili

niihubiri kwa ujasiri ile siri ya injili...hata nipate ujasiri katika huku kunena jinsi inipasavyo kunena” (Efe 6: 19-20).

- Paulo aliwaandika ujumbe unaofanana kwa waumini wa Kolosai: “jitoeni wenyewe katika kuomba, mkikeshwa katika kuomba huku na shukurani; Mkituombea na sisi pia, kwamba Mungu atufungulie mlango kwa lile neno lake, tuinene siri ya Kristo, ambayo kwa ajili yake nimefungwa, ili niidhihirishe, kama inipasavyo kunena.” (Col 4:2-4).
- Paulo pia aliliambia kanisa la Wathesalonike, “...tuombeane, ili ujumbe wa Bwana uenee kwa haraka na kutukuzwa vilevile kama ilivyo kwenu; na tukaokolewe na watu wasio haki, wabaya; maana si wote walio na imani. Lakini Bwana ni mwaminifu, atakayewafanya imara na kuwalinda na yule mwovu” (2The 3:1-3).


Ni wazi katika mistari hii kwamba kanisa la kwanza waliomba kimikakati kwa ajili ya kuenea kwa injili na dhidi ya kuvutwa na uovu ambao unarudisha nyuma kuenea kwa injili.. Hitaji la maombi kama haya linahitajika leo. Katika kuanzisha na kuweka mkakati wa upandaji kanisa, **yachukulie maombi kwa makini**. Usifanye chochote bila maombi. Huduma yako ya kueneza upandaji kanisa lazima izaliwe kutokana na maombi na kisha kwa kuendelea iza kwa maombi kuanzia mwanzo mpaka mwisho.

## II. JINSI YA KUPANUA MAOMBI KWA UINJILISTI NA UPANDAJI KANISA

Katika sehemu iliyopita, tumeona kwamba mtume Paulo aliyaona maombi kama kipengele muhimu cha uinjilisti na upandaji kanisa. Ni njia zipi za kiutendaji unazoweza kuhusisha waumini kuombea huduma yako ya upandaji kanisa? Mawazo mbalimbali yamejadiliwa katika sehemu hii. Vipengele muhimu kwa kuhamasisha maombi ya upandaji kanisa:

- Mwombe Mungu akuongoze kwa watu wenye mzigo katika eneo lako unalolenga.
- Ujitoe kutawanya taarifa nzuri kati ya kazi yako ya upandaji kanisa na kundi lako la maombi.
- Tia moyo kila mara, maalumu, maombi mazito kwa ajili ya injili kuingia kwenye mioyo ya watu wanaoishi katika eneo lako unalolenga na dhidi ya mvuto wa uovu unaowaweka watu katika vifungo vya Shetani na kuzuia kuenea kwa injili katika eneo lako unalolenga.

### Kielelezo 3.1 Mifumo ya Maombi ya Kimkakati



### A. Maombi ya Kikundi Kiini

Kama itakavyozungumziwa kwenye somo la kikundi kiini, vikundi ni sehemu ambayo watu wanaweza kukutana na Kristo katika neno lake na katika maisha ya waumini walio kwenye vikundi kiini. Vikundi kiini vinatarajiwa kukua na kuongezeka na kwa kila mkutano wa kikundi kiini, muda unatakiwa utumike kuomba marafiki wasio wakristo, jamaa, na wenzi wa wana kikundi. Vikundi kiini pia vinaweza vikataka kutembea katika jamii huku wakiomba kwa ajili ya tukio muhimu la uinjilisti. Viongozi wa vikundi kiini wanaweza kufanya watu kukaa wakijua tukio maalumu la kuomba (zingatia Mwongozo 2 Vikundi Kiini Somo la 4, "Uinjilisti wa Vikundi Kiini").

### B. Maombi ya Utatu

Maombi ya utatu ni mkusanyiko wa watu au familia tatu waliojitoa kukutana pamoja mara kwa mara (kwa wiki au kila baada ya wiki mbili) kuomba kwa ajili ya marafiki 9 wasio wakristo, wenzi, au majirani ambao wangependa waone wamekuwa wakristo. Kwa uhakika, hao walioombewa inatakiwa wawe watu ambao wana kikundi wanawaona au kuongea nao. Maombi ya utatu yamezungumziwa kwa undani zaidi katika ziada 3A.

Maombi ya utatu ni ya maana wakati mpanda kanisa anapokuwa na viini vya waumini walio mstari wa mbele katika eneo lake linalolengwa wanaotaka kumsaidia upandaji kanisa. Wanakuwa njia nzuri ya kuhusisha waumini wapya kuomba jamaa zao na marafiki ambao hawajaokoka. Kwa nyongeza, maombi ya utatu ni ya mafanikio kwa kuhusisha makanisa yaliyopo katika uinjilisti wa jamii zao wenyewe.

### C. Maombi ya Kutembea

Maombi ya kutembea siyo wazo jipya. Huko Ulaya, njia nyingi mashuhuri zilitengenezwa na watawa waliokuwa wakitembea na kuomba kwenye safari ya kwenda kuzulu kanisa kuu la mji hadi kanisa kuu mjini. Maombi ya kutembea yanawawezesha washiriki kwenda nje kuona na kuwa mahali palipo na mahitaji. Tunapokuwa tumejifungia ndani, hatuwezi kuwa sawa na kama mtu unayeona uso kwa uso hali halisi ya maisha na mahitaji. Kutembea na kuzungukia ujirani kwa maombi inatoa mtazamo mpya kwa ujumla katika ujirani huo na mahitaji yake kuliko kufanya matembezi ya kupendeza kuzungukia ujirani huo huo.

Katika upandaji kanisa, maombi ya kutembea ni zana inayoweza kusaidia kuvunja ardhi iliyolimwa na kutopandwa kitu na kutayarisha udongo wa mioyo ya watu kupokea injili. Maombi ya kutembea ni lazima yafanywe na kundi la wapanda kanisa au watu wengine wenye mzigo wa eneo maalumu linalolengwa upandaji kanisa. Wafanya maombi ya kutembea wanahitaji kutembea na kuomba kuzunguka, katikati, na kwenye eneo linalolengwa kwa kurudia rudia. Wanatakiwa kufanya hili wakimsikiliza Roho Mtakatifu.

Maombi ya kutembea yanatakiwa kufuatiwa na uinjilisti wa kimikakati. Uinjilisti lazima utanguliwe na kufuatana na maombi. Kama wewe na kundi lako la upandaji kanisa mnakwenda kusambaza vitabu, kuonyesha filamu ya Yesu, kulisha masikini, au kufanya aina nyingine ya shughuli ya uinjilisti, ufunguo muhimu kwa aina hiyo ya huduma ya nje inatakiwa kuhusisha maombi kabla na baada ya shughuli. Maombi ya kutembea yana tabia ya kuvunja ardhi ngumu na kuandaa mioyo na nyumba kwa kupanda mbegu ya neno la Mungu. Mitaa ambayo imeombewa mara nyingi kwa njia hii ina matunda zaidi kuliko mitaa ambayo haijaombewa.

Maombi ya kutembea yanaweza kufanywa kwa njia nyingi: Mtu peke yake, au kikundi kidogo. Michanganuo ifuatayo miwili ni mifano halisi ya jinsi maombi ya kutembea yalivyotumika kama sehemu ya huduma ya upandaji kanisa.

#### Mchanganuo 1:

Ujirani uliojulikana kuwa na idadi kubwa ya familia zenye matatizo ulikuwa umelengwa kupandwa kanisa. Matatizo ya kijamii kama vile kukosa ajira, kuvunjika kwa familia, madawa ya kulevya na ujambazi vilikuwa sugu. Mwanzoni mwa juhudi za upandaji kanisa, maombi ya kutembea yalikuwa yamepangwa katika kila mtaa kwenye ujirani huo. Walivyotembea na kuomba, walinukuru utambuzi wote Roho Mtakatifu aliowaonyesha. Waombaji wengine wengi walifuatia maombi hayo ya kwanza. Baadhi ya maombi ya kutembea yakafanyika kuzunguka shule, mengine katika na karibu na soko, mengine kwenye mzunguko wa ujirani. Na wengine walifanya kwenye misitu inayoangaliana na



ujirani. Katika misitu hiyo, iliyojulikana kama sehemu ambayo madawa yalikuwa yakitolewa na wenye nayo, alama za wachawi ziligunduliwa kwenye miti. Kikundi cha maombi ya kutembea walitumia muda kuombea nguvu hizo za uovu. Katikati ya miaka mitatu tangu ujirani ulipolengwa upandaji kanisa, matatizo ya kijamii yakawa yamekwisha, ujambazi ukapungua kwa asilimia 40 na kanisa la watu 70-80 likawa limepandwa. Kuna mguso wa kiroho sasa wa kutia changamoto nguvu ya uovu wa uvamizi, na Mungu anafanya kazi katika maisha ya wengi (DAWN Europa Mwongozo wa Maombi, August 1994, Uk 13)

### **Mchanganuo 2:**

Mpanda kanisa na familia yake walihamia katika nyumba za kupanga katika mji ambapo walikuwa na haja kuona kanisa limeanzishwa. Jioni sana moja, familia yote ilitembea kuzunguka nyumba nzima waliyopanga. Walisimama mbele ya kila mlango na kila mmoja akaomba watu walioko kwenye nyumba hiyo. Kijana mdogo aliomba kwamba kila mtu katika nyumba hiyo amwombe Yesu kuingia moyoni mwake. Msichana mmoja akaomba kwamba mahitaji ya fedha yatimizwe, msichana mwingine akaomba kwa ajili ya mahusiano mazuri katika familia. Mama yao akaomba kwa ajili ya afya ya jamaa katika familia hizo na baba akaomba kwa ajili ya baraka za Mungu kwa wote walio katika nyumba. Baada ya maombi ya kutembea, mpanda kanisa na familia yake waliona watu 14 katika nyumba hiyo wakienda kwa Yesu na kanisa dogo likaanza.

*Kutafakari kwa Vitendo Kwa Maombi ya Kutembea*

- Onyesha maeneo ya kufanya maombi ya kutembea. Utahitaji kuamua kama utachukua eneo dogo na mara kwa mara ukaliombea kwa kutembea (mf. Mara moja kwa wiki) au kuchukua eneo kubwa kidogo kidogo. Uamuzi huu unatakiwa kufanywa pamoja na mpanda kanisa au na kikundi ili kwamba maombi ya kutembea yaweze kuunganishwa na uinjilisti na shughuli za uinjilisti.
- Tenga muda maalumu kwa maombi ya kutembea. Maombi ya kutembea kwenye makundi ya wawili au watatu. Hii haitishi sana kwa watu kuona watu wawili au watatu wakitembea tembea pamoja, haitoshi wakiwa katika maongezi kuliko kundi kubwa au mtu mmoja. Tenga muda wa maombi kwa ajili ya maombi ya kutembea.
- Amua juu ya egemeo maalumu la maombi, kama vile ulinzi kwa watoto, maombi kwa ajili ya masikini, kumgeukia Kristo, mapatano ya ukabila, n.k. (Fungu la E chini lina orodha ya vichwa vilivyoshauriwa). Amua juu ya mstari wa kifungu maalumu wa kuegemeza maombi yako. Kwa mfano, unaweza ukataka kutumia vipande vya maneno ya maombi ya Yesu kuelekeza maombi yako. Au, unaweza kuchagua kuomba kwenye mistari ya Zaburi.
- Kutembea kwa taratibu, lakini kwa hatua zisizo za kusita, ukizungukia maeneo yanayozunguka iwezekanavyo, bila kukaza macho mara kwa mara. Omba macho yako yakiwa wazi na katika namna ya maongezi, ukimwambia Mungu juu ya mahitaji ya watu wanaokuzunguka, nyumba unazopita, shule, maduka au viwanda n.k. Wakati mwingine omba kimya kimya, hasa unapokuwa unakutana au kupishana na watu wengine.
- Mwishoni mwa maombi ya kutembea, shirikishaneni kwa pamoja. Andika mawazo na mvuto katika kitabu chako cha kumbukumbu. Weka tarehe ya maombi mengine ya kutembea.

### **D. Timu ya Kusaidia Maombi**

Kila mpanda kanisa au timu ya upandaji kanisa inatakiwa kujaribu kuandaa na kuanzisha timu ya kusaidia maombi. Hawa ni watu kutoka kanisani kwako au wakristo wengine marafiki au familia nyingine zenye mzigo wa kukuombea na timu yako, familia yako na huduma yako ya upandaji kanisa. Waombe watu wakuombe mara kwa mara, kama vile mara moja kwa wiki, kila siku, au kila mwezi. Andika majina ya wanaokusaidia katika maombi na siku walizojitua kukuombea kwenye kalenda. Hii itakusaidia kukumbuka anayekuombea na lini wanakuombea ili ujue nani wa kuwasiliana kwa maombezi ya haraka.

Timu inayokusaidia katika maombi inaweza kuamua kukutana pamoja na kuomba kwa kushirikiana kwa ajili yako na huduma—mara moja kwa mwezi au hata mara nyingi. Mmoja kati ya timu ya maombi anaweza kuchukua wajibu wa kuwasiliana na mpanda kanisa au timu ya upandaji kanisa kwa ajili ya kupata maombezi ya wakati huo na majibu kwa maombi. Timu ya maombi inahitaji kujulishwa majibu ya maombi na mahitaji mapya ya kuombea ili kwamba wafurahi juu ya yale Mungu anayofanya na ili kwamba kutiwa moyo kuendelea kuomba.

#### **E. Vichwa Vya Maombi ya Kimkakati**

Vikundi kiini, watembeaji, na timu ya kusaidia maombi wote wanahitaji vichwa maalumu juu ya nini wakazie juhudi za maombi yao. Ifuatayo ni mifano ya vichwa vya maombi vinavyoweza kutumika wakati wa maombi ya kutembea au na timu za maombi. Katika utafiti wako, utakuwa umejifunza vitu vingine maalumu vya kuombea pamoja na vilivyoorodheshwa hapa.

- Kwa ajili ya familia, ili kwamba watiwe nguvu na kubarikiwa, na Shukurani kwa Bwana.
- Kwa wasiokuwa na ajira, ili kwamba waweze kupata kazi.
- Kwa ajili ya makanisa na watu binafsi, ili kwamba wawe na kiu ya Mungu.
- Kwa ajili ya shule, kwamba walimu na wanafunzi wajue amani, mapatano na upendo wa Yesu.
- Masoko na mabenki, kwamba haki itendeke kuhusu pesa.
- Kwa serikali za mitaa, kuwa sehemu za haki mahali ambapo uamuzi mzuri unafanyika na madaraka yatumike sawasawa.
- Omba Mungu awadhahirishe walinda mlango, wale ambao wana nguvu katika jamii zao na kama wakiletwa kwa Kristo watafungua njia ya kusonga mbele kwa injili.

### **III. UTAFITI: UKUSANYAJI HABARI KWA AJILI YA MAOMBI**

Moja ya shughuli za kwanza ulizofanya kama mpanda kanisa ilikuwa ni kutafiti eneo lako unalolenga (Mwongozo 1, Maono ya KUM Somo la 4 “Kanunu za Utafiti”). Tumia utafiti huo sasa kama kiongozi.

Ulianza utafiti wako kwa kuonyesha makanisa na makundi ya umishenari yanaofanya katika eneo unalolenga. Omba kila mmoja kwa jina; kwa ajili ya kukua kwao kiroho; kwa ajili ya kufikia eneo lao, kwa tatizo lolote unalojua wanalo. Kanisa limefahamika kama linafanya mchango mzuri au mbaya kwenye eneo? Kuna historia yoyote ya mgawanyiko au ya ushirikiano? Kanisa linakua? Wapi? Omba kama Yesu alivyoomba katika Yohana 17:23, “kwamba waweze kuletwa katika umoja kamili kuufanya ulimwengu kujua kwamba umenituma na umewapenda kama unavyonipenda mimi.”

Kadiri unavyoendelea kuomba, kumbuka makundi tofauti uliyoyagundua katika shamba lako la mavuno ya utafiti. Kuna eneo lolote ambalo wamewahi kujulikana kama masikini, matajiri, ukahaba, mateso, n.k.? Muulize Mungu kukuonyesha jinsi unavyoweza kuwafikia watu katika makundi tofauti. Kuna hitaji lolote la kimwili ambalo unahitaji kuwa unalitimiza kwa jina la Kristo? Kuna kizazi chochote kipya, cha siri au cha kishetani au vitovu? Omba Mungu awatoe watu wake kutoka katika mvuto wa maovu kutoka katika makundi haya (Mt 6:3). Waombe viongozi wa serikali kwa majina na watu mashuhuri katika jamii. Muombe Mungu kukupa nafasi ya kukutana na watu ambao wanaweza kufungua milango kwa ajili ya injili.

Habari ulizopata katika utafiti wako zinatakiwa kuwa sehemu yako ya maombi ya kila siku kwa jamii unayolenga. Endelea kuzitumia kuonyesha maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa maombi ya kutembea na kukupatia ufahamu wa uinjilisti kwenye huduma zinazoweza. Shirikisha habari hizi kwa timu yako ya maombi na wengine wenye mzigo wa eneo lako unalolenga.

### **SULUHU**

Kuna msemo miongoni mwa wakristo kwamba “Jeshi la Mungu linasonga mbele kwa ushindi kwenye magoti yake.” Neno hili linachukua picha ya mkakati wa nafasi ya maombi katika kuendelea kwa ufalme wa Mungu ulimwenguni. Upandaji kanisa ni kazi ya kiroho, inayohusisha vita vya kiroho dhidi ya nguvu za giza (Efe 6). Kama mpanda kanisa, kazi yetu lazima izaliwe katika maombi, kuendelezwa

kwa maombi na kusindikzwa kwa maombi. Kwa namna hiyo tu ndiyo itazaa matunda yaliyokusudiwa na Mungu.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni jinsi gani unavyojitoa kwenye maombi (Col 4:2-4) au kuomba wakati wote (Efe 6:18) Kama Paulo alivyowasihia kufanya?
- Umeshawahi kuwa katika maombi ya kutembea? Eleza uzoefu wako. Ulifanya nini? Ulienda wapi? Ni mambo gani uliyoyaomba? Ni kwa jinsi gani iliwezesha huduma yako katika eneo hilo?
- Ni mawazo gani mengine ya kusaidia kuwezesha maombi kwa ajili ya huduma yako ya upandaji kanisa?
- Ni njia zipi unazoweza kuendelea kutaarifu timu yako ya maombi juu ya maombezi na majibu ya maombi?
- Ni aina gani ya habari unadhani ni mwafaka kushirikisha timu ya maombi na habari zipi si mwafaka kushirikisha?
- Toa mfano wa jinsi ulivyoona maombi yakiungana na uinjilisti. Matokeo yake yalikuwa ni yapi?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Kama hujafanya hivyo, anzisha timu yako ya maombi. Waombe angalau waumini watatu kuomba huduma yako kila wiki. Ni jinsi gani utaendelea kuwajulisha maombezi na majibu ya maombi?
- Fanya angalau mara moja maombi ya kutembea katika eneo lako unalolenga pamoja na timu yako ya upandaji kanisa au wengine wenye mzigo kuona eneo hilo limefikwa kwa ajili ya Kristo. Jadili uzoefu huu pamoja na mshauri au mkufunzi.

### **VYANZO**

- Livingston, Glenn. *Prayer that Strengthens and Expands the Church*. South Holland, IL: 1999. (This *Alliance for Saturation Church Planting* publication is available from The Bible League, 16801 Van Dam Road, South Holland, IL, 60473 USA. tel 1-800-334-7017. Email: BibleLeague@xc.org)
- Mills, Brian. *DAWN Europa Prayer Manual*. Birkshire, England: DAWN Europa, 1994.



## Maombi ya Utatu

### I. NINI MAANA YA MAOMBI YA UTATU?

Ni njia fupi inayofaa kuwaleta watu kwa Kristo. Unaungana tu na wakristo wengine wawili na kuomba pamoja mara moja kwa ajili ya wokovu wa marafiki tisa au jamaa wasiomjua Yesu Kibinafsi. Kisha furahi unapona Mathayo 18:19-20 inatimia: *“Tena nawaambia, ya kwamba wawili wenu watakapopatana duniani katika jambo lolote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni. Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo hapo katikati yao.*

### II. JINSI YA KUFANYA MAOMBI YA UTATU KUFANYA KAZI

- A. Chagua marafiki wakristo wawili au jamaa kufanya “utatu” wako.
- B. Kila mmoja wenu achague majina matatu ya watu wasiomjua Yesu kama mwokozi na Bwana wa maisha yao.
- C. Kubaliana muda wa kukutana mara moja kwa wiki kuomba pamoja kwa ajili ya watu wenu tisa. Mnaweza kukutana majumbani kwenu, sehemu mnakofanya kazi, shuleni au mbele ya kanisa.
- D. Omba kwa ajili ya watu tisa kwa majina kumkubali Kristo kama Bwana na mwokozi wa maisha yao. Ikiwa ni pamoja na mahitaji yao na ya jamaa katika familia zao.”
- E. Kadiri iwezekanavyo, kadiri Mungu anavyoweza, jihusishe mwenyewe na “watatu” kirafiki, kwa njia inayosaidia. Mwangalie Mungu kukupa nafasi ya kushirikisha habari ya injili na watu hawa. Ombeaneni mnapotaka kufanya hili.
- F. Wakati watu ambao umekuwa ukiwaombea wanapokuwa wakristo, endelea kuwaombea kadiri Mungu anavyokuongoza, lakini katika utatu wenu chagua marafiki wengine na jamaa wa kuombea ambao hawajamjua Yesu. Mwelekezo wa maombi ya utatu lazima uwe ni marafiki na jamaa wasiomjua Yesu Kipekee. Tambua: *Unaweza kutaka kuomba kama familia kwa kutumia wazo la “maombi ya utatu”!*

### III. KARATASI YA MAZOEZI KWA MAOMBI YA UTATU

- A. Washiriki wangu wa maombi ya utatu ni:

- \_\_\_\_\_
- \_\_\_\_\_

- B. Tunaombea:

Orodhesha majina ya marafiki tisa wasiookoka ambao maombi yako ya utatu yatawaombea mara moja moja

Orodha yangu:	Orodha 2	Orodha 3

---

## **NJIA ZA KUJIFUNZA BIBLIA**

---



# Utangulizi Kwenye Njia Za Kujifunza Biblia kwa kufuata Neno

## KURUHUSU BIBLIA KUTUFUNDISHA

### ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kutambulisha njia za kujifunza Biblia kwa kufuata neno la Mungu, na kuelezea kwa nini njia hii ni bora kwa njia zingine za kujifunza Biblia.

### ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kufahamu tofauti kati ya kutumia mawazo na kufuata neno
- Kushawishika kuwa njia ya kufuata neno ni njia bora kuliko “njia za kawaida” za kufanya mafunzo ya Biblia.

### ☞ Wazo Kuu

- Kutumia mawazo na kufuata neno ni hoja zenye mwelekeo tofauti.
- Njia ya kujifunza kwa kufuata neno ni bora zaidi kujifunza kitu kipya kutoka katika neno
- Hatua za njia ya kulifuata neno ni : uchunguzi, kulifafanua, kuitumia.
- Wakati njia ya kujifunza kwa kufuata inapokuwa haikuharakishwa, inatoa msingi imara wa kuelewa Biblia.

### ☞ Ziada

1A Jinsi Tulivyopata Biblia.

## UTANGULIZI

Biblia ni kitabu muhimu ambacho kimewahi kuandikwa. Inadaiwa kuwa neno hai la Mwenyezi, Mungu asiye na mwisho, aliyejitoa kijidhihirisha kwa mtu aliye na mwisho. Biblia pia ni zana muhimu zaidi kwa mpanda kanisa wa kisasa au mchungaji. Neno la Mungu “hai na lenye nguvu” lina uwezo wa kuiingia mioya na nafsi za hao tunaotafuta kuwaleta kwa Bwana. Linatuandaa kwa kila kazi njema, ambayo kwa hakika inaelezea huduma yetu ya kuongeza makanisa kuzunguka ardhi. Linasimama kama kiwango ambacho tunapima na kuathimini kila mafundisho, matendo, mapokeo na akili ya kibinadamu inayoweza kupotosha, lakini Biblia inasimama kidete kama kweli ya Mungu. Mafundisho yake wakati wote ni ya kweli. Unabii wake mara zote unatimia. Neno lake linatusaidia kuleta waliopotea na kukataa uovu. Biblia ni ya lazima kwenye maisha yetu ya ukristo na huduma.

Kwa kuwa tunaamini kuwa Biblia ilitolewa kwetu na Mungu kuwa maelekezo yetu, tunahitaji kuikabili kwa uangalifu na kuichukua kwa usahihi (2Tim 2:15). Asili ya maandiko inataka kwamba tunaisoma kwa kusudi la kujifunza kutokana nayo kuliko tu kuitumia kusema kile tunachotaka kusikia. Tunawezaje kuwa na uhakika kuwa tunalielewa neno? Njia ya kujifunza kwa kufuata neno imeandaliwa kumsaidia kila muumini—awe ni wa kawaida au mchungaji—ni bora kuelewa mafundisho ya neno la Mungu. Somo hili litatambulisha njia rahisi na ya mafanikio, na masomo yanayofuata yataelezea kila hatua kwa undani zaidi.

Njia ya kujifunza kwa kufuata neno imeandaliwa kumsaidia kila muumini—awe ni wa kawaida au mchungaji—ni bora kuelewa mafundisho ya neno la Mungu.

## I. KUFUATA NENO DHIDI YA KUPUNGUZA

Kupunguza na kufuata ni aina mbili za kumaanisha au kutolea uamuzi. Zote zinashughurika na ujumla na maalumu. Zote ni njia za kufikia suluhu. Kwa jinsi hiyo, zinafanya hivyo kwa tabia tofauti kabisa. Hoja ya upunguzaji inaendelea kutokea kwenye ujumla na kuelekea kwenye maalumu, na hoja ya kufuata inakwenda kutokea kwenye maalumu kuelekea kwenye ujumla. Njia zote zinatumiwa na wakristo kujifunza Biblia, lakini mara nyingi hawafahamu jinsi kila njia inavyogusa kujifunza kwao na matokeo.


### A. Njia ya Kupunguza

Hoja ya kujifunza kwa kupunguza neno inatumiwa na watu katika mapana tofauti tofauti ya ujuzi. Kupunguza ni ujuzi wa thamani, na vitabu vingi vimeandikwa juu ya somo hilo. Kusudio la somo hili siyo kushusha utoshelevu wa njia ya kupunguza, lakini kushauri kwamba ni njia hafifu ya kujifunza Biblia.

#### 1. Hoja ya kupunguza

Kwa ujumla, kupunguza mawazo inaelekea kutokea kwenye ujumla na kwenda wenye maalumu. Hii ina maana, inanza na wazo linalojulikana na kukubaliwa au mahali ambapo suluhu inatolewa. Kueleweka kulikopo kisha kunalinganishwa na hali fulani, na kisha uamuzi unafanywa. Msingi wa suluhu hii ni ukweli kwamba wazo la jumla ni kweli, na kwamba hali maalumu inafanana nalo. Kwa maneno mengine, wazo la jumla linatawala, au angalau kwa mguso mkuu kwa namna tunavyotazama hali fulani. Kwa mfano, kwa kuwa hatua zilizomalizika za barafu kawaida zinateleza, tutakaribia kila dozeni ya barafu kwa tahadhari—hata kama hatujawahi kuteleza kwenye barafu hiyo maalumu. Uzoefu wetu kwa ujumla na hatua kwenye barafu unatufikisha kwenye maana hii na suluhu ya kweli. Kielelezo 1.1 kinaonyesha hoja ya kupunguza.

Kielelezo 1.1 Hoja ya Kupunguza



Hoja ya kupunguza ina udhaifu mkuu. Kama kuelewa kwetu kwa ujumla ni makosa, hata uamuzi utakuwa makosa. Kwa mfano, inatokea Mrusi anasikia mtu fulani anaongea juu ya daktari. Urusi, madaktari wengi ni wanawake. Kwa hiyo, itakuwa na maana kwake kufasiri kwamba daktari ni mwanamke. Mara nyingi, kwa hiyo, itakuwa amekosea. Kuna wanaume madaktari pia Urusi, na katika nchi zingine madaktari wengi ni wanaume. Katika hali hii, mguso wa uzoefu wetu wa mwanzo unaweza kutuongoza katika mwelekeo mbaya. Tunadhania tunajua jibu, kuliko kuendea kuangalia alama zingine za jibu sahihi.

#### 2. Kujifunza Biblia kwa Njia ya Kutumia Wazo (Kupunguza)

Njia ya kutumia mawazo inaweza kutumika kujifunza Biblia, lakini udhaifu wake unapunguza matumizi yake. Tunapojifunza Biblia, ni muhimu *kuelewa kile Mungu anachosema*, kuliko tu kuweka kuelewa kwetu kwa aya. Kuna nyakati ambazo hatuwzi kuelewa mstari mgumu, na tunaegemeza kuelewa kwetu kwa ujumla kwa maandiko kupunguza ambacho *“pengine inachomaanisha.”* Kwa jinsi hiyo, hii inatakiwa kuwa

“kimbilio la mwisho” Hatua yetu ya kwanza lazima iwe kuomba, kuutafakari mstari, kuendelea kurudia kuusoma ili kujaribu kuweza kuelewa unavyotaka kusema. “Kama tunakata tamaa mapema” na kudhani kuwa uko “kama mistari mingine inayofanana,” tunaweza kupotosha neno la Mungu vibaya sana. Kwa mfano Agano Jipya linatumia “hamira” zaidi ya mara saba ikirejeza kwenye dhambi. Inaweza kuwa kwa hiyo jambo la maana na msingi kudhani kuwa mara kumi na moja (Mt 13:33) pia inahusu dhambi. Ingekuwa, kwa hiyo, makosa. Uchunguzi wa mandhali ya Mathayo 13:33 inaonyesha kuwa katika mstari huo, ina maanisha kwenye ufalme wa Mungu!

### 3. Njia ya “Kawaida”

Hata hivyo, njia ya kutumia wazo pengine ndiyo njia kuu inayotumika katika kujifunza Biblia. Matokeo yake, wachache wanajifunza vizuri kutoka kwenye Biblia. Kwa kuwa wanakwenda kwenye Biblia walishakuwa na hali ya kuelewa ina maana gani. Hawawezi kugundua na kujifunza kutoka katika wingi wa maana ya maneno.

Walimu wa Biblia mara nyingi wanafahamu kilichopo wanachotaka kusema, na kwa kifupi wanakwenda kwenye Biblia kutafuta mstari unaoonekana kusaidia kuelewa kwao. Neno la Mungu kwa hiyo linatumika kama nguzo ya ujumbe wetu, badala ya kuruhusiwa kuwasilisha wazo ambalo Bwana alikuwa amelikusudia kusema.

Walimu wa Biblia mara nyingi wanafahamu kilichopo wanachotaka kusema, na kwa kifupi wanakwenda kwenye Biblia kutafuta mstari unaoonekana kusaidia kuelewa kwao.


## B. Kutumia Njia ya Kujifunza kwa Kufuata Neno

Njia ya kujifunza Biblia kwa kufuata neno ni kinyume katika namna nyingi na njia ya kujifunza kwa kutumia wazo. Inachunguza umaalumu wa hali, na kisha kujaribu kuunda kanuni ya jumla kutokana na maneno. Kwa kawaida ilitumika katika hali hizo ambazo hatuna kanuni ambazo zinaonekana kufaa, na kwa hiyo kutokuweza kutumia njia ya mawazo.

### 1. Hoja katika Kutumia Neno

Utumiaji kimuhimu ni utaratibu wa kutumia ujuzi uliokwisha kuwepo. Utumiaji, kwa kutofautisha inahusu *kujifunza*. Tunadhani kwamba hatujui majibu, na kuchunguza ukweli kwa karibu ili kujaribu kuelewa *yana maana gani*. Katika njia hii, msisitizo ni juu ya mambo maalumu na ukweli wa hali halisi. Kielelezo 1.2 kinaonyesha mwendelezo wa njia ya kujifunza kwa kuongozwa na neno.

### Kielelezo 1.2 Njia ya Kujifunza Kwa Kufuata Neno



### 2. Kujifunza Biblia kwa Kufuata Neno

Tunapotumia njia ya kujifunza Biblia kwa kufuata neno, tunakuja kwenye maandiko kama wanaojifunza. Tunakiri kwa mtu na kwetu wenyewe kwamba bado hatujui majibu yote. Kusudi letu ni kupata ufahamu. Tunakwenda kwa kujitoa kwa uangalifu kuchunguza maandiko, na kumruhusu Bwana kuzungumza nasi kupitia hayo. Njia ya kujifunza kwa



kutumia mawazo mara nyingi inapelekea mahubiri ya haraka—na njia ya kujifunza kwa kutumia neno inapelekea kukua kiroho.

### 3. Njia Bora

Njia ya kujifunza kwa kufuata neno ni ya juu zaidi kwa njia ya kutumia mawazo kwa sababu inayafanya maandiko kuwa mamlaka, kuliko ufahamu wetu. Ni bora vilevile kwa sababu inaoana na hatua ya kuelewa na kutumia kanuni za kibiblia katika maisha yetu. Tunapokuwa tunajifunza Biblia, tunaangalia juu ya jinsi Mungu alivyotenda na watu katika hali maalumu, na wakati maalumu na katika utamaduni maalumu. Kazi yetu ni kuchukua ukweli huu na kutunga kanuni za kibiblia kutokana nao. Na kisha tunatafsiri kanuni hizo kwenye hali zetu zinazofanana ili kwamba kwa usahihi tuutumie katika maisha yetu. Utaratibu wa njia ya kujifunza Biblia kwa kufuata neno kwa hiyo ni:

- Uchunguzi wa ukweli katika mazingira ya kimaandiko.
- Ufafanuzi kupata kanuni ambayo mstari unafundisha.
- Matumizi ya kanuni kulinganisha hali katika maisha yetu.


## II. HATUA ZA KUJIFUNZA BIBLIA KWA KUFUATA NENO

Hatua tatu za kujifunza Biblia kwa kufuata neno kila moja ni muhimu. Zinajenga kwa kuendelea juu ya moja kwa nyingine kutuongoza kutokana na maandiko ya Biblia kwenye matumizi sahihi katika maisha yetu. Ki kawaida, hatua tatu zinauliza maswali matatu tofauti juu ya maandiko.

- Inasemaje? (Uchunguzi)
- Ina maana gani? (Ufafanuzi)
- Nifanye nini? (Matumizi)

Uhusiano kati ya kila hatua umeonyeshwa katika kielelezo 1.3. Tambua maendeleo ya msingi kupitia hatua hizi tatu, ukianza na maandiko ya Biblia, na kumaliza na matumizi katika maisha yetu ya ukristo. Kama hatua hazikumalizika katika utaratibu mzuri, matokeo yake ni kombo.

Kielelezo 1.3 Hatua Tatu



### A. Uchunguzi—Linsema Nini?

Hatua ya kwanza ya kujifunza Biblia kwa kufuata neno ni uchunguzi. Vilevile ni hatua muhimu sana –kama ulivyo muhimu msingi wa jiwe katika ujenzi wa nyumba. Katika hatua hii, tunayachunguza maandiko, tukiangalia undani tunaoweza kupata kutoka humo, na kuandika uchunguzi wetu. Ufunguo kwa hatua hii ni kuuliza mtiririko wa maswali usioisha kama “nani”, “Nini”, “kwa nini”, “Lini”, n.k.” Maswali haya yanatusaidia kukazia juu ya kile *Biblia inachosema*, kuliko kuiwekea mawazo yetu. Tunaangalia pia kwenye maana ya mazingira ya mstari,

kifungu, ukurasa na kitabu kugundua na kuelewa hali ilivyokuwa wakati kifungu kilipoandikwa. Katika hatua hii, ni muhimu *kutofafanua kutumia* andiko. Ni lazima tugundue habari zote kwanza—katika hatua inayofuata (Ufafanuzi ) tutaangalia nini inachomaanisha.

#### **B. Ufafanuzi—Nini inamaanisha?**

Utaratibu wa ufafanuzi una hatua tatu. Sehemu ya kwanza ni kuchunguza *nini kifungu kilikuwa kimekusudiwa kwa wasikilizaji wa mwanzo*. Hatua ya pili ni kutunga ujumbe wa fungu kama kanuni ya kibiblia inayoweza kutumiwa kwenye hali nyingine zinazofanana,

Hii ni hatua ngumu, inayohitaji makini na mawazo ya kimaombi, na uongozi wa Roho Mtakatifu. Katika hatua hii, tunahitaji kulinganisha ufahamu wetu wa kihistoria wa kwanza, kijiografia, kisiasa, kiutamaduni, na hali ya kidini pamoja na ukweli kuwa hatujafunuliwa katika hatua ya uchunguzi. Kila ukweli ambao tumeupata katika uchunguzi utarudisha nyuma kazi yetu hapa. Sasa ni wakati wa kulinganisha maandiko haya na vifungu vingine vinavyofanana kuona kama vinaweza kutusaidia kulielewa—kuwa mwangalifu kwamba hayapotoshi ukweli wa maandiko tunayojifunza. Kama maana ya kifungu bado haiko wazi, inaweza kuwa muhimu kurudi kwenye hatua ya uchunguzi na kuendelea kuchimbua juu ya habari zaidi.

#### **C. Matumizi—Nifanye Nini?**

Hatua ya mwisho ya njia ya kujifunza kwa kulifuata neno ni matumizi. Katika hatua hii, tunachukua matokeo ya hatua ya ufafanuzi na kuamua namna kanuni itakavyotumika katika hali zetu. Kwa kuwa tumeangalia kwa uangalifu katika maana ya mazingira ya kwanza, na kujua undani wake, tunaweza kuangalia mazingira yanayofanana katika siku zetu.

Ugumu wa hatua hii ni kuonyesha ni hali gani leo ina tabia sawa na hali ya kwanza. Tunaweza tu kusema, “Hivi ndivyo asemavyo Bwana” kama tunaweza kuonyesha kwamba usawa huu upo. Kama hali zetu ni sawa na kifungu cha kibiblia, kisha tunaweza kudhani kuwa Bwana anatarajia kutoa ujumbe kwenye maisha yetu. Katika hali hiyo, kazi muhimu ni kueleza kimaalumu na kwa uwazi “Nini tunatakiwa kufanya.”

### **III. KUJENGA PIRAMIDI IMARA**


Ni muhimu kutovuka moja ya hatua, au kubadili utaratibu. Haiwezekani kusema kwa usahihi kabisa maana ya kifungu kabla ya kuanza kwanza kufanya uchunguzi kikamilifu, na haifai kuuliza ni nini tufanye bila kujua maana ya maandiko. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwamba tunatumia muda unaofaa kutumia njia ya kujifunza kwa kufuata neno sawasawa.

#### **A. Kuharakisha Utaratibu**

Kosa la kawaida katika kutumia njia ya kujifunza kwa kufuata neno ni kutumia muda kidogo sana katika ngazi ya uchunguzi. Mtu anayejifunza Biblia anatupa jicho haraka kwenye fungu na kudhani kuwa anajua nini linasema. Hii inavunja utaratibu wa kijifunza. Matokeo yake ni kulielewa fungu ambalo ni sawa sawa na wakati utaratibu ulipoanza. Neno halikuruhusiwa kutuzungumzia au kutufundisha. Kama tunaliendea neno la Mungu kwa njia hii, kuelewa kwetu kwa biblia kutadumaa. Biblia ni hai na yenye nguvu. Hatuwezi kamwe kuelewa undani wa mafundisho yake. Mara zote kuna kitu zaidi kwa mwanafunzi yeyote cha kujifunza kwenye neno—kama tutatoa muda na juhudi kulielewa.

Mara zote kuna kitu zaidi kwa mwanafunzi yeyote cha kujifunza kwenye neno—kama tutatoa muda na juhudi kulielewa.
--

#### Kielelezo 1.4 Misingi Mizuri na Mibaya



Wakristo wengi wanawahisha utaratibu kwa sababu wako kwenye haraka ya kwenda kuandaa ujumbe kwa wengine. Au, wanaweza kuwa wavivu. Kwa njia yoyote, matokeo ya maandalizi haya hafifu ni mahubiri dhaifu, bila nguvu ya Mungu nyuma yake. Kuharakisha kwenye utaratibu kunaweza kulinganishwa na piramidi iiyoelekezwa juu chini kushoto kwa kwa kielelezo 1.4. Uchunguzi wa kizembe unapanuliwa katika ufafanuzi wa haraka, au ufafanuzi uliokwisha kuwepo “unang'ang'anizwa” kwenye andiko linaloweza kuuunga mkono au la. Mwishoni, mahubiri au ujumbe unajengwa juu ya msingi huu unaotikisika. Kwa bahati mbaya, Hii inaweza kuwa aina kuu ya mafundisho katika makanisa leo.

#### B. Msingi Imara

Piramidi ya mkono wa kulia katika kielelezo 4.1 inaeleza matumizi sahihi ya njia ya kujifunza kwa kufuata neno. Tambua uchunguzi huo ndio wenye sehemu kubwa, ikifuatiwa na ufafanuzi, na matumizi ndiyo ndogo zaidi. Kwa hiyo, matumizi ni imara na hai—ikiwa yamesimama kwenye mafundisho kamili ya neno.

Njia ya kujifunza Biblia kwa kulifuata neno inaweza kulinganishwa na uchimbaji wa madini. Kwanza, tani za miamba zikiwa zimebeba dhahabu zinavunjwa katika vipande vidogovidogo na kuoshwa (uchunguzi). Inayofuata, Miamba iliyovunjwa inachekechwa kutafuta vipande vya dhahabu (ufafanuzi). Mwisho, vipande vya dhahabu vinayeyushwa na kuundwa katika mapambo ya viti vingine kwa ajili ya wateja (matumizi). Utaratibu unazalisha kiasi kidogo cha dhahabu ukiulinganisha na uzito wa kwanza wa miamba. Hata hivyo, matokeo yanakuwa ya thamani sana. Katika njia inayofanana, matokeo ya kujifunza neno kwa kutumia njia ya kujifunza kwa kulifuata neno ina thamani kwa kila juhudi zinazotakiwa.

#### SULUHU

Njia ya kujifunza kwa kulifuata neno ni njia nzuri ya juu ya kujifunza neno. Inapelekea kuielewa Biblia sawasawa, inawezesha kukua kwa kweli kiroho na kujifunza. Kwa kuwa, ni njia bora siyo tu kwa wachungaji na wahubiri, lakini pia kwa kila mkristo. Tunahitaji wote kujifunza kutoka kwenye maandiko. Kila mpanda kanisa hatakiwi tu kuiweza njia hii, lakini pia kuifundisha kwa kila muumini katika uangalizi wake.

Masomo yafuatayo yataelezea kwa undani zaidi jinsi ya kutumia hatua zote tatu za njia ya kujifunza kwa kufuata neno. Muda pia utatolewa wa kutumia na kujisikia huru kwa kila hatua ya utaratibu. Juhudi zinazohitajika zitakuwa zaidi kuliko kuwekwa sawa kwa matokeo mapya ya kuelewa neno la Mungu aliye hai.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni nini msingi wa jinsi ya tofauti kati ya kupunguza na Kuingiza
- Kwa nini njia ya kujifunza kwa kufuata neno ni njia bora ya juu ya kujifunza Biblia, ukilinganisha na njia ya kujifunza kutumia mawazo?
- Ni nini hatari ya “kawaida” kutumia kujifunza Biblia na kuhubiri?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Utakapojifunza Biblia tena, andika muda uliotumia katika uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi. Kufuatana na mida hii, tathimini kama unatumia njia ya kujifunza kwa kufuata neno, njia ya kujifunza kutumia mawazo au njia nyingine katikati ya hizo.
- Katika kutayarisha somo litakalofuata juu ya uchunguzi, chukua mfano wa kifungu kidogo cha maandishi ya kujifunza (isiwe zaidi ya aya au vingine). Tumia angalau masaa mawili kwa maombi ukichunguza kifungu na kumuuliza Mungu kufungua masikio yako kwa vitu ambavyo hujaviona. Andika uchunguzi wako. Ni nini umejifunza?



# Jinsi Tulivyopata Biblia

---

## BIBLIA NI YA KUTEGEMEWA

Biblia mara nyingi imeshambuliwa, bila kujali mafundisho yake wazi juu ya asili yake ya kimungu na miujiza na unabii unaotimizwa ambao umedhihirisha mamlaka yake. Inaeleweka kwamba Shetani asingesalimisha juhudi zozote kudhoofisha zana yetu yenye nguvu zaidi. Anawataka watenda kazi wa Bwana kuwa na mashaka juu ya thamani yake, kuuliza juu ya usahihi wake, kuidharau, au kuikataa. Lakini kuelewa mwanzo na kutokea kwa Biblia kutoka kwa Mungu na kuja kwetu inatusaidia kuwa wenye shukurani kwenye zana hii ya ajabu na ukati wake kwenye kufaulu kwa huduma zetu.

Imeandikwa zaidi ya mara 40 na waandishi tofauti, katika lugha tatu, kwa kitambo cha zaidi ya miaka 1400, Biblia ni kitabu kikuu kilichoandikwa kinachoongoza katika historia. Hata usawa wake, uthabiti wake na kukosa hitilafu kunadhihirisha kuwa Mungu mwenyewe ndiye mwandishi wake, akimuongoza kila mwandishi wa kibinadamu kuhakikisha kuwa matokeo ni sawasawa na alivyopanga.

## JINSI TULIVYOIPOKEA BIBLIA

Mungu ameagiza, na bado anaagiza kuleta Biblia ya kutegemewa kwetu. Hii ilianza na mwandishi wa kwanza, na inaendelea tunapofungua neno lake leo. Kuna hatua mbalimbali za utaratibu huu.

### A. Uuvio

Neno uvuvio maana yake hasa ni Mungu “pumuliwa” au “kupumulia nje” na kuthibitisha kuwa Biblia ni matokeo ya Mungu (Tim 3:16). Kwa sababu Biblia ni matokeo ya asili, inatakiwa kutumiwa kama hivyo.

Biblia si matokeo tu ya mawazo ya mwanadamu, isipokuwa neno la Mungu, lililosemwa kwa kutumia midomo ya watu na kuandikwa kwa kalamu ya watu. Mitume na manabii wote walidai kusema na kuandika maneno ya mwingine: Mungu mwenyewe. Hata Yesu, mwana wa Mungu alitabiri kwamba alisema maneno hayo tu aliyopewa na baba yake. Kufuatana na 2Petro 1:20-21, “bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.” Ni muhimu kutambua kuwa Biblia yenyewe ilivuliwa, siyo wanadamu waandishi wa Biblia. Zaidi, uvuvio unamaanisha siyo kwenye thamani ya kile kilichoandikwa lakini kwa asili yake ya mwanzo na tabia yake.

### B. Utunzwaji

Tangu mwanzo, asili ya kipekee ya Biblia ilieleweka. Watu waaminifu wamefanya utunzaji wa hali ya juu mara zote katika kunakiri kwa usahihi maandiko ya Biblia. Wamefanya makosa madogo, na namba kubwa ya karatasi zenye maandishi zilizogunduliwa zimetuwezesha kutafuta kwa kusahihisha makosa ambayo yalikuwa yamefanyika. Sehemu katika Biblia ambapo tunakosa ushahidi wa kutosha kufahamu kwa usahihi mwanzo wa somo ni mara chache sana, na sehemu hizi hakuna hata moja yenye mambo au mafunzo ya muhimu.

Ukitafakari makundi ya walionakiri, miaka mingi ya kunakiri, Lugha za aina mbalimbali ambazo Biblia ilinakiriwa, upana wa kijografia. Na wengine wengi walijaribu kuiangamiza Biblia, Inashangaza kwamba tuna kitu cha kusadikika namna hiyo, Maandiko sahihi. Mungu kwa uwazi amefanya kazi kuitunza ili tuitumie.

### C. Kiwango

Neno, ‘sheria’ limeazimwa kutoka kwenye neno la kiyunani linaloamaanisha kanuni au kiwango. Kanuni zimekuwa zikitumiwa na wakristo tangu karne ya 4 kutambua orodha ya vitabu vyenye mamlaka vinavyohusu Agano Jipya au la Kale ambapo vitabu vingine vyote vilipimwa.

Waangalizi wengi wa zamani (Padiri) na mabaraza ya kanisa yalichangia kwenye kazi ya uwekaji kanuni, kwa msaada wa Mungu. Walichunguza ushahidi wa vitabu vyenyewe, uthibitisho wa mwandishi, kukubaliana kwa kitabu na vitabu vingine vinavyokubaliwa, na kukubaliwa kwa vitabu na kanisa. Kutokea kwa sheria za Agano la Kale na Jipya ulikuwa ni utaratibu badala ya tukio na kubainika chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu.

Kufikia wakati wa kipindi cha Yesu, Agano Jipya lilikuwa na sheria, mitume na maandishi. Mwanzoni mwa kuanza kwa ukristo, vitabu vyote 39 vya Agano la Kale vilikuwa kwa ujumla vimekubaliwa, pamoja na orodha ya kikanuni inayohesabika kama 170 BK. Kuanza kwa kanuni ya Agano Jipya, ikiwa na vitabu 27, ilimalizika katika karne ya 4. Kumekuwa na makubaliano kwa ujumla katika kanisa kwamba Biblia imeundwa na vitabu 66. Tofauti kwenye mapatano haya yanahusu Apocrypha.

Vitabu vya Apocrypha ni vimekataliwa na Waprotestanti, lakini vimekubaliwa na makanisa ya Othodox na Romani Katoliki. Kwa jinsi hiyo, kuna tofauti sana kati ya vitabu vya Apocrypha na vitabu vingine 66. Vitabu vya Apocrypha havidai kuwa maandiko, vina makosa yaliyo wazi, na vilikataliwa kwa hali ya kanuni ya jamii ya Wayahudi. Kwa jinsi hiyo, vitabu vya Apocrypha vina namna ya kusali kwa utaratibu wa ibada ya makanisa ya Othodox na Romani Katoliki. Vitabu vya Apocrypha vina kazi mbalimbali ambazo kanisa la Kiroma liliona kuwa msaada wakati wa mabadiliko ya mahangaiko dhidi ya Waprotestanti, ambavyo vinaweza kuwa vimevuta baraza la halmashauri ya kupindisha kuvihusisha kwenye kanuni ya kanisa la Romani Katoliki kwenye 1548 BK.

#### D. Tafsiri

Watu wa Mungu wametumika kwa jasho ili kwamba kila mtu aweze kusikia neno katika lugha zao. Kazi ni kubwa sana, na inayoendelea. Lugha za kisasa na tamaduni mara nyingi zinatofautiana sana kutoka nyakati za Biblia, na kila mara zinabadilika. Wanaogeza lugha lazima wachague maneno bora na vifungu vitakavyochukua maana ya lugha ya mwanzo na kuendelea kuwa rahisi kwa mtu mwingine wa umri wowote na kiwango cha elimu kuelewa. Hakuna lugha iliyogeuzwa iliyo kamili, lakini fedha ya kuendeleza, ugunduzi wa karatasi za maandiko mapya, na kukua katika kuelewa Biblia vinasaidia katika kazi hii isiyoisha. Kulinganisha kila mara na lugha ya mwanzo ya maandiko ni muhimu kuhakikisha kwamba mageuzo yoyote maalumu yanabeba kwa usahihi maana ya neno la Mungu. Mungu anatomia wenye vipawa, wasomi, watu wenye uwezo, wanaotegemea maelekezo yake na hekima katika hatua hii muhimu, inayoendelea.

#### E. Nuru

Wakristo wanapokuwa wanasoma, wanajifunza, na kutafakari juu ya neno, Roho Mtakatifu anadhihirisha maana. Hatua ya nuru pia haina mwisho, au inatakiwa isiwe na mwisho. Ni juhudi za pamoja. Mtu hawezi kujifunza bila Roho (1Kor 2:11-14; Zab 119:18), na Roho hafundishi bila juhudi za mtu (2Tim 2:15; Zab 119:97-99; Mdo 2:1-5).

Kufundisha neno la Mungu ni heshima kubwa (2Tim 4:17) lakini pia majukumu yasiyo ya mzaha (Yak 3:1). Halitakiwi kamwe kuchukuliwa kwa mzaha, bila maandalizi kwa maombi. Hata hivyo, Mungu amefanya utoaji unaohitajika kwetu wa kuwa na maandiko ya kutegemea katika lugha zetu, na ametuwezesha kuelewa neno lake kwa msaada wa Roho wake Mtakatifu. Hakuna kinachopungua isipokuwa uamuzi wetu wa kulichukua kwa usahihi, na kwa uaminifu kulitumia kuendeleza maisha yetu yote ya ukristo na kisha huduma yetu kwa wengine. Ni upendeleo wa namna gani kuweza kuwa sehemu ya hatua hii ya kulipeleka neno hili hai la Mungu kwa wahitaji, na kwa ulimwengu unaopotea!

#### SULUHU

Mungu amesimamia uhamishaji wa neno lake kutokea mwanzo wa kuandikwa kwake mpaka tunapolifungua kutafuta maelekezo yake kwa ajili ya maisha yetu. Nakala tuliyo nayo mikononi mwetu inafaa kwa matumizi katika yote kukua binafsi na katika huduma. Kwa jinsi hiyo, ni hai, kitabu cha kiroho, na kinaweza kueleweka tu tunapokikaribia kwa maombi na kwa heshima na kumruhusu Roho Mtakatifu kufungua macho yetu kwenye ukweli uliommo. Shukurani kwa Mungu kwa kitabu hiki cha ajabu cha kutuelekeza.



# Kuchunguza Neno la Mungu LINASEMAJE?

## ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kueleza kwa wapanda kanisa jinsi ya kujifunza Biblia kwa kanuni ya njia ya kujifunza Biblia kwa kulifuata neno “uchunguzi.”

## ☞ Wazo Kuu

- Kujifunza Biblia kwenye mafanikio lazima kuzungukwe na maombi.
- Maana ni muhimu zaidi.
- Kuna maswali sita ya ufunguo ya kuuliza kuhusu kila fungu.

## ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujua jinsi ya kuandaa maswali ya uchunguzi wa kujifunza Biblia kwa kufuata neno.
- Awe amejitoa kujifunza neno la Mungu kwa uangalifu.

## ☞ Ziada

2A Lugha ya Biblia

## ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Somo hili linafuatiwa na warsha ya saa moja itakayozingatia juu ya kutumia kanuni za uchunguzi. Somo hili ni la mifano ya maswali ya uchunguzi kwa Yeremia 1. Unatakiwa kusisitiza kwenye aina ya maswali yaliyolizwa, kwa sababu wanafunzi watatakiwa kuandaa maswali yao wenyewe katika somo la warsha.

## UTANGULIZI

Wakristo wote wanatakiwa kuweza kujifunza Biblia kwa ajili ya ukuaji wao wa kiroho na pia kwa ukuaji wa wale walio chini ya uangalizi wao. Mungu amempa kila muumini Roho Mtakatifu kuwa mwalimu wake mkuu. Ngoja tuisahau kamwe umuhimu wetu wa kutegemea juu ya Roho wa Mungu kutufundisha na kutuwezesha kutii kile tunachojifunza. Kwa msaada wa Mungu, inawezekana kwa kila muumini kuelewa Biblia hata kama kitabu pekee tulichonacho ni Biblia. Kwa kuongeza, Mungu amewapa baadhi ya watu nafasi maalumu ya kusaidia watu wake kugundua ukweli wa maandishi na kuyatumia kwa usahihi katika maisha yao. Ni muhimu hasa kwamba wapanda kanisa kujua jinsi ya kusaidia wengine kujua ukweli wa Mungu kwa njia ya kujifunza Biblia.

Moja ya njia bora za kugundua kiutaratibu, kuelewa, na kuutumia ukweli wa Mungu ni njia ya kujifunza Biblia kwa kufuata neno. Njia ya kujifunza kwa kufuata neno inapelekea kwenye hatua ya kugundua kwa kupitia hatua tatu za msingi zinazoitwa “uchunguzi” “ufafanuzi” na “matumizi.” Roho Mtakatifu anatufundisha, lakini Mungu pia anatutarajia tujifunze neno lake kwa uangalifu tukitumia kila rasilimali alizoweka katika upeo wetu. Tunatakiwa kamwe tuisichague kati ya kujifunza kwa bidii au kumtegemea Roho mtakatifu—yote ni muhimu.

Mungu anatutarajia kujifunza neno lake kwa makini tukitumia kila rasilimali alizoweka katika upeo wetu.

Somo linakazia katika hatua ya kwanza ya kujifunza Biblia kwa kufuata neno—uchunguzi. Kama lilivyoeleza somo lililotangulia, uchunguzi ni kama msingi wa piramidi. Kama tukifanya kazi kamili ya uangalifu ya uchunguzi, matokeo ya ufafanuzi na matumizi vitakuwa sahihi zaidi. Lengo letu lazima


liwe kuelewa sawasawa nini Mungu anataka tuelewe na kufanya, na kwa hiyo uchunguzi ni hatua ya maana katika utaratibu.

## I. UCHUNGUZI—MAANDISHI YANASEMAJE

Uchunguzi unahusisha kwa undani na ukweli unaonekana katika kifungu kilichochaguliwa. Unajibu swali “maandiko yanasemaje?” Waziwazi unaonyesha watu, mahali, matukio, hali ya mambo, vitu, muda, uhusiano, maoni ya watu, mawazo n.k. yalivyokuwa katika akili ya mwandishi wakati maandiko yalipoandikwa.

Kielelezo 2.1

Mwanafunzi wa serikali katika ngazi ya juu ya uandishi ametumia muda usiohesabika akijaribu kufumbua maana ya maandiko yaliyoandikwa na mtu. Katika namna nyingi, utaratibu huu umeendelea kwa mamia ya miaka hata maelfu ya miaka tangu kuandikwa kwa maandiko, kwa ufahamu mpya unaoendelea kuibuka. Chukua dakika kufikiri baadhi ya maandishi wakuu wa ngazi ya juu wa nchi yako, na utafutaji wa maana ya maandishi yao. Kama juhudi hizi ni thabiti, ni kwa kiwango gani zaidi tungekazana kuelewa lililo hai, lenye nguvu, lisilokwenda chini neno la Mwenyezi Mungu. Kusoma haraka fungu la Biblia, na kudhani kuwa tumelielewa kabisa kabisa ni kunena ujinga.. Kuna mambo zaidi ya kuelewa mara zote.



### A. Jiandae Kwa Ajili ya Uchunguzi

Kwa kuwa Biblia ni pumzi ya neno la Mungu, hatuwezi kuisogelea kama vitabu vingine. Kuna vigezo mbalimbali vitakavyoathiri endapo tunaelewa au la.

#### 1. Imani

Maandiko yanasema kwamba, “mtu bila Roho” Hawezi kuyaelewa mambo yanayotoka kwa Mungu (1Kor 2:14). Kwa kuwa ni hao tu waliotubu dhambi zao na kumtumaini Kristo kwa ajili ya wokovu wana Roho Mtakatifu, mtu asiyeamini haiwezi Biblia. Hii haina maana kwamba waumini peke yao ndio wanaoweza kuhusika katika mafunzo ya Biblia. Ina maana kwamba wakati wasioamini wanapokuwepo, wanapungukiwa kwa yale watakayoweza kuelewa. Roho Mtakatifu ana haja ya kuwaonyesha ukweli wa dhambi, haki, na hukumu kutoka kwenye maandiko, ili kuwaongoza kwenye wokovu. Kwa hiyo, kujifunza Biblia kwa wasioamini inatakiwa kukazia katika msingi wa ukweli wa injili.

#### 2. Maombi

Kujifunza Biblia kwa sawasawa wakati wote kutazungukwa na maombi. Kabla ya kuanza kujifunza, tunatakiwa kuomba na kuungama dhambi yoyote au vipingamizi vingine vinavyotuzuia kutokujifunza kutoka katika neno. Tunatakiwa kuomba pia kwa ajili ya kuerevuka (Zab 119:18; Efe 1:18). Wakati wa mafunzo yetu, inasaidia pia kuomba kwa ajili ya uwazi kila tunapona kitu ambacho hatukielewi. Na mwisho, tunapokuwa tumemaliza kujifunza, tunatakiwa kuomba juu ya jinsi Mungu atataka tutumie kile tulichojifunza katika maisha yetu wenyewe na katika maisha ya wengine.

Kujifunza Biblia kwa sawasawa wakati wote kutazungukwa na maombi.

#### 3. Utayari wa Kutii

Yakobo anatuambia kuwa hatutakiwi kulisikia neno, lakini kulitii (Yak 1:22-25). Yesu pia alisema kuliweka neno lake katika matendo ni sawa na kujenga nyumba juu ya mwamba (Mt 7:24). Kutokuyatii, kwa jinsi hiyo, ilikuwa sawa na kujenga juu ya mchanga (Mt 7:26). Kwa hakika, Yesu anaonekana kusema kwamba kutoa ukweli wa kiroho kwa ambao hawako tayari kutii ni kama mpumbavu kutoa lulu kwa nguruwe (Mt 7:6). Mungu hana mzaha juu ya jinsi tunavyokubali neno lake. Kadiri tunavyojua, ndivyo tutakavyohukumiwa zaidi.



#### 4. *Kujichunguza Mwenyewe*

Ni kweli kwamba mchungaji au mpanda kanisa anawajibika kufundisha neno kwa wengine. Tumeambiwa “kulisha kondoo” (Yoh 21:17). Lakini hatumpi udhuru wa kulitumia kwanza katika maisha yake mwenyewe. Kila mpishi mzuri anaonyesha chakula kinapokuwa kinapikwa kuonyesha kama kiko tayari au hakiko tayari kuwapatia wengine. Mwishoni kabisa, mara kwa mara tunatakiwa kuangalia matumizi kwetu wenyewe, hata kama lengo ni kuhubiri kwa wengine. Kwa jinsi hiyo, hata ni faida zaidi kama tukishiriki kwa moyo chakula kuliko tu kukionyesha kama mfano.

Mara kwa mara tunatakiwa kuangalia matumizi kwetu wenyewe, hata kama lengo ni kuhubiri kwa wengine.

Mwanafunzi wa maandiko hatakiwi kamwe kujisikia kama amefikia hatua ya kuelewa neno la Mungu kwa ukamilifu—hii haiwezekani. Ni bora zaidi kuwa “anayejifunza”, anayekua siku kwa siku kwa kujifunza neno na maombi, kuliko kujifanya unyago kama “mtaalamu.” Huduma ya kufundisha itakuwa tajiri na yenye mafanikio zaidi kama mwalimu anashirikisha nje wingi wa ukweli aliojifunza kutoka kwa Bwana siku kwa siku.

#### 5. *Utayari wa Kujifunza*

Yaendee maandiko kwa akili wazi. Uwe tayari kumruhusu Mungu kukufundisha hasa neno lake linasemaje. Wakati wote uwe tayari kujionyesha unachoamini kwenye mwanga wa neno la Mungu. Usiogope kubadili mtazamo wako kama Mungu amekuonyesha ukweli kuhusu kitu.

### **B. Chukua Muda wa Kutosha**

Kuna kanuni zilizohakikishwa za kuelewa kwa ujumla mtazamo wa fungu. Kama utaratibu ukiharakishwa, matokeo ya kuelewa somo yatakuwa finyu. Ni muhimu kutumia uvumilivu na nia ya kuendelea kufanya kazi mpaka somo limeeleweka.

Hatua ya kwanza ni **kusoma maandiko mara kadhaa** kupata kuelewa maana ya fungu kwa ujumla. Hii inachukua muda, lakini inazaa matunda mengi. Kuna vifungu vingi ambapo ni rahisi kusitishwa chini kwenye mambo mengi labda uwe na utambuzi wa kisa kwa ujumla katika mambo mbalimbali uliyosoma. Kuelewa vizuri kwa ujumla mwelekeo kutakusaidia kutunza mzani sawa na kugawanya muda wako kikamilifu kwa sehemu tofauti chini ya masomo.

### **C. Angalia Mandhali**

Neno ‘mandhali’ linahusu mistari inayozunguka fungu lililosomwa. Kuelewa mandhali ni moja ya zana zenye thamani sana za kujifunza Biblia, lakini hata hivyo mara nyingi inaachwa. Tunapoangalia mandhali, tunatafuta kuelewa ni nini kisa au kichwa cha kitabu, ukurasa, na aya ya mistari tunayojifunza. Kuangalia katika mandhali ina maanisha kuchunguza.

- Mistari inayoendelea na inayofuata inazungumzia nini?
- Ni nini kisa cha aya?
- Ni nini kisa cha ukurasa?
- Ni nini madhumuni na kisa cha kitabu?
- Fungu liko kwenye agano la Kale au agano Jipya na hii ina maana gani?

Mfano mzuri wa umuhimu wa mandhali ni Wafilipi 4:9, ambapo Pauli anaahidi kwamba Mungu “atakupa haja zako zote.” Wengi wanalielewa hili kama ahadi isiyo ya masharti kwa kila mmoja. Wengi wanatambua kuwa kwa kuwa Wafilipi wameandikiwa waumini, hii ahadi ni kwa wakristo tu. Kwa jinsi hiyo, unapojifunza kwa undani mandhali inadhahirisha kuwa Wafilipi ni “barua ya shukurani” kwa kanisa la Filipi kwa zawadi waliyomtumia Paulo kupitia kwa Epafura. Mandhali ya mstari wa 18 unaonyesha kuwa Mungu alikuwa amependezwa na zawadi hii. Kwa hiyo, Mandhali inaonyesha mstari wa 19 ni ahadi kwa wote waliojitoa kusaidia kifedha wamishenari wanaopanda makanisa (Paulo) aliyekuwa akihubiri injili kwa waliopotea (Urumi wakati huo).

Kuelewa mandhali ni moja ya zana yenye thamani ya kujifunza Biblia.

Baadhi ya Biblia zina maandishi kabla ya kila kitabu yanayoelezea kitabu hicho kinahusu nini. Haya yanaweza kuwa ya msaada. Kuna kamusi zingine na vitabu vinavyopatikana ambavyo vinajadili mpangilio na mwanzo wa kitabu cha Biblia au ukurasa. Kwa jinsi hiyo, ni vizuri kupunguza matumizi ya rasilimali hizi mpaka katika hatua ya ufafanuzi. Hakuna badala la kusoma maandiko wewe mwenyewe na kuyaruhusu kukuzungumzia uongozwe na Roho Mtakatifu. Katika hatua ya uchunguzi, kazania kile *unachokiona* katika maandishi na mandhali. Uwe na muda wa kumsikiliza Mungu kabla hujahamia kwenye maelezo ya watu, hata kama wanaweza kuwa walimu walio na vipawa au maandishi.

Kuchunguza mandhali kunahusu kusoma zaidi kuliko tu kifungu ulichojifunza—ni pamoja na mistari inayozunguka, ukurasa, au kitabu. Tunarudi nyuma na kutazama fungu kutoka mbali kabla hatujaendelea kuangalia kwa karibu. Ufahamu na maandishi juu ya mandhali lazima viandikwe kwa uangalifu. Vitakuwa muhimu sana katika hatua ya ufafanuzi.

Rudi nyuma na angalia fungu kwa umbali kabla hujaliingilia kwa ukaribu.

#### D. Chunguza Muundo

Ukiwa umeangalia fungu kutoka mbali, ni wakati sasa kuangalia kwa karibu. Soma fungu mara kadhaa, ukiangalia na kuandika yoyote kati ya mambo yafuatayo ya muundo:

- Maneno ya ufunguo—Nukuu kila neno au maneno ambayo yamerudiwa. Mara nyingi hii inaonyesha kisa.
- Ulingano au tofauti—Kuna ambacho kinafanana na kitu kingine, au cha kinyume?
- Mwendelezo wa wazo—Kitu kimoja kinajengwa juu ya kingine? Vimeunganishwa kwenye wazo jingine kama mnyororo?
- Vitenzi—Kuna aina fulani ya matendo? Kuna amri ambayo tunatakiwa kuitii?
- Viunganishi—Kitu fulani kinalingana na kitu fulani? Mara nyingi kiunganishi “lakini” kinaonekana katika kutofautisha, na maneno “Sawa na” au “kama” yanaweza kuonyesha ulinganisho.
- Vielelezo—Angalia katika akili yako vitu au matendo ambayo yameelezwa.
- Aina ya maandishi—Fungu linaweza kuwa historia, unabii, fumbo la maneno, mafundisho, hoja, mifano au uwezekano mwingine mwingi. Ziada 2A imeorodhesha mengi ya haya. Hakuna aina ya maandishi katika fungu vilevile yatakayoathiri tafsiri katika hatua itakayofuata, kwa hiyo inatakiwa iandikwe kwa uangalifu sasa.

#### E. Uliza Maswali: Nani? Nini? Wapi? Lini? Jinsi gani? Na kwa nini?


Njia nzuri ya kugundua yaliyomo na maana ya fungu la maandiko ni kuuliza maswali ya ufunguo juu yake, na kuandika majibu. Kielelzo 2.2 kinaonyesha maswali sita ambayo yanatakiwa kuulizwa na kujibiwa. Kuna , bila shaka, maswali mengine yanayowezekana, lakini haya ndiyo muhimu zaidi. Maswali mengine huwa ni mabadiliko ya haya sita.

Kimawazo, unatakiwa kuuliza kila mfumo wa maswali haya unayoweza kufikiria (kadiri yanavyokuwa mengi ndiyo inakuwa vizuri). Mifano ya mabadiliko ya maswali haya imeonyeshwa katika hatua inayofuata. Kadiri unavyouliza maswali, kwa uangalifu andika maswali na majibu kwenye kipande cha karatasi. Utahitaji kuyatumia katika hatua ya ufafanuzi.

Kama ukiuliza swali na huwezi kupata jibu, nukuru maswali na uyarudie baadaye. Usije ukaacha kuyajali maswali hayo. Yanaweza kuwa muhimu. Badala yake, yaombe, yatumie kwenye sala, na mulize Mungu kukuonyesha majibu. Uwe tayari kuchukua muda na juhudi kwa haya, lakini itakuwa na maana utakapofika kwenye kuelewa sawasawa fungu. Utakapokuwa tu unaweza kuyatumia kwa ujasiri katika maisha yako, na kufundisha “Hivyo asema Bwana...” kwa wengine.

Kama huwezi kupata jibu la swali, lirudie baadaye.

## Kielelezo 2.2 Ufunguo wa Maswali ya uchunguzi



### II. MFANO WA UCHUNGUZI

Tunakwenda kutumia maswali sita kuona ni nini tunaweza kugundua juu ya ukweli wa Mungu katika kifungu cha agano la Kale juu ya kijana aliyeitwa kumtumikia Mungu. Tunapokuwa tunajifunza fungu hili, litakuwa wazi ya kwamba alikuwa ameitwa kuchukua msimamo ambao ulikuwa tofauti kabisa na wa wakati ule. Hakuna shaka wengine kati yenu wataweza kujifaninisha na masumbuko ambayo kijana huyu ilimpasa kuyakabili anapokuwa ameitika wito wa Mungu. Kifungu kinapatika katika Yeremiah1.

Fungua Biblia hii katika fungu hili, omba kwa ajili ya kupata mwanga, na kisha tafuta majibu ya maswali yafuatayo. Nukuru *aina* ya *maswali* yaliyoulizwa. Katika kujifunza kwako baadaye, utahitaji kuunda maswali yanayofanana na haya kuyauliza juu ya vifungu unapokuwa unavisoma. Andika majibu karibu na kila swali.

#### A. Nani?

- Kwa nani sehemu hii ya maandishi inatolewa (mstari 1)?
- Ni watu gani wametajwa katika fungu hili (mstari wa 1-2)?
- Ni wafalme gani wamenukuriwa katika mstari wa 2-3?
- Ni watu gani Mungu anawaita kuleta misukosuko katika nchi (mstari 15)?
- Mstari wa 18-19 unaorodhesha vipingamizi vikuu vya Yeremia. Watu hawa watakuwa kina nani
- (Mengine)?

#### B. Nini?

- Ni tukio gani mashuhuri limenukuriwa mwanzoni mwa mstari 2?
- Inawezekana kueleza nafasi ya Yeremia ilikuwa nini katika mstari wa 2?
- Kama ni hivyo, Nafasi hiyo ilikuwa nini?
- Kufuatana na mstari wa 2, ni tukio gani lilitokea mwishoni mwa utawala wa Sedekia?
- Nini kilimtokea Yeremia katika mstari wa 3?
- Nini ilikuwa “Neno la Bwana” lililomjia (mstari wa 5)?
- Nini sifa nne maalumu zilizotolewa na Mungu kwa ajili yake mwenyewe katika mstari wa 5?
- Katika mstari wa 5, Nini ilitakiwa kuwa nafasi ya Yeremia?
- Nini kilikuwa kiwango cha jukumu la Yeremia? Ilikuwa tu ni kwa taifa la Israeli, au kwa upana zaidi?
- Nini yalikuwa majibu ya Yeremia katika mstari wa 6?

- Ni nini majibu ya Mungu kwa Yeremia katika mstari wa 7-8?
- Ni nini masharti mawili Mungu anayompa Yeremia katika mstari wa 7-8?
- Nini uchaguzi alio nao Yeremia kutokana na mstari wa 7?
- Ni hisia zipi za Yeremia ambazo Mungu anazizungumzia katika sehemu ya kwanza ya mstari wa 8?
- Ni sababu mbili zipi zinazotolewa kwa Yeremia ya kwamba asiogope (mstari wa 8)
- Mungu anamfanyia nini Yeremia katika mstari wa 9?
- Mstari wa 10 unaelezea kazi ya Yeremia. Asili ya kazi hiyo ilikuwa nini?
- Ni maendeleo yapi yaliyogunduliwa katika mstari wa 10?
- Ni vitu viwili vipi ambavyo Mungu alimwonyesha Yeremia katika mstari wa 11-16?
- Mstari wa 12 unaelezea nini kuhusu kile anachokifanya Mungu?
- Kutokana na mstari wa 14 -16, Kitu gani kilikuwa karibu kuwapata watu wa Mungu?
- Ni sababu gani maalumu ambayo inamfanya Mungu kuleta hukumu juu ya watu wake(mstari wa 16)?
- Ni maelekezo yapi Mungu anampa Yeremia katika mstari wa 17?
- Ni amri zipi zimerudiwa kutoka mwanzo?
- Ni ahadi gani mpya katika (mstari wa 17)?
- Watu watafanya nini kwa Yeremia katika mstari 18 (mstari wa 19)
- Ni ahadi gani Mungu anampa Yeremia kwa ajili ya vita vilivyo mbeleni (mstari wa 19)?
- (Mengine)?

**C. Wapi?**

- Mpangilio wa fungu hili uko wapi kulingana na mstari wa 1?
- Ni wapi hili linapatikana?
- Ni wapi watu walioelezwa katika mstari wa 15 wanakotoka?
- (Mengine)?

**D. Lini?**

- Ni kipindi gani cha muda ulioelezwa katika yaliyomo kwa ujumla katika kitabu hiki?
- Katika mstari wa 5, lini Mungu alijua (kumchagua) Yeremia?
- Katika mstari wa 5, lini Mungu alimtenga Yeremia kwa ajili ya huduma?
- Tukio katika mstari wa 18 lilitokea lini?
- (Mengine)?

**E. Kwa nini?**

- Kwa nini Mungu “analinda” katika mstari wa 12?
- Kwa nini Mungu anatangaza hukumu juu ya watu wake (mstari 16)?
- (Mengine)?

**F. Jinsi Gani?**

- Jinsi gani Yeremia ameelezewa katika mstari wa 1?
- Jinsi gani baba yake Hilikia ameelezewa?
- Jinsi gani Yeremia anamzungumzia Mungu katika mstari wa 6?
- Jinsi gani Yeremia anaitikia neno la Mungu katika mstari wa 6?
- Jinsi gani Mungu anamwelezea Yeremia katika mstari wa 18?

Tumia nafasi iliyotolewa chini kuorodhesha uchunguzi mwingine uliofanya kuhusu Yeremia 1:

**MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Mandhali ina maana gani?
- Ni maswali yapi sita ya ufunguo ya kuuliza kwenye fungu?
- Lini, wakati wa kujifunza Biblia, tunapotakiwa kuomba?

**UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

Kama hukuwa na muda wa kumaliza uchunguzi wa Yeremia 1, fanya hivyo kabla ya somo linalofuata. Angalia kama unaweza kuuliza maswali mengine yanayofaa ya fungu lilelile. Yatunze maswali hayo na majibu kwa matumizi katika somo la 4.



# Lugha ya Biblia

---

Tunapojifunza neno la Mungu, tunaangalia kusudio, maana halisi. Tunataka kuelewa ujumbe ambao Bwana anataka kuwasilisha kupitia neno. Lakini ni muhimu kutambua kwamba, kama maandishi mengine ya maana, maandishi wa Biblia mara kwa mara walitumia vielelezo vya semi kuwasilisha ukweli. Kwa nyongeza, walitumia maandishi mengi ya aina nyingi katika maandishi yao. Kujifunza Biblia kwa usahihi kunahitaji kwamba tunatambua tofauti hizi na kulielezea kila fungu kulingana na aina ya lugha na maandishi yaliyotumika.

## I. AINA ZA LUGHA ZA KITENDAWILI KATIKA BIBLIA

### A. Fumbo

Fumbo linalinganisha vitu viwili visivyofanana kwa kutumia maeneo kama “sawa na” “kama” au “kuliko.” Zaburi 1 inalinganisha mtu mwenye haki na mti uliopandwa karibu na chemichemi ya maji. vyote vinazaa mtunda na kufanikiwa.

### B. Mfano

Mfano ni fumbo katika mfumo wa hadithi ndefu. Yesu aliwasaidia wanafunzi kuelewa ufalme wake kwa kuwaeleza mfano juu ya wafanyakazi waliokuwa wanalipwa sawasawa ingawa wengine walikuwa wamefanya zaidi kuliko wengine walivyofanya. Anaanza na maneno “Kwa maana ufalme wa mbinguni *umefanana* na mtu mwenye nyumba aliyetoka alfajiri kwenda kuajiri wakulima awapeleke katika shamba lake la mizabibu...” (Mt 20:1).

### C. Methali

Methali inalinganisha vitu viwili visivyolingana bila kutumia maneno dhahiri kama vile “fanana na” “kama.” Katika Yeremia 1:18, Bwana alimwambia Yeremia, “Maana, tazama, nimekufanya leo kuwa mji wenye boma, na nguzo ya chuma, na kuta za shaba...”

### D. Methali ndefu

Methali ndefu ni mfano wa maneno. Katika Waamuzi 9:7-15, Yothamu anaeleza habari juu ya mtini wenye miiba kuwa mfalme juu ya miti mingine inayozaa kumwelezea kiongozi mharibifu.

### E. Kukoleza

Kukoleza inaelezea kitu kwa namna ya undani zaidi kuleta maana. Yesu aliposema kwamba mtu anayehukumu na ana boriti kwenye macho yake na hajijui, Anasema kitu ambacho kwa mwili hakiwezekani. Alitaka kusema, kwa hiyo, ni kwamba mtu ambaye hazijui dhambi zake mwenyewe hawezi kabisa kuthamanisha dhambi za mwingine.

### F. Maneno Machungu

Maneno Machungu yanateta kwa kutumia sifa isiyostahili au ya mzaha. Paulo anateta kiburi cha Wakorintho kwa kuandika, “Mmekwisha kushiba, mmekwisha kupata utajiri—na mmemiliki pasipo sisi!” (1Kor 4:8).

Kuamua ni lini maandishi wa kibiblia walitumia lugha ya vitendawili au kimaandishi ni kazi isiyo ya mzaha. Litakuwa kosa zito kuacha moja ya amri za Mungu kwa kudai kuwa ni lugha ya kimethali. Kwa upande mwingine, kusema kwamba kila mstari kwenye Biblia unatakiwa kufafanuliwa kabisa inapelekea kwenye baadhi ya matatizo ya kutatanisha. Wakati Bwana aliporejeza kwa Yeremia kama “mji wenye boma, na nguzo ya chuma, na kuta za shaba...” Hakuwa dhahili anaaongea katika akili hasa (Yer 1:18). Ni sawa na wakati Bwana aliposema

kuwa alikuwa akimchagua Yeremia “kungoa na kubomoa, kuharibu na kuangamiza...” (Yer 1:10).

Tunawezaje kujua tofauti kati ya lugha halisi na vitendawili? Unaweza kuuliza maswali rahisi kama haya:

- Je fungu linaeleza kuwa ni kitendawili? (“Sikiliza mithali nyingine...” Mt 21:33).
- Fungu linageuka kuwa la upuuzi au kutowezekana linapokuwa linafafanuriwa kihalisi? (“Ninaona chungu kinachochemka, na mdomo wake unaelekea upande wa kaskazini...Toka kaskazini mabaya yatatokea, na kuwapata wote wakaa katika nchi hii...” Yer 1:13-14).
- Fungu linamwelezea Mungu, aliye Roho, kana kwamba ana mwili na tabia zingine za kweli? (“Ndipo Bwana akaunyoosha mkono wake akanigusa kinywa changu...” Yer 1:9).

Kama maswali ya hapo juu hayahusiki, kisha mstari huenda unaweza kufafanuriwa hasa hasa.

## II. AINA ZA MAANDISHI KATIKA BIBLIA

### A. Historia

Biblia imejaa hesabu ya kihistoria na habari za maisha ya watu. Kwa mfano, kitabu cha Waamuzi kinaeleza historia ya Waisraeli kati ya kipindi chaYoshua cha ushindi wa nchi na utawala wa mfalme Sauli. Kitabu cha Nehemia ni kumbukumbu za Nehemia za kujenga upya ukuta wa Yerusalemu. Vitabu vya injili ni habari za maisha ya Yesu na mafundisho yake. Kitabu cha Matendo kinaandika matukio makuu katika historia ya kanisa la kwanza.

### B. Maelekezo

Katika Biblia yote, utakuta maelekezo, amri, kanuni, mithali, mafundisho na ushauri wa vitendo. Sehemu kubwa ya kitabu cha Mambo ya Walawi kina maelekezo yote ya makuhani wa Kiisraeli. Mithali inatoa ushauri juu ya fedha, mahusiano, na kazi. Barua za Paulo kwa makanisa maalumu zina mafundisho na maelekezo kamili kwa maisha ya kikristo.

### C. Unabii

Maandishi mengi ya kiunabii ni hesabu ya mahubiri yaliyoandikwa yaliyohubiriwa mwanzoni kwa watu wa Mungu. Isaya, Yeremia, na Ezikieli, Vitabu vikubwa vya kinabii, ni mkusanyiko wa mahubiri yanayopima kazi ya manabii hawa. Vitabu hivi havikukusudiwa kusomwa kutokea mwanzo mpaka kumaliza kama kuwa kitu kimoja. Siri ya kuelewa vitabu hivi ni kutafuta mwanzo na mwisho wa mahubiri binafsi na kusoma kutoka mahubiri hadi mahubiri. Karibu mahubiri yote yalishughurika na wakati wa mbele kupita wa muda wa maisha ya mitume.

### D. Mashairi

Katika maandishi ya ushairi ya Biblia kila hisia za mwanadamu zimeelezwa. Vitabu vingi vya kibiblia vina mashairi. Zaburi na Wimbo Ulio Bora kwa ujumla ni mashairi na vitabu vingi vya kinabii vimejaa mashairi.

### E. Ufunuo wa Kinabii

Baadhi ya unabii umeandikwa katika aina ya maandiko yanayojulikana kama maafa ya mwisho. Neno maafa ya mwisho lina maana “funua” kwa sababu linafunua matukio yatakayotokea mbeleni. Vifungu vya maafa ni alama hasa na ni muhimu kuelewa alama ili kuweza kutafsiri fungu. Ujumbe wa kati katika maandiko ya maafa ni kuja kwa mara ya pili kwa Kristo na hatima yake ya ushindi dhidi ya Shetani. Hasa hasa, uumbaji wote unahusishwa katika tukio la kuja. (kimebuniwa kutoka Inch na Bullock, eds., 1981. Maandishi na maana ya maandiko. Baker Book House.)



# Warsha ya Uchunguzi

## ☞ Kusudi la Somo

Kusudi ya warsha hii ni kuwapa wanafunzi nafasi ya kuunda mazoezi na kujibu maswali ya uchunguzi ya mafunzo ya kujifunza kwa kufuata neno.

## ☞ Wazo Kuu

- Wakati wote kuna maswali mazuri ya kuuliza.

## ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka kila mshiriki anatakiwa:

- Awe anaweza kutayarisha maswali ya uchunguzi ya kujifunza Biblia kwa kufuata neno.
- Kujua umuhimu wa kujifunza fungu kwenye vikundi.

## ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Ni muhimu kuyaleta makundi pamoja kwa muda wa dakika 15 kulinganisha matokeo. Hii inatakiwa kuonyesha kwamba kuna uwezekano mwingi wa maswali yanayoweza kwa kawaida kumponyoka mtu, au hata kundi kidogo. Vilevile inapunguza nguvu ya kusoma maandishi pamoja katika kikundi badala ya kuwa na mtu mmoja "kuhubiri" anachoona katika maandiko.

Uwe na karatasi na kalamu za mkaa za ziada zilizopo kwa ajili ya wanakikundi kutumia. Vilevile, utahitaji ubao wa kuweka matangazo, ubao wa choki, au kitu kingine kinachokuwa sawa kwa kuandikia maswali na majibu wakati kikundi kinapokutana mwisho wa baraza.

## MUUNDO WA WARSHA

Kifungu tutakachotumia kwenye warsha yetu kitakuwa ni Matendo 17:1-10a. Muundo wa warsha hii ni kama ifuatavyo:

- Gawanyika katika makundi ya watu 3-4
- Tumia dakika 35 kusoma fungu, anzisha maswali ya **uchunguzi**, na andika majibu.

Tumia dakika 15 zilizobaki za warsha kuunda makundi tena na linganisha maswali na majibu yaliyopatikana. Tengeneza orodha ya maswali kati ya haya yanayotawala na uchunguzi kutoka kila kundi. *Kisha chagua swali bora zaidi* kwa kila kikao kwenye vikao sita. Haya ni maswali ambayo yatasaidia zaidi au yanayodhihirisha, na ambayo utatumia kama utaongoza wengine katika mafunzo haya.

## HATUA

Tumia hatua zifuatazo zilizokuwa zimeandaliwa katika somo la 2

- Omba kwa ajili ya werevu.
- Soma fungu mara kadhaa.
- Chunguza mandhali na andika uchunguzi wako.
- Uliza kila mchanganyiko wa maswali sita ya ufunguo ambayo unaweza kufikiria, na andika majibu unayopata. Siyo kila swali litafaa kwenye fungu hili, lakini andika lile linalohusiana.
- Chagua swali moja bora zaidi kwa kila kipindi kwa ajili ya matumizi kama ungetakiwa kufundisha fungu hili.



## KAZI YA KIKUNDI

Tumia majedwali hapo chini kuanza kuandika maswali yako na majibu yako. Tumia karatasi za ziada kama inavyohitajika.

### MANDHALI

*Kisa cha somo la mstari unaozunguka fungu lililojifunzwa.*

- Mistari inayoendelea—
- Mistari inayofuata—
- Aya/ sehemu-
- Ukurasa (17)-
- Kitabu (Matendo)—
- Agano Jipya—

### MUUNDO

*Muundo wa fungu unaendana na fasihi na aina ya lugha.*

- Maneno ya ufunguo –
- Ulinganifu au utofauti –
- Mwendelezo wa mawazo -
- Vitenzi -
- Viunganishi–
- Vielelezo –
- Aina ya maandishi-

<b>MASWALI YA UFUNGUO</b> <i>Uliza na jibu mchanganyiko wa maswali yote sita ya ufunguo yanayowezezana</i>	
<b>Maswali Yako:</b>	<b>Majibu Yako:</b>
<b>Nani?</b> 1. 2. 3. 4. 5. 6. 7. 8. 9. 10. <i>[Zungushia swali uliloona kuwa la msaada zaidi]</i>	
<b>Nini?</b> 1. 2. 3. 4. 5. 6. 7. 8. 9. 10. <i>[Zungushia swali uliloona kuwa la msaada zaidi]</i>	
<b>Wapi?</b> 1. 2. 3. 4. 5. 6. 7. 8. 9. 10. <i>[Zungushia swali uliloona kuwa la msaada zaidi]</i>	

<b>Maswali Yako:</b>	<b>Majibu Yako:</b>
<p><b>Lini?</b></p> <ol style="list-style-type: none"><li>1.</li><li>2.</li><li>3.</li><li>4.</li><li>5.</li><li>6.</li><li>7.</li><li>8.</li><li>9.</li><li>10.</li></ol> <p><i>[Zungushia swali uliloona kuwa la msaada zaidi]</i></p>	
<p><b>Jinsi Gani?</b></p> <ol style="list-style-type: none"><li>1.</li><li>2.</li><li>3.</li><li>4.</li><li>5.</li><li>6.</li><li>7.</li><li>8.</li><li>9.</li><li>10.</li></ol> <p><i>[Zungushia swali uliloona kuwa la msaada zaidi]</i></p>	
<p><b>Kwa nini?</b></p> <ol style="list-style-type: none"><li>1.</li><li>2.</li><li>3.</li><li>4.</li><li>5.</li><li>6.</li><li>7.</li><li>8.</li><li>9.</li><li>10.</li></ol> <p><i>[Zungushia swali uliloona kuwa la msaada zaidi]</i></p>	



# Kufafanua Neno la Mungu LINA MAANA GANI?

---

## ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kutoa kielezo kwa wapanda kanisa jinsi ya kujifunza Biblia kupitia kanuni ya “ufafanuzi” ya kujifunza Biblia kwa kufuata neno.

## ☞ Wazo Kuu

- Umuhimu wa ufafanuzi wa uangalifu.
- Makosa ya kawaida katika ufafanuzi.

## ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujua kanuni za msingi za kufafanua maandiko
- Kujitoa kujifunza neno la Mungu kwa uaminifu.

## ☞ Ziada

4A Jedwali za Biblia

## ☞ Ushauri kwa Wakufunzi

Somo hili linafuatwa na warsha ya saa moja kukuza ujuzi katika kufafanua fungu.

## UTANGULIZI

Mbali na Roho Mtakatifu na maombi, Biblia ni rasilimali ya muhimu tuliyonayo kama wapanda kanisa. Neno la Mungu hai na lenye nguvu pekee lina uwezo kuingia ndani ya mioyo na nafsi za hao tunaotafuta kuwaleta katika ufalme wa Mungu. Linatuandaa kwa kila kazi nzuri, ambayo yakini inaelezea huduma yetu ya kuzidisha makanisa kuzunguka ardhi. Linasimama kama kiwango pekee ambacho tunapimia na kuthamani kila mafundisho, matendo, au mapokeo ya kanisa. Historia, mapokeo, na akili ya mwanadamu inaweza kupotosha, lakini Biblia inasimama kidete kama ukweli wa Mungu

Ni muhimu, kwa hiyo, kwetu kujua jinsi ya “kuligawanya neno la ukweli kiusahihi.” Adui Shetani hajabakiza hata juhudi kidogo za kuharibu Biblia na ukweli wake. Kwa karne nyingi, migongano mingi imetokea kwa kuelewa kwa uongo ya kile Biblia inachosema. Hutaki kuwa na hatia ya kuongeza au kuunga mkono kuelewa huko kwa uongo juu ya neno la Mungu.


## I. UFAFANUZI—HATUA YA PILI YA NJIA YA KUJIFUNZA KWA KUFUATA NENO

Kufafanua kunajibu swali la “somo lina maanisha nini?” kipindi hiki kinaonyesha baadhi ya mipaka ya ufahamu wa nini maandiko hasa yanasema. Hii haijakusudiwa kuwa ndiyo tiba kwa somo hili, isipokuwa ni utangulizi. Tunataka pia kuchukua fungu sawa ambalo tumekuwa tukishughulikia la Yeremia sura 1 na kutumia kanuni hizi kupata kuelewa waziwazi juu ya fungu hili.

Hatua ya ufafanuzi inafuata hatua ya uchunguzi ya kujifunza Biblia kwa kufuata neno. Hii inaonekana wazi, lakini mara nyingi wote wanaojifunza Biblia mara nyingi wanakimbilia hatua hii bila kufanya kazi ya uchunguzi. Matokeo yake, ufafanuzi wao unakuwa wa makosa, kwa kuwa wanakuwa hawana ukweli wa kuweza kufafanua kwa usahihi.

Hatua za uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi zinaweza kulinganisha na utaratibu wa kujenga

**Kielelezo 4.1**



nyumba. Uchunguzi itakuwa *ukusanyaji wa vifaa*. Ufafanuzi wakati ambapo mwenye nyumba *anajenga nyumba* kutokana na vifaa. Matumizi ni hatua ambapo mwenye nyumba anahamia katika nyumba na *kuishi ndani yake*. Kila hatua ina umuhimu sawa, na zote zinategemeana. Kama vifaa vinakosekana (uchunguzi), itakuwa si rahisi kumaliza nyumba. Kama nyumba haikujengwa kwa uangalifu (ufafanuzi), kuishi ndani ya nyumba hiyo kutakuwa hatari. Kama hakuna anayeishi ndani ya nyumba (matumizi), kujenga nyumba hiyo ni kupoteza muda.


Pamoja na huo ulinganifu wote akilini, inatakiwa kuwa wazi kwamba ufafanuzi unapaswa ufanywe kwa uangalifu, kwa maombi, na kwa kufikiri. Kama inatokea katika hatua fulani unakuta kwamba huna uhakika wa kutosha kufumbua maana ya fungu, unatakiwa kurudi kwenye hatua ya uchunguzi na kujiuliza maswali zaidi. Hasa, hii ni kawaida. Mara chache sana tunanukuru kila kitu muhimu kwenye fungu, chochote zaidi ya mjenzi kamwe haishiwi na vifaa na kwenda kupata vingine.

Ufafanuzi unapaswa ufanywe kwa uangalifu, kwa maombi, na kwa kufikiri.

**II. UTARATIBU WA UAFANUZI**

Tunapofafanua kifungu cha maandiko, tunatafuta kwa uangalifu kuelezea hali ya mwanzo ya Biblia, na hali ya ujumbe ambao Mungu anawasilisha katika hali hiyo. Tunaweza kwa hiyo kwa uangalifu na kwa maombi kudhani kwamba Mungu huzungumza katika njia sawa kwa hali sawa— inayopelekea kanuni ya kibiblia kwa ujumla.

**Kielelezo 4.2 Kutumia njia ya kujifunza kutumia mawazo kugundua kanuni za Biblia**



Kwa hiyo, ufafanuzi unahusu:

- Kuelewa asili, hali ya kibiblia na watu.
- Kuutambua ujumbe uliowasilishwa kwa watu hao na kwa muda huo.
- Kutunga kanuni inayofupisha hali hizi halisi, na ambayo itafaa katika hali inayofanana katika kipindi chochote—hasa leo.

Kanuni inayotoka kwenye ufafanuzi inaweza kuwa maonyo, ahadi, changamoto, n.k. kitu cha muhimu ni kuelewa hali ya mwanzo kwa uwazi wa kutosha ambapo tunaweza kusema “hivyo asema Bwana” kwa ujasiri tunapolitumia katika maisha yetu na maisha ya wengine.

#### **A. Chekecha Ukweli wa Uchunguzi Kupata Ule wa Ufunguo**

Ufafanuzi zaidi ni ufundi ambao ni sayansi. Hii ni, zaidi tu ya kufuata kanuni fulani—ingawa kanuni na mipaka ipo. Mazoezi, maombi, na umakini wa kuongozwa na Roho Mtakatifu ni muhimu ili kukuza uwezo wa kuchuja katika hakika kutoka kwenye hatua ya uchunguzi, kutambua zile muhimu zaidi, na kuelewa ujumbe mkuu wa fungu.

#### **B. Kuonyesha Wazo Kuu la Mwandishi**

Tunaporejea kwa mwandishi wa fungu, akilini tuna yote mwanadamu mwandishi, na vilevile Mungu ambaye ameelekeza uandishi. Pamoja na baadhi ya unabii pekee ambao mwanadamu mwandishi hakuuelewa, wazo la mwandishi na la Mungu linatakiwa liwe sawa.

Katika hali fulani, wazo kuu linaweza kuwa wazi katika fungu. Kawaida, kwa jinsi hiyo, itakuwa muhimu kuangalia dalili na uchunguzi wa ufunguo. Mandhali kawaida ni kionyesho muhimu zaidi cha kichwa au wazo kuu. Neno lililorudiwa au kipande cha maneno ni alama pia za maana. Kila fungu litakuwa tofauti, lakini utakuwa ukiangalia habari zifuatazo:

- Ni somo gani mwandishi anaandika juu yake?
- Ni nini anasema juu ya somo?

Hali muhimu ni kuweza kutengeneza muhtasari wa mambo haya mawili katika sentensi fupi. Hii inaweza kuchukua kabisa majaribio machache kabla haijawa sawa. Kuendeleza agizo la kujenga nyumba, hii ni sawa na kuweka msingi sawasawa. Maelezo ya ujazo wa ujumbe wa fungu utajengwa juu ya maelezo haya, kama itakavyokuwa kwa matumi

Hali muhimu ni kuweza kutengeneza muhtasari wa mambo haya mawili katika sentesi fupi.

#### **C. Kuonyesha Mtiririko wa Mawazo Kwenye Fungu**

Mara wazo kuu la mwandishi linapokuwa limeelezwa, hatua inayofuata ni kueleza jinsi anavyojenga wazo hilo katika kifungu. Ni mtindo gani anatomia? Kwa nini? Ni njia gani au hoja gani? Kwa nini amechagua njia hii kuwasilisha hili? Inatakiwa iwezekane kunukuru yote yaliyomo katika fungu na hali au hisia iliyowakilishwa. Kifungu kidogo kinatakiwa kiwe kinatia moyo, kinagusa moyo, kinakabili, kinapoza, kinatoa changamoto, n.k.

### **III. KANUNI ZA MSINGI ZA UFAFANUZI**

Ingawa ufafanuzi ni sehemu muhimu ya ujuzi unaohitaji kuendelezwa kwa vitendo, kuna baadhi ya taratibu za msingi ambazo zinatakiwa zifuatwe. Taratibu zilizoenezwa hapo chini zinakubali kama Biblia ni pumzi ya neno la Mungu, na kwamba Mungu anakusudia tuisome na kuelewa. Siyo kila mtu anakubaliana na maoni hayo, na hiki ndicho chanzo cha kutoelewana kwa dini nyingi duniani, vilevile chanzo cha madhehebu mengi.

#### **A. Kanuni za Ujumla Za Ufafanuzi wa Kibiblia**

1. Biblia ni neno la Mungu lenye mamlaka.
2. Biblia inajifafanua yenyewe vizuri, ikionyesha tabia ya Mungu.
3. Imani inayookoa na Roho Mtakatifu ni muhimu ili kuelewa maandiko.
4. Unatakiwa kufafanua historia, matendo, tabia, uzoefu binafsi, n.k. katika mwanga wa maandiko na siyo maandiko katika mwanga wa mambo haya.
5. Kusudi la kwanza la Biblia siyo kuongeza maarifa yetu, isipokuwa kubadili maisha yetu.
6. Kila mkristo ana haki, uwajibikaji, na nafasi ya kuchunguza na kufafanua neno la Mungu kwa msaada wa Roho Mtakatifu.

**B. Kanuni za Kufafanua kibiblia za Kifasihi, Kihistoria, na Kitheolojia.**

1. Unatakiwa kufafanua maneno kulingana na maana yake katika mandhali ya kihistoria na kiutamaduni ya mwandishi. Mara zote fikiria jinsi wasikiaji wa kwanza ambavyo wangukuwa wameelewa na kuuchukulia ujumbe.
2. Ni muhimu kuelewa fasihi ya fungu kabla hujajaribu kuelewa ukweli wa kitheolojia ambao linafundisha.
3. Lugha ya kitendawili kawaida ina wazo kuu moja. Usijaribu kusoma mambo mengi katika aina hiyo ya fungu. (Tazama ziada 2A “Lugha ya Biblia” katika maelezo ya aina za lugha ya mithali).
4. Hutakiwi kuwa muwazi juu ya somo kuliko maandiko yalivyo wazi. Usiongeze mawazo yako tu au mapokeo ya dini kwa kile ambacho Biblia inasema, kwa kuwa unaweza au wengine kuamini mawazo hayo kama ni ya kimaandiko.

**C. MAKOSA YA KAWAIDA YA KUEPUKA KWENYE KUFAFANUA**

Makosa ya kawaida matatu katika kufafanua yanatokea kwa sababu ya kushindwa kukumbuka kile hasa maandiko yanachosema.

1. *Ubao wa springi*

Kosa la aina hii linachukua jina lake kutoka ubao wa springi ambao wana kumfuu hutumia kuwasaidia kuruka juu. Ubao huu wa springi siyo kiini chao cha kucheza—unawasaidia tu kuanza. Kosa hili linatokea wakati mfafanuzi anapokuwa ameshajua anachotaka kusema, na hahitaji hasa kugundua maana ya fungu dogo. Kwa kifupi huaagalia juu ya fungu na “kurukia” kutoka pale kwenda kwenye topiki au mafundisho mengine anayotaka hasa kujadili. Hii inamtukana Bwana, aliyeliandika neno kuwakilisha ukweli kwetu.

2. *Maigizo*

Njia hii pia ni ya kawaida, lakini kama ambavyo haikubaliwi. Inahusika na kuacha maana halisi wazi ya maandiko na kujaribu kutafuta baadhi ya ujumbe uliofichika. Kwa hakika kuna baadhi ya vifungu ambavyo ni vigumu kuvielewa. Kwa jinsi hiyo vifungu vingi zaidi vinaleta maana tunapoangalia kwa uangalifu maneno na fasihi. Hatutakiwi kamwe kuangalia “maana iliyofichika” wakati mwingine inapokuwa imeelezwa kiwaziwazi. Hata katika hali ya fungu gumu, ni vizuri kukubali kuwa hatuelewi kuliko kujaribu kutunga aina fulani za maana ambazo ni ngumu kuziunga mkono

Hatutakiwi kuangalia “maana iliyofichika” mwingine inapokuwa imeelezwa kiwaziwazi.	kamwe “maana wakati inapokuwa imeelezwa kiwaziwazi.
---	--

3. *Kutojali Ufunuo Unaoendelea*

Haiwezekani kuelewa fungu kama tunasahau asili ya kuendelea kwa andiko. Mungu wakati mwingine anabadili njia anayoshugulika na watu. Mfano, katika Agano la Kale, Mungu alihitaji mfuatano wa sadaka ya wanyama halisi. Kwa jinsi hiyo, sadaka hizi zilikuwa za muda tu. Wakati mwana kondoo kamili wa Mungu alipokufa pale kalivari, Alikamilisha mahitaji yote ya Agano la Kale, Alikamilisha mahitaji yote ya Agano Jipya (Ebr 9:12). Hakuna sadaka ya aina yeyote inayohitajika katika Agano Jipya. Kama mtu angepaswa kutoa mwana kondoo kwa ajili ya dhambi zake leo, ingekuwa matusi kwa Kristo. Kwa hiyo, majadiliano ya ufafanuzi yanatakiwa kufanywa kwa uangalifu, na kwa mafundisho mapana ya neno akilini.

**D. Tumia “Usaidizi” Lakini Utumie Kwa Uangalifu**

Kuna zana nyingi na misaada ambayo inasaidia katika utaratibu wa ufafanuzi. Hivi ni pamoja na mafafanuzi, vitabu vidogo vya Biblia, maandishi ya Biblia, mtajo wa sehemu nyingine ya kitabu, kamusi, kitabu cha ramani, na vitabu vingine vingi. Kwa kiasi hivi vinasaidia, havitakiwi kuwa badala ya juhudi binafsi za mtu katika kuelewa fungu. Vimokusudiwa *kusaidia*, na siyo *kukufanyia kazi wewe*. Vitumie kadiri inavyohitajika kuelewa mambo ambayo haiko wazi kwako. Uwe mwangalifu hasa na mwingiliano wa marejeo ya Biblia. Mara nyingi, yanarejesha tu kwenye mstari mwingine wenye neno au fungu dogo la maneno sawa. Mstari uliorejeshwa unaweza au usiweze kuwa unahusiana na kisa cha fungu.

#### **IV. MFANO WA UFAFANUZI**

Rejea nyuma kwenye notisi zako za Yeremia 1, na pitia katika hatua ya ufafanuzi kadiri muda unavyoruhusu. Fuata utaratibu ulioonyeshwa hapo chini.

##### **A. Chuja Uchunguzi kupata Uhakika Hasa**

Ninapoangalia katika uchunguzi wangu wa Yeremia 1, inaonyesha kwangu kuwa uchunguzi wa muhimu zaidi ni (Orodhesha):

##### **B. Eleza Wazo Kuu**

Somo la ukurasa ni:

Kitu ambacho Yeremia anasema juu ya somo hili ni:

Maelezo mafupi ya wazo kuu, yanayoelekeana na mawazo mawili ya juu ni:

##### **C. Elezea Mtiririko wa Mawazo**

Yeremia anaanzisha wazo kuu la fungu kwa:



#### D. Baadhi ya Maswali ya “Maana”

Kadiri unavyfanyia kazi maelezo ya hapo juu, inaweza ikasaidia ukifikiria maswali yafuatayo juu ya *maana ya maandishi*. Huenda utafikiria maswali mengine mazuri, au hata bora zaidi. Haya yametolewa uweze kuanzia katika utaratibu.

##### *Mstari wa 5*

- Ina maana gani kwamba Bwana “alimjua” Yeremia?
- “Kutengwa” ina maana gani
- Ni nini baadhi ya mtazamo wa maelezo “...kabla hujazaliwa nalikutenga...?”

##### *Mstari wa 6*

- Kwa nini Yeremia anaweza kujifikiria mwenyewe kama “mtoto?”
- Kwa nini unadhani Yeremia alijibu kwa njia aliyotumia?

##### *Mstari wa 7*

- Ni jinsi gani unaweza kutofautisha tabia ya wito kutoka kwa Mungu na ule unaouona katika mstari huu?
- Jibu lako linasema nini juu ya Mungu na tabia yake katika swali linalofuata?

##### *Mstari wa 8*

- Ni nini neno la Bwana linasema juu ya kuitika kwa watu kwenye huduma ya Yeremia ya mbeleni
- Ni mvuto gani uliokuwepo kwa Yeremia kukutana na upinzani?

##### *Mstari wa 9*

- Ni jinsi gani Bwana “aliweka” maneno yake ndani ya Yeremia?

##### *Mstari wa 10*

- Nini unafikiri kifungu kidogo “kung’oa na kubomoa, kuharibu na kuangamiza, kujenga na kupanda” kinamaanisha?
- Ni nini unaweza kudhani tabia ya Yeremia inayoweza kumwezesha kufuata katika mpango wa Mungu?

##### *Mstari wa 12*

- Ni kanuni gani unayopata katika mstari huu inayohusu kuhusika kwa Mungu katika huduma ya hao aliowaita?

##### *Mstari wa 16.*

- Ni nini mstari huu unaonyesha juu ya tabia ya Mungu, hata unapokuja wakati wa kuhukumu watu wake mwenyewe?
- Mungu alifanya haki kwa kile alichopanga kufanya kwa watu wake? Kwa nini?

##### *Mstari wa 17*

- Nini ingeweza kuwa sehemu ya “kuwa tayari” kwa Yeremia?
- Kwa nini unadhani Bwana alirudia alichokuwa ameshasema nyuma (mstari 8)?

##### *Mstari wa 18*

- Ni nini maana na umuhimu wa mstari wa kifungu kidogo “mji wenye boma, nguzo ya chuma, na kuta za shaba?”
- Kwa nini watu wa mstari wa 18 kuwa wapinzani kwa Yeremia na ujumbe wake?
- Ni jinsi gani Mungu anajenga boma na kuandaa watu wake leo kusimama kwa ajili yake?

##### *Mstari wa 19*

- Mstari hii inaonyesha nini juu ya tabia ya Mungu na kujitoa kwa watu anaowaita?

### **E. Kanuni za Kibiblia**

Hatua ya mwisho katika utaratibu wa kutafsiri ni kujaribu kueleza maana ya fungu kama ufupisho wa kanuni ya Biblia. Maelezo haya yanatakiwa yawe sawa kabisa na “wazo kuu” kwenye kipengele cha 1V.B. juu. Kwa jinsi hiyo, wazo kuu katika 1V.B. imehusishwa na mandhali maalumu ya Yeremia 1, zaidi ya miaka 2500 iliyopita. Kanuni unayotaka kuunda sasa inatakiwa ikubalike wakati wote, na hasa leo.

Mfumo wa kanuni ingekuwa kitu kama: “katika hali ya aina hii tunatakiwa...” au “wakati hili linapotokea, Mungu ata...” Kuweka maneno yale yale ya kanuni ya kifungu maalumu yatatofautiana, ndiyo. Vilevile, kanuni inatakiwa kuwa maalumu iwezekanavyo. Hatua hii siyo rahisi, lakini ni muhimu. Na kwa msaada wa Mungu, inawezekana.

Kutokana na kujifunza kwangu Yeremia 1, Ninapata kanuni hizi za kibiblia zisizokuwa na mpaka (ziandike):

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Ni makosa yapi matatu ya kawaida katika kufafanua?
- Ni swali gani ufafanuzi unajibu?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Malizia maswali yoyote yaliyobakia katika somo hili ambayo hujamaliza.
- Anza kufanya katika hatua ya kufafanua kwa kutumia Matendo 17:1-10.



## Jedwali za Biblia

---

Katika kurasa zifuatazo kuna majedwali mawili yanayoweza kuwa msaada kwako:

- Kielelezo cha 4A. kinatoa picha kubwa ya Mpango wa Mungu wa milele katika Agano la Kale na Jipya.
- Kielezo 4A.2 kinaonyesha vipindi vya kihistoria vya Biblia.


**Kilelezo 4A.1 Historia ya Ukombozi wa Ulimwengu Katika Agano la Kale (AK) na Agano Jipya (AJ)**

Jedwali hapo chini limekusudiwa kutoa PICHA KUBWA YA Biblia kwa kuonyesha kwamba Agano la Kale na Agano Jipya zimeungana katika kutangaza kusudi la Mungu la mielele. Kuanzia katika Kutoka, Mungu alimuumba mtu (mwanaume na mwanamke) kuwa na uhusiano naye. Mtu alipotenda dhambi, uhusiano huo ulivunjika. Hesabu ya jinsi Mungu alivyoanza kuujenga tena huo uhusiano inaanzia katika Kutoka 3:15 na kuishia katika Ufunuo22. Kwa hakika, Biblia kwa msingi ni historia ya mpango wa Mungu wa ukombozi.

AK	Anguko/dhambi: Mwa 3:1-14	Ahadi iliyorudiwa kwa Ibrahimu: Mwa 12	Ahadi ya Mkombozi: Mwa 3:15, 21	Ahadi iliyorudiwa kwa Ibrahimu: Mwa 12	Utaratibu wa kujitoa ulianzihwa chini ya sheria ya Musa/Fidia ya Damu: Kutoka	Watu waliochaguliwa kuwa Mashshidi wake ulimwenguni kote
	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mtu (mwanaume &amp; mwanamke) waliumbwa kwa <u>MFANO WA</u> Mungu 1:27</li> <li>Kuwa na uhusiano na Mungu, 3:8</li> <li>Kuwa na uhusiano na wengine, 2:24</li> <li>Kuzaliana 1:28</li> <li>Kutawala dunia 1:28</li> <li>Kupokea baraka za Mungu, 1:28</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuabudu sanamu</li> <li>Uhusiano na Mungu kuvunjika</li> <li>Maumivu na mateso</li> <li>Kujaribu kutawalana</li> <li>Wote chini ya laana.</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>“Kizazi”cha mwanamke kingekanyaga kisigino cha nyoka</li> <li>Mungu alifanya mavazi ya ngozi kwa ajili yao</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Nitawabariki</li> <li>Kupitia kwako mataifa yote yatabarikiwa</li> <li>Mungu alichagua taifa moja kuwa watu wake na kumfanya kujulikana ulimwenguni kote</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Isa 53:7</li> <li>Kut 12:13 Mwana kondoo kutolewa kwa ajili ya dhambi. (Picha ya mwana kondoo wa Mungu ambaye angechukua dhambi ya ulimwengu).</li> <li>Mambo ya Walawi</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Yos 2:8-14; 4:24</li> <li>2Sam 7:25-26</li> <li>1Fal 8:41-43</li> <li>Isa 43:10-12; 54:5; 55:4, 5; 59:20; 60:16</li> <li>Kum 7:13-14</li> <li>Zak 13:1</li> <li>(na kuongeza mengi zaidi)</li> </ul>

AJ	Yesu : Kondoo wa Mungu anayechukua dhambi za ulimwengu	Injili: Yesu mkombozi alikuja	Matendo: Historia ya masimulizi ya ukombozi yaliyochukuliwa mpaka miisho ya dunia	Watu waliokombolewa kubadilishwa katika mfano wa Kristo: “Tunatakiwa tuishije?”	Ufunuo: Hatima ya ukombozi
	<ul style="list-style-type: none"> <li>Jn 1:29</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mt 1:21</li> <li>Yn 3:16, 17</li> <li>Lk 4:18, 19</li> <li>Lk 19:10</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Yerusalem 2 &amp; 6:7</li> <li>Yudea &amp; Samaria 6:8 - 9:31</li> <li>Palestina &amp; Syria 9:32 - 12:24</li> <li>Sehemu ya Mashariki mwa ulimwengu 12:25-19:20</li> <li>Mpaka Urumi 19:21-25:31</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Rum 3:24; Rum 4:22-25; Rum 6:11-14;</li> <li>Rum 8:29</li> <li>2Kor 3:18</li> <li>Efe 4:21-33</li> <li>Col 1:15-22</li> <li>1Pet 5:1, 10</li> <li>1The 2:19</li> <li>Yuda 24, 25</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>(Umbaji wa) Mbingu mpya na Dunia mpya (21:1)</li> <li>Kila kitu kufanywa upya (21:5)</li> <li>Watumishi wake watatawala naye (22:5)</li> <li>Wamebarikiwa wale wanaoosha mavazi yao (22:14)</li> </ul>

**Kilelezo 4A.1 Chronology of the Bible**



NJIA ZA KUJIFUNZA  
BIBLIA

SOMO LA **5**

# Warsha ya Kufafanua

## **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwapa wafunzwa nafasi ya kufanya zoezi la hatua ya ufafanuzi na kujifunza kwa kufuata neno.

## **Wazo Kuu**

Lengo la ufafanuzi ni kuelewa maana iliyokusudiwa na mwandishi.

## **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka kila mshiriki anatakiwa:

- Kuanza kutumia kanuni za ufafanuzi.
- Ni vizuri kuelewa maana ya Matendo 17:1-10a.

## **Ushauri kwa Wakufunzi**

Warsha: Gawanya wafunzwa katika makundi mdogo ya watu 3-4. Makundi yote yafanyie kazi fungu hilo hila lililoshauriwa mwishoni mwa saa ya kwanza. Dakika zote 15 za mwishoni mwa warsha ni vikundi kujadili kuelewa kwao kwa fungu kwa pamoja.

## **MUUNDO WA WARSHA**

Fungu tutakalotumia kwa warsha yetu ni Matendo 17:1-10a. Utaratibu wa warsha hii ni kama ifuatavyo;

- Tutagawanyika katika makundi ya watu 3-4.
- Tutakuwa na dakika 35 za kusoma fungu na kupitia hatua za ufafanuzi kama ilivyoonyeshwa katika somo la 4.
- Katika dakika 15 za mwishoni tutajiunda tena katika vikundi na kushirikishana kuelewa kwetu kwa fungu, na kuchagua maswali ya 'ufafanuzi' ya ufunguo.

## **KAZI YA KIKUNDI**

Kutokana na matokeo ya somo la 3, kila mfunzwa anapaswa awe tayari ana ufahamu juu ya Matendo 17:1-10a. Utahitaji kurejea katika uchunguzi wako wa somo hilo ili kumaliza somo hili. Kwa hakika, inaweza kuwa muhimu kufanya uchunguzi mwingine wa fungu kama yanatokea maswali ambayo huwezi kuyajibu.

Tumia utaratibu sawa na uliotumia kufafanua Yeremia 1 katika somo la 4.

### **A. Chuja Uchunguzi Kupata Ufunguo wa Kweli**

Ninapoangalia katika uchunguzi wangu wa Matendo 17:1-10a, inaonekana kwangu kana kwamba uchunguzi mkuu ni (orodhesha):

*Mandhali ya fungu:*

*Wasikilizaji wa kwanza:*

*Hali ya Mwanzo:*

*Ukweli na Uchunguzi mwingine:*

**B. Taja Wazo Kuu**

Somo la fungu ni:

Kitu ambacho Luka anasema juu ya somo hili ni:

Maelezo mafupi ya wazo kuu, yanayoelekeana na mawazo ya hapo juu, ni:

**C. Elezea Mtirirko wa Mawazo**

Luka anaanzisha wazo kuu la fungu kwa kusema:

**D. “Maswali ya Ina Maanisha Nini”**

Unapokuwa unafanyia kazi fungu hili katika vikundi, andika chini maswali ya ufunguo uliyouliza juu ya maana ya fungu lililokusaidia zaidi kuelewa *nini mstari unamaanisha*.

*[Zungushia maswali ambayo ni ya msaada ambayo ungetumia kama ungekuwa unaongoza mafunzo ya kikundi cha fungu hili.]*

**E. Eleza Kanuni Ya Kibiblia**

Kanuni isiyo ya wakati wote katika fungu hili ni:

**UFUPISHO**

Tumia nafasi hapo chini kuchukua notisi wakati makundi yanapokutanika pamoja kujadili kuelewa kwao kwa fungu. Nukuru jinsi wengine walivyokubaliana au walivyotofautiana kutokana na kuelewa kwako. Jaribu kufika katika makubaliano ya maana ya fungu.

Chagua maswali mawili mazuri zaidi ya ‘kufafanua’ kwa ajili ya kikundi kujifunza kutoka miongoni mwa yale “yaliyopendeza” vikundi na yaandike chini.

1.

2.

**VYANZO**

Hendricks, Howard G., and William Hendricks. Living By the Book. Chicago, IL” Moody Press, 1991.





# Kutumia Neno la Mungu NINATAKIWA NIFANYE NINI?

## ☞ Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kueleza mfano kwa wapanda kanisa jinsi ya kujifunza Biblia kwa kanuni ya 'matumizi' ya kujifunza Biblia kwa kufata neno.'

## ☞ Wazo Kuu

- Tunatakiwa kutii kanuni za kibiblia tunazojifunza, au vinginevyo zoezi linakuwa bure.
- Hali yetu lazima iendane na mandhali ya kibiblia ili matumizi kuwa halali.

## ☞ Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kujua jinsi ya kutumia kanuni ulizojifunza kutoka katika maandiko
- Kujua jinsi ya kutayarisha maswali ya kimatumizi ya kujifunza kwa kufuata neno.
- Kuanza kutumia kanuni za matumizi zilizotolewa katika somo hili.

## ☞ Ushauri kwa Wakufunzi


Mkazo katika somo hili unatakiwa kuwa matumizi ya matendo ambayo kila mtu anaweza kuyafanya katika maisha na huduma yake. Wafunzwa wanatakiwa watiwe moyo kufanya matumizi haya binafsi.

## UTANGULIZI

Kwa baadhi ya sababu, sehemu ngumu ya maisha ya ukristo ni katika kutumia ukweli wa maandiko katika maisha ya kila siku. Tunaweza tukapata maarifa ya kutosha na imani yetu inaweza kukua kutokana na kujifunza kwetu Biblia. Kwa jinsi hiyo, vinginevyo labda tuelewe jinsi ya kuweka katika matendo kile tulichojifunza, kujifunza hakutatunufaisha sana. Katika masomo yanayoendelea, tumekusanya zana zetu (uchunguzi) na kuziunda katika kanuni ya kibiblia (ufafanuzi). Na sasa ni wakati wa kuishi katika ukweli (matumizi). Matumizi dhahili yanauliza swali la "Nini nifanye?"

Tunapoonyesha *tunachotakiwa kufanya*, bado tunahitaji kutii kile Biblia inachofundisha. Yesu alifundisha kwamba wanafunzi wake wanapaswa kufundisha wengine "...kutii kila nilichokuamuru" (Mt 28:20). Mtume Paulo anaongea juu ya kutumia kilichofunzwa kwa namna hii "Mnifuate mimi kama nami ninavyomfuata Kristo" (1Kor 11:1). Mtume Yohana anaandika kwamba "Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake" (1Yoh 2:3). Vilevile, tunahitaji kutafuta njia ya vitendo **kutumia** ukweli tunaajifunza tunapojifunza Biblia. Mtume Yakobo anaandika, "...Imani peke yake, kama hajaambatana na matendo, imekufa" (Yak 2:17).

### Kielelezo 6.1




Katika somo hili tunataka kujifunza fungu la Yeremia 1. Tutajifunza maandishi hayo tena, tukiangalia kanuni za kibiblia ambazo tunaweza kutumia katika maisha yetu. Wakati kanuni zitamhusu kila mmoja, matumizi ya vitendo yanaweza kutofautiana kutoka mtu mmoja hadi mtu mwingine kwa sababu matatizo yetu ni tofauti.

## I. MATUMIZI—HATUA YA TATU YA KUJIFUNZA KWA KUFUATA NENO

Kuna mambo mawili muhimu ambayo lazima yashughulikiwe katika hatua ya matumizi. Ya kwanza ni ukweli kwamba matumizi lazima yafanyike na mtu mwenyewe, kuliko kwa wengine tu. Haijalishi kama mafunzo ni kwa ajili ya kukua binafsi, au kuwafundisha wengine. Kama hatulitumii kwetu wenyewe kwanza, tunageuka kuwa wanafiki. Chochote tunachofundisha kwa wengine kinatakiwa kitoke wakati wote nje ya kile tulichokwisha kujifunza na kukitumia katika maisha yetu wenyewe. Kisha tunaweza kuwafundisha wengine kama hitaji linatokea.

Kipengele kingine cha pili muhimu ni kuhakikisha kuwa *mandhali* yetu ni sawa na *mandhali ya mwanzo*. Hatuwezi, na tunatakiwa tusingumie ujumbe uliotolewa kwa wahusika wa kibiblia katika maisha yetu wenyewe labda hali yetu iwe inaendana. Kwa hiyo, mengi ya hatua ya matumizi ni pamoja na kuuliza “Nini katika maisha yangu kinaendana na hali iliyoelezewa katika fungu?”

### Kielelezo 6.2 Kulinganisha Mandhali



## II. UTARATIBU WA MATUMIZI

Matumizi sahihi ya kutafakari yanaanza na maana na desturi ya maeneo muhimu katika maisha yetu na huduma ambayo itaathiriwa na kanuni za kibiblia ambazo tumeziona katika maana, maswali ya mawazo ya mtiririko juu ya ambacho tunapaswa kufanya kwa kuitikia ujumbe. Kama kawaida, hatua hii lazima izungukwe na maombi, na kusindikizwa na utayari wa kujifunza na kukua katika Bwana.

### A. Mambo ya Kutumia

Hatima ya lengo la matumizi ni kuendeleza tabia ya mtu na ufanisi mkubwa wa huduma. Kuna idadi ya maeneo au mambo ambayo tunatakiwa kuyafikiria tunapojaribu kutumia ujumbe wa fungu kibinafsi. Mambo haya ni pamoja na maisha yetu na huduma. Baadhi ya mifano imeorodheshwa hapa:

Imani: Nini ninachoweza kujifunza juu ya imani binafsi.

Nia: Ni nia ipi nzuri na mbaya? Ni nini matokeo yake? Ni jinsi gani naweza kubadili isyofaa?

Matendo: Nini ninatakiwa nianze kufanya? Ni nini ninatakiwa niache?

- Dhambi: Ni dhambi ipi imeonyeshwa wazi kwangu? Nitawezaje kuweka mambo sawa na Mungu /na wengine?
- Changamoto: Ni changamoto zipi zimewekwa wazi kwangu katika maisha binafsi? Katika uhusiano na wengine? Katika huduma?
- Ahadi: Ni ahadi zipi naweza kudai kama zangu? Kuna masharti? Ni nini – katika maisha yangu na katika huduma?
- Tabia: Ni sifa zipi za tabia ninazohitaji kukuza katika maisha yangu na katika huduma?

### B. Maswali ya Kawaida

Hendricks anaorodhesha idadi ya maswali ya matumizi yanayosaidia yanayoweza kuulizwa kwenye fungu lolote la maandiko. Ni haya”

- Kuna mfano kwangu wa kufuata?
- Kuna dhambi ya kuepuka?
- Kuna ahadi ya kudai?
- Kuna maombi ya kurudia?
- Kuna amri ya kutii?
- Kuna masharti ya kutimiza?
- Kuna mstari wa kukariri?
- Kuna kosa la kuwekea alama?
- Kuna changamoto ya kukutana nayo?

### C. Maswali Maalumu

Ukiwa umeuliza maswali kwa ujumla ya matumizi ya Yeremia 1, inasaidia pia kuangalia katika kila mstari au sehemu na kuuliza maswali zaidi maalumu. Kama tofauti kutoka hatua ya nyuma, kwa jinsi hiyo, maswali haya moja kwa moja yanaendana na *unachotakiwa kufanya* kama matokeo ya fungu. Kuna idadi isiyo na mwisho ya maswali haya maalumu, kwa kuwa ni tofauti kwa kila fungu. Unapungukiwa tu na ubunifu wako. Jambo muhimu ni kufungua moyo wako kwa Bwana, na kumruhusu kukuonyesha anachotaka kiwe tofauti katika maisha yako.

Baadhi ya maswali ya mfano yameorodheshwa hapo chini. Jisikie huru kuongeza unapolifanyia kazi fungu.

#### *Mstari wa 5*

- Mafundisho ya mstari huu yanakwambia nini binafsi juu ya uhusiano wako na Mungu Muumbaji?
- Mstari huu unasema nini kwako binafsi juu ya wito wako katika huduma?
- Kama huna ufahamu wazi juu ya wito, nini mstari unakwambia?
- Mstari huu unasema nini kwako binafsi juu ya mapenzi ya Mungu katika maisha yako?
- Unajua mapenzi ya Mungu katika maisha yako ni nini katika hatua hii?
- Ni nini matokeo ya mstari huu uliyonayo kuhusu imani yako katika Mungu Mwenyezi?
- Unakubaliana? Unakubali wazo hili bila kusita?

#### *Mstari wa 6*

- Unajilinganisha na kusita kwa Yeremia kukubali changamoto ya Mungu?
- Ni nini kimekuwa “udhuru”?
- Bado unatoa udhuru? Unahitaji kufanya nini juu yake?

*Mstari wa 7*

- Unafikiaje binafsi juu ya majibu ya Mungu kwa Yeremia?
- Unafikiriaje binafsi juu ya kukosekana kwa uwazi wa “kunyumbuka” kwa upande wa Yeremia kukataa wito wa Mungu?
- Kunaonekana kutokuwa na nafasi kwa Yeremia kufanya uamuzi wake mwenyewe. Unajisikiaje binafsi juu ya kutokuwa na uchaguzi wa hakika katika hali ya kuitwa na Mungu? Ungekuwa na uchaguzi?
- Mstari huu unaleta shida kwa upande wa uhuru wa mwanadamu wa kuchagua na Utukufu wa Mungu?
- Kama hili linaleta matatizo, utaitikiaje?

*Mstari wa 8*

- Mstari huu unamaanisha nini kwako binafsi?
- Utatumiaje hili binafsi katika hali ya maisha na huduma yako?

*Mstari wa 9*

- Unaweza kuelezea mazingira ambayo Mungu “amekutana” nawe binafsi

*Mstari wa 10*

- Ni nini mistari hii inasema kwako binafsi juu ya hatima ya lengo la Mungu kwenye huduma yako?
- Unaweza kuona usawa kati ya kazi ya Yeremia na yako kama mpanda kanisa?
- Kulikuwa na vipingamizi ambavyo Yeremia ilimbidi kukabiliana navyo ili kufikia lengo la kujenga na kupanda upya. Nini baadhi ya vipingamizi unavyokutana navyo unapofikia kuelekea kwenye kusudio sawa la kujenga ufalme wa Mungu kwa kujenga makanisa mapya?
- Unajisikiaje juu ya matazamio ya kuwa katika nafasi ambayo unaweza kwenda kinyume na mapokeo na viongozi ambao wanaweza kupinga wazo lako la upandaji kanisa.?
- Ni jinsi gani utashughulika na vipingamizi na hao ambao wanawezekana wakakupinga?

*Mstari wa 12*

- Ni kwa jinsi gani unaona kanuni ya mstari huu ikileta maana kwako binafsi?
- Mstari huu unafanya nini kwenye ujasiri wako kama mpanda kanisa?

*Mstari wa 16*

- Unashughulikaje na swala la “miungu mingine” katika maisha yako mwenyewe?
- Ni nini unahitaji kufanya kuhakikisha kuwa utii wako ni kwa Mungu tu na siyo kwa “miungu” kama vile mali, utaifa, n.k.?

*Mstari wa 17*

- Unapimaje utayari wako katika hatua hii kuweza kusimama kwa ajili ya Mungu dhidi ya upinzani wote?
- Unahitaji kufanya nini binafsi kujitayarisha katika misukosuko yote?
- Ni eneo gani katika maisha yako linahitaji kusaidiwa kiroho?

*Mstari wa 18*

- Mungu alimuimarisha Yeremia. Ni jinsi gani Mungu amekuimarisha kusimama kwa ajili yake.
- Ni nini Mungu amekupatia kuwa nawe katika misukosuko yote?

- Ni jinsi gani hili linakufanya kujisikia juu ya Mungu na msaada wake kwako na katika huduma?

### **UFUPISHO**

Mtumizi ninayoyaona kwa maisha yangu na huduma katika Yeremia 1 ni:

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Unakubaliana kwamba ni muhimu mara nyingi kutumia mafundisho kwetu wenyewe kabla ya yote? Kwa nini hiyo ni muhimu?
- Ni jinsi gani 'mandhali yanapelekea matumizi ya fungu?

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Kama hukupata muda wa kukamilisha somo hili kama kikundi, fanya hivyo kabla ya warsha nyingine ili kwamba uwe unafahamu kanuni.

### **VYANZO**

Hendricks, Howard G., and William Hendricks. *Living By the Book*. Chicago, IL Moody Press, 1991.



# Warsha ya Matumizi

## **Kusudi la Somo**

Kusudi la somo hili ni kuwapa wafunzwa nafasi ya kufanyia mazoezi hatua ya matumizi ya kujifunza kwa kutumia neno.

## **Wazo Kuu**

- Tunatakiwa kutumia ujumbe wa fungu kwenye maisha yetu kabla ya yote.

## **Matokeo Yanayotarajiwa**

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Awe anajua jinsi ya kutumia ujumbe wa Matendo 17:1-10a kwenye maisha yake mwenyewe na huduma.

## **Ziada**

7A Waefeso—Njia ya Kujifunza kwa Kuongozwa na Neno

## **Ushauri kwa Wakufunzi**

Warsha hii inaendana na mbili nyingine zinazoendelea. Wagawanye wafunzwa katika makundi ya watu 3-4. Toa dakika 15 mwisho wa saa kukutana pamoja na kulinganisha matokeo.

## **MUUNDO WA WARSHA**

Tutaendelea kujifunza Matendo 17:1-10a. Tutakuwa tunatumia uchunguzi uliopita na ufafanuzi. Muda huu, kwa jinsi hiyo, tutakuwa tunaangalia matumizi katika maisha yetu wenyewe na huduma.

- Gawanyika katika makundi ya watu 3-4.
- Chukua dakika 35 kufanyia kazi hatua za matumizi, na amua jinsi gani ni vizuri kutumia fungu katika kila eneo la maisha yako na huduma.
- Tumia dakia 15 za mwisho kujiunda kwenye makundi na jadili matumizi yenu, na kuchagua maswali ya 'matumizi' yanayofaa kuweza kutumiwa katika kuongoza mafunzo ya kufata neno katika kifungu hiki.

## **KAZI YA KIKUNDI**

Tumia utaratibu ufuatao kukusaidia kufika katika matumizi yanayokubaliwa na ya msaada katika maisha yako.

### **A. Kumbuka Kanuni ya Kibiblia**

Ziandike tena upya kanuni za kibiblia ambazo umepata kwa aliji ya Matendo 17:1-10a kutoka somo la 5:

### **B. Linganisha Mandhali**

Ili matumizi yako yakubalike, mandhali yako yanatakiwa yaendane na mandhali ya kwanza ya kibiblia.

1. *Kwa kifupi elezea Mandhali ya kwanza ya kibiblia ya Matendo 17:1-10*

2. *Kwa kifupi eleza mandhali ya wakati huu (wewe ni nani, ni nini unafanya, n.k.):*
  
3. *Andika maelezo mafupi angalau ya jinsi moja ambayo mandhali yako yanafanana na ya Matendo 17 (Kumbuka: Hii itatofautiana kwa namna ya kila mmoja kwenye kikundi, lakini pia kutakuwa na mlingano wa kutosha ambao mtaweza kusaidiana)*

### **C. Fikiri juu ya Jambo la Matumizi**

Soma katika fungu na angalia kama mojawapo ya jambo lolote linaloonekana kufaa katika hali yako. kama ni hivyo, Nakiri jinsi zinavyohusiana. Pengine kuna mada zingine zinazofaa. Kama ndiyo, zinukuru hapo chini.

- Imani
- Nia
- Matendo
- Dhambi
- Changamoto
- Ahadi
- Tabia
- *(Mengine)*
- *(Mengine)*

### **D. Maswali ya Jumla**

Uliza maswali ya jumla ya matumizi yaliyorodheshwa hapo chini. Andika majibu yako kwa kila linalofaa.

- Kuna mfano ambao naweza kufuata?
- Kuna dhambi ya kuepuka?
- Kuna ahadi ya kudai?
- Kuna maombi ya kurudia?
- Kuna amri ya kutii?
- Kuna masharti ya kufuata?
- Kuna mstari wa kukariri?
- Kuna kosa la kunukuru?
- Kuna changamoto ya kukutana nayo?

## E. Uliza Maswali Maalumu

Sasa mnapokuwa mnafanya kazi ya fungu kwa pamoja, fikiria maswali maalumu kwa kila mstari ambalo unakazia “Nini ninapaswa kufanya?” Yaandike maswali hayo, na majibu katika nafasi inayofuata:

*[Zungushia maswali bora mawili ambayo unaweza kutumia katika kuongoza kikundi kujifunza kwa kufuata neno katika maandishi haya.]*

### UFUPISHO

Mtakapokutana tena, jadili na linganisha matumizi mnayoona katika fungu. Mwisho, linganisha maswali ya ‘matumizi’ ambayo kila kundi limechagua, na chagua mawili ambayo yatakuwa ya msaada zaidi kama mngekuwa mlikuwa mnaongoza mafunzo ya kujifunza kwa kufuata neno ya fungu.

1.

2.

### MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Ni kitu gani muhimu zaidi unachotakiwa kufanya kama matokeo ya kusoma fungu hili?
- Ni nini umeona kama matokeo ya njia hii ambacho ni kipya kwako?

### UTEKELEZAJI WA AZIMIO

- Umeendelea mbele sasa katika hatua ya uchunguzi, ufafanuzi, na matumizi. Kabla ya semina ijayo, utatakiwa kuanza kwa ufupi njia ya kujifunza Biblia kwa kufuata neno kwa kutumia kanuni uliyojifunza. Utakuwa na dakika 20 za kutoa mafunzo haya ya Biblia wakati wa warsha katika semina hiyo. Semina ijayo itajadili kanuni za kuongoza kujifunza kwa kufuata neno.
- Katika hatua hii, kazi yako ni kujifunza fungu kwa kutumia njia ya kujifunza kwa kufuata neno, na kutayarisha uchunguzi mwingi, ufafanuzi, na matumizi na maswali ya matumizi iwezekanavyo. Unatakiwa kuonyesha maana ya fungu, na matumizi wakati wa muda huu wa maandalizi. Kisha, kutoka katika maswali yako yote, chagua maswali 5-6 ya uchunguzi, 2-3 maswali ya ufafanuzi, na 1-2 maswali ya matumizi ambayo yatafaa kuongoza wafunzwa wengine kugundua na kutumia mafundisho ya fungu.



- Unaweza kuchagua fungu moja kati ya yaliyoorodheshwa chini kwa mafunzo yako. Tafadhali linganisha uchaguzi wako na wafunzwa wengine ili kwamba kila mmoja asifanye fungu lilelile. Kama mfano kwa ajili yako, Ziada 7A ni mfano wa kujifunza Biblia kwa kufuata neno katika kuanzisha kanisa huko Efeso katika Matendo 19:1-10. Mafunzo yako yanatakiwa kuwa na muundo unaofanana, lakini hata hivyo utakuwa na maswali tofauti, wazo kuu, na matumizi.
- Mfano wa vifungu vya kuchagua:
  - Matendo 13:4-12 (Pafo)*
  - Matendo 13:13-52 (Antiokia)*
  - Matendo 14:1-7 (Ikonio)*
  - Matendo 14:8-20 (Listra na Derbe)*
  - Matendo 16:11-40 (Filipi)*
  - Matendo 17:10-15 (Beroya)*
  - Matendo 17:16-34 (Athene)*
  - Matendo 18:1-17 (Korintho)*

#### **VYANZO**

Hendricks, Howard., and William Hendricks. Living By the Book. Chicago, IL: Moody Press, 1991.



# Waefeso—Njia ya Kujifunza Biblia Kwa Kufuata Neno

## JINSI PAULO ALIVYOANZISHA KANISA

---

### UTANGULIZI

Yesu alitumuru kufanya wanafunzi katika mataifa yote. Tunaweza kufanya hivi? Ni kiasi gani unachoweza kukamilisha? Ni watu wangapi unaoweza kuwaleta kwa Yesu tuseme kwa muda ...wa miaka miwili? Ni ukubwa gani wa eneo la kijiografia utaweza kueneza injili kwa kipindi hicho? Katika Matendo 19, mtume Paulo aliweza kutangaza injili kwa kila mmoja katika eneo kwa kipindi kifupi cha muda. Kama tunataka kuwa wafanisi wa upandaji kanisa, tutahitaji kujifunza jinsi Paulo alivyoweza kufanya hili, na kujaribu kutumia njia ileile aliyotumia. Ngoja tuangalie njia Paulo alizotumia katika upandaji huu wa kanisa wenye mafanikio.

### I. MAOMBI

Chukua muda katika kuomba kwamba Mungu aweze kufungua macho yetu na mioyo kuelewa jinsi anavyotaka kusema nasi kupitia fungu hili.

### II. SOMA MATENDO 19:1-10

Soma fungu kwa uangafu na kwa kutafakari—au kwa Sauti au kimya

### III. UCHUNGUZI

Hatua ya kwanza ni kugundua nini Biblia *inasema*. Angalia kwa karibu kwenye fungu na kisha jibu maswali hapo chini.

*Kutoka katika mandhali (Matendo 18:18-28):*

- Wakati Paulo alipofika Efeso katika Matendo 19:1, alipata baadhi ya wafuasi. Ni **jinsi gani** unafikiri watu hawa kuwa wafuasi?
- **Nani** alihusika kufanya hawa wafuasi, na kwa **jinsi gani**

*Kutoka katika fungu (Matendo 19:1-10):*

- **Ni** udhaifu gani Paulo aligundua kati ya wafuasi hawa , na **alifanya nini** juu yake
- **Wapi** Paulo alianza kazi yake kwa waefeso?
- **Ni** mabadiliko gani Paulo alifanya katika mbinu yake na **kwa nini?**
- **Nini** yalikuwa matokeo ya huduma ya Paulo huko Efeso?

### IV. UFAFANUZI

Hatua ya pili ni kuamua nini Biblia *inamaanisha*. Tafakari juu ya ujumbe wa mistari hii kwa kujadili maswali yafuatayo:

- **Kwa** nini Luka anakazia kwenye itikio la Paulo la mafundisho ya Roho Mtakatifu katika mistari ya kwanza minane ya kifungu hiki?
- Katika mstari wa 8, Paulo anatoa hoja kwa kushawishi. Kutoka kwenye maandishi, **nini** ilikuwa itikio kwa kila mmoja juu ya njia hizi, na **ipi njia** unayofikiri fungu limekusudia kutia moyo?





---

# **UINJILISTI**

---



# Utangulizi Kwenye Uinjilisti

## MUNGU KUUPENDA ULMWENGU JINSI HII

---

### Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kutambulisha asili, hitaji, nia na sehemu ya uinjilisti katika mkakati wa KUM.

### Wazo Kuu

- Uinjilisti ni utaratibu, na siyo tukio tu.
- Ujuzi na uzoefu katika uinjilisti unaweza kuendelezwa.
- Utaratibu wa uinjilisti haujakamilika mpaka waumini waliokomaa zaidi wameanza kufuasa wakristo wapya na kuwasaidia kukua katika imani.

### Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kufahamu hitaji la haraka la waliopotea na ongezeko la nia ya upendo wa agape kuwainjilisha.

### Ziada

1A Daraja

### Ushauri kwa Wakufunzi

Uwafanye washiriki kusoma mstari uliochaguliwa katika sehemu ya 11 kwa sauti. Chukua muda uleule kufanya marudio ya maombi ya utatu. Watie moyo washiriki kuunda maombi yao ya utatu kabla ya mafunzo yajayo ya semina.

## UTANGULIZI

Uinjilisti ni kazi muhimu kwa kila muumini. Kwa hao walioshiriki katika kazi ya upandaji kanisa, Uinjilisti siyo kitu kisicho muhimu. Kwa hakika, upandaji kanisa bila uinjilisti haiwezekani. Tunaweza kupata tumaini katika utaratibu kutoka Mathayo 4:19, ambapo Yesu aliwapa changamoto wanafunzi kumfuata kwa maneno, "Nifuateni...nitawafanya wavuvi wa watu." Yesu alitaka wavuvi hawa wenye uzoefu kutumia maisha yao kujenga kanisa lake. Tunapomfuata Kristo, kuchunguza sheria zake na kumtii, anapenda pia kutufanya kuwa wavuvi wa watu, kuweza kuwavutia na kuwaleta watu kwake. Bwana peke yake anaweza kutufanya kuwa wavuvi wafanisi wa roho.

Kuna njia nyingi za kukamata samaki. Tunatumia mitumbwi mikubwa, mitambo migumu na neti kubwa sana kuwakamata maelfu. Tunatupa neti ndogo kukamata baadhi. Na tunatumia miiba ya seng'eng'e na vivutio vya kuvutia kuwakamata mmoja baada ya mwingine. Hatukamati samaki kila tunapotupa wavu au jarife, lakini tunaweza tukawa tunajifunza kutokana na kila uzoefu. Tunatakiwa kwenda sehemu samaki zilipo na kuchagua njia inayofaa ili kuwakamata.

Katika njia inayofanana, kuna njia nyingi sana za kuleta wanaume, wanawake, vijana na watoto kwa Kristo. Kuna, hasa, injili moja ya kweli. Tunapokuwa tunaihubiri injili hii, Roho Mtakatifu wa Mungu anauthibitishia ulimwengu hatia kuhusu dhambi, haki na hukumu (Yoh 16:8) na kuwaleta watu kwenye imani inayobadili—maisha. Kazi yetu ni kuunganisha njia za ufanisi na mikakati kuwaleta watu kwa Kristo na kuwashirikisha katika kanisa. Tutakuwa tunafikiria juu ya baadhi ya njia hizi na mikakati katika somo hili.

## I. ASILI YA UINJILISTI

Uinjilisti una maana “kueleza habari njema.” “Habari njema” ya kwamba Yesu Kristo amefanya wokovu kuwa rahisi na kupatikana kama zawadi ya bure ni habari njema kuwahi kuchoma sikio la mwanadamu na moyo. Uinjilisti ni pamoja na kuwasaidia walio nje ya imani ya Yesu Kristo kusogea kuelekeza imani ndani yake. Kwa jinsi hiyo, uinjilisti si mwisho wa utaratibu. Uinjilisti wa kweli ni kama mguu wa kwanza wa mbio za mashindano. Mara watu wanapokuwa wameletwa kwa Kristo lazima “wakabidhiwe” kwa mfuasishaji ambaye atawasaidia kulisha maisha yao mapya ndani ya Kristo. Mbio hazijakamilika mpaka ushirika wa wanaoamini umepandwa na mwili wa Kristo unaongezeka kwa uinjilisti mwingine na ufuasishaji. Kuangusha kirungu cha polisi baada ya hatua ya uinjilisti haikubaliwi.

### A. Utaratibu

Utaratibu huu wa uinjilisti ni njia moja muhimu ambayo Bwana anahusisha wakristo, kwa ushirikiano wa kazi ya Roho Mtakatifu, kujenga ufalme wa Mungu—kanisa la Yesu Kristo. Wakati kazi ya Roho Mtakatifu ndani ya mioyo ya watu haionekani, juhudi za wakristo za uinjilisti ni za uma au binafsi.

Uinjilisti unianza binafsi, kwa maombi. Hii ni pamoja na maombi ya mtu binafsi na pia “maombi ya utatu” (angalia maombi ziada 3A “Maombi ya Utatu”). Maombi ya utatu yana wakristo watatu wanaoamini wakikutana mara kadhaa kuomba watu watatu marafiki au jamaa ambao hawajaokoka. Kikundi kinakutana kuomba watu hawa mpaka wanapokuwa waumini au misukosuko inapozuia kikundi kuendelea kuomba pamoja. Watie moyo watu wengine kuomba unapokuwa unajihusisha katika kazi ya uinjilisti, Ukifuata mfano wa Paulo katika Waefeso 6:19-20 na Wakolosai 4:2-6. Tunapomba, tunamwomba Mungu:

- Kuandaa mioyo ya hao ambao anaotaka tuwajulishe habari njema.
- Kutuongoza kwa hao walio tayari.
- Kutusaidia kutoa injili katika njia wazi na inayoleta maana.
- Kuutunza ujumbe uliopandwa.

Kihadharani, tunatumia kama kianzio cha kukutana na Mungu kwa kushirikisha imani zetu tunapokuwa tunaendelea na shuguli zetu za kila siku katika maisha. Tunaanzisha uhusiano mwema na watu katika jamii zetu. Tunatumia muda kuwa na watu ili waweze kusoma maisha yetu na sisi tuone maisha yao. Tunajenga daraja la kuaminiana na mtu pekee, familia, kupanua ushuhuda na mvuto kwa Kristo. Uinjilisti mara kwa mara ni pamoja na shughuli maalumu iliyoandaliwa kuleta usikivu wa injili. Inaweza ikawa kupitia tendo la ufadhili au kuchangia kitabu kidogo cha sala, au inaweza kuwa vigumu kama kuandaa juhudi za kufikia mkoa kwa kutumia mkanda wa *senema ya Yesu* au mwenye kipawa cha uinjilisti.

### B. Ujumbe

Katika barua kwa kanisa jipya lililoanzishwa Urumi, Mtume Paulo aliandika maneno haya:

*“Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia” (Rum 1:16).*

Ni nini habari ya injili—“habari njema”—tunayoeleza? Paulo analifanya wazi na rahisi onyesha la injili katika 1Wakorintho 15:3-7. Katika fungu hili, anachanganua yaliyomo katika injili katika sehemu sambamba mbili—ungamo na tumaini. Wanatheolojia wanaweza kuandika ukubwa usiohesabika wa yaliyomo katika injili. Kwa hiyo maana halisi ya “habari njema” imefupishwa katika maandishi haya.

Sehemu za injili zinaonekana wazi kama tunatoa nakala ya mstari kama ilivyoonyeshwa hapo chini:

**Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu [kulingana na maandiko]**

-Ya kwamba alizikwa

**Ya kwamba alifuka siku ya tatu [kulingana na maandiko]**

-kwamba alionekana na Petro, na kisha kwa wale kumi na wawili ...

Katika mfumo huu ni rahisi kuona viini vikuu viwili—kufa na kufufuka kwa Kristo. Vyote vilikamilishwa “kulingana na maandiko” na kila kimoja kina ushahidi wa kutosha. Ushahidi wa kifo chake ilikuwa ni mazishi yake, na ushahidi wa kufufuka kwake ilikuwa ni kuonekana kwake kwa waumini. Angalia kwa karibu katika kila kiini kikuu.

1. *Tubu—(kwa sababu alikufa)*

Kuna mengi yaliyohifadhiwa katika maelezo haya. Kwanza kabisa, Ni lazima tukubali kwamba tu wenye dhambi mbele za Mungu. Kama kungekuwa na kitu chochote ambacho tungefanya kujiokoa kungekuwa hakuna sababu ya Kristo kufa. Lakini hakuna kabisa tunachoweza kufanya kupata upendeleo wa Mungu. Hakuna kitu kama hicho cha mtu mwenye haki (Rum 3:10,20). Ni lazima tujitweze wenyewe katika rehema zake. Tunahitaji neema, na siyo haki (Efe 2:8,0).

Kifo cha Kristo pia kina maanisha kwamba kifo chake kinatosheleza kutuokoa sisi. Hii isingekuwa rahisi kama hangekuwa mwana wa Mungu—Mungu—mwana—Mungu katika mwili. Mungu asingekufa mpaka Yesu alipochukua mwili wa kibinadamu na kuuva. Lakini mtu wa kawaida asingekufa kwa ajili ya kila mmoja. Anaweza kufa tu kwa ajili ya dhambi zake. Kwa hiyo Yesu pekee, kama Mungu nafsi angeweza kutosheleza gadhabu ya Mungu dhidi ya dhambi na kutoa wokovu kwetu kwa neema.

Sehemu ya kwanza ya injili ni pamoja na utupu wetu usiofaa na uungu utoshelevu wa Kristo. Hakuna hata mmoja aliyeokoka kwa usafi mpaka wanapokubali mamlaka ya Kristo na kutubu.

2. *Mtumaini Kristo—(kwa sababu alifufuka)*

Sehemu ya pili ya injili inahusu tumaini. Ni muhimu kuungama, lakini hiyo tu haitoshi kutuokoa. “Wakristo” wengi wanaamini Krsito alikufa kwa ajili ya dhambi, lakini wanadhani wanahitaji kufanya aina ya kazi kuustahili wokovu wake. Huu ulikuwa ni uzushi Paulo alioukabili huko kwa wagalatia. Baadhi walifundisha kuwa ni lazima wote kuamini na kutunza sheria ili kuweza kuokoka. Paulo alililaumu wazo hilo katika upeo mzito unaowezekana (Gal 1:8-9; 2:15-16; 3:3, 11). Kujitua kwa Kristo kulitoshia kutuokoa. Hatuhitaji na hatuwezi kuongeza chochote kupitia juhudi zetu wenyewe..

### C. Wastani

Maonyesho yenye nguvu sana ya ujumbe wa injili ni ule tunaoushuhudia kwa maisha yetu. Namna tunavyoishi inaleta uhai kwa maneno tuliyoyaongea. Uaminifu wetu, huruma, na uwazi ni dhana muhimu inayotumiwa na Bwana kutufanya “chungu na nuru” mahali pale tunapoishi. Shairi rahisi linatupa changamoto:

*Unaandika injili, ukurasa kwa siku,*

*Kwa matendo unayofanya na maneno unayosema.*

*Watu wanasoma unachoandika, upotofu au kweli.*

*Injili ni nini kulingana na wewe?*

## II. HITAJI LA UINJILISTI


### A. Watu Kiroho Wamepotea na Kutengwa na Mungu Milele Bila Yesu Kristo

Siyo tu kwamba kila mtu ametengwa kiroho na Mungu, lakini pia kila mtu hawezi kabisa kujiokoa mwenyewe. Kwa sababu ya dhambi Mungu mtakatifu hapatikani kwake. Endapo kama mtu binafsi anatambua hali yake au la amekata tamaa na kuangamizwa endapo kama hatapokea suluhu lililotolewa na Yesu Kristo na si mtu mwingine. Tafadhali angalia Ziada 1A “Daraja” kwa njia rahisi kuelezea jinsi Kristo anavyokuwa daraja kati ya Mungu na sisi.

- Warumi 1:8ff
- Yohana 14:86
- Marko 6:23
- Warumi 3:9-20,23
- Ezekieli 3:16-21
- Waefeso 2:1-3



Kielelzo 1.1 Hatua za Uinjilisti



### B. Tu njia ya Bwana ya Kuufikia Ulimwengu

Tangu kipindi cha Kristo, Wafuasi wameamriwa kwa jukumu la kumuwakilisha Bwana na ufalme wake duniani. Mitume walikuwa wa kwanza kupokea amri. Walielewa kuwa walitakiwa kuwa mashahidi—kwamba walitakiwa kuwa wasemaji na mabalozi wa Kristo. Taratibu hizi zinzonyesha kuwakilisha ukweli kwa uaminifu tunapokuwa tumeuelewa na uaminifu wa kumuwakilisha Mungu ambaye ametununua na kututuma nje.

Paulo alielewa wajibu huu kama mdeni au wajibu ambao alidaiwa na Bwana kwa waliopotea. Wakati ni kweli kwamba Mtu anaweza kuokoka kwa neno la Bwana na kwa Roho Mtakatifu peke yake, hili si la kawaida kabisa. Kwa hakika, Hata wakati Kristo mwenyewe alipomwambia Paulo juu ya barabara ya Damaskasi, alimtuma Anania kukamilisha utaratibu wa uinjilisti katika maisha ya Paulo. Mungu anapenda kutumia wanaume na wanawake wanaomjua kama njia ya kuwafikia waliopotea.

- 2 Wakorintho 5:16-21
- Matendo 1:8
- Marko 16:15
- Mathayo 28:18-20
- Warumi 1:14-17
- 2 Timotheo 4:5b

### C. Wengi Wako Tayari Kusikia na Kuelewa Suluhu kwa Mashaka Yao ya Kuchagua Kati ya Mambo Mawili

Mwana falsafa wa kifransa Blaise Pascal alinukuru kwamba ndani ya mtu kuna sura ya Mungu iliyofagiliwa, ambayo Mungu peke yake anaweza kujalizia kikamilifu. Kupitia vizazi, watu wametafuta suluhu kwa mashaka yao ya kiroho. Orodha hapo chini ni mfano tu wa kati ya mengi katika Agano Jipya ambao kwa uwazi wangejadili hali zao kwa tumaini la kutatua matatizo yao. Kuna wengine kama wao ambao watasikiliza injili kama tutaenda kwao na kuiweka wazi.

- Nikodemu—Yohana 3
- Mtu aliyezaliwa kipofu—Yohana 9
- Mwanamke kisimani—Yohana 4
- Umati wa Yerusalemu—Matendo 2
- Zakayo—Luka 19
- Mjakazi wa Ethiopia Matendo 8

### D. Injili Ina Uwezo wa Kubadilisha

#### 1. Injili inabadilisha hali halisi ya kiroho

Injili inawahamisha watu kutoka katika ufalme wa shetani na kuwapeleka katika ufalme wa Mungu, kutoka kwenye giza na kuwapeleka kwenye nuru, kutoka kwenye kifo kwenda kwenye uzima. Siyo tena maadui wa Kristo na watumwa wa dhambi sisi (na hao wanaokuja kwenye imani kupitia ushuhuda wetu) wamekuwa sehemu ya nyumba ya Mungu (Wakolosai 1:10-14).

2. *Injili inabadilisha ulimwengu mzima*

Injili iko inabadilisha maisha—katika eneo kubwa sana la mataifa yote, katika vijiji vilivyofichika milimani, katika mapori yenye mito inayotiririka, miongoni mwa vijana wenye matatizo, miongoni mwa familia zenye matatizo, miongoni mwa wafanya biashara wenye kazi nyingi, na viongozi wa kisiasa wenye usumbufu. Katika mabara yote, injili inampenyo. Familia, jamii, na taifa ulimwenguni kote wanabadilishwa na injili ya Yesu Kristo.

3. *Injili inabadilisha jamii*

Watu wanaokuja kwa Kristo na kujitoa wenyewe kwa Roho Mtakatifu anayekaa ndani yao, jumuiya ya hao wanaompenda Kristo wanaweza kuambukiza maadili mema kwa msalaba uliohusishwa vizuri mbele ya uso wa taifa lako

4. *Injili inabadilisha mtu pekee*

Wote walioweka imani yao ndani ya Kristo kwa kusikia habari ya injili wana ushuhuda wa jinsi neema ya Mungu ilivyowabadilisha kwa undani kila mtu pekee, kumfanya kila mmoja kuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo. Mtu pekee na familia wameguswa kwa undani.

5. *Injili inabadilisha maisha sasa*

Injili ya kujitoa maisha kwa Yesu imetukombo. Tumeokolewa kutoka katika adhabu ya dhambi! Zaidi ya hayo, Tutaokolewa kutoka kwenye uwepo wa dhambi. Kwa jinsi hiyo, kwa sasa tumeokolewa kutoka kwenye nguvu ya dhambi. Injili inaleta mabadiliko leo (Kor 15:55-56; Rum 5:8-10).

6. *Injili inabadilisha hali yetu ya mbele*

Kwa hao wanaokuja kwenye imani kwa sababu ya kazi ya Roho Mtakatifu ndani yetu, tunaweza tukaambukiza siyo kizazi chetu tu, lakini hata kinachokuja pia. Tunaweza kuwa msingi wa vizazi vya kiroho ndani na nje ya familia zetu wenyewe.

7. *Injili inabadilisha umilele wetu*

Mabadiliko yaliyoletwa na injili yanagusa siyo tu maisha yetu ya muda, lakini hatima yetu ya milele pia. Sisi kama mabibi arusi wa Kristo, kanisa, ni ushuhuda wa milele katika anga la roho za neema ya Mungu na rehema (Efe 3:10, 11).

### III. NIA YA UINJILISTI

#### A. Inawezekana Kuinjilisha Nje ya Wajibu au Mapatano na Mungu au Wengine

Paulo aliandika kwa Warumi 1:14 kwamba alikuwa mdeni kwa hao ambao walikuwa hawajasikia habari ya injili. Alihisi wajibu wa kushirikisha kile alichokuwa nacho, injili, kwa wengine. Watu wa Mungu wamejiita wenyewe watumishi wake, wakimaanisha kuwa shughuli zao zilikuwa angalau kwa upande wa kuwa wamevutiwa kwa kuitikia mamlaka ya Mungu, Bwana wao

Katika Wakolosai 1:28, mtume Paulo anaongelea juu ya lengo lake la huduma ya injili, "...tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo." Mara nyingi kinachowavutia watumishi wa Mungu kwenye uinjilisti ni maelekezo ya mbali ya kuona lengo la kusudi la Mungu linakamilika ulimwenguni. Tumaini na utoshelevu pekee vinaweza kutuchochea tunapokuwa tunatumikia injili.

#### B. Inawezekana Kuinjilisha Nje ya Hofu ya Mungu na Hukumu Yake

Pengine kutoka muda hadi muda kule kujisikia upendo juu ya Mungu na watu kunakuwa hakupo, na hali ya kazi haituvuti. Wakati mwingine ukweli kwamba tunawajibika kwa Mungu na siku moja tutajibu kwake juu ya kazi yetu ya kuchochewa na kujisikia hofu ndani yetu. Hata hofu hii inaweza kutuvuta kwenye huduma. Mungu alimwonya Ezekieli kwa lugha ya ukali kuchukua ujumbe wake kwa watu wake au kubeba matokeo (Eze 3:16-21). Yona alinjilisha baada ya kuwa ametapikwa na samaki (Yon 2).

### C. Inawezekana Hata Kuinjilisha kwa Ujumla Pasipokuwa na Sababu Inayofaa

Katika moja ya barua za Paulo kwa kanisa changa, alinukuru kuwa baadhi wameitangaza injili “kwa fitina na husuda” (Flp 1:15). Aliendelea kusema yadhuru nini? Kwamba injili ya Kristo ilikuwa imehubiriwa ndiyo ilikuwa na maana kwa Paulo. Alifurahia kwamba Kristo alikuwa anahubiriwa bila kujali nia zao mbaya! (Flp 1:15-18).

### D. Tunatakiwa Kuinjilisha Kwa Upendo Wetu Kwa Kristo Na Kwa Waliopotea


Muumini anayekua anajikuta zaidi anakua mwenyewe katika upendo kwa Kristo na, matokeo yake, kwa hao ambao Kristo anawapenda—kanisa na waliopotea. Paulo alizungumzia upendo wa Yesu “watubidiisha” kumshawishi mtu (2Kor 5:14).

Inaonekana kutokana na kusoma 1Yaohana kilichowavutia na kumchochea mtume Yohana kuitangaza injili ilikuwa haja ya kuwashirikisha idadi ya watu waliokuwa wakiongezeka katika ushirika wa kanisa.

## IV. SEHEMU YA UINJILISTI KATIKA MKAKATI WA KUM

Mkakati wa kueneza upandaji kanisa unategemeana zaidi na juhudi za kiujilisti zilizoelekezwa. Kueneza uinjilisti kunaendana na kueneza upandaji kanisa. Cha kwanza na msingi wa kazi ya uinjilisti. kuwaleta watu kwenye imani ndani ya Kristo—lazima kufanikishwe kwa kazi inayoendelea ya kuwalisha na kuwaandaa waumini wapya na kuwafuasa. Lakini katika kazi ya baadaye, hatujaribu kukataa sehemu nyeti ya makusudio mema, kuendelea na kazi ya kiujilisti, kujenga daraja kati ya waliopotea na kuwaleta kwenye imani. Kuna uwiano ambao unatakiwa kuwepo kati ya kuwaambia habari njema na kuwasaidia kuelekea kwenye imani. Kuacha pengine kunahatarisha kazi ya Mungu ambayo tunahusika nayo.

### Kielelezo 1.2 Kutunza Uwiano



Tunahitaji kuwasaidia hao ambao Mungu ametupa kufuasa, lakini tunatakiwa tusiridhike tu na idadi ya waliokwisha kuingia kwenye imani. Lazima tusingahau kazi ya uinjilisti. Lazima tuwe tumejitoa na wenye bidii katika wajibu wetu wa kuwafikia waliopotea kwa injili. Bila watu kuendelea kuletwa katika imani (kwa kufikiri mzunguko wa upandaji kanisa), hakuna kuendeleza zaidi, hakuna maendeleo zaidi ya viongozi, na hakuna tumaini kwa ongezeko linaloendelea la makanisa. Uinjilisti lazima uchukue nafasi ya kwanza katika kueneza upandaji wa kanisa. Kuandaa na kuhamasisha waumini wote kufanya kazi ya uinjilisti itakuwa ndiyo kiungo cha kwanza katika mkakati wowote wa KUM.

## MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI

- Unaamini kwamba Mungu angeweza kukutumia wewe kuwafikia wengine kwa ajili yake?
- Ni jambo gani la muhimu ambalo limewahi kukutokea wewe binafsi?
- Kama hiyo ni kweli, ni nini, kisha, jambo muhimu unaloweza kufanya maishani kufanya mguso dhahiri kwa watu wengi unaowajua?
- Ni nini “kazi ya uinjilisti”? (2Tim 4:2)

- Ni nini zaidi kinakuvuta kushirikisha injili?
- Unaweza ukafikiri Watu kumi katika wale mlio na uhusiano nao wanaohitaji uhusiano binafsi na Kristo?
- Ni mipango gani uliyonayo ya kuongeza juhudi za uinjilisti.

#### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**


Ukiwa na waumini wengine wawili, unda maombi ya utatu kukutana na kuomba mara kwa mara kwa ajili ya wokovu wa hao ambao Mungu amewaweka moyoni mwako (tazama maombi ziada 3A: Maombi ya Utatu).

#### **VYANZO**

- Coleman, Robert. *The Master Plan of Evangelism*. Old Tappan, NJ: Spire Books, 1964.
- Little, Paul E. *How to Give Away Your Faith*. Madison, WI: IV Press, 1968.
- Maisel, John. *Is Jesus God?* Budapest, Hungary: Central European Bible Institute, 1991.
- McDowell, Josh. *More than a Carpenter*. Minneapolis, MN: Worldwide Publications, 1977.



## Daraja



Mchoro wa daraja unaweza kuwa njia yenye mafanikio ya uinjilisti. Unaweza kukuta hatimaye inasaidia kutengeneza mchoro wa kawaida wa hili kwenye kipande cha karatasi tupu wakati unashirikisha habari njema (kwa mstari wa Biblia unaoendana) na rafiki ambaye hajaokoka. Mawakilisho ya mdomo na ya maandishi mara nyingi yana nguvu zaidi kuliko kutumia vyombo vya habari peke yake.



# Kuanzisha Ushuhuda Wako Binafsi

HIKI NDICHO MUNGU  
ALICHONIFANYIA

## Kusudi la Somo

Kusudi la somo hili ni kuelezea thamani na maandalizi ya ushuhuda binafsi.

## Wazo Kuu

- Ushuhuda binafsi una nguvu na ni njia isiyo ya kutisha kushuhudia waliopotea.
- Ushuhuda binafsi utakuwa wa mafanikio kama umeandaliwa kwa uangalifu kwa kuweka habari muhimu zaidi.
- Ushuhuda binafsi unaeleza yale ambayo Mungu ameyafanya katika maisha yako—siyo mahubiri.

## Matokeo Yanayotarajiwa

Wakati yaliyomo katika somo hili yanapoeleweka, kila mshiriki anatakiwa:

- Kuelewa uwezekano wa matokeo ya kiroho kwa ushuhuda binafsi.
- Kuanzisha dakika tatu—tano za ushuhuda binafsi kuwashirikisha wengine.

## Ushauri kwa Wakufunzi

Hili ni somo la masaa-mawili. Katika saa ya kwanza ni kuwatambulisha washiriki juu ya ushuhuda binafsi ni nini na kuwasaidia kuandika ushuhuda wao binafsi. Saa ya pili inatakiwa itumike kufanya mazoezi ya kushirikishana shuhuda zao (wazo la V. katika muhtasari). Ingawa somo limeandikwa kwa pamoja, unaweza kuamua kuacha siku chache katikati ya masaa mawili kuwapa washiriki muda wa kujifunza shuhuda zao na kabla hawajashirikishana darasani.

Hakikisha kuwa shuhuda siyo ndefu zaidi ya dakika tano. Fikiria kutumia saa ya kusimamisha kuhakikisha kuwa hili halivunjwi. Inachukua uadilifu mkuu kuweza kuwa na ushuhuda mfupi, lakini kutakuwa na hali ambapo utakuwa na muda wa kushirikisha ushuhuda mfupi tu. Inaweza kuwezekana zaidi mkiigawanyika katika makundi mawili au matatu kwa ajili ya kushirikishana ushuhuda.

## I. ASILI YA USHUHUDA

### A. Tumeitwa Kuwa Mashahidi

Katika Matendo 1:8, Yesu anawaahidi wanafunzi wake kwamba watapokea nguvu akisha kuwajilia juu yao Roho Mtakatifu na kwamba watakuwa mashahidi wake. Lakini ushahidi ni nini? Katika chumba cha mahakama ya haki, shahidi ni yule anayeitwa kuja kueleza aliyoyaona juu ya wengine. Anawambia ukweli juu ya tukio nyeti, kama alivyoliona. Shahidi hatarajiwi kujua kila kitu au kulinganisha ukweli mbalimbali. Anatarajiwa kueleza anachokumbuka na kwa uaminifu. Yale ambayo shahidi anayawakilisha ni ushuhuda wake.

### B. Tumeitwa Kutoa Ushuhuda


Kila mmoja wetu aliyeweka imani yake ndani ya Kristo pia ana ushuhuda wa kushirikisha. Ni nini umekuwa uzoefu wako na Kristo? Ushuhuda wetu ni wa kipekee kama alama za vidole na vipande vya barafu. Ushuhuda wetu unatoa ufahamu wenye thamani kwa wengine juu ya jinsi Mungu anavyofanya kazi miongoni mwa watu. Hii ni habari muhimu wasioamini wanahitaji kufanya uamuzi waliojulishwa juu ya Kristo. Shuhuda zetu pia zinatia moyo wale wanaompenda Mungu. Tunapokuwa tunawaambia kazi ya Kristo katika maisha yetu, wengine wanavutiwa kwenye imani ya juu na utii.

## II. THAMANI YA USHUHUDA

### A. Kushinda upinzani kwenye Injili

Watu wanasikiliza kwa kuchagua. Watu unaotaka kuwaleta kwenye imani wanaweza kupinga majadiliano ya kitheolojia juu ya wokovu. Lakini wataweza kwa urahisi na haraka kusikia habari yako binafsi jinsi ulivyomwamini Kristo. Watu wanapenda kusikiliza habari za kuvutia. Endapo wanakubali au la, wanataka uwape sababu nzuri za kuamini. Ushuhuda wako, unaushirikisha kwa uaminifu, kwa ufupi na ubunifu, unaweza kutumiwa na Roho kufungua macho yao na akili zao kuona ukweli wa kiroho katika namna mpya.

#### Kielelezo 2.1 Kushinda Vizuizi Kwa Ushuhuda Binafsi



### B. Kumshinda shetani katika vita vya kiroho

Tunapokuwa tunashirikisha imani zetu watu wengine, tumejihusisha bege kwa bega na Mungu katika vita vya kiroho, kushambulia ufalme wa shetani. Katika Ufunuo 12:10-12, tunasoma yafuatayo:

*"...sasa kumekuwa wokovu na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku. Nao wakamshinda kwa damu ya mwana-kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa. Kwa hiyo shangilieni, enyi mbingu, nanyi mkaao humo!"*

Tambua njia ambayo mshitaki wa ndugu zetu, shetani, alishindwa.. "kwa damu ya mwanakondoo" na "kwa neno la ushuhuda." Kazi iliyomalizika ya Kristo na uhusiano wetu kwa Kristo ni mambo mawili Mungu anayotumia kumshinda mwovu. Ushuhuda wako wa imani katika Kristo na uaminifu wako kwa Kristo ni zana muhimu Mungu anayotumia kujenga kanisa lake. Hata kama tunakutana na ugumu, kuugua au hatimaye kifo, tunashinda na shetani anapoteza! Kwa hiyo waambie watu Mungu alichokifanya maishani mwako!

## III. MIFANO YA USHUHUDA

Maandiko yamejaa hesabu ya watu wakitoa shuhuda zao binafsi. Soma yafuatayo kama mifano ya ushuhuda binafsi na tazama unachoweza kujifunza kutokana nayo. Tumia njia unayojifunza katika masomo juu ya masomo ya kufuata neno.

### A. Mwanamke Kisimani (Yoh 4:28-29)

- Ni nini alisema?
- Ni kwa nani alishuhudia?
- Kwa nini alichagua mfumo huu wa ushuhuda?

**B. Mtu aliyezaliwa kipofu**

- Ni kwa nani alishuhudia?
- Ni nini alichosema?
- Ni tukio lipi lilikuwa la ushuhuda?
- Ni jinsi gani ushuhuda ulipokelewa?
- Ni jinsi gani alishughulikia upinzani?

**C. Majadiliano ya Paulo (Matendo 9, 22, na 26)**

Katika vifungu hivi, tambua jinsi Paulo alivyosisitiza juu ya tofauti ya hali zenye uzoefu unaofanana kugusa wasikilizaji tofauti.

- Sura ya 9 ni hesabu ya Luka ya kubadilishwa kwa Sauli.
- Sura ya 22 ni kumbukumbu ya Luka ya ushuhuda wa Paulo uliokatizwa mbele ya Wayahudi wa Yerusalemu.
- Sura ya 22:2-23 ni kumbukumbu ya Luka ya ushuhuda wa Paulo mbele ya mfalme Agripa.

**D. Ushuhuda wa Paulo Juu ya matukio katika Yerusalemu**

**IV. UTAYARISHAJI WA USHUHUDA**

Tafadhali chukua ukumbusho wa sehemu hii kuandaa toleo la ushuhuda wako binafsi wa dakika 3-5. Muombe Mungu kukusaidia kukumbuka maongezi yako kwa uwazi. Tengeneza baadhi ya notisi juu ya wazo la ufunguo au mistari unayotaka kuhakikisha unaihusisha. Ni bora kama ungetenga kitu kimoja maalumu kilichokuleta kwenye imani ndani ya Kristo—Kitu ambacho wengine , wasio wakristo, wanaweza kujilinganisha nacho. Katika ushuhuda wako, shirikisha katika migawanyo hii mitatu mipana:

**Kilelezo 2.2 Ushuhuda wangu**

***Ushuhuda wangu***

*Maisha yangu kabla . . .*

*Jinsi nilivyomtumaini Kristo. . .*

*Maisha yangu sasa . . .*

**A. Maisha yako yalikuwaje kabla hujakutana na Kristo?**

Hii italenga kwenye maeneo ya hitaji ambayo ulimwamini Kristo kuwa angeyatimiza katika maisha yako. Kama inatoa mazingira ya kawaida kati yako na mtu unayetaka kumleta kwenye imani. Kwa nini ulimhitaji Kristo? Jaribu kutenga jambo la wazi lililokufanya kufikia kwenye kutubu.



## B. Ni jinsi gani ulikuja kwa Kristo?

Ni nini hasa kilitokea? Ni lini ulimtumaini Kristo? Ni nini ulifanya? Ni mstari gani Roho Mtakatifu alitumia katika maisha yako? Je kuna mtu alikusaidia katika utaratibu huu? Fanya hili kuwa msingi iwezekanavyo; jifanye kana kwamba msikilizaji ni anayemtafuta—Mungu na uzoefu wako utatumika kana kwamba ni sura halisi ambayo anaweza kujilinganisha nayo.

## C. Ni jinsi gani kumjua kwako Kristo kumebadili maisha yako?

Ni hali gani imani yako imekuwa nayo katika maisha yako? Ni kwa njia zipi za kimatendo maisha yako yamebadilika? Kumekuwa na mabadiliko yaliyokushangaza? Matarajio yako yametimia? Usizungumzie tu wakati uliopita—zungumzia injili inachofanya katika maisha yako leo. Usiepuke isivyolazimu kuzungumzia juu ya magumu—wasio wakristo wanayotakiwa kujua kwamba wakristo wana magumu kwa sababu wanayo, wasio wakristo kawaida wana matatizo. Wasikilizaji wanatakiwa kujua Kristo ni nanga katika misukosuko na kwamba maisha ya wakristo yanatoa nguvu ya kuishi.

## V. KUSHIRIKISHA USHUHUDA BINAFSI

Sasa kwamba umetayarisha ushuhuda wako binafsi, chukua muda wa kuushirikisha kwa wafunzwa wengine. Kila mshiriki anahitaji nafasi ya kushirikisha ushuhuda wake. Tumia dakika tano kusikiliza kila ushuhuda isizidi dakika kutoa matokeo. Ushuhuda unapokuwa umeshirikishwa, tumia mawazo yafuatayo kutafakari ufanisi wa kila moja.

### A. Ukamilifu

Ushuhuda unasimulia historia yote? Una sehemu zote tatu?

- Maisha kabla ya Kristo: Ni kitu gani asiye mkristo anachoweza kujilinganisha nacho?
- Misukosuko wakati wa mabadiliko: Inakuwaje hali ya asiye mkristo?
- Maisha tangu ulipompata Kristo: Ni jinsi gani maisha yako ni tofauti na ya asiye mkristo?

### B. Uwazi

Ushuhuda utakuwa rahisi kwa asiye mkristo kuelewa, au umejawa na lugha ya dini ambayo inaweza kumchanganya asiyeamini? Unaonekana kama mahubiri au ni msaada wa mapendekezo kwa rafiki?

### C. Injili

Yote ni mambo muhimu ya injili yaliyogusiwa katika ushuhuda? Wakati haiwezekani kwenda kwa undani kuhusu yote kwa hili katika ushuhuda mfupi. Yote au baadhi ya mambo yafuatayo yanatakiwa yafanyike sawasawa.

#### 1. Taarifa mbaya

- Tu wenye dhambi, na mshahara ni mauti
- Mungu ni mtakatifu, na hatuwezi kumpendeza
- Yesu—mwana wa Mungu alikufa badala yetu

#### 2. Habari njema

- Tunaokolewa kwa imani—si kwa matendo yetu
- Tumezaliwa upya katika familia ya Mungu kama watoto wake
- Tuna uhakika wa maisha ya milele

### D. Ufupisho

Shuhuda hizi zinatakiwa zisiwe ndefu zaidi ya dakika tano. Kuna jambo lolote ambalo si muhimu kwenye ushuhuda? Hatuhitaji kusimulia historia yote sasa—uinjilisti na utaratibu.

### **MASWALI YA KUTAFAKARI, MARUDIO NA MATUMIZI**

- Wapi baadhi ya sehemu na ni zipi baadhi ya nyakati katika siku yako au juma wakati ambao ungeweza kushirikisha ushuhuda wako?
- Ni vipengele gani vya maongezi ya kawaida vinavyoweza kuwa tayari kutoa “ufunguaji” kwa utangulizi wa kawaida wa ushuhuda wako? Unasafiri katika usafiri wa umma?
- Unapata muda wa mapumziko au kula chakula kazini? Mwombe Bwana kuandaa “muda wa kimungu” kwa ajili yako kuweza kushirikisha ushuhuda wako.

### **UTEKELEZAJI WA AZIMIO**

- Shirikisha ushuhuda wako wakristo wengine angalau watatu watakaoweza kuona kama uko wazi katika kuwakilisha kwako.
- Uwe tayari kushirikisha tena ushuhuda wako wakati wa mafunzo yajayo au wakati wa semina hii
- Kwa maombi weka mpango ambao utaletea kushirikisha ushuhuda wako kwa watu wawili wasio wakristo au watu unaowasiliana nao katikati ya wiki mbili. Mwombe Mungu kuandaa “muda wa kimungu” kwa ajili yako kushirikisha ushuhuda wako (pengine bila maonyo ya kuendelea) katikati ya wiki zingine nne.